




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA UFANISI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22



MACHI 2023



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, Tambukareli, 41104 Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: +255(026)2321759, Nukushi: +255(026)2117527, ocag@nao.go.tz, info@nao.go.tz Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Kumb. Na. CGA.319/421/01B

29 Machi 2023

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
40400 DODOMA.




YAH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA UFANISI 2021/22

Kwa mujibu wa Kifungu cha 143 (4) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, ninawasilisha kwako Ripoti ya Jumla ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi 2023.

Ninawasilisha.

Charles E. Kichere
Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali



Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

Kufanya kazi kwa ushirikiano

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.



Kufanya kazi kwa utaalum

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

Kufanya kazi kwa uadilifu

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

YALIYOMO

| | |
|--|-----|
| ORODHA YA MAJEDWALI | vii |
| SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI | x |
| SHUKRANI | xiv |
| MUHTASARI | xvi |
| SURA YA KWANZA | 1 |
| 1.1 USULI WA UKAGUZI WA UFANISI | 2 |
| 1.2 MAMLAKA YA KUFANYA UKAGUZI WA UFANISI | 3 |
| 1.3 MADHUMUNI YA RIPOTI | 3 |
| 1.4 MTAZAMO WA RIPOTI YA JUMLA | 5 |
| 1.5 UMUHIMU WA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU | 7 |
| 1.6 UHALALI WA UKAGUZI | 8 |
| 1.7 MCHAKATO WA UTHIBITISHO WA TAKWIMU NA TAARIFA ZILIZOTOLEWA | 9 |
| 1.8 MUUNDO WA RIPOTI | 10 |
| SURA YA PILI | 11 |
| MAELEZO YA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU | 12 |
| 2.1 UTANGULIZI | 12 |
| 2.2 USULI KUHUSU MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU | 12 |
| 2.3 TAASISI MUHIMU, NA MFUMO WA KISHERIA UNAOSIMAMIA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO | 14 |
| 2.4 WAHUSIKA WAKUU KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO | 15 |
| 2.5 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO | 15 |

| | | |
|-----|---|------------|
| 2.6 | MAHITAJI YA UKAGUZI KATIKA KUTEKELEZA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU | 17 |
| 2.7 | UKAGUZI WA UFANISI ULIOFANYIKA KUHSIANA NA MPANGO PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU | 19 |
| 2.8 | MIFUMO YA UGHARAMIAJI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA MAENDELEO YA TAIFA YA MIAKA MITANO | 30 |
| | UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU NCHINI | 32 |
| 3.1 | UTANGULIZI | 32 |
| 3.2 | USULI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU NCHINI | 32 |
| 3.3 | MALENGO YA UKAGUZI | 35 |
| 3.4 | MATOKEO YA UKAGUZI | 36 |
| 3.5 | HITIMISHO MAHUSUSI LA UKAGUZI | 57 |
| | SURA YA NNE..... | 58 |
| | USIMAMIZI WA MIFUMO YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA | 59 |
| 4.1 | UTANGULIZI | 59 |
| 4.2 | USULI..... | 59 |
| 4.3 | UHUSIANO KATI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA USIMAMIZI WA MIFUMO YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA..... | 60 |
| 4.4 | MIKAKATI NA JITIHADA ZA SERIKALI KATIKA USIMAMIZI WA MIFUMO YA UTOAJI NA UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA AFYA | 61 |
| 4.5 | MALENGO NA MAWANDA YA UKAGUZI | 63 |
| 4.6 | MATOKEO YA UKAGUZI | 64 |
| 4.7 | ATHARI KWA UFIKIAJI WA MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU..... | 109 |
| 4.8 | HITIMISHO LA UKAGUZI | 110 |
| | SURA YA TANO..... | 112 |
| | SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU | 113 |



| | | |
|---|--|-----|
| 5.1 | UTANGULIZI..... | 113 |
| 5.2 | USULI | 113 |
| 5.3 | UHUSIANO WA SAYANSI, UBUNIFU NA TEKNOLOJIA NA MIPANGO YA MAENDELEO YA TAIFA YA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU | 114 |
| 5.4 | MALENGO NA MAWANDA YA UKAGUZI | 116 |
| 5.5 | MATOKEO YA UKAGUZI..... | 117 |
| 5.6 | MCHANGO WA UKAGUZI KATIKA KUFIKIA MALENGO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU | 137 |
| 5.7 | HITIMISHO LA UKAGUZI | 137 |
| SURA YA SITA | | 139 |
| MAZINGIRA NA USALAMA WA CHAKULA | | 140 |
| 6.1 | UTANGULIZI..... | 140 |
| 6.2 | USULI KUHUSU MAZINGIRA NA USALAMA WWA CHAKULA | 140 |
| 6.3 | MALENGO NA MAWANDA YA UKAGUZI | 146 |
| 6.4 | MATOKEO YA UKAGUZI..... | 148 |
| 6.5 | MCHANGO WA KAGUZI KATIKA KUFIKIA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO PAMOJA NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU..... | 175 |
| 6.6 | HITIMISHO LA UKAGUZI | 177 |
| SURA YA SABA | | 180 |
| USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA NA UWEKEZAJI WA MALI ZA SERIKALI..... | | 181 |
| 7.1 | UTANGULIZI..... | 181 |
| 7.2 | USULI KUHUSU USIMAMIZI WA UONDOSHAJI WA MAGARI YA SERIKALI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA SERIKALI. | 181 |
| 7.3 | MALENGO NA MAWANDA YA UKAGUZI | 185 |
| 7.4 | MATOKEO MAKUU YA UKAGUZI..... | 186 |
| 7.5 | ATHARI ZA KUTOFIKIWA KWA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO | 209 |



| | | |
|--|---|------------|
| 7.6 | HITIMISHO LA UKAGUZI | 210 |
| SURA YA NANE | | 212 |
| MIPANGO MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI YA WATU | | 213 |
| 8.1 | UTANGULIZI | 213 |
| 8.2 | USULI KUHUSU URASIMISHAJI WA MAKAZI HOLELA | 213 |
| 8.3 | UHUSIANO KATIKA YA MIPANGO MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI, NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU NA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO | 214 |
| 8.4 | MALENGO NA MAWANDA YA UKAGUZI | 215 |
| 8.5 | MATOKEO YA UKAGUZI | 217 |
| 8.6 | MCHANGO KATIKA KUFIKIA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO YA TAIFA YA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU | 226 |
| 8.7 | HITIMISHO LA UKAGUZI | 227 |
| SURA YA TIS A | | 229 |
| USAMBAZAJI WA MAJI | | 230 |
| 9.1 | UTANGULIZI | 230 |
| 9.2 | USULI WA UENDESHAJI NA UKARABATI WA MIUNDOBINU YA USAMBAZAJI WA MAJI ... | 230 |
| 9.3 | UHUSIANO WA USAMBAZAJI MAJI NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO | 231 |
| 9.4 | MIKAKATI NA JITIHADA ZA SERIKALI KUHUSU UPATIKANAJI WA MAJI | 232 |
| 9.5 | MALENGO NA MAWANDA YA UKAGUZI | 232 |
| 9.6 | MATOKEO YA UKAGUZI KUHUSU UENDESHAJI NA UKARABATI WA MIUNDOBINU YA USAMBAZAJI MAJI | 233 |
| 9.7 | ATHARI KATIKA KUFIKIA MPANGO WA PILI NA WA TATU WA MAENDELEO YA TAIFA YA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEU | 258 |
| 9.8 | HITIMISHO LA UKAGUZI | 259 |
| SURA YA KUMI | | 261 |



| | |
|--|-----|
| HITIMISHO NA MAPENDEKEZO | 262 |
| 10.1 UTANGULIZI | 262 |
| 10.2 HITIMISHO LA UKAGUZI LA UJUMLA..... | 262 |
| 10.3 HITIMISHO MAHUSUSI | 263 |
| 10.4 MAPENDEKEZO YA UKAGUZI..... | 269 |
| MAREJELEO..... | 273 |
| VIAMBATISHO | 282 |



ORODHA YA MAJEDWALI

| | |
|--|-----|
| Jedwali Na. 6.1: Hali ya Upungufu wa Vifaa katika Maeneno ya Kuingilia Nchini . | 150 |
| Jedwali Na 6.2: Hali ya Hatua za Udhhibiti wa Viumbe Vamizi Nchini | 154 |
| Jedwali Na.6.3: Hali ya Vifaa vya Kudhibiti Viumbe Vamizi katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Rungwe | 156 |
| Jedwali Na. 6.4: Idadi ya Vikao Vilivyopangwa dhidi ya Vilivyofanyika | 161 |
| Jedwali Na. 6.5: Vikao vya Nusu Mwaka na Mwisho wa Mwaka..... | 162 |
| Jedwali Na. 6.6: Muhtasari wa Utekelezaji wa Mikakati ya Usindikaji na Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo kuanzia Mwaka 2017/18-2021/22..... | 163 |
| Jedwali Na. 7.1: Magari Mabovu ambayo Yameegeshwa na Hayatumiki kufikia Mwezi Septemba 2022 | 187 |
| Jedwali Na. 7.2: Hali ya Uundaji wa Bodi za Utafiti | 189 |
| Jedwali Na. 7.3: Hali ya Mali za Taasisi Zilizosajiliwa katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)..... | 190 |
| Jedwali Na. 7.4: Hali Halisi ya Magari Yaliyosajiliwa katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali dhidi ya Idadi Halisi ya Magari Yanayomilikiwa na Taasisi za Umma | 191 |
| Jedwali Na. 7.5: Tofauti ya Takwimu kati ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Timu ya Ukaguzi | 192 |
| Jedwali Na. 7.6: Thamani ya Awali ya Magari Ikilinganishwa na Gharama Zote za Ununuzi na Bima Pekee katika Wizara ya Fedha na Mipango | 194 |
| Jedwali Na. 7.7: Muda Uliotumika Kutoa Vibali vya Uondoshaji wa Magari ya Serikali | 194 |
| Jedwali Na 7.8: Mali Zisizohamishika dhidi ya Uwekezaji wa Dhamana za Kiserikali | 202 |
| Jedwali Na. 9.1: Miundombinu ya Usambazaji Maji Isiyofanya Kazi katika Miradi ya Usambazaji Maji Iliyotembelewa..... | 236 |
| Jedwali Na. 9.2: Hali ya Uandaaji wa Mipango, Ratiba na Taratibu za Uendeshaji | 239 |
| Jedwali Na. 9.3: Hali ya Upatikanaji wa Mipango Mbalimbali katika Mamlaka za Maji Zilizotembelewa | 242 |
| Jedwali Na. 9.4: Hali ya Utunzaji wa Kumbukumbu za Ukarabati wa Miradi ya Usambazaji wa Maji | 246 |
| Jedwali Na. 9.5: Kasoro za Miundombinu ambazo Hazikurekebishwa katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Zilizotembelewa | 247 |

| | |
|--|-----|
| Jedwali Na. 9.6: Mapato ya Mwaka Yanayopotea kutokana na Maji Yasiyo ya Mapato kwa Miaka ya Fedha 2019/20 na 2020/21 | 252 |
| Jedwali Na. 9.7: Ufuatilia Uliofanyika kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira | 257 |



ORODHA YA VIELELEZO

| | |
|--|-----|
| Kielelezo Na. 3.1: Uhusiano wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano | 34 |
| Kielelezo Na. 6.1: Teknolojia Zilizobuniwa na Kushirikishwa kwa Wadau kwa Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2017/18 hadi 2021/22..... | 170 |
| Kielelezo Na.9.1: Asilimia ya Matumizi ya Miundombinu Kulingana na Uwezo wa Miundombinu | 235 |
| Kielelezo Na.9.2: Kiasi cha Madeni katika Mamlaka za Maji Zilizotembelewa kuanzia Mwaka 2019/20 hadi 2021/22 | 241 |
| Kielelezo 9.3: Asilimia ya Bajeti ya Uendeshaji na Ukarabati Inayolipwa kama Ankara za Umeme katika Mamlaka za Maji | 244 |
| Kielelezo Na.9.5: Hali ya mita za maji zisizofanya kazi | 254 |
| Kielelezo Na. 9.6: Asilimia ya Wateja Wasio na Mita kutoka katika Jumuiya za Utoaji wa Huduma za Maji Zilizotembelewa | 255 |



SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI



Nina furaha kuwasilisha Ripoti yangu ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi. Ripoti hii inajumuisha ripoti 12 zinazoelezea juhudi mbalimbali za Serikali za kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu ili kufikia Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.

Wakaguliwa wakuu walikuwa Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maji; Ofisi ya Makamu wa Rais - Idara ya Mazingira; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Afya; na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu. Wakaguliwa wengine walikuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Mamlaka ya Serikali Mtandao; Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia; Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania; Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma; na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii; Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini; na mamlaka za maji na usafi wa mazingira.

Ripoti hii inalenga kutoa taarifa kwa wadau (wabunge, maafisa wa serikali kuu na serikali za mitaa, wanahabari, wafadhili, na asasi za kijamii na zisizo za kiserikali kuhusiana na matokeo ya ukaguzi yaliyo kwenye ripoti za ukaguzi wa ufanisi zilizofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kufikia mwezi Machi 2023. Ufafanuzi wa kina kuhusiana na taarifa zilizoandikwa kwa kifupi unapatikana kwenye ripoti husika za ukaguzi ambazo zilikabidhiwa kwa maafisa masuuli (makatibu wakuu) wa wizara husika.

Ripoti hii inawasilishwa kwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 [Marejeo ya Mwaka 2021] ya Mwaka 2008.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila taarifa aliyotoa kwa mujibu wa Ibara ndogo ya pili ya Ibara iliyotajwa. Mara taarifa hiyo inapopokelewa, Rais atamwelekeza waziri husika kuwasilisha taarifa hiyo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge kabla ya siku saba kupita tangu kikao cha kwanza cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanza. Ibara hiyohiyo inamruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha ripoti yake kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwapo Rais, kwa sababu zozote zile, atashindwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa Spika kama sheria inavyotaka.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 [Marejeo ya Mwaka 2021] kumeimarisha uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu katika kutimiza majukumu yake ya kikatiba. Uhuru wa utendaji wa Ofisi yangu unatarajiwa kuniwezesha kupata taarifa na kuwa na udhibiti muhimu wa rasilimali zote zilizopo kwa ajili ya Ofisi, ikiwa pamoja na rasilimaliwatu na fedha, ambazo zitaiwezesha Ofisi yangu kufanya kazi bila kuingiliwa na mtu au mamlaka yoyote, zikiwemo zile ninazozikagua.

Sheria hii imepanua mawanda ya ukaguzi utakaofanywa na Ofisi yangu kwa kunipa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi na aina zingine za ukaguzi kadiri nitakavyoona inafaa, zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha kama ambavyo Ofisi yangu imekuwa ikifanya kwa miaka mingi.

Taarifa hii imeniwezesha kutoa maoni huru kwa Bunge kuhusiana na matumizi sahihi ya rasilimali za umma na juhudi mbalimbali za Serikali katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu ili kufikia Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030.

Maoni hayo huru yametolewa katika kuangalia usimamizi wa utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu; mifumo ya utoaji wa huduma za afya; sayansi, ubunifu na teknolojia; mazingira na uhakika wa chakula; uwekezaji na mali za serikali; urasimishaji wa makazi holela; na uendeshaji na ukarabati wa miradi ya usamabazi maji.

Lengo kuu la kufanya kaguzi hizi lilikuwa kuchambua changamoto katika maeneo husika; na kuangalia iwapo rasilimali zilizotengwa zimetumika kwa ufanisi kwa kuzingatia uwekevu, tija, na ufanisi kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge kwenye maeneo yaliyotajwa. Ni mihimu kufahamu kwamba, wakati Ofisi yangu inafanya ukaguzi na kutoa ripoti ya utendaji wa serikali kuu, serikali za mitaa, na mashirika ya umma kulingana na sheria katika taratibu zilizopo, wajibu wa kuhakikisha kuwapo kwa ufanisi, uwekevu, na tija katika matumizi ya rasilimali za umma ni wa maofisa masuuli. Wakati huohuo, ni wajibu wa maofisa masuuli kuhakikisha kuwa hatua zinachukuliwa katika mapungufu na mapendekezo yanayotolewa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Ni matarajio ya Bunge kwamba, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapata uhakika kuhusu utoaji wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali za umma katika serikali kuu, mashirika ya umma, na serikali za mitaa; na kuhusiana na tija na ufanisi kwenye utekelezaji wa programu mbalimbali za Serikali. Ofisi yangu inachangia kwa kutoa mapendekezo ili kuboresha utendaji katika sekta ya umma.

Hivyo, serikali kuu, serikali za mitaa, mashirika ya umma, na Ofisi yangu kwa pamoja, zina mchango mkubwa kwa Bunge na katika kujenga imani kwa umma katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ingawa majukumu ya taasisi za serikali na ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi huenda yakatofautiana, matarajio ya ufanisi wa matumizi ya rasilimali za umma linabaki kuwa lengo la pamoja.

Ili kukidhi matarajio ya wabunge na umma kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya mapitio ya njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kupanua wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta ya umma. Aidha, Ofisi yangu inahakikisha kuwa ukaguzi wake unalenga maeneo ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu; na ili kuimarisha usimamizi katika sekta ya umma. Hivyo, kazi ya ukaguzi ya Ofisi yangu ni chachu katika kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma.

Ninapenda kutambua weledi na dhamira ya wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa juhudi kubwa walizofanya katika kutimiza malengo tuliyojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na ukosefu wa

fedha za kutosha, ukosefu wa vitendeakazi, mishahara duni, na wakati mwingine, kufanya kazi kwenye maeneo yasiyofikika kirahisi.

Ninatarajia kuwa Bunge na umma kwa ujumla utaipa umuhimu taarifa hii katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa rasilimali za umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania.



Charles E. Kichere

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali



SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioweka mazingira wezeshi kwangu kuweza kutimiza wajibu wangu wa kikatiba. Ninapenda kumshukuru kila mfanyakazi katika Ofisi yangu kwa jitihada zake ambazo zimeniwezesha kutoa ripoti hii kwa wakati. Ninalazimika kuishukuru familia yangu na familia za wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa uvumilivu waliouonesha katika kipindi chote cha kutimiza takwa hili la kikatiba.

Ninapenda kuishukuru Serikali na Bunge letu tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuisaidia Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake.

Vilevile, shukrani za pekee ziende kwa jumuiya ya wahisani hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Swideni (SNAO); Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Swideni (Sida); Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Mradi wa Ushirikiano wa Uswisi na Ujerumani (GFG Project) ukisimamiwa na Ushirikiano wa Kimataifa wa Ujerumani (GIZ); Benki ya Dunia kupitia Programu ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP); na wengine wote waliitakia mema Ofisi yangu ambao walichangia kwa njia moja au nyingine kwa nia ya kuleta mabadiliko katika Ofisi yangu. Michango yao katika kuimarisha ujuzi wa wafanyakazi, mfumo wa teknolojia za habari na mawasiliano, na nyenzo mbalimbali imechangia kwa kiasi kikubwa katika mafanikio ya Ofisi yangu.

Halikadhalika, ninapenda kuwashukuru wadau wengine wote, ikiwa pamoja na maofisa masuuli wa taasisi nilizozikagua kwa kutoa mchango mkubwa na taarifa muhimu zilizohitajika kwa ajili ya uandaaji wa ripoti mahususi za ukaguzi wa ufanisi ambazo ndizo zimewezesha uandaaji wa ripoti hii ya jumla.

Shukrani za kipekee ziende kwa jamii ya wanataaluma na wataalamu wa kada mbalimbali kutoka Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, maofisa wastaafu wa serikali, na wataalamu wa kujitegemea kwa uhakiki wa kina ambao umeongeza thamani ya ripoti zetu.

Ninapenda pia kuitambua Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC) ambayo itachambua na kujadili ripoti hii pamoja na ripoti za ukaguzi wa ufanisi. Ninasubiri kwa shauku kubwa maoni na maagizo yatakayotokana na mijadala ya ripoti hii. Mwisho, ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa umma Tanzania nzima, bila kusahau wajibu wa walipakodi ambao ripoti hii imetolewa kwao. Michango yao muhimu katika kujenga taifa haiwezi kupuuzwa. Mwenyezi Mungu awabariki nyote kwa kadiri mnavyojitoa katika kuendelea kusimamia uwajibikaji zaidi katika matumizi ya rasilimali za umma.



MUHTASARI

Taarifa hii ya jumla ya ukaguzi inaelezea mapungufu yaliyobainika, hitimisho, pamoja na mapendekezo katika ripoti 12 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanyika kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022. Ripoti hizo 12 zilihusu utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu nchini; usimamizi wa magari ya serikali; usimamizi wa mavuno kupitia viwanda vya usindikaji wa kilimo; udhibiti wa kampuni binafsi zinazojihusisha na ugawaji na udhibiti wa viwanja; ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji; usimamizi wa viumbe vamizi; na udhibiti wa malipo yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa watoa huduma za afya walioidhinishwa, usimamizi wa mifumo ya teknolojia za habari na mawasiliano (TEHAMA) Serikalini; udhibiti wa vifaa vya mionzi; udhibiti wa vituo binafsi vya afya; usimamizi wa shughuli za utafiti na uvumbuzi; na usimamizi wa miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na mifuko ya jamii ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii.

Hata hivyo, ripoti hii haikusudii kuwa mbadala wa ripoti 12 zilizoandaliwa na kutolewa katika mwaka wa fedha 2021/22. Kwa taarifa zaidi msomaji anashauriwa kusoma ripoti ukaguzi husika.

Mambo Makuu Yaliyobainika katika Ukaguzi

(a) Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi ulibaini kuwa Serikali imeandaa mikakati ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano kama ilivyobainishwa kutoka katika Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hata hivyo, maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi:

Mipango isiyojitosheleza na isiyojumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano: Ukaguzi ulibaini kuwa, viashiria 167 kati ya viashiria 240 vya Malengo ya Maendeleo vinatekelezeka nchini, vilijumuishwa katika hatua za awali kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Pia, ilibainika kuwa kati ya viashiria 167, viashiria 83 vilijumuishwa kikamilifu kwenye mpango huo; na viashiria 84 vilijumuishwa kwenye sera na mikakati ya kisekta inayotekelezwa nchini. Viashiria 73 vilivyobaki ni muhimu lakini havikujumuishwa katika mifumo ya maendeleo ya taifa (kama Mpango wa pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano au sera na mikakati ya kisekta)

na vilihitaji uchambuzi wa kina kabla ya kujumuishwa na kuanza kuwezesha uzalishaji wa taarifa.

Mipango isiyojitosheleza na kujumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu katika mipango ya maendeleo ya miaka mitano ilisababisha kuwapo kwa viashiria vya malengo visivyojumuishwa kwa muktadha wa kitaifa. Hali hii ilisababishwa na mapitio yasiyojitosheleza katika uwiano wa mipango-mkakati ya sekta za wizara, tawala za mikoa, na serikali za mitaa kulingana na utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu.

Utekelezaji usiotosheleza wa hatua za kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu: Ukaguzi ulibaini uwepo wa utekelezaji usiotosheleza kutoka katika sekta za wizara, tawala za mikoa, na serikali za mitaa kwa ajili ya kufanikisha mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano ambayo imejumuisha malengo ya maendeleo endelevu kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

Hali hii ilisababisha kuwapo kwa ufuatiliaji hafifu wa mfumo wa uratibu wa utekelezaji wa malengo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika ngazi za chini hivyo kuzuia ufuatiliaji na tathmini bora ya ajenda za kikanda na kimataifa.



Ukusanyaji usioridhisha wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu: Ukaguzi ulibaini ukusanyaji usiotosheleza wa rasilimali kwa ajili ya utoaji wa taarifa zinazohitajika katika kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Hali hii ilitokana na uhimizaji wa utekelezaji usioridhisha wa vyanzo vilivyoanzishwa vya ukusanyaji wa rasilimali-fedha, hivyo kusababisha kushuka kwa uchangiaji kutoka vyanzo vya mapato vilivyoibuliwa hivyo kusababisha kutegemea misaada au mikopo ya kimataifa.

(b) Udhhibiti wa Huduma za Afya kwa Vituo Binafsi na Hiari vya Huduma za Afya

Ukaguzi ulibaini jitihada zinazofanywa na Wizara ya Afya kuandaa mfumo wa usajili wa Vituo binafsi na hiari vya huduma za afya. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

Ubora usioridhisha wa huduma katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya: Ukaguzi ulibaini utoaji wa huduma za afya usiokidhi ubora unaofanywa

na vituo binafsi na hiari. Katika vituo binafsi 514 vya huduma za afya, ni 18% tu ya vituo hivyo ndiyo vilikidhi kiwango cha huduma cha nyota 3 na zaidi.

Vile vile ukaguzi ulibaini uwepo wa huduma za madawa ya binadamu pamoja na maabara zisizokidhi kiwango. Hii ni pamoja na kuwapo kwa huduma za madawa ya binadamu na maabara zisizosajiliwa, watumishi wasio na sifa stahiki, ukosefu wa eneo maalumu kwa ajili ya kutolea dawa, utunzaji mbovu wa dawa, na ukosefu wa majokofu kwa ajili ya kuhifadhi dawa.

Mapungufu katika usajili wa vituo binafsi na hiari vya afya: Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Afya ilifanikiwa kusajili vituo binafsi vya huduma za afya kwa 87% ya vituo vyote vilivyoomba usajili. Muda wa usajili wa vituo binafsi vya huduma za afya ulitofautiana kwa kuwa ulichukua wastani wa siku 28 hadi 269. Sababu kuu za tofauti hizo kutokuwapo kwa muda maalumu uliowekwa kisheria kwa ajili ya usajili wa vituo vya afya, ukosefu wa mkataba wa huduma kwa mteja na kukosekana kwa ufanisi wa mfumo wa usajili mtandaoni.

Idadi ndogo ya kaguzi katika vituo vya huduma za afya vya binafsi na hiari: Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na idadi ndogo ya kaguzi zilizofanywa na Wizara ya Afya kupitia Bodi ya Usajili wa Vituo vya Huduma za Afya na Bodi ya Usajili wa Maabara katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya. Mathalani, Bodi ya Usajili wa Vituo vya Huduma za Afya haikufanikiwa kukagua asilimia 70 ya vituo binafsi vya afya vilivyopangwa kukaguliwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/22. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa Bodi ya Usajili wa Vituo vya Huduma za Afya ilifanikiwa kufanya ukaguzi wa vituo kati ya 108 na 460 kuanzia mwaka wa fedha 2016/217 hadi 2021/22. Kwa upande mwingine, Bodi ya Usajili wa Maabara iliweza kukagua kati ya 4% na 13% tu ya maabara binafsi za huduma za afya zilizosajiliwa. Aidha, Baraza la Wafamasia halikukagua maduka ya dawa yaliyoambatishwa katika vituo binafsi na hiari vya afya.

(c) Udhhibiti wa Malipo Yanayofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Vituo vya Huduma za Afya Vilivoidhinishwa

Ukaguzi unatambua jitihada zinazofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya katika kuboresha udhibiti wa malipo yanayofanywa katika vituo vya huduma za afya kwa lengo la kuhakikisha kuwa kuna mwendelezo wa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

Kuwapo kwa madai yasiyostahili na malipo yasiyo sahihi: Ripoti ya Kupambana na Udanganyifu na Ripoti ya Uhakiki wa Madai Yaliyokwishalipwa kwa kipindi cha miaka ya fedha 2019/20 hadi 2021/22 zilibainisha kuwapo kwa madai yasiyostahili na yasiyo sahihi yaliyoibuliwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Jumla ya shilingi trilioni 1.7 zililipwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, ambapo kati ya hizo, shilingi bilioni 14.5 zilitokana na madai yasiyostahili na yasiyo sahihi. Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na ongezeko la kiasi cha madai haya kutoka shilingi bilioni 4.3 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilion 4.6 mwaka 2020/21 na shilingi bilioni 5.6 mwaka 2021/22.

Kuwapo kwa madai yasiyostahili na yasiyo sahihi kulisababishwa na ubadhirifu wakati wa utambuzi na usajili wa wagonjwa kwenye vituo vya huduma za afya, huduma za kumwona daktari pamoja na huduma za vipimo, mapungufu katika kuzingatia mwongozo wa matibabu ya kawaida na makubaliano ya kimkataba, mifumo ya udhibiti yenye mapungufu, na kukosekana kwa tathmini ya kutosha ya utendaji.

Vituo vya huduma za afya kutosimamia na kutunza kumbukumbu za kweli na sahihi za wagonjwa katika vituo vyote vya huduma: Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu za huduma zinazotolewa katika vituo vya huduma za afya.

Hali hii ilisababishwa na kukosekana kwa matokeo ya wazi ya kimkataba kwa kutofuata matakwa ya kumbukumbu za matibabu kwa huduma zinazotolewa na vituo vya huduma za afya. Jambo hili lilisababisha kutofautiana kwa taarifa kati ya madai yaliyowasilishwa kutoka vituo vya afya na huduma halisi zinazotolewa hali ambayo inaweza kutoa nafasi ya malipo ya huduma ambazo hazikutolewa.

Uhakiki wa taarifa za uanachama katika vituo vya afya kutofanyika ipasavyo: Ilibainika kuwa uhakiki wa taarifa za wanachama katika vituo vya afya haukufanyika ipasavyo kwa sababu mbalimbali kwa kuwa vipengele vingi katika kadi za uanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya havikutosha kusaidia utambuzi na uhakiki wa wanufaika wakati wa utoaji wa huduma.

Hali hii ilisababishwa na Mfumo wa Usimamizi wa Madai na Mifumo ya Taarifa za Afya inayotumiwa na vituo vya huduma za afya kushindwa kutambua taarifa muhimu za wanufaika kama vile saini, alama za vidole, na picha ambazo zingeweza kusaidia kutambua wanufaika. Hali hii ilitoa mwanya kwa

wagonjwa au watoa huduma kutumia vibaya kadi hivyo kusababisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kulipa fedha kwa watoa huduma kwa huduma zisizostahili na hatimaye kusababisha hasara kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

(d) Udhhibiti wa Vyanzo vya Mionzi

Ukaguzi unatambua juhudi zinazofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika kudhibiti na kukuza matumizi salama na ya amani ya teknolojia ya nyuklia nchini. Hata hivyo ukaguzi ulibaini mambo yafuatayo:

Wastani wa 66% ya vituo vya vyanzo vya mionzi vilivyosajiliwa nchini havikuwa na leseni ya kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi kutoka Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania: Ukaguzi ulibaini kuwa, vituo vyenye vyanzo vya mionzi vilivyopatiwa leseni na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania vilianza 31% hadi 37% katika kipindi cha miaka 4 iliyopita kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2021/22, ambapo kiwango cha juu cha idadi ya leseni zilizotolewa kilikuwa 37% katika mwaka 2020/21. Kwa wastani, 66% ya vituo vilivyosajiliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) havikupewa leseni katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2021/22. Kukosekana kwa mfumo mzuri wa leseni ulisababisha Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kupoteza wastani wa shilingi milioni 424.7.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa hatua za utekelezaji za kusimamisha vituo visivyokuwa na leseni za kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi hazikutekelezwa ipasavyo na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Mhalani, 94% ya vituo vilivyokuwa na mapungufu hayo viliendelea kufanya kazi bila kuchukuliwa hatua na Tume kwa kipindi cha 2018/19 hadi 2021/22.

83% ya vituo vyenye vyanzo vya mionzi vilivyosajiliwa kutokaguliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika mwaka 2021/22: Ukaguzi ulibaini kuwa Tume ilifanya ukaguzi kwa 7% hadi 42% tu ya vituo vyote vyenye vyanzo vya mionzi vilivyosajiliwa nchini, na idadi hii ilishuka hadi 4% kwa mwaka wa fedha 2019/20 na 16% kwa mwaka 2021/22. Kwa wastani, katika kipindi cha miaka minne, 83% ya vituo vilivyosajiliwa havikukaguliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Hii ilichangiwa zaidi na uhaba wa rasilimali-watu hasa wakaguzi wa usalama wa mionzi katika Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

Kaguzi chache zilizofanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania zilichangia kutotekelezwa kwa mahitaji ya usalama katika vituo vyenye

vyanzo vya mionzi. Mahitaji hayo ni pamoja na kutokuwapo kwa ishara za onyo la kuwapo kwa mionzi, kukosekana kwa maofisa usalama waliofunzwa, uhaba wa majengo yenye ulinzi wa kutosha kwa vyanzo vya mionzi, na uhifadhi duni wa vyanzo vya mionzi.

(e) Usimamizi wa Shughuli za Utafiti na Ubunifu

Ukaguzi unatambua juhudi za Serikali katika utafiti na shughuli za uvumbuzi kupitia uanzishwaji wa Dirisha la Ubunifu ndani ya Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia (NFAST). Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalibainika:

Utekelezaji usioridhisha wa mikakati na mipango iliyoungwa ya kutambua na kusajili shughuli zote za utafiti na uvumbuzi: Ukaguzi ulibaini kuwa Tume ya Sayansi na Teknolojia nchini (COSTECH) haikuweza kutekeleza kimamilifu mikakati na mipango iliyoandaliwa ya kubainisha na kusajili shughuli za utafiti na uvumbuzi. Badala yake ilizalisha mihtasari ya sera 4 kati ya 15 iliyopangwa; na mijadala 2 kati ya 5 iliyopangwa kuhusu sayansi, teknolojia na uvumbuzi ilifanyika.

Hali hii ilichangiwa na kuchelewa kwa ruzuku ya serikali, uhaba wa wafanyakazi, kutoshirikiana na wadau wengine kama vile taasisi za utafiti na maendeleo na taasisi za elimu ya juu au wadau wengine wakuu wanaohusika. Kasoro nyingine ilikuwa tofauti katika uanzishaji wa kitaasisi ambapo taasisi za utafiti na maendeleo na taasisi za elimu ya juu hazikusaidia utekelezaji wa mpango huo, hivyo Tume haikuweza kutekeleza mipango yake ipasavyo.

Utambuzi na usajili wa shughuli za utafiti na uvumbuzi usio na tija: Kupitia Kituo chake cha Maendeleo na Uhamishaji wa Teknolojia, Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania haikufanya usajili wa kutosha wa teknolojia na rasilimali za teknolojia na nguvukazi za ndani. Hali hii ilisababishwa na kukosekana kwa kanuni zilizowekwa bayana za kutekeleza majukumu yake katika tathmini, usajili, na usimamizi wa mikataba ya uhamisho wa teknolojia. Mapungufu haya yanaweza kusababisha marudio ya teknolojia ambapo teknolojia iliyopo inakiliwa na kutangazwa kuwa teknolojia mpya nchini; na uwezekano wa kuwa na maendeleo ya teknolojia zinazohatarisha maisha ya binadamu na mazingira kwa ujumla.

Matumizi ya kiwango cha chini ya fedha zilizopo kwa ajili ya kurasamisha kibiashara na shughuli za uvumbuzi zinazofadhiliwa kupitia Mfuko wa Taifa

wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia: Tume iliweza kusajili vumbuzi 9 kati ya 58 mwaka 2019 sawa na 15.5% na zilifanywa kuwa za kibiashara; na 49 zilizobaki (84.5%) zilikuwa vumbuzi zilizosajiliwa au zilikuwa katika hatua zingine za uendelezaji au hazikuwa na hali ya uendelezaji kuelekea kuwa za kibiashara. Hali hii ilichangiwa na kasi ndogo kutokana na ufuatiliaji usiojitosheleza ili kuhakikisha kuwa uvumbuzi unafanyika kibiashara.

(f) Usimamizi wa Mipango na Uanzishaji wa Mifumo ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini

Ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao iliweza kuwashirikisha wadau katika kukusanya mahitaji wakati wa ununuzi wa mifumo ya TEHAMA. Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yanapaswa kufanyiwa maboresho:

Uangalizi usiotosheleza wa Wizara kuhusu upatikanaji wa miradi ya TEHAMA inayofanywa na taasisi za umma: Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilikuwa na mfumo wa ufuatiliaji wa mipango ya serikali mtandao usiokuwa na muunganiko, vile vile miongozo ya upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA ya Serikali ilikua ya zamani sana. Tathmini ya shughuli za ufuatiliaji wa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilibaini kuwa kulikuwa na ukosefu wa zana za ufuatiliaji, utekelezaji duni wa shughuli za ufuatiliaji, na utoaji duni wa taarifa za shughuli za ufuatiliaji. Ilibainika pia kuwa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imekuwa ikitegemea miongozo ilivyopitwa na wakati wa kusimamia upangaji na upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma. Zaidi ya hayo, Taasisi za umma hazikuwa na mipango madhubuti ambayo ingetoea muda mwafaka na taratibu ya kufanya mapitio ya miongozo ilivyopitwa na wakati.

Usimamizi usioridhisha wa uanzishaji wa miradi ya TEHAMA: 86% maandiko ya miradi yalirudishwa kwenye taasisi husika za umma kwa sababu ya makosa mbalimbali. Hii ilitokana uaandaji wa miradi ya mifumo ya TEHAMA usiokuwa na mpango maalum. Katika uaandaji huu, ilibainika kuwa mahitaji ya msingi yaliyokusanywa ni watumiaji wa mfumo pekee huku mahitaji ya wadau yakikosekana. Hii hatimaye ilisababisha uchanganuzi wa mahitaji usiotosheleza. Pia, uchambuzi uliofanywa ulionesha kuwa sababu kuu ya ucheleweshaji huo ni taratibu za ndani za mapendekezo ya miradi yaliyowasilishwa kwa watumishi mbalimbali ndani ya Mamlaka ya Serikali Mtandao ambao walipaswa kutoa maoni juu ya mapendekezo hayo na kutoa ushauri wao kabla ya vibali vingine vya juu vya usimamizi kutolewa. Kwa

hiyo, ucheleweshaji wa utoaji wa maelezo ya ushauri ulichelewesha pia muda wa utekelezaji wa miradi iliyowasilishwa na hivyo kuathiri malengo yaliyokusudiwa ya miradi husika.

(g) Usimamizi wa Viumbe Vamizi katika Mazingira ya Nchikavu

Ukaguzi ulibaini uwepo wa jitihada zilizofanyika, ambapo Serikali iliweka mipango mbalimbali inayolenga kuhakikisha kuna udhibiti wa viumbe vamizi nchini. Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalibainika:

*Uzuiaji usiotosheleza wa viumbe vamizi:*Ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na wizara za kisekta, haikuchukua hatua zenye tija ili kuzuia uingiaji na ueneaji wa viumbe vamizi nchini. Hali hii ilidhihirishwa na utambuzi na usimamizi usiojitosheleza wa njia zinazotumiwa na viumbe hawa wakati wa uingiaji na ueneaji wao. Vilevile, ilibainika kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Wizara ya Kilimo, kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), hawakufanikiwa kudhibiti ipasavyo viumbe vamizi katika mipaka ya nchi.

Udhibiti usiotosheleza wa viumbe vamizi katika mazingira: Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na wizara za kisekta, haikuchukua hatua zenye tija za kudhibiti viumbe vamizi nchini. Hali hii inadhihirishwa na ukweli kwamba, taasiss hizi hazikuandaa kanzidata ya taifa ya viumbe vamizi. Kutokana na kukosekana kwa kanzidata hiyo, nchi inakosa taarifa za za kina kuhusu viumbe vamizi ambavyo vimeingia na kuenea katika maeneo mbalimbali. Hivyo, nchi ina hatari kubwa ya kukosa namna bora ya kufuatilia kukua na kuenea kwa aina mbalimbali za viumbe vamizi.

Udhibiti usiofaa huongeza hatari ya viumbe vamizi kuingia na kuenea katika mazingira hususani ya nchi kavu. Hali hii inaleta madhara katika mifumo ya ikolojia kwa kuwa inaweza kubadilisha mfumo wa haidrolojia, virutubisho, na makazi ya viumbe na hivyo kusababisha hatari ya kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai.

Uzuiaji na udhibiti usiojitosheleza wa viumbe vamizi ulisababishwa na uratibu mdogo miongoni mwa wadau na ufuatiliaji na tathmini isiyotosheleza ya hatua za kuzuia na kudhibiti viumbe vamizi ndani ya nchi.

(h) Usimamizi wa Usindikaji na Uongezaji Thamani wa Mazao ya Kilimo

Ukaguzi ulibaini uwepo wa hatua mbalimbali ambapo, serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, iliweka mikakati iliyolenga kuhakikisha kuwa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo nchini unafanyika ipasavyo. Hata hivyo, mapungufu yafuatayo yalibainika:

75% ya sera, mikakati na malengo yanayohusiana na usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo hayakutekelezwa: Sera zinazosimamia shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo zilitekelezwa kwa 25%. Pia, utekelezaji wa jumla wa malengo na viashiria vya kuongeza ukauji wa usindikaji wa mazao ya kilimo na uongezaji thamani ya mazao hayo ulifikiwa kwa 12.5% na 14% mtawalia. Hali hii ilisababishwa na mifumo ya fedha isiyojitosheleza, kukosekana kwa teknolojia sahihi za usindikaji wa mazao ya kilimo, uhusiano usioridhisha wa masoko ya mazao yaliyosindikwa, na athari za utekelezaji usiofaa wa mikakati ya kuendeleza ukauji wa biashara ndogo na za kati.

Uwezesaji wa upatikanaji wa teknolojia za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo: Ukaguzi ulibaini kuwa upatikanaji wa teknolojia za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ni kikwazo kimojawapo kinachoathiri viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo nchini kutokana na kukosekana kwa teknolojia muhimu zinazohitajika kwa ajili ya usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao. Vilevile, kulikuwa na uwezo usioridhisha wa teknolojia zilizopo kuwezesha usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo, pamoja na matumizi ya mashine za teknolojia ya kizamani katika usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo.

Upatikanaji usiotosheleza wa teknolojia za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo: Upatikanaji wa teknolojia za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo haukujitosheleza. Hali hii ilidhihirishwa na ukweli kwamba, gharama ya teknolojia za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo nchini ni kubwa kuliko teknolojia za nje ya nchi kwa kuanzia 8% hadi 76%. Aidha, kulikuwa na urithishaji usioridhisha wa teknolojia hususani kwa wasindikaji wa bidhaa za kilimo kwani ndani ya miaka mitano, ni 42% tu ya teknolojia zote zilizozalishwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ndizo zilirithishwa. Miongoni mwa sababu za upatikanaji duni wa teknolojia za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo ni pamoja na kutopewa kipaumbele maendeleo ya kiteknolojia hasusan katika vituo vya maendeleo ya teknolojia nchini.

(i) Usimamizi wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na jitihada mbalimbali zilizofanywa na wizara katika kuboresha uondoshaji wa magari ya Serikali. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:

Magari 547 ya serikali yalika kwa muda mrefu bila kutumika: Mapitio ya ripoti mbalimbali yalibaini kuwa hadi Septemba 2022, magari 547 yalika kwa muda mrefu bila kutumika katika karakana za Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) na baadhi ya taasisi za serikali. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa magari haya hayakuwepo kwenye mpango wa matengenezo wala uondoshaji. Magari hayo hayakuwa yanatumika kwa sababu mbalimbali kama vile kupata ajali, kutofanyiwa matengenezo, kuegeshwa, na kusubiri vibali vya uondoshaji.

Madhara makubwa ya kuwapo kwa magari ya serikali ambayo hayatumiki kwa muda mrefu bila kuondoshwa ni pamoja na hugaribika zaidi na kwa kasi, na hivyo kupungua kwa thamani ya magari wakati serikali inapoamua kuyaondosha.

Tathmini isiyotosheleza ya magari yatakayoondoshwa: Ukaguzi ulibaini kuwa utambuzi wa magari haukufanyika ipasavyo kwa sababu taasisi hazikuwa na bodi za tathmini. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, ni taasisi moja tu kati ya kumi taas zilizotembelewa, afisa masuuli aliunda bodi za ukaguzi ili kutathmini na kubainisha magari ya kuondoshwa au kubadilishwa.

Mapungufu wakati wa uthaminishaji wa magari: Mapitio ya ripoti za uthaminishaji wa magari zilizofanywa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi yalionesha kuwa uthaminishaji ulizingatia bei ya ununuzi na gharama za bima pekee huku ukiacha gharama zingine za awali kama vile kodi, ushuru wa bidhaa, na gharama za vibali. Hivyo, thamani ya magari ilikuwa chini ikilinganishwa na thamani yake halisi jambo lililoathari thamani ya magari yaliyoondoshwa.

Hii ilisababisha uthaminishaji usio sahihi kwa magari, na kusababisha mapato kidogo kutokana na magari yanayoondoshwa.

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kulikuwa na tofauti ya 83% ya thamani ya magari kwa kujumuisha gharama za bima pekee ikilinganishwa na thamani zilizojumuisha gharama zote za ununuzi.

(j) Usimamizi wa Uwekezaji wa Mali Zisizohamishika

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma imefanya jitihada kwa kutenga bajeti kwa ajili ya uwekezaji, ufuatiliaji, na ukaguzi wa miradi ya uwekezaji. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini maeneo yafuatayo yanayohitaji maboresho zaidi.

Kuwapo kwa mali chakavu zisizohamishika katika uwekezaji: Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ilikuwa na majengo chakavu na yaliyo katika hali mbaya. Dosari zilizobainika ni pamoja na nyufa kwenye sakafu na kuta, dari mbovu, fangasi na rangi za ukutani kubanduka, paa kuvuja, na kuvunjwa kwa madirisha. Kasoro zingine zilizobainika ni madoa kwenye mbao za dari, ubovu wa vyoo na milango, uchakavu wa sakafu, na kutu kwenye mabati.

Uchakavu wa majengo ulichangiwa na mapungufu kwenye kuweka bajeti ya ukarabati na kutofanyika kwa matengenezo ya kutosha. Hali hii ilisababisha idadi ndogo ya watu kukaa au kutokaliwa na watu kabisa. Idadi ndogo ya wakazi katika majengo haya ilisababisha kushuka kwa mapato. Kwa mfano, kwa miradi iliyo chini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, viwango vya mapato vilishuka kutoka kati ya 96% na 81% kwa mwaka wa fedha 2017/18 hadi 15% kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa Jengo la Water Front. Kwa Jengo la Julius Nyerere Pension Tower, mapato yalishuka kati ya 75% na 95% katika mwaka wa fedha 2017/18 hadi 20% kwa mwaka wa fedha 2021/22. Kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, kiwango cha mapato kilishuka kutoka 28% katika mwaka wa fedha 2017/18 hadi 21% katika mwaka wa fedha 2021/22.

Baadhi ya uwekezaji wa mali zisizohamishika kuendeshwa kwa hasara: Ukaguzi ulibaini kuwa, katika baadhi ya uwekezaji wa mali zisizohamishika wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, ulitumia jumla ya shilingi bilioni 323.6 katika miradi 10 ya uwekezaji katika majengo ambayo hayakukamilika kwa matumizi na baadhi kutelekezwa. Kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, jumla ya shilingi bilion 3.3 zilitumika katika uwekezaji usio na faida. Mali hizo ni pamoja na kiwanja cha biashara na makazi cha Ununio Jijini Dar es Salaam pamoja na nyumba za makazi Njedengwa Jijini Dodoma.

Uwekezaji katika Mali Zisizohamishika Hazikuzalisha Mapato Yaliyokusudiwa: Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulikusanya mapato kidogo ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa katika soko la fedha. Wastani wa mapato yaliyokusanywa kutokana na uwekezaji wa mali ulikuwa 18% wakati mapato yanayokusanywa kutoka soko la fedha yalikuwa 67% na kufanya tofauti ya 49%.

Kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, ukaguzi ulibaini kuwa miradi ya Kinyerezi na Kijichi haikuingiza mapato yoyote kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2020/21. Vilevile, mauzo ya nyumba na mradi wa viwanja yalikuwa na ukusanyaji usioridhisha kwani yalileta hasara kwa Mfuko.

(k) Usimamizi wa Urasimishaji wa Makazi Holela

Ukaguzi ulibaini kuwa Serikali ilipata mafanikio kadhaa katika utekelezaji wa usimamizi wa urasimishaji wa makazi holela. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini maeneo yafuatayo yanahitaji maboresho zaidi.

Wizara, ofisi za ardhi za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa hazikuunganisha ipasavyo shughuli za urasimishaji katika mipango-mkakati yao na mipango ya mwaka: Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) hazikuunganisha ipasavyo shughuli za urasimishaji katika mipango-mkakati yao. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita (kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2021/22), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, haikutenga bajeti yoyote kwa ajili ya urasimishaji (kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2018/19). Kwa miaka mitatu iliyobaki (kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22), wizara ilitenga bajeti ya jumla ya shilingi milioni 160, sawa na wastani wa shilingi milioni 53 kwa mwaka.

Kwa upande mwingine, OR-TAMISEMI haikutenga fedha katika bajeti zao ili kuwezesha shughuli za urasimishaji katika serikali za mitaa kwa miaka mitano iliyopita (kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2021/22). Hali hii ilisababisha kuwapo kwa usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa shughuli za urasimishaji nchini na hivyo kusababisha kuchelewa kwa utekelezaji wake.

Upimaji usiotosheleza wa makazi rasmi: Ukaguzi ulibaini kuwa, hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya viwanja 2,315,170 vilipangwa kupimwa, ambapo kati ya hivyo, viwanja 1,137,437, sawa na 49%,

vilipimwa. Kushindwa kufikia lengo la upimaji viwanja kulitokana na malipo ya kugharamia urasimishaji yasiyojitosheleza kutoka kwa wananchi. Ukaguzi ulibaini kuwa katika halmashauri 8 zilizotembelewa, ni 18% tu ya wananchi ndio walikamilisha uchangiaji wa gharama za urasimishaji katika viwanja vyote vilivyotambuliwa.

Hali hii ilitokana na mipango isiyojitosheleza ya kufanya kampeni kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kuchangia urasimishaji wa makazi. Hivyo, kukosekana kwa fedha za kuendeleza kulipia shughuli za urasimishaji.

(I) Uendeshaji na Ukarabati wa Miradi ya Usambazaji wa Maji

Ukaguzi ulibaini kuwa Serikali ilipata mafanikio kadhaa katika shughuli za uendeshaji na ukarabati wa miradi ya usambazaji maji nchini. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji maboresho zaidi.

Uendeshaji usioridhisha wa miundombinu ya usambazaji wa maji: Ukaguzi ulibaini kulikuwa na matumizi madogo ya miundombinu ya maji, ambapo katika mamlaka nane za maji safi na usafi wa mazingira zilizotembelewa, ni mamlaka moja tu ndiyo iliweza kutumia miundombinu kwa asilimia 100, huku mamlaka zilizobaki zilitumia chini ya asilimia 80. Pia, kulikuwa na miundombinu ya usambazaji wa maji isiyofanya kazi ambayo ni visima vya maji, mfumo wa kutibu maji, Mfumo wa Udhibiti wa Usimamizi na Ukusanyaji wa Data, pamoja na pampu katika mamlaka tano kati ya nane za usambazaji wa maji safi na usafi wa mazingira.

Hali hii ilisababishwa na mipango ya uendeshaji na ukaguzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji isiyojitosheleza, ukusanyaji wa ankara za maji kutoka kwa wateja usioridhisha, mipango isiyotosheleza ya vipuri na vifaa kwa ajili ya ukarabati, ukaguzi wa maji, na udhibiti wa uvujaji wa maji, pamoja na mipango ya matumizi bora ya nishati ya umeme isiyojitosheleza.

Ukarabati usioridhisha wa miundombinu ya usambazaji wa maji: Ukaguzi ulibaini kutofanyika kwa ukarabati wa kutosha wa miundombinu ya usambazaji wa maji kutokana na kuharibika kwa baadhi ya miundombinu ya maji. Mapungufu haya yalisababishwa na kukosekana kwa mipango ya ukarabati wa tahadhari wa miundombinu pamoja na ukaguzi usiotosheleza wa mitandao ya miundombinu ya usambazaji wa maji safi na majitaka.

Ufuatiliaji wa utendaji wa mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira usiojitosheleza: Ukaguzi ulibaini ufuatiliaji usiojitosheleza wa utendaji katika mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini. Kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22, Wizara ya Maji haikufanya ufuatiliaji wa shughuli na kazi za ukarabati zilizofanywa na mamlaka za maji. Wizara ilitegemea taarifa zilizowasilishwa na mamlaka hizo kwa njia ya mitandao na kufanya ufuatiliaji bila kuwa na mipango.

Hitimisho la Ujumla la Ukaguzi

Ukaguzi unatambua juhudi za taasisi zilizokaguliwa katika kuboresha utendaji wao ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili na Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao dhima yake kuu ni mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu.

Hata hivyo, ukaguzi ulionesha uwepo wa mapungufu katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano nchini hususan kwenye usimamizi wa mifumo ya utoaji wa huduma za afya, sayansi, ubunifu na teknolojia, mazingira na usalama wa chakula, usimamizi wa mali na uwekezaji wa serikali, mipango miji na uendelezaji wa makazi pamoja na usimamizi wa usambazaji wa maji nchini. Mapungufu haya yanahitaji hatua za haraka kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali kuelekea kufikia mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya jamii yanafikiwa kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mapendekezo ya Ukaguzi

Wizara, Idara na Mamlaka za Serikali zinashauriwa:


- (i) Kuandaa mwongozo na mfumo wa uondoshaji wa magari utakaoelezea mchakato mzima na hatua muhimu za uondoshaji ili kuepusha ucheleweshaji wa uondoshwaji wa magari ya Serikali;
- (ii) Kukagua utendaji kazi (kuhusu michakato ya usajili na ukaguzi wa vituo vya huduma za afya ukaguzi wa kitabibu na upangaji wa bei za huduma za afya) pamoja na kuandaa mifumo na mikakati ya uhibititi itakayohakikisha kuwa vituo binafsi vya afya vinatoa huduma bora za afya na kwa bei nafuu;

-
- (iii) Kuendeleza udhibiti thabiti (ikiwemo ya mifumo ya TEHAMA na miongozo) katika vituo vya afya na Ofisi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuhakikisha kuwa madai yatakayolipwa ni sahihi na ya kweli kwa huduma zote za afya;
 - (iv) Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa vyanzo vya mionzi ili kuhakikisha kuwa vyanzo vya mionzi havidhuru watumiaji, umma, na mazingira kwa ujumla;
 - (v) Kutengeneza mfumo wa kina wa usimamizi wa utafiti na uvumbuzi na unapaswa kujumuisha michakato ya kutambua, kufuatilia, na kutathmini shughuli zote za utafiti na uvumbuzi;
 - (vi) Kufanya tathmini ya kina ya mahitaji kabla ya kutekeleza mfumo wowote wa TEHAMA ili kubaini mahitaji mahsusi ya taasisi za umma;
 - (vii) Kuhakikisha usimamizi madhubuti wa viumbe vamizi kwa kuchukua hatua madhubuti za kuzuia na kudhibiti viumbe hawa nchini;
 - (viii) Kuhakikisha kuna usimamizi madhubuti wa shughuli za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo kwa kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi;
 - (ix) Kuandaa mpango wa uwekezaji na utunzaji wa mali za uwekezaji kwa kufanya matengenezo, uendeshaji, na ufuatiliaji wa uendeshaji wa mali hizo;
 - (x) Kuandaa mkakati wa kina ili kuwezesha usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa shughuli za urasimishaji wa makazi holela nchini; na
 - (xi) Kuandaa mikakati ya kina ili kuwezesha uendeshaji na ukarabati madhubuti wa miradi ya usambazaji maji safi na majitaka ili kuhakikisha kuwa miradi inakuwa endelevu.

UTANGULIZI

SURA YA KWANZA

1




1.1 Usuli wa Ukaguzi wa Ufanisi

Sura hii inawasilisha masuala ya msingi yanayohusiana na mchakato mzima wa ukaguzi. Masuala hayo ni mamlaka ya kufanya ukaguzi wa ufanisi; madhumuni ya ripoti; mtazamo wa ripoti ya jumla; umuhimu wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu; uhalali wa ukaguzi; mchakato wa uthibitisho wa takwimu na taarifa zilizotolewa; na muundo wa ripoti hii.

Ukaguzi wa ufanisi huchunguza iwapo shughuli, mipango, mifumo au miradi ya Serikali inayohusisha ukusanyaji au matumizi ya fedha za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika ya umma inafanya kazi kwa kuzingatia kanuni tatu yaani uwekevu, ufanisi na tija. Kanuni hizi ni kama zinavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na 1.1**.

Kielelezo Na 1.1: Kanuni za Ukaguzi wa Ufanisi



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Taarifa Iliyotolewa kutoka Mwongozo wa Ukaguzi wa Ufanisi wa Mwaka 2021

Ukaguzi wa ufanisi pia unabainisha iwapo malengo yaliyowekwa mwanzoni mwa shughuli yalifikiwa. Taarifa hizi huwezesha kufahamu iwapo, kwa kiasi kikubwa, uwekevu, ufanisi, na tija ilizingatiwa wakati wa utekelezaji wa

shughuli. Mapendekezo ya uboreshaji hutolewa kwenye maeneo yanayohisiwa kuwa na mapungufu.

Ukaguzi wa ufanisi katika sekta ya umma ni muhimu kwa vile unalenga kukuza uwajibikaji, uwazi, na utendaji kazi katika shughuli za Serikali ili wananchi wake wapate huduma bora na kwa wakati. Ukaguzi wa ufanisi hutumika pia kama msingi wa kujifunza na kufanya maboresho.

Katika ukaguzi wa ufanisi, mambo mbalimbali huzingatiwa katika kuchagua maeneo ya kumakinikia. Mambo haya ni pamoja na kilio cha umma na umuhimu wa eneo hilo kuhusiana na maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya wakati mahususi.

1.2 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi wa Ufanisi

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kisheria ya kufanya ukaguzi wa ufanisi na Kifungu cha 28 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 kinachosema kuwa:

“Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa madhumuni ya kuzingatia wekevu, ufanisi, na tija ya matumizi yoyote ya rasilimali za taasisi, atahitaji taarifa, kuchunguza, na kutoa taarifa kadiri atakavyoona inafaa juu ya:

- a) Matumizi ya fedha za umma na matumizi ya rasilimali kwa wizara, idara, wakala, mamlaka za serikali za mitaa, na mashirika na taasisi zingine zote za umma;
- b) Uendeshaji wa utendaji wa kazi zao kwa maofisa masuuli, wakuu wa idara, na watendaji wakuu wa vyombo vyote hivyo; na
- c) Uzingatiaji wa sheria, kanuni na sera za mazingira na viwango vya ndani ya nchi”.

1.3 Madhumuni ya Ripoti

Ripoti hii ya jumla inalenga kuwapa taarifa muhimu wabunge, Serikali, vyombo vya habari, umma, pamoja na wadau wengine ili waweze kufanya maamuzi yatakayoongeza uwekevu, tija, na ufanisi katika shughuli za serikali.

Ripoti hii inabainisha masuala mbalimbali yaliyoonekana katika kaguzi za ufanisi dhidi ya yale yaliyotarajiwa, pamoja na mchango wake katika kutekeleza Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21 na 2021/22 - 2025/26) na kuyafikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ripoti hii pia inatoa tathmini ya utendaji wa taasisi za serikali katika kutimiza majukumu yao katika Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaolenga kuleta mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu.

Maeneo yaliyoguswa katika ripoti hii ni pamoja na usimamizi wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu; usimamizi wa mifumo ya utoaji wa huduma za afya; usimamizi wa sayansi, uvumbuzi na teknolojia; na usimamizi wa mazingira na uhakika wa chakula. Maeneo mengine yaliyoguswa katika ripoti hii ni usimamizi wa uwekezaji na mali za serikali; usimamizi wa urasimishaji wa makazi holela; na usimamizi wa uendeshaji na ukarabati wa miradi ya usamabazi wa maji safi na majitaka.

Pia, ripoti inawasilisha matokeo ya tathmini ya kiwango ambacho shughuli za Serikali zimechangia kufikia malengo ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. **Jedwali Na. 1.1** linatoa muhtasari wa ripoti za ukaguzi wa ufanisi pamoja na taasisi zilizokaguliwa.

Jedwali Na. 1.1: Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi na Taasisi Zilizokaguliwa

| Ripoti ya Ukaguzi | Tasisi Zilizokaguliwa |
|---|---|
| Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu | Wizara ya Fedha na Mipango, na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| Usimamizi wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali | Wizara ya Fedha na Mipango, na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora |
| Usimamizi wa Usindikaji na Uongezaji Thamani wa Mazao ya Kilimo | Wizara ya Uwekezaji, Viwanda, na Biashara; na Wizara ya Kilimo |
| Usimamizi wa Urasimishaji wa Makazi Holela | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| Uendeshaji na Ukarabati wa Miradi ya Maji Safi na Majitaka | Wizara ya Maji; Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini; na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira |

| Ripoti ya Ukaguzi | Tasisi Zilizokaguliwa |
|--|---|
| Usimamizi wa Viumbe Vamizi katika Mazingira ya Nchikavu | Ofisi ya Makamu wa Rais - Idara ya Mazingira |
| Udhibiti wa Malipo Yaliyofanywa na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Vituo vya Huduma za Afya | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| Usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini | Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mamlaka ya Serikali Mtandao |
| Udhibiti wa Vyanzo vy Mionzi | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania |
| Usimamizi wa Vituo Binafsi vya Utoaji wa Huduma za Afya | Wizara ya Afya |
| Usimamizi wa Shughuli za Utafiti na Ubunifu | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia |
| Usimamizi wa Uwekezaji wa Mali za Serikali Zisizohamishika Zinazosimamiwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma; na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii | Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu; Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma; na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi Mwaka 2023

1.4 Mtazamo wa Ripoti ya Jumla

Ripoti hii inalenga kuwasilisha matokeo ya juhudi na shughuli mbalimbali za Serikali katika mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya rasilimali-watu kama zinavyohusishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu sambamba na utekezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Kwa kutambua umuhimu wa ajenda hii katika kuleta mabadiliko kwenye maisha ya wananchi, Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Umma za Ukaguzi lilijumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu kama kipaumbele mtambuka katika Mpango-mkakati wake wa Mwaka 2017 hadi 2022 huku likitoa wito kwa wanachama wake kuchangia katika ufuatiliaji na mapitio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ndani ya muktadha wa juhudi mahususi za maendeleo endelevu za kitaifa na mamlaka ya taasisi husika za ukaguzi.

Tanzania, kama nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa, inashiriki utekezaji wa Ajenda ya 2030. Ajenda hii inasisitiza kuwapa kwa mpango

jumuishi wa hatua za kupata suluhisho la kiuchumi, kimazingira, na kijamii kwa ajili ya kufikia maendeleo endelevu unaojumuisha malengo 17 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Malengo ya Maendeleo Endelevu, pamoja na masuala mengine muhimu, yanaweka jitihada katika kukabiliana na umaskini na njaa, kupunguza ukosefu wa usawa, kujenga jamii zenye amani na haki, kukuza usawa wa kijinsia, na kulinda maliasili. Kwa kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kabambe na yanaingiliana, mafanikio na kutumika kwake ni mchakato mgumu na unahitaji ushirikiano wa pamoja.

Kadhalika, kuzinduliwa kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 kama zana ya kuelekeza juhudi za taifa katika kufanikisha malengo ya kiuchumi na kijamii, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeandaa Mpango wa Muda Mrefu wa Mwaka 2011/12 mpaka 2025/26. Utekelezaji wa Mpango huu umegawanywa katika awamu kuu tatu za mpango wa maendelo wa miaka mitano ambayo inalenga kuelekeza jitihada za kitaifa kuelekea kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi ikiwa sambamba na kupunguza umaskini na na kuleta maendeleo ya watu.



Mipango ya taifa ya maendeleo ya miaka mitano inaingiliana na inaandaliwa kulingana na maudhui. Maudhui ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Pili (2016/17 - 2020/21) ni “Kukuza viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu”; wakati maudhui ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (2021/22 - 2025/26) ni “Kujenga uchumi shindani wa viwanda kwa maendeleo ya watu”.

Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa unalenga kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, ambayo ina lengo la kuigeuza Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati na kuendeleza mageuzi ya kuwa nchi ya viwanda kufikia mwaka 2025. Jitihada za kuondoa umaskini; na kuboresha hali ya maisha, utawala bora, na uwajibikaji zimejumuishwa kwenye Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa.

Kwa hiyo, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa unaendelea kuweka mkazo ulioanzishwa na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kuhusu mageuzi ya kiuchumi, maendeleo ya viwanda, maarifa, na uwezo wa kushiriki kikamilifu kwenye biashara za kimataifa.

Taasisi kuu za umma za ukaguzi, kwa kuzingatia mamlaka na majukumu yao, zina jukumu muhimu. Taasisi hizo ndio msingi wa kuwapo kwa taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika, na shirikishi kwa maendeleo endelevu na zinazoweza kusaidia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Hivyo, ripoti hii ya jumla imetokana na uchambuzi uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutoka kwenye kaguzi 12 za ufanisi zilizotathmini athari za shughuli za Serikali katika kuwezesha kufikiwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

1.5 Umuhimu wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo unalenga kutumia rasilimali ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Dira hii inakusudia kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa kipato cha kati na kuendeleza mageuzi ya kuwa nchi ya viwanda kufikia mwaka 2025. Ufikiaji wa Dira kutaifanya nchi kuwa na maisha bora na endelevu; kuwa na amani, utulivu na umoja; kuwa na uongozi bora na utawala wa sheria; kuwa na jamii iliyoelimika; na kuwa na uchumi imara na wenye ushindani.

Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo unalenga kutekeleza mipango-mkakati na makubaliano ya kisekta, kikanda na kimataifa ikiwa pamoja na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliyopitishwa tarehe 25 Septemba 2015 na nchi wanachama 193 za Umoja wa Mataifa ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii. Mipango hii ya maendeleo inaweka bayana orodha ya maeneo ya vipaumbele na shughuli za kimkakati ambazo ni muhimu ili kuimarisha kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu.

Malengo ya Maendeleo Endelevu yana seti 17 za malengo tarajiwa zenye malengo mahususi 169 yanayoelekeza hatua za serikali, mashirika ya kimataifa, asasi za kiraia, na mashirika mengine katika kipindi cha miaka 15 (2016 - 2030). Ajenda ya 2030, ambayo ilifanikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia, ni dira ya dunia nzima kwa watu, sayari, na ustawi wa muda mrefu. Ajenda inaweka mkakati wa siku zijazo, ikiongoza ulimwengu kuelekea njia endelevu zaidi na thabiti. Inaelekeza pia mabadiliko ya viwango vya maisha na mapito kwa njia jumuishi zaidi za maendeleo zenye nguvu na endelevu.

Seti 17 za malengo tarajiwa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yanalenga kuondoa umaskini katika nyanja zake zote; kuimarisha afya bora na ustawi; kuwa na elimu bora na usawa wa jinsia; kuwapo kwa maji safi na usafi wa mazingira; na kuwapo kwa nishati safi na nafuu.

Kadhalika, seti 17 za malengo tarajiwa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu zinalenga kuhakikisha kunakuwa na kazi zenye staha na ukuaji kiuchumi; kuwa na viwanda, uvumbuzi na miundombinu; kupunguza matabaka; kuwa na miji na jamii endelevu; kuwa na matumizi na uzalishaji bora; kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; kuhifadhi maisha ya viumbe chini ya maji na juu ya ardhi; kuwa na amani, haki na taasisi imara; na kuwa na ushirika wa malengo.

Malengo haya yote yamehusishwa kwenye maeneo makuu matatu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo ni malengo ya uchumi, jamii na mazingira.

1.6 Uhalali wa Ukaguzi

Kama moja ya nchi zilizosaini Ajenda ya 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu, Tanzania imechukua hatua za kujumuisha ajenda hii katika muktadha wa kitaifa. Wakati wa uanzishaji wa Ajenda ya 2030, Tanzania ilikuwa ikiandaa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, hivyo sehemu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliakisiwa katika mpango huo.

Aidha, kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Tanzania imejiwekea matarajio ya kufanikisha lengo la kuwa na ukuaji wa uchumi kwa angalau asilimia 8 kwa mwaka. Viwango hivyo vya ukuaji vinachukuliwa kuwa muhimu katika kupunguza umaskini na kuisukuma Tanzania kutoka nchi isiyoendelea hadi nchi ya uchumi wa kipato cha kati yenye kiwango cha juu cha maendeleo ya binadamu. Dira ya Taifa ya Maendeleo ina maono ya kubadili uchumi ambao awali ulitegemea uzalishaji wa chini wa kilimo hadi kufikia uchumi wa kilimo wenye tija.

Ili Malengo ya Maendeleo Endelevu yafikiwe, kila mmoja, kama vile Serikali, Bunge, sekta binafsi, asasi za kiraia na mtu mmojammoja, anapaswa kutimiza wajibu wake.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kama mkaguzi wa nje wa Serikali, ni kiungo muhimu katika kuhakikisha kuwa Serikali inatekeleza wajibu wake wa kutoa huduma zinazohitajika kwa wananchi na kulijulisha Bunge kuhusu utendaji wa serikali na hatua zinazopaswa kuchukuliwa kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanafikiwa.

Hivyo, ili kuitikia wito huo wa kuchangia kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeunganisha ukaguzi wake wa ufanisi na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030. Kadhalika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeunganisha ukaguzi wake wa ufanisi na maeneo ya vipaumbele na shughuli za kimkakati za Mpango wa Maendeleo wa Taifa ili kutathmini utekelezaji wake na kutoa mapendekezo ya maboresho zaidi. Baadhi ya malengo hayo yamewezeshwa kupitia kaguzi 12 zilizofanyika.

1.7 Mchakato wa Uthibitisho wa Takwimu na Taarifa Zilizotolewa

Ukaguzi wa ufanisi ulifanywa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Ukaguzi kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi. Viwango hivyo vinaitaka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kupanga na kufanya ukaguzi ili kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa utakaokuwa msingi mzuri wa matokeo, hitimisho, na mapendekezo kulingana na lengo au malengo ya ukaguzi.

Kwa kufuata kanuni za ukaguzi, Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maji; Ofisi ya Makamu wa Rais - Idara ya Mazingira; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Afya; Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Mamlaka ya Serikali Mtandao; Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia; Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii; Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini; na mamlaka za maji na usafi wa mazingira zilipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni yao kuhusu matokeo ya ukaguzi na kusahihisha makosa yaliyojitokeza katika rasimu ya ripoti hii.

Vilevile, kwa kuzingatia viwango vya ukaguzi, taasisi zilizokaguliwa kama zilivyotajwa hapo juu, zilipewa fursa ya kujadili na kutoa maoni juu ya matokeo ya ukaguzi binafsi na kusahihisha upotoshaji wa ukweli wakati wa kuandaa ripoti za ukaguzi wa ufanisi ambapo matokeo yote yalitolewa.

1.8 Muundo wa Ripoti

Ripoti hii ina sura 10 kama zilizopangwa kwenye **Kielelezo Na.1.2:**
Kielelezo Na.1.2: Mpangilio wa Sura Zilizounda Ripoti Hii

Sura ya Pili: Maelezo kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Sura ya Tatu: Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sura ya Nne: Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya

Sura ya Tano: Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Shughuli za Sayansi, Ubunifu na Teknolojia



Sura ya Sita: Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Mazingingira na Uhakika wa Chakula

Sura ya Saba: Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usimamizi wa Mali na Uwekezaji Serikalini na Uondoshaji wa Magari ya Serikali

Sura ya Nane: Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Mipango-miji na Maendeleo ya Makazi ya Watu

Sura ya Tisa: Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Usambazaji wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira

Sura ya Kumi: Hitimisho na Mapendekezo ya Jumla ya Ripoti

**MAELEZO YA MPANGO WA PILI NA TATU WA
MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO
NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU**

SURA YA PILI

2



MAELEZO YA MPANGO WA PILI NA TATU WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO NA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU

2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu maelezo ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Masuala muhimu yanayoelezewa ni taasisi muhimu na mfumo wa kisheria unaosimamia utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; wahusika wakuu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; na mikakati ya utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Masuala mengine yanayoangaziwa ni mahitaji ya ukaguzi katika kutekeleza Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu; ukaguzi wa ufanisi uliofanyika kuhusiana na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu; na mifumo ya ufadhili katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa ya miaka mitano.

2.2 Usuli kuhusu Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mwaka 1999 Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ambayo ni nyenzo ya kuunganisha juhudi za taifa katika kufikia malengo ya maendeleo tarajiwa ya kijamii na kiuchumi.

Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2015 umegawanywa katika mikakati ambayo ipo kwenye Mkakati wa Kupunguza Umaskini ambayo ni Mkakati wa Miaka Mitatu wa Kupunguza Umaskini (2000/2001 - 2002/2003) uliofuatiwa na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini - Awamu ya Kwanza (MKUKUTA I - 2005/2006 - 2009/2010) pamoja na Awamu ya Pili (MKUKUTA II - 2010/11 - 2015/16).

Kufuatia tathmini ya kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 iliyofanyika mwaka 2009/2010, Serikali iliandaa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Miaka 2011/12 - 2025/26 ambao utekelezaji wake uligawanywa katika mipango ya maendeleo ya miaka mitanomitano, ambapo kila mpango ulikuwa na maudhui mahususi.

Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 - 2015/16) uliokuwa na dhima ya “Kufungua Fursa Fiche za Ukuaji wa

Uchumi”, uliainisha maeneo ambayo hatua zingechukuliwa, zingefungua fursa za kiuchumi. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 ulikuwa na dhima ya “Kujenga Uchumi wa Viwanda”. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) wenye dhima ya “Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”, lengo ni kuakisi malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kujenga uchumi shindani ambao ni imara, wa kipato cha kati, wa viwanda, na unaoweza kushindana kikanda na kimataifa bila kupoteza lengo la kuleta maendeleo ya watu.

Mipango hii ya maendeleo inalenga kujenga msingi wa kuibadilisha Tanzania ili kuhakikisha makubaliano ya kimataifa na kikanda (k.m. Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu) yameingizwa katika mipango ya maendeleo ya taifa na mifumo ya utekelezaji wa mipango hiyo.

Kama mwanachama wa Umoja wa Mataifa, Tanzania inatakiwa kutekeleza seti 17 za Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kufikia maendeleo endelevu ya watu. Malengo ya Maendeleo Endelevu yanashabihiana na ni kabambe, ambayo yanalenga kutatua changamoto za kimaendeleo zinazowakabili Watanzania na dunia kwa ujumla. Changamoto hizo zinataka kuchukuliwa kwa hatua za kutokomeza njaa, kulinda mazingira, na tabianchi¹.

Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanajumuishwa katika muktadha wa kitaifa na kutekelezwa ipasavyo. Juhudi zimefanywa ili kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu yameingizwa katika mipango na mikakati ya kisekta. Hivyo, utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya kitaifa pia utaathiri mafanikio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na malengo ya kitaifa ya maendeleo. Katika kuhakikisha kuwa kuna utekelezaji mzuri wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini, Kundi la Bunge la Maendeleo Endelevu (PGSD) limepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi ya mitaa na kutoa maoni na miongozo ya mara kwa mara.

Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kuwa malengo haya ya mipango ya maendeleo na Malengo ya Maendeleo Endelevu si tu yanafikiwa bali pia kanuni za tija, ufanisi, na uwekevu zinadumishwa kwa kiwango cha juu na taasisi zinazohusika wakati


¹<https://sustainabledevelopment.un.org/memberstates/tanzania>, Sustainable Development Goal (SDG) Implementation, Follow-up and review in Tanzania - 2017

wa kutekeleza programu na shughuli zitakazoweza kufikiwa kwa malengo hayo.

2.3 Taasisi Muhimu, na Mfumo wa Kisheria Unaosimamia Utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Mfumo unaosimamia utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unajumuisha sera, mipango-mkakati, na bajeti kwa mashirika yenye dhamana ya utekelezaji. Kadhalika, kila sekta ya uchumi imeendelea kuongozwa na sheria zao. Kwa hiyo, utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaongozwa na sheria ambazo zipo chini ya wizara, idara na wakala husika, tawala za mkoa, mamlaka za serikali za mitaa, na wadau wengine. Vyombo, mifumo ya kisheria, na wadau muhimu katika utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wameelezwa hapa chini. **Kielelezo Na. 2.1** hapa chini kinaelezea baadhi ya sheria muhimu katika utekelezaji wa .

Kielelezo Na. 2.1: Mfumo wa Kisheria katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano



Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi Mwaka 2023

2.4 Wahusika Wakuu katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kitaifa ya miaka mitano unagusa wizara, idara na wakala mbalimbali za serikali, tawala za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, na wadau wengine katika utekelezaji wa shughuli za kila siku zilizopagwa katika mipango yao ya maendeleo ya kila mwaka. Utekelezaji umegawanyika katika ngazi zote zikiwemo mipango, uratibu, utekelezaji, na ufuatiliaji na tathmini ya mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Wafuatao ni wadau muhimu katika utekelezaji wa mipango.

Kielelezo Na. 2.2: Watendaji Muhimu na Majukumu Yao katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano




Chanzo: Uchambuzi wa Ukaugu Mwaka 2023

2.5 Mikakati ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Nyaraka za kimkakati ni zana muhimu za kuongoza utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Nyaraka hizi hutoa maelezo juu ya maeneo maalumu ya kimkakati. Mikakati hii inaongoza mageuzi ya kitaasisi na kisera katika utekelezaji wenye tija wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021) kama unavyowasilishwa katika **Kielelezo Na. 2.3** hapa chini.

Kielelezo Na. 2.3: Muhtasari wa Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano



Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi kutoka kwenye Mikakati ya Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo Mwaka 2023

(a) Mpango wa Utekelezaji - Sehemu ya Kwanza

Mpango huu unaelezea maeneo ya kuzingatia na vipaumbele vya miradi ya kimkakati. Mpango-kazi pia unaonesha maendeleo na hali ya maeneo au miradi, changamoto na fursa, malengo ya utekelezaji, shabaha, shughuli, muda wa utekelezaji, chanzo cha fedha, majukumu, na wadau mbalimbali.

(b) Mkakati wa Fedha - Sehemu ya Pili

Mkakati huu unaonesha utekelezaji na makusanyo ya fedha kwa vyanzo vya kawaida na vipya kwa ajili ya kugharamia Mpango. Mkakati pia unajumuisha mafunzo na uzoefu kutoka nchi zilizochaguliwa na hatua zilizopendekezwa

kuchukuliwa ili kutambua kiasi kilichokadiriwa cha kugharamia Mpango.

(c) Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini - Sehemu ya Tatu

Mkakati huu ni chombo cha usimamizi wa matokeo chenye kusisitiza uratibu, kuzingatia muda, viashiria vya utendaji, utoaji wa maoni, na taratibu za usahihishaji wa utekelezaji. Mkakati huu unaonesha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

(d) Mkakati wa Mawasiliano - Sehemu ya Nne

Mkakati huu unafafanua mbinu inayopaswa kutumika kuhakikisha kuna mtiririko mzuri wa taarifa na kukuza ushirikiano kwa wadau wote katika kipindi chote cha utekelezaji kisha kujadili matokeo yaliyotarajiwa na athari za utekelezaji wake badaye.

2.6 Mahitaji ya Ukaguzi katika Kutekeleza Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mahitaji ya kufanya kaguzi za ufanisi zinazoelezea dhamira za Malengo ya Maendeleo Endelevu yanatokana na umuhimu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi za kitaifa na kimataifa katika kuelezea maendeleo ya kiuchumi kwa njia endelevu. Mahitaji ya ukaguzi yanayoelezea dhamira za Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaweza kufafanuliwa zaidi kama inavyooneshwa katika vifungu vifuatavyo.

(a) Jukumu la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Dhima ya kwanza ya Kongamano la Kimataifa la 22 kwa Taasisi Kuu za Umma za Ukaguzi lilikuwa kutoa wito kwa wanachama wake kuchangia ufuatiliaji na mapitio ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kongamano hilo liliainisha umuhimu na dhamira ya kufanya kaguzi zinazohusisha kuangalia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa njia mbalimbali. Kongamano hilo lilizaa Azimio la Abu Dhabi ambalo liliweka chachu kwenye kuangalia utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu.

Kadhalika, mwaka 2015, Kamati ya Kubadilishana Maarifa pamoja na taasisi kuu za umma za ukaguzi kupitia mikakati yake ya maendeleo, zilizindua jukwaa la jamii la Malengo ya Maendeleo Endelevu na kuhamasisha jukumu

la taasisi za ukaguzi kufanya kaguzi za Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hayo yote ni miongoni mwa sababu za kukagua utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

(b) Utekelezaji usioridhisha wa Malengo ya Maendeleo ya Endelevu

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21) na Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Maandalizi ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (Machi 2018), Lengo Na. 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linataka kukomesha umaskini wa aina zote; kuwapo kwa afya bora na ustawi, elimu bora, usawa wa kijinsia, maji safi na usafi wa mazingira, nishati nafuu na safi, kazi yenye heshima; na ukuaji wa uchumi na uvumbuzi wa viwanda na miundombinu. Shabaha nyingine ni kupunguza utofauti wa usawa, kuwapo kwa miji na jumuiya endelevu, matumizi na uzalishaji kwa uwajibikaji, mpango wa tabianchi, uhai wa viumbe chini ya maji, uhai wa viumbe juu vya nchikavu, amani, haki na taasisi imara; na kuwapo kwa ubia wa malengo wakati wa kurejesha na kusimamia rasilimaliasilia kwa uendelevu.

Ripoti hiyo ilionesha kuwa, Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaunganisha pande tatu za maendeleo endelevu yaani uchumi, jamii, na mazingira kwa malengo yanayohusiana kwa karibu. Malengo ya Maendeleo Endelevu hayagawanyiki kwa maana kwamba hakuna lengo moja lililo tofauti na lingine, na yote yanahitaji mbinu za kina na shirikishi.

Hata hivyo, ripoti hiyo imeonesha kuwa changamoto kadhaa ziliikabili Tanzania wakati wa utekelezaji wa Malengo ambazo ziliikwamisha kufikia baadhi ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Changamoto hizo ni pamoja na ufanisi mdogo katika utendaji kazi wa mamlaka za serikali za mitaa kutokana na kutokuwa na uwezo; ushiriki na ushirikishaji mdogo wa sekta binafsi; uwezo na ushiriki mdogo wa watekelezaji (wahusika wakuu katika ngazi ya chini); na kushindwa kufikia Lengo Na. 8 ambalo ni kuendeleza ushirikiano wa kimataifa kwa ajili ya maendeleo.

(c) Tathmini ya Tanzania katika katika Kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu

Haja ya kaguzi za ufanisi katika Malengo ya Maendeleo Endelevu inatoa fursa ya kupima mafanikio yake. Mathalani, kupitia ukaguzi wa eneo hili, nchi

inaweza kujitathmini iwapo Wizara ya Fedha na Mipango, ambayo ni wizara kiongozi pamoja na OR-TAMISEMI, kama mratibu wa mamlaka za serikali za mitaa, ambazo ni watekelezaji wakuu, hutekeleza Ajenda ya 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu katika muktadha wa kitaifa kupitia utambuzi na ukusanyaji wa rasilimali na uwezo wa utekelezaji; na ufuatiliaji na utoaji wa taarifa kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

2.7 Ukaguzi wa Ufanisi Uliofanyika kuhusiana na Mpango Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, nimefanya kaguzi 12 za ufanisi ambazo zinaelezea utekelezaji wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu. Maudhui ambayo yamehusishwa kwenye kaguzi hizi ni yale yanayohusiana na maendeleo ya watu na mageuzi ya kiuchumi kama yalivyoainishwa kwenye Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mipango yote hii imeweka maeneo ya vipaumbele ambayo ni muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wake madhubuti.



Maeneo ya vipaumbele kwa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kuimarisha ukuaji wa viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi; kuchochea maendeleo ya watu; kuboresha mazingira rafiki ya uendelezaji biashara na kampuni; na ufanisi wa utekelezaji. Kadhalika, maeneo ya vipaumbele kwa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani; kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza ujuzi.

Maendeleo ya watu yanalenga kufanikisha kufikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu na mipango ya maendeleo ya taifa. Dhima ya maendeleo ya watu ni uboreshaji wa watu katika nyanja zote za uma, binafsi, jamii, siasa, na uchumi. Mageuzi ya kiuchumi yanazitaka nchi kufanya maboresho ya sera za kiuchumi kwa kuzingatia ushirikishaji, mageuzi mbalimbali ya ajira za kutosha ambazo zitajumuisha watu wote, kulinda dunia, na kuimarisha misingi ya ekolojia katika nyanja ya uchumi.

Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni zana zilizokubalika katika kutathmini maendeleo ya

uchumi na watu kimataifa na kitaifa mtawalia.

Muhtasari wa kaguzi za ufanisi zilizofanywa na maudhui yake kwa kuzingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu ni kama unavyowasilishwa hapa chini.

2.7.1 Ukaguzi wa ufanisi wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi huu unahusishwa na maeneo yote ya vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa sababu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uliandaliwa mwaka 2015 wakati Ajenda ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ilipoanza kutumika. Hali hii ilisababisha baadhi ya malengo na viashiria vyake viingizwe moja kwa moja kwenye mpango huo.

Kadhalika, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni mwendelezo wa jitihada za Serikali za kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 kwa nia ya kuboresha kiwango cha maisha kwa wanachi wote. Aidha, Mpango huu unalenga kutekeleza mipango-mkakati na makubaliano ya kisekta, kikanda na kimataifa ikiwemo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii.

Hivyo, kupitia mageuzi, Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu yamehusishwa kwenye mipango ya maendeleo ya nchi.

2.7.2 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali

Ukaguzi huu unahusishwa na eneo la kipaumbele kinachohusu maendeleo ya watu. Kipaumbele hiki ni sehemu ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na kinacholenga kuangalia shughuli za kimkakati zinazohusiana na uongozi bora na utawala wa sheria. Uongozi bora na utawala wa sheria ni miongoni mwa misingi muhimu ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Hii ni kwa sababu, uongozi bora unatoa misingi ya mwelekeo wa maendeleo ya taifa, wakati utawala wa sheria unalenga kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, miongozo, na taratibu wakati wa kufanya maamuzi.

Serikali ya Tanzania inaendelea kutilia mkazo maeneo ya uongozi na uwajibikaji kama nyenzo ya kukabiliana na usimamizi usioridhisha wa rasilimali za serikali, rushwa, utoaji hafifu wa huduma, ukwepaji kodi, na urasimu, masuala yenye athari hasi kwenye kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu. Hivyo, kutambulika kwa eneo hili la kipaumbele kunategemea kuwapo kwa uongozi bora na uwajibikaji.

Kwa kuzingatia kiwango cha pesa kinachotumika kufanya ununuzi, matenegenezo, na upatikanaji wa mafuta ya kuendeshea magari ya serikali, mkazo unawekwa kwenye ufanyaji wa uamuzi sahihi unaozingatia sheria na miongozo iliyopo kwenye uondoshaji wa magari ya serikali. Kadhalika, ni kwa kupitia eneo hili la kipaumbele, taasisi za ununuzi zinakumbushwa kuwa na usimamizi mzuri wa magari yao, kuanzia siku ambayo gari linanunuliwa hadi litakapofikia wakati wa kuondoshwa kwa lengo la kuongeza thamani yake.

2.7.3 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo

Ukaguzi huu unahusishwa na maeneo matatu ya vipaumbele yaliyopo kwenye Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maeneo hayo ya vipaumbele ni pamoja na kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma, maendeleo ya watu, na kuendeleza ujuzi.

Awamu zote mbili za Mpango zinaweka mkazo kwenye kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma, eneo ambalo linahusishwa moja kwa moja na ukaguzi huu kupitia moja ya shuguli zake za kimkakati ambayo ni kilimo. Shughuli hii ya kimkakati inalenga kuimarisha mnyororo wa thamani kwenye mazao, kukuza ujuzi kupitia mnyororo wa thamani, na kuongeza thamani ya mauzo ya mazao, ubora na viwango.

Ukaguzi huu pia unahusishwa na shughuli za kimkakati za uhakika wa chakula na lishe, masuala ambayo yapo chini ya eneo la kipaumbele la maendeleo ya watu. Kadhalika, awamu zote mbili za mpango zinaziimarisha jamii katika kuongeza kasi ya uzalishaji na kuimarisha lishe ili kupunguza matatizo ya kiafya yanayotokana na lishe duni kupitia programu mbalimbali za lishe na uwekezaji kwenye mazao.

Pia, ukaguzi unahusishwa na shughuli ya kimkakati ya ujuzi wa kujiajiri ambayo ni sehemu ya kipaumbele cha kuongeza ujuzi iliyopo kwenye

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Eneo hili la kipaumbele linalenga kuongeza idadi ya watu wenye ujuzi wa teknolojia za kisasa za kilimo.

Kwa upande mwingine, ukaguzi huu unahusishwa na lengo namba 2, malengo madogo 2(a) na 2(c) la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linataka kukomesha njaa na kuimarisha uhakika wa chakula, lishe, na kilimo endelevu.

Katika lengo hili, ukaguzi ulilenga kuimarisha jitihada za uwekezaji kupitia maboresho yaliyopo ya teknolojia za kilimo ili kuongeza uwezo wa uzalishaji wa mazao kwa nchi zinazoendelea. Pia, ukaguzi ulilenga kuwa na mikakati sahihi itakayowezesha kuwapo kwa masoko ya mazao, na upatikanaji kwa wakati wa taarifa za masoko ya mazao vikiwemo vihenge na maghala ili kuzuia upandaji holela wa bei za mazao.

Zaidi, ukaguzi unahusishwa na lengo namba 12, lengo dogo la 12.3 linalotaka kuongeza uhakika wa chakula katika ngazi ya wauzaji na walaji, na kuzuia upotevu wa chakula kuanzia kupindi cha kilimo hadi baada ya mavuno.

2.7.4 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa urasimishaji wa makazi holela

Ukaguzi huu unahusishwa na eneo la kipaumbele cha maendeleo ya watu, likiwa miongoni mwa vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Eneo hili la kipaumbele linalenga kuangalia shughuli mbili za kimkakati ambazo ni mipango-miji, nyumba, na maendeleo ya watu; na uongozi bora na utawala wa sheria.

Kwa upande wa shughuli za kimkakati zinazohusiana na mipango-miji, nyumba, na maendeleo ya makazi, ukaguzi huu unalenga kuimarisha upangaji wa miji na upimaji na utoaji wa hati za ardhi kwa lengo la kuwekeza na kuhakikisha kuwapo kwa makazi ya watu, na kuhakikisha makazi holela yanarasimishwa.

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulilenga kuangalia shughuli za kimkakati zinazohusiana na uongozi bora na utawala wa sheria. Eneo hili linalenga kuhakikisha kuna mifumo ya uongozi ili kuimarisha utawala wa sheria kwa kuzingatia kuna uwajibikaji, uwazi, ushirikishaji, na mazingira yasiyoshawishi vitendo vya rushwa.

Kwa kupitia shughuli hizi za kimkakati, ukaguzi ulilenga kuimarisha utaratibu wa utoaji wa huduma katika sekta ya umma na binafsi; na kuimarisha mifumo ya uongozi na uratibu wa shughuli za serikali.

Kadhalika, ukaguzi huu unahusishwa na lengo namba 11, malengo madogo ya 11.1 na 11.3 ya Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linakusudia kufanya miji na makazi ya watu kuwa salama na endelevu. Kipekee, lengo hili linakusudia kuhakikisha kuna makazi salama, ya gharama nafuu, na yenye huduma za msingi; kuboresha makazi holela; kuimarisha ushirikishaji; ukuaji wa miji ulio endelevu; na kuwa na upangaji na uendeshaji jumuishi wa makazi ya watu.

2.7.5 Ukaguzi wa ufanisi wa uendeshaji na ukarabati wa miradi ya maji safi na majitaka

Ukaguzi huu unahusishwa na eneo la kipaumbele cha maendeleo ya watu. Eneo hili ni sehemu ya vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kinachokusudia kuangalia shughuli za kimkakati za usamabazaji wa maji safi na usafi wa mazingira.

Kwa kuzingatia umuhimu wa maji safi na majitaka kwenye maendeleo ya watu, kupitia shughuli za kimkakati za usambazaji wa maji safi na usafi wa mazingira, ukaguzi huu utaimarisha usambazaji wa miundombinu ya maji safi na salama; utunzaji wa programu za vyanzo na rasilimali za maji; na usimamizi na ufuatiliaji wa maji safi.

Kwa upande mwingine, ukaguzi huu unahusishwa na lengo namba 6, malengo madogo ya 6.1 na 6.4 ya Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linakusudia kuhakikisha kuna usimamizi endelevu wa maji safi na usafi wa mazingira kwa watu wote. Lengo hili hususani linataka kufanikisha usawa wa upatikanaji wa maji safi ya kunywa kwa gharama nafuu kwa watu wote. Kadhalika, linalenga kutekeleza usimamizi shirikishi wa vyanzo vya maji katika ngazi mbalimbali kufikia mwaka 2023.

2.7.6 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu

Ukaguzi huu unahusishwa na eneo la kipaumbele cha kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma. Eneo hili ni miongoni mwa vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kinachoangalia usimamizi wa shughuli za kimkakati za mazingira na maliasili. Katika shughuli hizo za kimkakati, ukaguzi huu unahusishwa moja kwa moja na utunzaji wa bayoanuai.

Kadhalika, ukaguzi huu unahusishwa na lengo namba 15, lengo dogo la 15.8 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linataka kutunza, kurejesha, na kuimarisha matumizi endelevu ya mfumo wa ikolojia ya mazingira ya nchikavu. Pia, linalenga kuwapo kwa usimamizi endelevu wa misitu, na kukabiliana na hali ya jangwa, mmomonyoko wa udongo, na upotevu wa bayoanuai.

2.7.7 Ukaguzi wa ufanisi wa udhibiti wa malipo yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa vituo vya huduma za afya

Jitihada zinahitajika ili kuondoa msongamano wa magonjwa na kukabiliana na changamoto kadhaa zinazoibuka za afya kwa kuwa na mfumo madhubuti wa kuwezesha kifedha utoaji wa huduma za afya. Hivyo, ukaguzi huu unahusishwa na eneo la kipaumbele la Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano linalotaka kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma hususani huduma za bima ya afya.

Eneo hili la kipaumbele linatilia mkazo kwenye mambo makuu matatu ya huduma za bima ya afya ambayo ni kuwa na programu za kujenda uelewa wa masuala y bima ya afya kwa wananchi; kuwa na huduma za bima ya afya zinazolenga mahitaji ya wananchi; na kujenga mfumo rahisi wa madai ya huduma za bima, utoaji wa malalamiko, na ushughulikiaji wa malalamiko katika eneo la bima ya afya.

Ukaguzi huu pia unahusishwa na eneo la kipaumbele la maendeleo ya watu ambalo linaweka msisitizo kwenye afya bora, hifadhi ya jamii, na uongozi bora. Kwa upande wa uongozi bora, mkazo umewekwa kwenye kuimarisha na kupanua mawanda na kufikika kwa huduma za bima ya afya. Kadhalika, kwa upande wa hifadhi ya jamii, lengo ni kuimarisha huduma za ustawi wa jamii zinazohusisha huduma za afya na msaada wa kisaikolojia kwa makundi

yaliyo katika mazingira hatarishi na jamii kwa ujumla. Kwa upande wa uongozi bora, ukaguzi huu utaimarisha utoaji wa huduma katika sekta za umma na binafsi.

Kadhalika, ukaguzi huu unahusishwa na lengo namba 3 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa linataka kuhakikisha kuna afya bora kwa wote na kwa umri wote. Lengo hili ni dhahiri kwa sababu, huduma za bima ya afya ni miongoni mwa maeneo muhimu ya kuwezesha kifedha mifumo ya huduma za afya. Hivyo, lengo hili likisimamiwa vizuri, litawezesha kufikiwa kwa lengo la kuwa na huduma za afya kwa watu wote duniani.

2.7.8 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa mipango na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini

Ukaguzi huu unahusishwa na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kupitia maeneo ya vipaumbele na shughuli za kimkakati. Hili ni eneo la kipaumbele la kuimarisha ukuaji wa viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi, ambalo ni sehemu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Lengo hili linataka kuimarisha uchumi kwa kuweka mkazo kwenye uvumbuzi na matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma.

Ukaguzi pia uliangalia eneo la kipaumbele linalohusiana na kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma, ambalo ni sehemu ya vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Eneo hili la kipaumbele linaweka mkazo kwenye uwekezaji na utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA nchini. Kadhalika, linalenga kuimarisha utoaji wa huduma kupitia serikali mtandao.

Pia, ukaguzi huu unaelezea namna ambavyo Serikali inatekeleza lengo namba 9 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linataka kuweka mkazo wa kuwa na miundombinu ya TEHAMA na kuimarisha ukuaji wa viwanda na uvumbuzi shirikishi.

Maboresho ya namna miundombinu ya TEHAMA inapatikana, yanatakiwa yawezeshe upatikanaji wa miundombinu ya TEHAMA yenye ufanisi na yenye kuleta matokeo chanya. Hatua hii itasaidia kuimarisha uwajibikaji na ushirikishaji kwa ngazi zote.

2.7.9 Ukaguzi wa ufanisi wa udhibiti wa vyanzo vy mionzi

Ukaguzi huu unahusishwa na maeneo mawili ya vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Moja ya maeneo hayo ya vipaumbele ni maendeleo ya watu yanayolenga shughuli za kimkakati za afya ambazo lengo lake ni kusimamia magonjwa yasiyoambukiza.

Eneo lingine la shughuli za kimkakati ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma zinazotilia mkazo shughuli za kimkakati za usimamizi wa mazingira na maliasili. Ukaguzi huu utasaidia kupunguza athari za uharibifu wa mazingira kwa binadamu.

Kadhalika, ukaguzi huu unahusishwa na lengo namba 3 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa linalotaka kupunguzwa kwa idadi ya vifo na magonjwa yanayohusishwa na mionzi. Pia, linahusishwa na lengo namba 13 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa linalotaka kuchukuliwa kwa hatua za haraka ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

2.7.10 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa vituo binafsi vya utoaji wa huduma za afya



Ukaguzi huu ulilenga kufanikisha eneo la maendeleo ya watu ambalo ni sehemu ya vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Eneo hili la kipaumbele linatekelezwa kupitia shughuli mbili za kimkakati ambazo ni afya, na uongozi bora na utawala wa sheria.

Kupitia shughuli ya kimkakati ya afya, ukaguzi ulilenga kuimarisha na kuwezesha uwekezaji binafsi kwenye eneo la afya; na kupitia uongozi bora na utawala wa sheria, ukaguzi ulilenga kuimarisha mifumo ya uongozi kwa kuhakikisha kuwa vituo vya afya vinaendesha shughuli zake kwa kuzingatia matokeo, uwajibikaji, uwazi, na bila rushwa.

Ukaguzi pia ulilenga kuangalia utekelezaji wa lengo namba 3 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ambalo linakusudia kuhakikisha kuna utoaji wa huduma za afya kwa ngazi zote za vituo vya afya vya umma na binafsi.

2.7.11 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa shughuli za tafiti na uvumbuzi

Ukaguzi huu ulilenga kufanikisha maeneo matatu ya vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambayo ni kuimarisha ukuaji wa viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi; kuchochea uchumi shirikishi na shindani, na utoaji wa huduma; na uendelezaji wa ujuzi.

Kwa kuanzia na eneo la kipaumbele la kuimarisha ukuaji wa viwanda kwa mageuzi ya kiuchumi, lengo ni kuimarisha uchumi kwa kuweka mkazo kwenye uvumbuzi na matumizi ya TEHAMA kwenye utoaji wa huduma. Kwa upande wa kuendeleza ujuzi, mkazo unawekwa kwenye kuimarisha uvumbuzi, kubadilishana ujuzi, teknolojia, na ujuzi wa kujiajiri.

Eneo la kipaumbele la kuchochea uchumi shirikishi na shindani na utoaji wa huduma linalenga kuwa na vituo bora vya TEHAMA, kuwezesha tafiti za ndani na maendeleo ya TEHAMA, uvumbuzi wa kiTEHAMA, uimarishaji wa shughuli vumbuzi mbalimbali, na kusajili wataalamu wa TEHAMA.

Kwa upande mwingine, ukaguzi huu unahusishwa na lengo namba 9, lengo dogo 9.5 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hili linalenga kuimarisha tafiti za kisayansi, kuboresha uwezo wa kiteknolojia wa sekta za viwanda, kuhamasisha uvumbuzi, na kuongeza idadi ya tafiti.

2.7.12 Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uwekezaji wa mali za Serikali zisizohamishika zinazosimamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii

Ukaguzi huu unahusishwa na maeneo mawili ya vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambayo ni maendeleo ya watu na uwekezaji na ukuzaji wa biashara.

Kuhusu uwekezaji na ukuzaji wa biashara, ukaguzi umehusishwa na shughuli za kimkakati za kuimarisha mageuzi ya mazingira rafiki ya biashara na uwekezaji. Hulusani, ukaguzi ulilenga kupiga hatua za kitaifa na kikanda zinazohusiana na kupunguza gharama za kufanya biashara zinazolenga kushughulikia vikwazo vinavyoathiri uwekezaji na mwenendo wa biashara.


Aidha, ukaguzi unahusishwa moja kwa moja na ukaguzi wa shughuli za kimkakati za hifadhi ya jamii ambazo ziko chini ya kipaumbele cha maendeleo ya watu. Hususani, ukaguzi ulilenga kuimarisha usimamizi wa fedha za uwekezaji za wananchi na miradi ya hifadhi ya jamii.

Kwa upande mwingine, ukaguzi unahusishwa na lengo namba 10, lengo dogo 10.4 la Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Lengo hilo linataka kupitishwa kwa sera za fedha, mishahara, na ulinzi wa kijamii, na kufikia usawa. Hali hii imeoneshwa katika sehemu ya mishahara ya watumishi ya pato la taifa inayojumuisha mishahara na mifuko ya uhifadhi wa jamii.

Kielelezo Na. 2.4 kinatoa muhtasari wa uhusiano kati ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu.



Kielelezo Na. 2.4: Uhusiano kati ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu



Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi kutokana na Taarifa za Maelengo ya Maendeleo Endelevu na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano Mwaka 2023

2.8 Mifumo ya Ugharamiaji katika Utekelezaji wa Mpango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano

Kwa mujibu wa Mkakati wa Fedha wa Mwaka 2018 wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka wa Mitano, mafanikio ya mpango ambayo yamejikita katika kuimarisha mabadiliko ya kiuchumi, maendeleo ya watu, maendeleo ya viwanda, na kukuza ufanisi wa utekelezaji yanabebwa na ukusanyaji bora wa rasilimali-fedha na mapato, na utaratibu mzuri wa ugharamiaji.

Ugharamiaji wa utekelezaji unajumuisha vyanzo vya kawaida vya kodi na mapato na vyanzo vipya vya fedha. Chanzo cha kawaida cha fedha kinajumuisha mapato ya kodi, mapato yasiyo ya kodi, ukopaji wa ndani, na fedha za nje. Vyanzo vipya vya fedha pia vimeanzishwa ili kuongezea vyanzo vya kawaida. Vyanzo hivi vinajumuisha vyanzo vya fedha vya ndani na nje kupitia fursa zinazohusiana na bidhaa mpya ambazo zinajumuisha dhamana ya soko la nje; dhamana za serikali za mitaa/dhamana za manispaa; ufadhili wa mabadiliko ya tabianchi; taasisi za fedha za maendeleo; Mfuko wa Usawa wa Pensheni; ubia wa binafsi na umma; na uwekezaji wa moja kwa moja wa kutoka nje.



UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU NCHINI

SURA YA TATU

3

2 ZERO HUNGER



3 GOOD HEALTH AND WELL-BEING



4 EDUCATION



8 DECENT WORK AND ECONOMIC GROWTH



9 INDUSTRY, INNOVATION AND INFRASTRUCTURE



10 REDUCED INEQUALITIES



11 SUSTAINABLE CITIES AND COMMUNITIES



14 LIFE BELOW WATER

15 LIFE ON LAND

16 PEACE, JUSTICE AND STRONG INSTITUTIONS

17 PARTNERSHIPS FOR THE GOALS

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU NCHINI

3.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini. Pia, inaelezea usuli kuhusu eneo la ukaguzi, uhusiano wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, juhudi na mikakati ya Serikali katika kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu, malengo na mawanda ya ukaguzi.

3.2 Usuli kuhusu Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Nchini

Mwaka 2015, Umoja wa Mataifa ulipitisha Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu² kukiwa na shabaha 169 za matarajio ya kufanikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi zilizotia saina Ajenda ya Mwaka 2030, ilichukua hatua za kuhusisha Ajenda ya Mwaka 2030 katika muktadha wa kitaifa kwa kuimarisha malengo na shabaha katika mfumo wake wa mipango ya maendeleo.

Wakati wa upitishaji wa Ajenda ya Mwaka 2030, Tanzania ilikuwa katika maandalizi ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, hivyo ajenda hiyo ilihusishwa moja kwa moja katika mpango huo. Malengo yote 17 yalijumuishwa ili kutoa dira ya utekelezaji wa mipango ya serikali, taasisi za kimataifa, asasi za kiraia, na taasisi zingine katika miaka 15 iliyofuata (2016 - 2030).

Ajenda ya Mwaka 2030 inalenga kuweka mipango ya siku zijazo, kuubadilisha ulimwengu kuelekea kwenye njia endelevu na yenye nguvu, na kuleta mabadiliko ya kiuchumi na uboreshaji wa viwango vya maisha ya watu katika hatua ya mpito kwa njia jumuishi na endelevu za maendeleo.

Kwa mantiki hiyo, ukaguzi huu ulilenga kutathmini kiwango ambacho Tanzania imesimamia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliyopitishwa pamoja na shabaha zake zilizowekwa.

² Azimio la Umoja wa Mataifa Na. 70/1


3.2.1 Uhusiano wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano

Malengo ya Maendeleo Endelevu yanatekelezwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano ambayo yamejumuishwa katika nguzo za mipango ya maendeleo ya taifa ambazo zimegawanywa zaidi katika shabaha mbalimbali na kupitishwa katika mipango-mkakati ya sekta na bajeti kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 3.1** hapa chini.

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unatoa mwongozo na uelewa wa dira ya maendeleo ya muda mrefu ya nchi wenye maudhui ya "*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*", ikiwa ni mwendelezo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wenye maudhui ya "*Kukuza Viwanda kwa Mageuzi ya Kiuchumi na Maendeleo ya Watu*". Hivyo, utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya miaka mitano hutekeleza moja kwa moja Malengo ya Maendeleo Endelevu.



Kielelezo Na. 3.1: Uhusiano wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano



Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi kutoka Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano, Azimio la Umoja wa Mataifa Na. 70/1 na Mapatio ya Hiri ya Taifa ya Mwaka 2019

3.2.2 Mikakati na juhudi za Serikali katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imeweka mipango mbalimbali inayolenga kuhakikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu yanahusishwa katika muktadha wa kitaifa na yanatekelezwa vizuri. Zifuatazo ni hatua kuu za kimkakati na juhudi za Serikali za kuboresha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

- (a) Kuwa na mipango ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu - Wizara ya Fedha na Mipango, kwa kushirikiana na wadau wengine, iliandaa mipango ifuatayo ya kitaifa ambayo ililenga kuelekeza juhudi za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.
 - (i) Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025
 - (ii) Mpango wa Muda Mrefu 2011/2012 - 2025/2026
 - (iii) Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 - 2020/2021)
 - (iv) Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 hadi 2025/2026)
 - (v) Mpango Mkuu wa Takwimu Tanzania - Awamu ya Kwanza
 - (vi) Mpango Mkuu wa Takwimu Tanzania - Awamu ya Pili

- (b) Kuwa na mikakati ya utekelezaji wa Mpango ya Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano - Wizara ya Fedha na Mipango imeandaa mikakati ya utekelezaji wa mpango huo ambayo ni pamoja na mpango wa utekelezaji, mkakati wa ufuatiliaji na tathmini, mkakati wa fedha, na mkakati wa mawasiliano. Pia, Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imeanzisha mikakati ya kukuza ukusanyaji wa rasilimali-fedha katika taasisi za kiserikali kuliko kutegemea chanzo cha fedha kilichozoeleka.

3.3 Malengo ya Ukaguzi

Ukaguzi huu ulilenga kutathmini iwapo Wizara ya Fedha na Mipango na OR-TAMISEMI zilisimamia ipasavyo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kupitia mipango ya kitaifa na utekelezaji katika ngazi za chini za Serikali. Malengo mahususi yalikuwa kutathmini endapo:

- (i) Wizara ya Fedha na Mipango imetoa na kuwezesha utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa na kuimarisha Malengo ya Maendeleo

Endelevu;

- (ii) Taasisi zenye dhamana ya utekelezaji zimetokeleza hatua za kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu;
- (iii) Wizara ya Fedha na Mipango na OR-TAMISEMI zimesimamia ipasavyo ukusanyaji na matumizi ya rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu;
- (iv) Wizara ya Fedha na Mipango na OR-TAMISEMI zimefuatilia ipasavyo ufanisi wa kiutendaji wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Katika ukaguzi huu, wakaguliwa wakuu walikuwa Wizara ya Fedha na Mipango na OR-TAMISEMI. Wizara ya Fedha na Mipango ina jukumu la kuongoza na kuratibu upangaji na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu wakati OR-TAMISEMI ni mratibu na msimamizi wa mamlaka za serikali za mitaa ambazo ni watekelezaji wakuu na wanufaika wa msingi wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Wadau wengine muhimu walikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, kama mratibu wa wizara zote za kisékta; na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ambayo ina jukumu la utoaji wa takwimu za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini.

Ukaguzi ulihusu kipindi cha miaka sita ya fedha kuanzia 2016/17 hadi 2021/22/. Kipindi hiki kilichaguliwa ili kutoa mwenendo wa utendaji katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini kuanzia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

3.4 Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa utendaji wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ukaguzi ulibaini masuala yafuatayo yanayohitaji maboresho zaidi ili kuwa na utekelezaji madhubuti.

3.4.1 Utekelezaji Usiojitosheleza wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi ulibaini utekelezaji usiojitosheleza wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kama ilivyothibitika wakati wa kupitia taarifa za utekelezaji wa hatua za kufikia malengo yaliyowekwa. Mapungufu hayo yalisababishwa na Mipango na ujumuishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano isiyoridhisha; utekelezaji

usioridhisha wa hatua za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu; ukusanyaji usioridhisha wa rasilimali kwa ajili utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu; na ufuatiliaji usioridhishawa mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Sababu hizi zinazoelezea mapungufu ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu zinafafanuliwa kwa kina hapa chini.

3.4.1.1 Mipango na ujumuishaji usiojitosheleza wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano


Mapitio ya Taarifa ya Kitaifa ya Takwimu kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu - Mafunzo na Mapendekezo ya kuanzia Mwaka 2016 hadi 2018 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu yalibaini uhusiano mkubwa kati ya Malengo ya Maendeleo Endelevu na vipaumbele vinavyotekelezwa na mifumo ya maendeleo ya taifa. Ilibainika kuwa, kati ya viashiria 244 vya Malengo ya Maendeleo Endelevu, viashiria 240 vilikuwa muhimu na vinatekelezeka nchini. Ilibainika kuwa ni viashiria vinne tu vya Malengo ya Maendeleo Endelevu ndivyo havitekelezeki kwa mazingira ya nchi yetu kutokana na mipango na mwelekeo wake wa kijiografia. Viashiria hivyo ni:

- (a) Kiashiria namba 13.a.1 kinachohusu kiasi kilichokusanywa cha dola za Marekani kwa mwaka 2020 na 2025 kinahusishwa na kuelekea katika ahadi ya dola bilioni 100;
- (b) Kiashiria namba 14.7.1 kinachohusu uvuvi endelevu kwa asilimia ya pato la taifa katika nchi ndogo za visiwa zinazoendelea;
- (c) Kiashiria namba 17.7.1 kinachohusu jumla ya fedha zilizoidhinishwa kwa nchi zinazoendelea ili kukuza uendelezaji, uhamishaji, usambazaji, na uenezaji wa teknolojia nzuri za mazingira; na
- (d) Kiashiria namba 17.9.1 kinachohusu thamani ya dola ya msaada wa kifedha na kitaalamu (ikiwa pamoja na kupitia ushirikiano wa Kaskazini-Kusini, Kusini-Kusini na shirikishi) iliyojitolea kwa nchi zinazoendelea.

Aidha, viashiria 167 kati ya 240 vilijumuishwa moja kwa moja au kwa sehemu katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Vilevile, ilibainika kuwa kati ya viashiria 167, viashiria 83 vilijumuishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano; na viashiria 84 vilijumuishwa katika sera na mikakati ya sekta inayotekelezwa nchini.

Viashiria 73 vilivyobaki ni muhimu lakini havikujumuishwa katika mifumo ya maendeleo ya taifa (kama vile Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano) na vinahitaji uchambuzi wa kina zaidi kabla ya kujumuishwa na kuanza kuwezesha uzalishaji wa taarifa kama inavyooneshwa katika Kielelezo Na. 3.2:

Kielelezo Na. 3.2: Uchambuzi wa Viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu Tanzania Bara



Chanzo: Ripoti ya Hiari ya Mapitio ya Taifa, Tanzania Mwaka 2019

Ukaguzi ulibaini kuwa kwa sekta³ zilizotembelewa katika mamlaka za serikali za mitaa na mapitio ya Taarifa ya Kitaifa ya Takwimu kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu, kati ya viashiria 27 vya Malengo ya Maendeleo Endelevu vya afya bora na ustawi (lengo namba 3), viashiria 18 sawa na asilimia 75 vilijumuishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa, katika sekta ya kilimo, kati ya viashiria 14, viashiria 10 vilijumuishwa kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano sawa na asilimia 71. Ni viashiria vinne tu ndivyo havikujumuishwa katika mipango ya kitaifa na upatikanaji wa taarifa, sawa na asilimia 29 ya viashiria vyote vya lengo la pili la kutokomeza njaa.

³ Sekta zilizokaguliwa katika ngazi za chini ni afya, kilimo na viwanda.

Mipango na ujumuishaji usiojitosheleza wa malengo katika Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pia ulibainika kwenye maeneo ya tathmini ya malengo na ujumuishaji wa malengo hayo kwenye mipango-mkakati na utoaji wa taarifa kama ifuatavyo.

(i) Mapitio yasiyoridhisha na ujumuishaji wa mipango-mkakati ya sekta za wizara, Sekretarieti za Mikoa, na Halmashauri kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Pili na Tatu unaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa wizara na taasisi za serikali, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa zinahusisha mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano katika mipango-mkakati yao. Ingawa ukaguzi ulibaini kuwa mipango-mkakati katika ngazi za wizara na taasisi za serikali ilipitiwa ili kuendana na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, mapungufu yafuatayo yalibainika:

- (a) Kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kulikuwa na ucheleweshaji wa mapitio ya mpango-mkakati ambapo, mapitio yalifanyika baada ya uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hadi mwezi Oktoba 2022, mpango-mkakati huo bado ulikuwa katika hatua ya rasimu.
- (b) Kwa Wizara ya Kilimo, ukaguzi ulibaini uwiano usioridhisha kati ya mpango-mkakati na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambapo mpango-mkakati uliopita ulimalizika mwaka 2022, na hakukuwa na mpango-mkakati mpya ulioandaliwa. Hivyo, Wizara ilitegemea mipango yake ya mwaka kama nyenzo za kuongoza utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi chote cha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.
- (c) Kwa Wizara ya Afya, ukaguzi ulipitia mipango-mkakati miwili na ilibainika kuwa mipango-mkakati yote miwili ilianza kufanya kazi mwaka mmoja baada ya uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hali hii ilionesha kwamba katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa kila mpango wa maendeleo wa taifa, hakukuwa na nyenzo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

-
- (d) Kupitia mapitio ya Ripoti ya Tathmini ya Mahitaji na Uwezo ya Machi 2022, ukaguzi ulibaini kuwa wizara na taasisi za Serikali, sekretarieti za mikoa, na halmashauri moja kati ya 10 haikuzingatia viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu wakati wa kufanya mapitio na tathmini ya mipango-mkakati yake. Uchambuzi wa ripoti hiyo ulibaini pia kwamba, licha ya uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, takribani moja ya tano (1/5) ya wizara na taasisi za Serikali, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa hazikuhisha mipango-mkakati yao. Matokeo yake, wizara na taasisi za Serikali, sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa, kwa uwiano uleule wa moja ya kumi (1/10), hazikujumuisha vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika mipango-mkakati yao.

Aidha, mapitio ya Ripoti ya Tathmini kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021) yalibaini utekelezaji usioridhisha wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kutokana na utekelezaji usioendana na mipango ya kila mwaka katika wizara na taasisi za Serikali, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa. Vile vile, ilibainika kuwa mipango mingi ya kila mwaka ya wizara na taasisi za Serikali, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa haikufungamana kimalifu na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mapungufu haya yalisababishwa na mawasiliano na tathmini zisizoridhisha wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na mapitio ya mipango-mkakati ya sekta za wizara. **Jedwali Na. 3.1** linaonesha kiwango cha mapitio ya mipango-mkakati katika mikoa iliyotembelewa.

Jedwali Na. 3.1: Kiwango cha Mapitio ya Mipango-mkakati katika Mikoa Iliyotembelewa

| Sekretarieti za Mikoa | Mpango-mkakati ulifanyiwa mapitio baada ya uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2016 | Mpango-mkakati ulifanyiwa mapitio sambamba na uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2016 | Mpango-mkakati ulifanyiwa mapitio baada ya uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2021 | Mpango-mkakati ulifanyiwa mapitio sambamba na uzinduzi wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2021 |
|-----------------------|--|---|--|---|
| Singida | Hapana | Hapana | Hapana | Hapana |
| Katavi | Hapana | Hapana | Hapana | Hapana |
| Tabora | Ndiyo | Hapana | Hapana | Hapana |
| Mwanza | Ndiyo | Hapana | Ndiyo | Hapana |
| Morogoro | Hapana | Hapana | Ndiyo | Hapana |
| Mtwara | Hapana | Hapana | Hapana | Ndiyo |

Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi wa mpango-mkakati wa Sekretarieti 6 za Mikoa Mwaka 2022

Jedwali Na. 3.1 linaonesha kuwa kati ya sekretarieti 6 za mikoa zilizotembelewa, hakukuwa hata moja iliyoandaa mpango-mkakati wake wakati Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unazinduliwa mwezi Juni 2016. **Jedwali Na. 3.1** linaonesha pia kuwa sekretarieti 2 kati ya 6 za mikoa zilipitia mipango-mkakati yao baada ya uzinduzi wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hali hii inaonesha kuwa mipango-mkakati haikujumuisha vipaumbele vya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

(ii) Utekelezaji usioridhisha wa mipango ya utoaji wa takwimu wakati wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepewa mamlaka ya kuzalisha na kusambaza takwimu rasmi kwa Serikali, jumuiya za wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla. Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatao kuhusiana na utekelezaji wa mipango ya utoaji wa takwimu.

(a) Mpangilio wa kitaifa wa uratibu wa utekelezaji na ufuatiliaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu usiyofanya kazi

Ukaguzi huu ulibaini kuwa, mbali na Kamati ya Wataalamu ya Ngazi ya Juu, Tanzania inahitaji utaratibu wa utekelezaji kwa kuzingatia takwimu za ajenda ya maendeleo, ukifanya kazi kama kamati ndogo ya Kamati ya Wataalamu ya Ngazi ya Juu ili kuratibu maslahi ya wadau na juhudi zinazohusu masuala ya takwimu katika siku zijazo. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Taifa wa Uratibu wa Utekelezaji na Ufuatiliaji uliandaliwa lakini haukuwa unafanya kazi. Matokeo yake, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa katika ngazi mbalimbali za serikali kwa ajili ya uwezesaji bora wa takwimu haukuwapo. Hali hii ilisababisha kukosekana kwa taarifa na takwimu za ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

(b) Mpangilio wa uratibu na ufuatiliaji katika ngazi ya taifa wa Malengo ya Maendeleo Endelevu haufanyi kazi vizuri

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na uwezesaji mdogo kwa ajili ya shughuli za kitakwimu. Bajeti za shughuli ziliwekewa ukomo na kupunguzwa pale upungufu wa rasilimali unapotokea. Aidha, mapitio ya ukaguzi wa bajeti za sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22 yalibaini ufinyu wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya utoaji wa takwimu na usimamizi wa shughuli za kitakwimu.

(c) Uelimishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu Usijitoshesheza

Ukaguzi huu ulibaini kuwa licha ya ahadi zilizotolewa katika uanzishaji wa mpangilio na taarifa na takwimu, hakukuwa na maoni au kauli kutoka kwa uongozi wa juu wa kisiasa katika shughuli zao mbalimbali na ushiriki wao katika kuelimisha umuhimu wa takwimu. Aidha, ukaguzi haukupata ushahidi wowote unaoonesha kuwapo kwa utoaji wa elimu ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na ushiriki wa viongozi wa kisiasa katika kuunga mkono maamuzi yanayotokana na utekelezaji wa malengo.

(d) Ufuatiliaji mdogo wa viashiria katika ngazi za chini

Ukaguzi ulibaini katika sekta tatu zilizokaguliwa kuwa kiolezo cha takwimu kuu kilichotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa halmashauri kwa ajili ya kutolea mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu hakikuwahi kutumika katika ukusanyaji wa taarifa. Pia, hakukuwa na mwongozo kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu wa jinsi ya kutumia kiolezo hicho. Vilevile, baadhi ya viashiria havikufuatiliwa na mamlaka za serikali za mitaa hivyo kusababisha ugumu kwenye kukusanya taarifa kwa ajili ya kutathmini mwenendo wa utekelezaji na kuchukua hatua.

(i) Sababu za mipango na ujumuishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Usioridhisha

Ukaguzi ulibaini kuwa kukosekana kwa mipango na ujumuishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kulitokana na kukosekana kwa mfumo wa uwiano wa takwimu unaoeleweka vizuri ambao ungeweza kupunguza ugumu wa ufuatiliaji wa taarifa. Sababu zingine ni kukosekana kwa uratibu na mwongozo kwa sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutoka OR-TAMISEMI kuhusu ukaguzi na uwiano wa mipango-mkakati; na uhaba wa watakwimu na wachambuzi wa taarifa kwa ajili ya utoaji wa mwenendo wa utekelezaji kwa ngazi za chini.

(ii) Athari za mipango na ujumuishaji duni wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Usiojitosheleza

Mipango na ujumuishaji usiotosheleza wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulichangia kucheleweshwa kwa utekelezaji wa Malengo hivyo kusababisha mgao usiotosheleza wa rasilimali za utekelezaji kutokana na kukosekana kwa taarifa za mwenendo wa utekelezaji. Mapungufu haya yanaweza kusababisha upotoshaji katika kufanya maamuzi juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa kila lengo kutokana na kutokuwapo kwa taarifa kuhusu mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

3.4.1.2 Utekelezaji Usioridhisha wa hatua za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu

Wizara na taasisi za Serikali, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa zilitakiwa kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu moja kwa moja kwa Wizara ya Fedha na Mipango. Ukaguzi ulibaini kulikuwa na utekelezaji usioridhisha katika wizara na taasisi za Serikali, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa wa kufanikisha Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uliojumuishwa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mapungufu haya yamejitokeza katika maeneo yanayoelezwa hapa chini.

(i) Uratibu na ushirikiano usio na tija baina ya taasisi za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa Jukwaa la kila Mwaka la Wadau Mbalimbali wa Malengo ya Maendeleo Edelevu lililojumuishwa wadau muhimu. Kupitia mahojiano ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Wizara ya Fedha na Mipango, ukaguzi haikupata ripoti za shughuli za jukwaa hilo zilizohusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Ukaguzi pia ulibaini kuwa, katika wizara zilizokaguliwa kulifanyika mabadiliko ya waratibu wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu bila kuteua waratibu wengine wa kushika nafasi zao. Hali hii ilithibitika katika OR-TAMISEMI ambao mratibu alibadilishwa bila kuteua mwingine ili kuendeleza shughuli za uratibu wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Hali hii iliashiria kuwapo kwa ufuatiliaji usiofaa wa mfumo wa uratibu wa utekelezaji wa Malengo ya Meendeleo Endelevu katika Wizara za Fedha na Mipango na OR-TAMISEMI katika ngazi za chini jambo lililozuia ufuatiliaji na tathmini bora ya ajenda za kimataifa na kikanda.

(ii) Mawasiliano yasiyo na tija baina ya wakala za Serikali katika ngazi mbalimbali za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mawasiliano yasiyo na tija ambayo yalithibitishwa na uelewa mdogo wa ujumuishaji wa Mpango wa Pili na Tatu

wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika mipango-mkakati ya mamlaka za serikali za mitaa. Ukaguzi ulibaini kuwa mpango wa uelimishaji haukutekelezwa ipasavyo katika ngazi za chini za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Katika sampuli tatu za sekta ya kilimo, afya, na viwanda na biashara, hakukuwa na ujumuishaji wa viashiria vyote katika ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa kutofautiana katika ukusanyaji wa takwimu kuhusu uwiano wa uhakika wa chakula. Hali hii ilileta ugumu wa kujua hatua kwa hatua viashiria vinavyotekelezwa. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi ya chini haukutosheleza kutokana na kukosekana kwa utaratibu wa wazi unaoonesha shabaha na viashiria vilivyotekelezwa na matokeo yake kutathminiwa.

Vivyo hivyo, uchambuzi wa ripoti ya tathmini ya mahitaji na uwezo ulibaini kuwa kukosekana kwa kujengeana uwezo kuhusu utoaji wa taarifa za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kulisababisha kutokuwa na uelewa wa kutosha wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa kila shabaha ya utekelezaji. Hali hii ilichangiwa na kuwapo kwa pengo la ujuzi wa wadau wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

(iii) Utekelezaji usio na Ufanisi wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika wizara zilizotembelewa

Wizara ya Fedha na Mipango, kupitia Kikosi Kazi cha Uratibu wa Kitaifa, ilikuwa na jukumu la kuripoti maendeleo kwa kuzingatia hatua zilizowekwa za utekelezaji ikiwa pamoja na ahadi za kimataifa. Ukaguzi ulichambua kiwango cha mafanikio na mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika sampuli tatu za kissekta ambazo ni afya, kilimo, na viwanda, uwekezaji na biashara kwa mujibu wa viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu kama inavyofafanuliwa hapa chini.

- (a) Kiwango ambacho sekta ya kilimo ilitekeleza lengo namba 2, kiashiria namba 2.1.2 kilibainika kwa mujibu wa takwimu zilizokusanywa katika Wizara ya Kilimo na mapitio ya kiambatisho cha takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Ukaguzi ulibaini kuwa, uwiano wa kujitosheleza kwa chakula ulikuwa sawa na asilimia 123 mwaka 2016 na asilimia 119

mwaka 2019 kama ilivyoripotiwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (tazama Jedwali Na. 3.2).

Jedwali Na. 3.1: Kiwango cha Utekelezaji wa Kiashiria Na. 2.1.2

| Maelezo ya Kiashiria cha Malengo ya Maendeleo Endelevu | Kiashiria cha Taifa | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
|--|-------------------------------------|------|------|------|------|
| Kuenea kwa Kukosekana kwa Chakula kwa Kiwango cha Wastani au Juu katika Idadi ya Watu, kulingana na Kiwango cha Uzoefu wa Ukosefu wa Chakula | Uwiano wa Kujitosheleza kwa Chakula | 123 | 120 | 124 | 119 |

Chanzo: Kiambatisho kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu Mwaka 2021

- (b) Hata hivyo, kwa kuzingatia takwimu za Wizara ya Kilimo, kama zilivyoboreshwa mwaka 2021, ilibainika pia kuwa kulikuwa na upungufu kutoka asilimia 126 (2016) hadi asilimia 115 (2019) za uwiano wa kujitosheleza kwa chakula. Hivyo, hali hii ilionyesha kuwapo kwa tofauti za takwimu zinazozalishwa kati ya Wizara ya Kilimo na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuhusu uwiano wa kujitosheleza kwa chakula nchini.
- (c) Kwa kuzingatia takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuhusu kiwango ambacho sekta ya afya imetekeleza lengo namba 3, ukaguzi ulibaini kuwa kati ya viashiria 24, ni viashiria vitano tu ndivyo vilitolewa kwa takwimu, sawa na viashiria vinne kwa mwaka 2016 na kiashiria kimoja kwa mwaka 2018. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa Wizara ya Afya haikutoa takwimu katika kiambatisho hicho kwa viashiria vilivyokosekana kwa kipindi cha ukaguzi.
- (d) Ukaguzi ulibaini kuwa katika sekta ya viwanda, uwekezaji na biashara, kiwango cha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu, kulikuwa na ongezeko kubwa la sehemu ya mauzo ya viwanda vya teknolojia za chini kutoka asilimia 1.02 hadi asilimia 9.62; mauzo ya viwanda vya teknolojia za kati kutoka asilimia 15.43 hadi 42.74; na mauzo ya viwanda vya teknolojia za juu kutoka asilimia 3.63 hadi 26.22. **Jedwali Na. 3.3** linaonesha kiwango cha utekelezaji wa kiashiria namba 9.3.1.

Jedwali Na. 3.2: Kiwango cha Utekelezaji wa Kiashiria namba 9.3.1

| Maelezo ya Kiashiria | Kiashiria cha Taifa | 2016 | 2017 | 2018 |
|--|--|-------|-------|-------|
| Uwiano wa viwanda vidogo katika jumla ya thamani ya viwanda vilivyoongezwa | Uwiano wa viwanda vidogo katika jumla ya thamani ya viwanda vilivyoongezwa | - | - | - |
| | Mpango wa II: Sehemu ya mauzo ya viwanda vya teknolojia za chini (%) | 1.02 | 0.92 | 9.62 |
| | Mpango wa II: Sehemu ya mauzo ya viwanda vya teknolojia za kati (%) | 15.43 | 10.64 | 42.74 |
| | Mpango wa II: Sehemu ya mauzo ya nje ya viwanda vya teknolojia za juu (%) | 3.63 | 6.02 | 26.22 |
| | Mpango wa II: Sehemu ya mauzo ya nje ya viwanda vya rasilimali (%) | 79.92 | 82.41 | 21.43 |

Chanzo: Kiambatisho kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu Mwaka 2021

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na uratibu usioridhisha kati ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuliosababisha kukosekana kwa taarifa kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ili kuhuisha kiambatisho cha takwimu za Malengo ya Maendeleo Endelevu. Matokeo yake, bado kuna taarifa zisizoridhisha za mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

(e) Kutofanya kazi kwa Mfumo wa Taifa wa Uratibu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mkakati wa ufuatiliaji na tathmini wa Mfumo wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano hutoa dira ya pamoja na uratibu wa jumla wa utekelezaji. Mipango hiyo inaeleza kwa pamoja jukumu na kutekeleza kazi kwa kuunganisha taasisi muhimu za utekelezaji za serikali na taasisi zisizo za serikali zinazounda ushirikiano ili kufikia malengo ya kipaumbele na matokeo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Taifa wa Uratibu uliandaliwa mwaka 2021 ili kuimarisha uratibu wa utekelezaji, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu. Licha ya kubuniwa kwa mfumo huo,

ukaguzi ulithibitisha kuwa haukufanya kazi kama ilivyokusudiwa. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa ripoti za mwaka za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Mapungufu haya yalitokana na utekelezaji usioridhisha wa kamati za ngazi za juu na Kamati ya Wataalamu.

(iv) Sababu za utekelezaji usioridhisha wa kufanikisha *Malengo ya Maendeleo Endelevu*

Ukaguzi ulibaini kuwa utekelezaji usioridhisha wa kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu ulisababishwa na ufuatiliaji usioridhisha wa mfumo wa uratibu wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango na OR-TAMISEMI kwenda ngazi za chini hivyo kuzuia ufuatiliaji na tathmini bora ya ajenda za kimataifa na kikanda. Pia, hali hiyo ilisababishwa na utekelezaji usioridhisha wa Mfumo wa Taifa wa Uratibu.

(v) Athari za utekelezaji duni wa ufanikishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Utekelezaji usioridhisha wa juhudi za kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu unaweza kusababisha kutofikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo mwaka 2030, mwaka uliowekwa kuwa ukomo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pia, kukosekana kwa uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu kunaweza kuleta athari katika kufanya maamuzi ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

3.4.1.3 Ukusanyaji Usioridhisha wa rasilimali-fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kwa mujibu wa mikakati ya Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Wizara ya Fedha na Mipango inatakiwa kuhakikisha inakusanya rasilimali-fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo. Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa ukusanyaji na matumizi yasiyoridhisha ya rasilimali-fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kama inavyofafanuliwa hapa chini.

(i) **Ukusanyaji usioridhisha wa rasilimali-fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu**

Wizara ya Fedha na Mipango ilitakiwa kuimarisha ukusanyaji wa kodi mbalimbali na kuweka mazingira ya kutambua vyanzo vipya vya mapato. Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango haikufanikiwa kukusanya rasilimali-fedha za kutosha kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mapitio ya Ripoti ya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yalibaini kuwa vyanzo vipya vya mapato vimefanikiwa kwa asilimia 19 tu kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 3.4** hapa chini.

Jedwali Na. 3.3: Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani katika Vyanzo Vipya

| Vyanzo vya Vipya | Lengo (Shilingi Bilioni) | Halisi (Shilingi Bilioni) | Tofauti | Asilimia ya Mafanikio (%) |
|---|--------------------------|---------------------------|---------------|---------------------------|
| Dhamana za Mamlaka za Serikali za Mitaa/Dhamana za Manispaa | 400 | 0 | 400 | 0 |
| Dhamana za Soko Huru | 3,450 | 0 | 3,450 | 0 |
| Ufadhili wa Mabadiliko ya Tabianchi | 699 | 27 | 671 | 4 |
| Ushiriki Binafsi wa Umma | 3,912 | 0 | 3,912 | 0 |
| Taasisi za Fedha za Maendeleo | 15,000 | | 15,000 | 0 |
| Mfuko wa Usawa wa Pensheni | 300 | 0 | 300 | 0 |
| Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa kutoka Nje | 29,565 | 8,437 | 21,127 | 40 |
| Jumla | 53,327 | 8,464 | 44,863 | 19 |

Chanzo: Ripoti ya Tathmini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Uchambuzi katika **Jedwali Na. 3.4** unaonesha kuwa, vyanzo viwili kati ya 7 vya ukusanyaji wa mapato vilifanikiwa kwa kiwango cha chini ya asilimia 50 wakati vyanzo vingine vilivyosalia havikufanikiwa na havikufanya makusanyo yoyote ya fedha sawa na asilimia sufuri.


(ii) **Utekelezaji usio wa ufanisi wa mapato ya ndani katika vyanzo vya vipya**

Wizara ya Fedha na Mipango ilipaswa kuanzisha na kuendeleza vyanzo vipya vya mapato ya ndani. Ukaguzi ulibaini kuwa vyanzo vipya vya mapato ya ndani vilivyoanzishwa ni pamoja na dhamana za manispaa, dhamana za

uraia na uhamiaji, dhamana za uhifadhi wa mazingira, ufadhili wa msongamano, miradi ya Mfuko wa Fedha, vyombo mbalimbali vya usawa, bima, na dhamana ya Kiislamu (Sukuk), na Mfuko wa Maliasili.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa vyanzo hivyo vipya vya mapato ya ndani havikuchangia chochote katika mapato licha ya kutajwa na kuanzishwa katika mikakati ya kifedha ya mipango ya maendeleo kama vyanzo vya mapato na mbadala wa mapato ya kodi. Hali hii ilitokana na ongezeko la mapato ya kodi kwenye bajeti ya taifa ikilinganishwa na vyanzo vingine vya mapato ya ndani kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 3.2** hapa chini.

Kielelezo Na. 3.2: Mchango wa Mapato ya Ndani na Kodi kwenye Bajeti ya Taifa



Chanzo: Mkaka Mapato Yasiyo ya Kodi Ut Mapato ya Kodi Mf Mikopo ya Ndani Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano


Kielelezo Na. 3.3 kinaonesha kuwa mapato ya kodi yaliongezeka kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2021/2022 huku vyanzo vingine vya mapato vikipungua kutoka asilimia 37 hadi asilimia 20 ya bajeti ya taifa. **Kielelezo Na. 3.3** kinaonesha pia kuwa vyanzo mbadala vya mapato kama vile hatifungani za manispaa vilikuwa na mchango mdogo wa mapato.

Ukaguzi ulipitia bajeti halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na kubaini kuwa

hatifungani za manispaa zilichangia asilimia sifuri katika bajeti kwa kipindi kilichotajwa hapo juu. Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na matumizi ya dhamana za manispaa hivyo kuthibitisha kuwa hazikuwahi kutoa dhamana hizo na hivyo kutochangia chochote katika bajeti za mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa.

Aidha, mkakati wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulionyesha kuwa na mchango mdogo kutoka vyanzo vya mapato ya ndani katika mamlaka za serikali za mitaa kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 3.4** hapa chini.

Kielelezo Na. 3.4: Ukusanyaji wa Mapato



Chanzo: *Mkakati wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano*

Kielelezo Na. 3.4 kinaonesha kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017, vyanzo vya mapato kutoka mamlaka za serikali za mitaa zimechangia si zaidi ya asilimia 10 ya pato la taifa. Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa kwa kipindi cha ukaguzi, si hati fungani za manispaa wala chanzo chochote mbadala cha mapato ya ndani kilichangia bajeti ya taifa. Ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbadala ulitarajiwa kuanza kutekelezwa katika bajeti ya kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024.

Katika mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa, ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati na hesabu zilizowasilishwa katika Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu vyanzo vya mapato na kubaini kuwa hakukuwa na utekelezaji na mchango wa vyanzo mbadala vya mapato ya ndani. Pia, vyanzo vya mapato vilibaki vilevile kwa kipindi kilichokuwa chini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

(iii) Ukusanyaji Usiojitosheleza wa rasilimali-fedha kwa ajili ya utoaji wa takwimu zinazohitajika kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mapitio ya mpango-mkakati wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu na uchambuzi wa utekelezaji yalibaini kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekuwa ikikabiliwa na uhaba wa rasilimali-fedha kwa ajili ya shughuli za kitakwimu kutokana na mikakati duni ya uanzishaji na ukusanyaji wa rasilimali-fedha. **Jedwali Na. 3.5** linaonesha kiasi cha rasilimali-fedha kilichopokelewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika kipindi cha kuazia mwaka 2016/17 hadi 2021/22.

Jedwali Na. 3.4: Uchambuzi wa Bajeti Iliyoidhinishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Bajeti Halisi Zilizotolewa

| Miaka ya Fedha | Bajeti Iliyoidhinishwa (Shilingi) | Bajeti Halisi (Shilingi) | Asilimia ya Bajeti Iliyopokelewa |
|----------------|-----------------------------------|--------------------------|----------------------------------|
| 2016/17 | 8,544,375,000.00 | 5,541,584,000.00 | 65 |
| 2017/18 | 6,263,246,000.00 | 5,772,657,200.00 | 92 |
| 2018/19 | 6,243,023,000.00 | 5,623,664,808.50 | 90 |
| 2019/20 | 6,395,150,000.00 | 5,994,704,752.44 | 93 |
| 2020/21 | 6,597,304,656.00 | 6,007,969,852.08 | 91 |
| 2021/22 | 10,117,748,000.00 | 8,719,715,928.38 | 86 |

Chanzo: Uchambuzi wa Ukaguzi wa Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati kwa Kipindi cha kuanzia Mwaka 2016/2017 hadi 2021/2022

Jedwali Na. 3.5 linaonesha kuwa, kiasi halisi cha fedha za bajeti kilichopokelewa hakikuwa asilimia 100 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2020/21. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2021/22 ukusanyaji wa rasilimali-fedha ulikuwa mdogo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2020/21 kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipokea asilimia 86 tu ya bajeti yake iliyoidhinishwa. Hata hivyo, bajeti iliyoidhinishwa ilikuwa kubwa kuliko miaka mingine ya fedha kutokana na zoezi la sensa lililofanyika mwaka 2022.

(iv) Sababu za ukusanyaji Usioridhisha wa rasilimali-fedha

Ukaguzi ulibaini kuwa uhaba wa ukusanyaji wa rasilimali-fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ulisababishwa na kupokea kutoka Wizara ya Fedha na Mipango rasilimali-fedha pungufu ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti. Hata hivyo, upungufu huu wa utoaji wa fedha haikuwa kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu pekee bali kwa serikali nzima. Pia, ukaguzi ulibaini kukosekana kwa mchango wa vyanzo vipya vya mapato hivyo kusababisha utegemezi wa bajeti kwenye mikopo ya nje. Hali hii ilisababisha kuongezeko kwa deni la taifa na kuwa na kasi ndogo ya ulipaji wa deni.

(v) Athari za ukusanyaji Usioridhisha wa rasilimali-fedha

Ukaguzi ulibaini kuwa ukusanyaji usioridhisha wa rasilimali-fedha uliathiri utekelezaji wa shughuli za kitakwimu katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikiwa pamoja na uandaaji wa takwimu zinazohitajika kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pia, hii iliathiri kasi ya kuongeza utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi za chini kutokana na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato.

3.4.1.4 Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa Mwenendo wa Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi ulibaini kuwa ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu haukufanyika kwa ufanisi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

(i) Ufuatiliaji Usiojitosheleza wa takwimu za maendeleo

Kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Ufuatiliaji na Tathmini wa Mwaka 2016/17 - 2020/21 na 2020/21- 2025/2026 mtawalia Wizara ya Fedha na Mipango ilipewa jukumu na mamlaka ya kufuatilia mwenendo na kuonesha matokeo kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pamoja na kufanya ufuatiliaji wa kila siku kwa mujibu wa mwongozo wa ushirikiano wa sera na upatikanaji wa taarifa ili kusaidia sekta za wizara, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango haikufuatilia mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo

Endelevu. Hali hii ilithibitishwa na kukosekana kwa ripoti za maendeleo kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Aidha, mapitio ya Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2021/22 yalibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango haikutenga fedha kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu ingawa shughuli hiyo iliingizwa na kupewa kifungu namba CO3SO1 katika Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati husika bila kupangiwa kiwango cha fedha kinachohitajika.

Ukaguzi ulibaini zaidi kwamba, Wizara ya Fedha na Mipango ilipokuwa ikifuatilia utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, hakukuwa na maendeleo ya teknolojia ambayo yalitumika. Ukaguzi ulibaini kuwa, sekta za wizara zilikuwa zikituma ripoti za maendeleo kwa mikono kwani hakukuwa na mfumo ambao sekta za wizara zingeweza kuelekeza ripoti zao za maendeleo kielekitroniki. Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2020/21, Wizara ya Fedha na Mipango haikuwa na idara maalumu iliyokuwa na jukumu la kufuatilia shughuli za utekelezaji wa shughuli za wizara hadi mwaka wa fedha 2021/22 muundo mpya wa wizara ulipoidhinishwa na kuanzisha idara maalumu ya ufuatiliaji na tathmini. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa, idara hiyo ilikuwa na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa miradi tu.

Hadi wakati wa ukaguzi huu, Wizara ya Fedha na Mipango ilikuwa haijafanya ufuatiliaji na tathmini kamili wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kutokana na ukosefu wa uwezo hususani uhaba wa rasilimali-watu na ujuzi unaohitajika.

(ii) Kuchelewa kufanyika kwa tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Mapitio ya ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yalibaini kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa ripoti ya mwisho ya tathmini kwa kukasimisha jukumu hilo kwa Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii, na ripoti hiyo iliandaliwa mwezi Machi 2021 ambapo ni mwishoni mwa utekelezaji wa Mpango husika. Hali hii inamaanisha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ilishindwa kufanya tathmini hiyo katikati ya muhula wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, yaani baada ya miaka miwili na nusu ya utekelezaji wake kama ilivyopaswa.

Hali hii ilisababishwa, kwa kiasi kikubwa, na uamuzi wa kuivunja Tume ya Mipango na kuifanya kuwa idara ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kuvunjwa kwa Tume ya Mipango kulivuruga maandalizi ya tathmini hiyo kutokana na ukweli kwamba katika muundo wa awali wa Wizara ya Fedha na Mipango, hakukuwa na mgawanyiko unaofaa wa kazi hiyo. Pia, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ucheleweshaji wa idhini ya mabadiliko ya muundo wa Wizata kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 ili kuchukua tume ya mipango kama idara ya wizara.

Kwa hiyo, kuchelewa kwa utekelezaji wa tathmini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kulizuia utoaji wa taswira ya mwenendo wa utendaji ambao Wizara ilipaswa kufuatilia na kutambua malengo ya Mpango ambayo yalikuwa nyuma ya ratiba ya utekelezaji.

(iii) Uhaba wa takwimu za kawaida za ubora na muundo wa uwiano kwa takwimu za maendeleo

Ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu inakusanya takwimu bora kwa asilimia 39 ya takwimu zinazohitajika kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Asilimia 61 iliyobaki ni takwimu za kiutawala. Ili kuongeza asilimia 39 zilizokusanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, takwimu zingine zilitarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya kiutawala vikiwemo OR-TAMISEMI na sekta za wizara na taasisi kwa kushirikiana na wazalishaji wengine wa takwimu.

Ukaguzi ulibaini kuwa vyanzo vya utawala vilikuwa na uwezo mdogo wa kutoa asilimia 61 za kuongeza asilimia 39 za Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Ukaguzi ulibaini pia kuwa, Kitengo cha Takwimu cha OR-TAMISEMI kilicho chini ya Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini, kiliweza kukusanya takwimu za kutosha katika sekta tatu tu, ambazo ni elimu, afya na kilimo, sawa na asilimia 10 ya sekta zote 30 zilizoainishwa nchini. Takwimu zingine zilipatikana nje ya mfumo lakini zinaweza kukusanywa kwa mikono wakati zikihitajika. Ukweli ni kwamba, takwimu zingine hazikufuatiliwa kutoka ngazi za chini na kufanya ukusanyaji wa takwimu hizo kuwa mgumu pale zinapohitajika.

Ukaguzi huu pia ulibaini zaidi kuwa kulikuwa na uwianishaji usiojitosheleza wa takwimu kwa ajili ya utoaji wa taarifa za utekelezaji kutoka taasisi za utekelezaji kama inavyohibitishwa na mapitio ya orodha ya viashiria vya lengo 9.3, ambapo Wizara inayohusika ya Viwanda, Biashara, na Uwekezaji

iliripoti takwimu tofauti na za Ofisi ya Taifa ya Takwimu na walitumia mizania tofauti. Kwa mfano, sehemu ya ajira za sekta ya viwanda kwa jumla ya ajira na mikopo kwa sekta binafsi kama sehemu ya pato la taifa, takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu ziliwasilishwa kwa asilimia, wakati takwimu kutoka wizara yenye dhamana ziliwasilishwa kwa tarakimu.

(iv) Athari za ufuatiliaji usiojitosheleza wa mwenendo wa utekelezaji katika kufikia Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano

Mapungufu yaliyoonekana kuhusu utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu yanaashiria changamoto katika kujumuisha na kuwezesha Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano; tathmini na ufuatiliaji wa takwimu za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu; na ukusanyaji wa rasilimali-fedha ili kuwezesha utekelezaji wa Malengo ya Malengo Endelevu. Matokeo haya yalionekana kuathiri mafanikio ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano.

Kwa kutambua utekelezaji madhubuti wa hatua zilizopewa kipaumbele katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ilipaswa kuhamasisha ukusanyaji wa rasilimali mbalimbali za fedha kutoka taasisi binafsi au taasisi za umma. Hata hivyo, ukusanyaji hafifu wa rasilimali kama nyenzo mbadala ya fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa Malengo ya Malengo Endelevu kulisababisha kasi ndogo ya utekelezaji wa Malengo kwani sasa imebaki miaka saba tu kabla ya muda wa utekelezaji wa malengo hayo ufikie tamati mwaka 2030.

Kwa hiyo, uzalishaji wa takwimu usioridhisha; na uratibu na ushirikiano kati ya taasisi za utekelezaji na wadau usiojitosheleza kutasababisha kuwepo kwa kiwango cha chini cha utekelezaji wa malengo yote 17 ifikapo mwaka 2030. Hali hii ina athari za moja kwa moja kwa mafanikio ya hatua za Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano hususani kwa kuzingatia kanuni za ufanisi, tija na wekevu. Hali hii inaweza pia kuhatarisha mafanikio ya mikakati na nguzo kuu za Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambazo ni viwanda, maendeleo ya binadamu, na ufanisi wa utekelezaji.

3.5 Hitimisho Mahususi la Ukaguzi

Kwa ujumla, ukaguzi unahitimisha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazikuongoza ipasavyo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi za chini za Serikali ili kuimarisha hali bora na endelevu ya maisha ya jamii nchini.

Mapungufu katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ulithibitishwa na uratibu, ushirikiano, na mawasiliano usiridhisha baina ya wadau wa utekelezaji. Kushindwa kuongoza ipasavyo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu katika ngazi za chini za Serikali kulisababisha kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa utekelezaji usioridhisha wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ulitokana na kushindwa kujumuisha vizuri Malengo ya Maendeleo Endelevu katika mifumo ya mipango na sera ya kitaifa; utoaji usioridhisha wa takwimu zinazohitajika kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu; ukusanyaji usioridhisha wa rasilimali-fedha zinazohitajika ili kuinua utekelezaji; na upotoshaji wa shughuli zinazopewa kipaumbele na mashirika ya utekelezaji. Sababu nyingine ni kukosekana kwa ushirikiano na mawasiliano ya kutosha katika utoaji wa takwimu hivyo kusababisha ufuatiliaji duni wa mwenendo wa utekelezaji kutoka ngazi za chini za serikali na wizara za kisekta, ili kuhakikisha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu unazingatia kanuni za ufanisi, tija na wekevu.

USIMAMIZI WA MIFUMO YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA

SURA YA NNE

4



USIMAMIZI WA MIFUMO YA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA

4.1 Utangulizi

Sekta ya afya ni muhimu kwa maendeleo ya binadamu. Sekta hiyo inajumuisha miundombinu, wataalamu, vifaatiba, vitendanishi, dawa, huduma za kinga na matibabu, na bima ya afya. Serikali ililenga kufikisha huduma muhimu za afya na kukidhi mahitaji ya wananchi wote, kuzingatia viwango vya ubora, na kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia taarifa zenye ushahidi kupitia mifumo thabiti ya afya.

Sura hii inawasilisha matokeo ya msingi ya ukaguzi yanayotokana na taarifa za ukaguzi wa ufanisi kuhusu usimamizi wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya pamoja na udhibiti wa vyanzo vya mionzi nchini. Taarifa hizi za ukaguzi wa ufanisi ni pamoja na:

- (a) Ukaguzi wa ufanisi katika udhibiti wa utoaji wa huduma za afya kwenye vituo binafsi vya afya;
- (b) Ukaguzi wa ufanisi kuhusu udhibiti wa malipo yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa vituo vya huduma za afya; na
- (c) Ukaguzi wa ufanisi kuhusu udhibiti wa vyanzo vya mionzi

4.2 Usuli

Vituo binafsi na hiari vya afya vina jukumu kubwa katika utoaji wa huduma za afya katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Zaidi ya asilimia 40 ya huduma za afya nchini hutolewa na sekta binafsi kupitia hospitali zaidi ya 2,000; vituo vya afya, zahanati, na maduka ya dawa 900; na zaidi ya vituo 8,000 vilivyoidhinishwa kutoa huduma za dawa nchini. Hivyo, udhibiti wa utoaji wa huduma za afya zinazotolewa na vituo binafsi na hiari nchini ni muhimu.

Kwa upande mwingine, ugharamiaji wa huduma za afya hufanyika kupitia mbinu mbalimbali, mojawapo ikiwa bima ya afya. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilikuwa 4,734,388 sawa na asilimia 8 ya Watanzania wote. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya shilingi bilioni 551.51 zilidaiwa na vituo vya afya ambapo, kiasi kilicholipwa ni shilingi bilioni 515.00 sawa na asilimia

93.38 ya madai yaliyowasilishwa kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya huku madai ya thamani ya shilingi bilioni 32.5 sawa na asilimia 5.89 yakikataliwa.⁴ Hivyo, tathmini ya ufanisi wa udhibiti wa utoaji wa huduma za afya kwa walengwa wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na uchakataji wa madai yanayotolewa na vituo vya afya ni muhimu.

Aidha, ongezeko kubwa la matumizi ya vyanzo vya mionzi nchini limeleta haja ya kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mionzi na kuhakikisha kuwa kiwango cha mionzi kinabaki katika hali isiyo na madhara kwa binadamu na mazingira.

4.3 Uhusiano kati ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Usimamizi wa Mifumo ya Utoaji wa Huduma za Afya

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unalenga kuimarisha mifumo ya usimamizi wa utoaji na upatikanaji wa huduma za afya. Mpango huo unatoa kipaumbele katika utatuzi wa changamoto za ubora katika huduma za afya. Vipaumbele muhimu vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na hatua endelevu za serikali kwa vituo vya afya ni kujenga na kukarabati vituo vya afya jumuishi; kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaatiba, vitendanishi, chanjo; na usanifu na kuwa na vifaatiba sahihi na uhifadhi wa bidhaa za matibabu.

Chini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali ina mkakati wa kukuza na kupanua wigo na mawanda ya utoaji huduma ya bima ya afya nchini. Pia, katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unalenga kudhibiti vyanzo vya mionzi, serikali imeweka hatua za kuchukua ili kukuza nishati ya atomiki na teknolojia ya nyuklia kwenye sekta ya viwanda. **Jedwali Na. 4.1** linaonesha uhusiano baina ya maeneo yaliyokaguliwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Jedwali Na. 4.1: Uhusiano wa Maeneo Yaliyokaguliwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

| Eneo Lililokaguliwa | Maeneo Muhimu ya Kipaumbele katika Mpango wa III | Hatua Muhimu |
|---------------------|--|---|
| Vituo vya Afya | Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Upatikanaji na Utoaji wa Huduma za Afya; | Ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya jumuishi; kubuni na kuanzisha vifaatiba |

⁴ Ripoti ya Utendaji Kazi wa Mwaka 2020/21

| Eneo Lililokaguliwa | Maeneo Muhimu ya Kipaumbele katika Mpango wa III | Hatua Muhimu |
|-------------------------------|---|--|
| | na Utatuzi wa Changamoto za Ubora katika Huduma za Afya | sahihi na uhifadhi wa bidhaa za matibabu; na kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaatiba, vitendanishi, na chanjo |
| Bima ya afya | | Kupanua wigo na mawanda ya huduma ya bima ya afya, pamoja |
| Udhibiti wa vyanzo vya Mionzi | Viwanda na Utoaji wa Huduma - Viwanda | Kukuza na kuendeleza matumizi salama ya nishati ya atomiki na teknolojia ya nyuklia |

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2020/21 - 2025/26)

Aidha, lengo la 3 la Malengo 17 ya Umoja wa Mataifa kwa Mwaka 2030 na ni **“Kuhakikisha afya bora na ustawi kwa watu wote na rika zote”**. Taarifa za ukaguzi wa ufanisi zilizowasilishwa katika sura hii zinashughulikia sekta ya afya hususani lengo dogo la 3.8 linataka serikali kufikia lengo la afya kwa wote, upatikanaji wa huduma bora muhimu za afya, na upatikanaji wa dawa za bei nafuu na chanjo kwa wote. Pia, ukaguzi ulilenga lengo dogo la 3.9 linaloitaka serikali kupunguza, kwa kiasi kikubwa, idadi ya vifo na magonjwa yanayotokana na kemikali hatarishi na hewa, na uchafuzi wa maji na udongo ifikapo mwaka 2030.

4.4 Mikakati na Jitihada za Serikali katika Usimamizi wa Mifumo ya Utoaji na Upatikanaji wa Huduma za Afya

Katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali imeweka jitihada za kukabiliana na changamoto ya ubora katika utoaji wa huduma za afya ambapo ni pamoja na kuongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini kutoka vituo 7,014 mwaka 2015 hadi vituo 8,783 Desemba 2020. Orodha ya vituo vya kutolea huduma za afya ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kufikia Juni 2022 ilionesha kuwa kulikuwa na zahanati 6,554, vituo vya afya 909, hospitali za wilaya 311, hospitali 74 za rufaa za mikoa na hospitali 18 za rufaa za kanda zilizosajiliwa na Mfuko huo nchini.

Mapitio ya Ripoti ya Tathmini ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ya Machi 2021 inabainisha kuwa, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2019, Serikali iliboresha upatikanaji wa huduma za afya ya msingi kupitia watumishi wapya wa afya waliopatiwa mafunzo takribani 6,180 kati ya 7,680 waliopelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya za msingi. Kati ya mwaka 2016/2017 na 2019/2020, Serikali imeajiri watumishi wa afya zaidi ya 11,832.

Pia, hadi kufikia mwezi Machi 2019, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulikuwa umesajili wanufaika 4,217,211, sawa na asilimia 8 ya Watanzania. Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imeongezeka kutoka 753,892 mwaka 2016/17 hadi 858,446 mwaka 2017/18 na 966,792 kufikia mwaka 2018/2019. Wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya walikuwa sawa na asilimia 7.4 ya Watanzania wote, wakati wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii walikuwa asilimia 23.6 ya Watanzania wote. Hadi kufikia mwaka 2019, Mfuko wa Afya ya Jamii ulikuwa na wanufaika 13,029,636 sawa na asilimia 25 ya Watanzania. Hivyo, kati ya mwaka 2015 na 2019, jumla ya wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii iliongezeka kutoka asilimia 20 hadi 33. Hata hivyo, ongezeko la wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii halikufikia lengo la asilimia 50 la Mpango wa Bima ya Afya ifikapo mwaka 2020.

Kwa upande mwingine, ili kuimarisha mifumo ya usimamizi wa afya na kufikia malengo ya sekta ya afya nchini, Serikali kupitia mikakati ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, iliweka viashiria vya mpango wa upatikanaji wa bima ya afya, ambapo kwa kipindi cha mwaka 2019/20 lengo lilikuwa kufikia asilimia 50, na asilimia 80 kufikia mwaka 2025/26. Vilevile, lengo la asilimia ya matumizi ya serikali kwenye sekta ya afya kwa kipindi cha mwaka 2019/20 lilikuwa kufikia asilimia 10 na hatimaye asilimia 12.2 ya bajeti yake mwaka wa fedha 2025/26.

Aidha, Serikali imechukua hatua ya kushughulikia changamoto ya wigo mdogo kwenye utoaji wa huduma ya bima ya afya ya taifa, ambapo iliidhinisha Muswada wa Sheria ya Uanzishaji wa Bima ya Afya kwa Wote na kusomwa kwa mara ya kwanza kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Septemba 2022 kabla ya kutungwa. Kuidhinishwa kwa Sheria hii kunatarajiwa kupanua wigo wa uanachama katika mfumo wa bima ya afya kwa kuzingatia kuwapo kwa makundi mbalimbali ya wanachama kutoka sekta zote za uchumi.

Aidha, katika kukuza na kudhibiti vyanzo vya mionzi, serikali imeboresha ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) ambalo liliboresha utekelezaji wa miradi kama vile uimarishaji na utekelezaji wa mradi wa kudhibiti saratani, uanzishaji wa mafunzo ya sayansi ya ujuzi wa mionzi kwenye Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela na ujenzi wa kituo cha unururishaji kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Nishati ya Nguvu za Atomiki.

4.5 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi huu ulikuwa na malengo mahususi na ulifanyika kwa kuzingatia mawanda maalumu kama inavyoelezwa hapa chini.

4.5.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu lilikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania wamesimamia ipasavyo utoaji wa huduma za afya; uzingatiaji wa udhibiti wa vituo vya kutolea huduma za afya kulingana na taratibu na viwango vilivyowekwa; uchakataji wa madai ya vituo vya afya ili kulinda afya za watu; na udhibiti madhubuti katika vyanzo vya mionzi.

Hususan, ukaguzi ulitathmini iwapo:

- (i) Wizara ya Afya ilikuwa na utaratibu madhubuti na mfumo bora wa usimamizi wa udhibiti wa utoaji wa huduma za afya zinazotolewa na vituo binafsi na hiari nchini;
- (ii) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeweka utaratibu madhubuti wa udhibiti wa uchakataji wa malipo ya madai ya vituo vya huduma za afya ili kuhakiki uhalisi, usahihi na ukamilifu wake; na
- (iii) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, inahakikisha udhibiti mzuri wa vyanzo vya mionzi nchini ili kupunguza hatari kwa watumiaji, umma na mazingira.

4.5.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi huu ulihusisha taasisi kuu nne ambazo ni Wizara ya Afya; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania; na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Ukaguzi ulijikita zaidi katika hatua zilizochukuliwa na Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa vituo binafsi na hiari vya afya vinatoa huduma bora za afya.

Aidha, ukaguzi ulilenga kutathmini udhibiti katika uchakataji na malipo ya madai ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya baada ya vituo vya afya kutoa huduma za afya kwa walengwa wanaostahili. Katika kipengele hiki, ukaguzi ulijikita katika kuangalia kiwango cha uzingatiaji wa makubaliano ya utekelezaji wa mwongozo wa viwango vya matibabu na mikataba kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na vituo vya kutolea huduma za afya nchini; utaratibu wa udhibiti wa madai kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuhakikisha kuwa madai halisi yanaidhinishwa kwa malipo; kuchukua hatua stahiki juu ya madai yasiyoidhinishwa ili kupunguza upotevu wa fedha; na ufuatiliaji na tathmini ya uandaaji wa madai.

Aidha, ukaguzi ulilenga hali ya ufanisi wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika kudhibiti vyanzo vya mionzi nchini. Katika eneo hili, ukaguzi ulijikita katika kuwapo kwa taratibu za utendaji kazi wa udhibiti wa vyanzo vya mionzi; utoshelevu wa ufuatiliaji wa vyanzo vya mionzi; na ufanisi wa taratibu kati ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania na wadau wengine katika kudhibiti vyanzo vya mionzi. Pia, ukaguzi ulitathmini ufanisi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kufuatilia utendaji wake na ule wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kuhusiana na udhibiti wa vyanzo vya mionzi.



Kaguzi zote tatu zilikusanya taarifa katika kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/22. Kipindi hiki kilizingatia mwenendo wa utendaji wa wizara na taasisi zilizokaguliwa na kwa kuzingatia maeneo ya ukaguzi yaliyoangaziwa.

4.6 Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya jumla ya ukaguzi yatokanayo na taarifa za ukaguzi wa ufanisi kuhusu udhibiti wa utoaji wa huduma za afya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya binafsi na hiari; ukaguzi wa ufanisi kuhusu udhibiti wa malipo yanayofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwenda katika vituo vya afya vilivyoidhinishwa; na ukaguzi wa ufanisi kuhusu udhibiti wa vyanzo vya mionzi.

Ukaguzi ulibaini upungufu katika shughuli za Wizara ya Afya katika kusimamia vituo binafsi na hiari vya afya. Pia, umebaini upungufu katika udhibiti uliowekwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wakati wa utoaji wa huduma za afya na uchakataji wa madai yanayotolewa na vituo vya afya. Aidha, mapungufu yalibainika katika udhibiti wa vyanzo vya mionzi unaotekelezwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

4.6.1 Mapungufu katika udhibiti wa utoaji wa huduma za afya kwenye vituo binafsi na hiari vya huduma za afya


Tangu mwaka 1977, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya jitihada kubwa za kuboresha utendaji wa vituo vya huduma za afya vya umma na binafsi. Wizara ya Afya imeweka jitihada za kuboresha mfumo wa udhibiti wa vituo binafsi vya afya nchini kwa kuandaa na kuanzisha sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu mbalimbali katika udhibiti wa vituo hivi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

4.6.1.1 Huduma za afya zinazotolewa na vituo binafsi na hiari kutokidhi viwango vya ubora

Wizara ya Afya ililenga kuwa na angalau asilimia 95 ya vituo vya huduma za afya vyenye kukidhi kiwango cha ubora cha nyota tatu na zaidi katika utoaji wa huduma za afya hadi kufika mwezi Juni mwaka 2021. Nyota hutumika kama kipimo cha viwango vya ubora wa utoaji wa huduma za afya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Vigezo vikuu vinavyozingatiwa katika upimaji wa viwango vya ubora wa huduma zitolewazo na vituo vya kutolea huduma za afya ni pamoja na kuzuia na kudhibiti maambukizi; ushughulikiaji wa wagonjwa wa dharura na mfumo wa rufaa; huduma za kitabibu; miundombinu ya vituo vya afya; matumizi ya takwimu za vituo vy kutolea huduma za afya kwa ajili ya uboreshaji wa mipango ya utoaji wa huduma za afya; tathmini ya utendaji kazi; na uwajibikaji kwa jamii katika ngazi ya vituo vya afya.

Ukaguzi huu ulichambua ukadiriaji wa nyota wa vituo kibinafsi 514 ili kubaini ubora wa huduma za afya, ambapo ilibainika kuwa ni asilimia 18 tu ndio vilipata kiwango cha nyota tatu na zaidi hadi kufikia mwezi Juni 2022 kama ilivyooneshwa katika **Kielelezo Na. 4.1**.

Kielelezo Na. 4.1: Ukadiriaji wa Nyota wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya




Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Tatu ya Ukadiriaji wa Nyota ya Mwaka 2021

Uchambuzi wa **Kielelezo Na. 4.1** unaonesha kuwa, asilimia 82 ya vituo binafsi vya huduma za afya vilivyopimwa vilikuwa na kiwango cha ubora chini ya nyota tatu, hivyo kutofikia kiwango cha chini kinachohitajika.

Uchambuzi zaidi kuhusu ukadiriaji wa nyota wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya kwa kuzingatia ngazi ya kituo ulionyesha kuwa, asilimia 88 ya zahanati zilikuwa chini ya ubora wa nyota 3; asilimia 77 ya vituo vya afya vilikuwa chini ya ubora wa nyota 3; na asilimia 44 ya hospitali zilikuwa chini ya ubora wa nyota 3 kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 4.2**.

Kielelezo 4.2: Ukadiriaji wa Nyota wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya kwa Kuzingatia Ngazi ya Kituo (Zahanati, Kituo cha Afya, na Hospitali)



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Ukadiriaji wa Nyota Tatu wa Ubora wa Utoaji Huduma za Afya ya Mwaka 2021

Uchambuzi wa **Kielelezo Na. 4.2** unaonesha kuwa, wakati wa awamu ya tatu ya tathmini ya ubora wa huduma za afya, zahanati zilikuwa na ubora duni ikilinganishwa na vituo vya afya na hospitali. Mapitio ya ukaguzi wa ripoti ya tathmini ya ukadiriaji wa nyota za ubora wa utoaji wa huduma za afya yalibaini kuwa, ukadiriaji wa chini ya kiwango stahiki ulichangiwa zaidi na utekelezaji duni wa baadhi ya vigezo vya ubora wa utaoaji wa huduma za afya hususani, huduma za kitabibu, huduma za dawa, na huduma za maabara.

Ukaguzi ulibaini mapungufu ya ubora wa huduma za afya katika maeneo yafuatayo:

(i) Huduma za dawa zisizotosheleza

Ukaguzi ilibaini kuwa, asilimia 84 ya vituo vya afya 132 vilivyotembelewa vilikuwa na mapungufu katika utoaji wa huduma za dawa. Maduka yote ya dawa yaliyoambatanishwa katika vituo binafsi vya huduma za afya vilivyotembelewa kwenye halmashauri sita za Igunga, Kongwa, Misungwi, Nyasa, Songea, na Tabora yalikuwa na mapungufu kama vile kutokuwa na watumishi wenye sifa, kutosajiliwa, kutokuwa na maeneo yaliyotengwa

maalumu kwa kutolea dawa, na utunzaji funi wa dawa zilizokwisha muda wa matumizi na zile ambazo bado zilikwa ndani ya muda wa matumizi.

(ii) Mapungufu katika utoaji wa huduma za maabara

Ukaguzi ulibaini kuwa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya katika mikoa iliyotembelewa vilikuwa na idadi kubwa ya maabara zilizoambatanishwa kwenye vituo hivyo vilizokuwa na mapungufu kama vile kutosajiliwa na kuwapo kwa watumishi wasiokidhi vigezo. Mathalani, Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa na idadi kubwa (95%) ya maabara zenye mapungufu hayo. Kwa ujumla, maabara zote zilizotembelewa kwenye halmashauri za Moshi, Mwanza, Misungwi, Kongwa, Igunga na Nyasa zilibainika kuwa na mapungufu yanayofanana kama vile kuwapo kwa maabara zisizosajiliwa, kutohuishwa kwa leseni za maabara, na kuwapo kwa watumishi wa maabara wasio na sifa. Kwa upande mwingine, mkoa wa Mbeya ulikuwa na idadi ndogo ya maabara zilizoambatanishwa kwenye vituo binafsi vya kutolea huduma za afya zilizokuwa na mapungufu.

(iii) Upungufu wa watumishi wenye sifa kwenye vituo binafsi na hiari vya kutolea huduma za afya



Ukaguzi ilibaini kuwa kulikuwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa afya katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya. Upungufu huo ulikuwa kati ya asilimia 84 hadi 87. Hospitali zilikuwa na kiwango kikubwa cha upungufu kwa asilimia 87, zikifuatiwa na vituo vya afya na zahanati zilizokuwa na upungufu wa asilimia 86.

Vituo vyote binafsi na hiari vya huduma za afya vilivyotembelewa vilikuwa na idadi ndogo ya watumishi chini ya kiwango kinachoruhusiwa. Idadi ya vituo vya huduma za afya vilivyokuwa na watumishi pungufu vilikuwa kati ya asilimia 50 na 100. Mathalani, asilimia 50 ya vituo binafsi na hiari vya afya vilivyotembelewa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Moshi vilikuwa na upungufu wa watumishi wa afya, huku vituo vyote vya huduma za afya vilivyotembelewa kwenye halmashauri 11 vingine vikiwa na upungufu wa rasilimali-watu kwa ajili ya afya.

Ukaguzi ulichambua sababu kuu tano za upungufu wa usimamizi wa udhibiti katika utoaji wa huduma bora za afya katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya. Sababu hizo ni:

-
- Usajili usio na tija wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya;
 - Usimamizi usioridhisha wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya;
 - Ukaguzi usioridhisha wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya;
 - Udhibiti usioridhisha wa bei za huduma za matibabu zinazotolewa na vituo binafsi na hiari vya huduma za afya; na
 - Ukaguzi usioridhisha wa kliniki katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya.

Sababu hizi kuu tano za mapungufu katika utoaji wa huduma bora za afya kwenye vituo binafsi na hiari vya utoaji wa huduma za afya zinafananuliwa hapa chini.

(a) Usajili usio na tija wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya

Ukaguzi ulibaini kuwa usajili wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya ulikuwa na mapungufu yafuatayo:


- ***Baadhi ya vituo binafsi na hiari vya huduma za afya vilivyotuma maombi ya usajili kutopata usajili***

Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya ilisajili kati ya asilimia 19 na 87 ya vituo binafsi vya afya vilivyoomba usajili. Ukaguzi ulibaini kuwa sababu ya usajili mdogo wa vituo vya huduma za afya katika kipindi cha mwaka 2018/2019 ni vituo kutokidhi mahitaji ya msingi ya usajili wa vituo vya huduma za afya kama vile miundombinu, zana na vifaatiba, na rasilimali-watu.

- ***Muda unaotumika kusajili vituo binafsi na hiari vya huduma za afya***

Ukaguzi ulibaini kuwa, ili kukamilisha usajili wa kituo binafsi cha huduma za afya, ilichukua wastani wa siku 389 kwa Mkoa wa Kilimanjaro; siku 319 kwa Mkoa wa Mbeya; siku 288 kwa Mkoa wa Ruvuma; siku 270 kwa Mkoa wa Tabora; siku 269 kwa Mkoa wa Dodoma; siku 255 kwa Mkoa wa Mwanza; na siku 191 kwa Mkoa wa Dar es Salaam. **Kielelezo Na. 4.3** kinaonesha mchanganuo wa wastani wa muda uliotumika kusajili vituo binafsi na hiari vya afya kimkoa.

Kielelezo Na. 4.3: Wastani wa Muda Uliotumika Kusajili Vituo Binafsi na Hiari vya Afya Kimkoa




Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu za Usajili za Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Afya Mwaka 2022

Kielelezo Na. 4.3 kinaonesha kuwa wastani wa muda mrefu zaidi wa siku 389 ulitumika kusajili vituo binafsi na hiari vya afya katika Mkoa wa Kilimanjaro, huku wastani mdogo wa muda wa kusajili vituo binafsi vya huduma za afya ulikuwa Mkoa wa Dar es Salaam.

▪ ***Muda unaotumika kusajili maabara binafsi na hiari za afya***

Ukaguzi ulibaini kuwa, wastani wa muda wa kusajili maabara binafsi na hiari za afya ulikuwa siku 438 kwa Mkoa wa Kilimanjaro; siku 489 kwa Mkoa wa Mwanza; siku 359 kwa Mkoa wa Mbeya; siku 337 kwa Mkoa wa Dar es Salaam; na siku 265 kwa Mkoa wa Dodoma kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 4.4**.

Kielelezo Na. 4.4: Wastani wa Muda Uliotumika Kusajili Maabara Binafsi na Hiari za Afya Kimkoa



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Usajili za Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Afya Miaka 2016/17- 2021/22

Kielelezo Na. 4.4 kinaonesha kuwa muda mfupi zaidi uliotumika kusajili maabara binafsi ya huduma za afya ulikuwa katika Mkoa wa Dodoma ambao ni siku 265; na wastani mrefu zaidi wa siku 489 ulitumika katika Mkoa wa Mwanza.

Ukaguzi ulibaini kuwa sababu za muda wa usajili kutofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine ni kutokuwapo kwa mwongozo wa muda maalumu kwa ajili ya usajili, kukosekana kwa mkataba wa huduma kwa mteja, na mfumo duni wa usajili.

- ***Usimamizi usioridhisha wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya***

Ukaguzi ulibaini kuwa usimamizi shirikishi wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya haukufanyika ipasavyo. Zaidi, ilibainika kuwa, timu za usimamizi wa afya za halmashauri hazikufikia malengo ya usimamizi shirikishi wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya katika halmashauri 14 zilizotembelewa. Kwa ujumla, timu za usimamizi wa afya za halmashauri zilitekeleza majukumu yake kwa wastani wa asilimia 15.3 ya usimamizi uliopangwa kusaidia vituo binafsi na hiari vya huduma za afya kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/22.

- ***Usimamizi shirikishi usiojitosheleza wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya***

Ukaguzi ulibaini mapungufu katika mipango ya usimamizi shirikishi katika ngazi ya serikali za mitaa nchini, ambapo kati ya halmashauri 14 zilizofikiwa na ukaguzi huu, 6 hazikuwa na mpango wa bajeti wa usimamizi shirikishi wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya kwa kipindi cha miaka 6 kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22, Halmashauri hizo ni Moshi, Misungwi, Mbeya Jiji, Mwanza Jiji, Kyela, na Ilala.

Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya haikutenga asilimia 10 ya mapato yatoanayo na makusanyo ya ada kwenda kwa timu za usimamizi wa afya za halmashauri kwa ajili ya kutekeleza usimamizi shirikishi kwenye vituo binafsi na hiari vya huduma za afya. Kwa kipindi cha miaka sita (2016/17 hadi 2021/22), Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya ilitoa kiasi cha shilingi milioni 85 kwa ajili ya usimamizi shirikishi kupitia timu za usimamizi wa afya za halmashauri sawa na asilimia 2 ya makusanyo ya ada ya kiasi cha shilingi bilioni 3.599. Hata hivyo, halmashauri 14 zilizotembelewa hazikupokea fedha hizo.

Aidha, timu za usimamizi wa afya za mikoa hazikuzisimamia ipasavyo timu za usimamizi wa afya za halmashauri. Ukaguzi ulibaini kuwa ni Timu ya Usimamizi wa Afya ya Mkoa wa Dodoma pekee ndiyo iliweza kufanya usimamizi shirikishi katika robo zote nne za mwaka. Kwa mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza, usimamizi shirikishi ulifanyika katika robo 3 kila mwaka, Hata hivyo, hali ya chini ya usimamizi shirikishi ilibainishwa kwenye Mikoa ya Kilimanjaro, Ruvuma, na Mbeya ambapo timu za usimamizi wa afya za mikoa zilifanya usimamizi shirikishi kwenye robo moja kila mwaka.

Ufuatiliaji wa usimamizi shirikishi haukuwa wa kuridhisha kutokana na taarifa za usimamizi shirikishi kwa ngazi za halmashauri na mikoa kutofikishwa Wizara ya Afya kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22.

(b) Ukaguzi usioridhisha kwenye vituo binafsi na hiari vya huduma za afya

Ukaguzi ulibaini mapungufu mbalimbali yanaohusu ukaguzi wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya kama ilivyoelezwa hapa chini.

▪ **Kiwango cha chini cha ukaguzi wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya**

Ukaguzi ulibaini kuwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/22, Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya haikufanya ukaguzi kwa asilimia 70 ya vituo binafsi vya afya vilivyosajiliwa nchini kinyume na mpango-mkakati wake wa miaka 2016/17- 2020/21. Vituo vya huduma za afya vilivyokaguliwa vilikuwa kati ya asilimia 10 na 52 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.2.

Jedwali Na. 4.2: Ukaguzi uliofanywa na Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya katika Vituo Binafsi na Hiari vya Huduma za Afya

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Vituo vya Huduma za Afya Vilivyosajiliwa | Idadi ya Vituo vya Huduma za Afya Vilivyokaguliwa | Asilimia (%) |
|----------------|---|---|--------------|
| 2016/17 | 240 | 0 | 0 |
| 2017/18 | 481 | 248 | 52 |
| 2018/19 | 806 | 108 | 13 |
| 2019/20 | 1165 | 121 | 10 |
| 2020/21 | 1309 | 172 | 13 |
| 2021/22 | 1474 | 460 | 31 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Ukaguzi wa Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya (2016/17- 2021/22) Mwaka 2022

Jedwali Na. 4.2 linaonesha kuwa ukaguzi ulikuwa wa kiwango cha chini ikilinganishwa na idadi ya vituo binafsi na hiari vya kutolea huduma za afya. Hali hii inatoa mwanya kwa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya kuendelea kufanya kazi bila kukaguliwa kwa muda mrefu.

Sababu za ukaguzi usioridhisha wa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya ni kukosekana kwa uchambuzi wa viashiria vya hatari vya vituo binafsi na hiari vya huduma za afya; kukosekana kwa mpango wa ukaguzi wa muda mrefu; hatua zisizoridhisha za kuhimiza uzingatiaji wa kisheria katika utoaji wa huduma za afya.

- **Kiwango cha chini cha ukaguzi wa maabara binafsi za afya**

Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Usajili wa Maabara Binafsi za Afya haikufanya ukaguzi wa kila mwaka kwa asilimia 100 katika maabara zilizosajiliwa kati ya mwaka wa fedha wa 2016/2017 na 2021/2022 kinyume na ilivyoainishwa katika mipango-mkakati ya Bodi. Kiwango cha ukaguzi kilikuwa cha chini, ambapo ni asilimia 0 hadi 13 tu ya maabara binafsi za afya zilizosajiliwa zilikaguliwa katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2021/2022 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.3.

Jedwali Na. 4.3: Kiwango cha ukaguzi kilichotekelezwa na Bodi ya Usajili wa Maabara Binafsi za Afya katika Maabara za Huduma za Afya Zilizoambatanishwa

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Maabara Zilizosajiliwa | Idadi ya Maabara Zilizokaguliwa | Asilimia ya Maabara Zilizokaguliwa |
|----------------|---------------------------------|---------------------------------|------------------------------------|
| 2016/17 | 1618 | 100 | 6 |
| 2017/18 | 1723 | 0 | 0 |
| 2018/19 | 1854 | 120 | 6 |
| 2019/20 | 1967 | 85 | 4 |
| 2020/21 | 2151 | 81 | 4 |
| 2021/22 | 2232 | 291 | 13 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Ukaguzi wa Bodi ya Usajili wa Maabara Binafsi za Afya Mwaka 2022

Jedwali Na. 4.3 linaonesha kuwa asilimia ya maabara binafsi za afya zilizokaguliwa zilikuwa kati ya asilimia 0 na 13 kutoka mwaka 2016/17 - 2021/22. Sababu za ukaguzi usioridhisha ni kukosekana kwa mpango madhubuti wa ukaguzi wa mwaka; kukosekana kwa uchambuzi wa viashiria vya hatari kwa maabara binafsi za afya; na kutokuwapo kwa ushirikiano kati ya Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya na Bodi ya Usajili wa Maabara Binafsi za Afya wakati wa kufanya ukaguzi.

- **Baraza la Wafamasia halikufanya ukaguzi wa maduka ya dawa katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya**

Ukaguzi ulibaini kuwa Baraza la Wafamasia halikukagua maduka yote ya dawa yaliyosajiliwa katika vituo binafsi na hiari vya afya ikiwa pamoja na maeneo ya kutolea dawa yaliyoidhinishwa, kama ilivyoainishwa katika mipango-mkakati wake wa mwaka 2016/17 hadi 2021/22. Zaidi, ilibainika kuwa vituo vyote 132 vilivyotembelewa katika halmashauri 14 nchini havikufanyiwa ukaguzi na Baraza la Wafamasia.

Kutokaguliwa kwa maduka ya dawa na sehemu zilizoizinishwa kutoa dawa kunaweza kusababisha kutozingatiwa kwa kanuni na viwango, hivyo kuhatarisha usalama wa wagonjwa. Hali hii ilitokana na kukinzana kwa majukumu ya udhibiti wa vituo binafsi vya huduma za afya, ambapo jukumu la Baraza la Ufamasia ni kusajili tu maduka ya dawa yanayojiendesha na si maduka ya dawa yaliyoambatanishwa katika vituo vya huduma za afya. Maduka ya dawa yaliyoambatanishwa na vituo vya huduma za afya yanatathminiwa na kuendesha kwa wakati mmoja na uanzishaji wa vituo vya huduma za afya unaofanywa na Bodi ya Usajili wa Vituo Binafsi vya Huduma za Afya. Hali hii inalizuia Baraza la Wafamasia, ambalo ndilo lenye dhamana ya kufanya na utaalumu wa kukagua wafamasia kwa ajili ya usajili wa maduka ya dawa.

(a) Udhibiti usioridhisha wa bei za huduma za matibabu kwa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya

Yafuatayo yalibainika kuhusiana na udhibiti wa bei za huduma za matibabu zinazotolewa na vituo binafsi na hiari vya huduma za afya nchini.

▪ **Udhibiti usioridhisha juu wa uwazi wa bei za huduma za matibabu**

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Afya haikuhakikisha kuwa bei za matibabu zinawekwa wazi kwenye vituo binafsi na hiari vya huduma za afya. Aidha, ilibainika kuwa, bei za huduma za afya zilitofautiana kwenye vituo binafsi na hiari vya afya katika mikoa yote iliyotembelewa. Katika Manispaa ya Tabora, ni asilimia 20 tu ya vituo binafsi na hiari vya huduma za afya vilivyotembelewa viliweka bei za matibabu, huku vituo vya afya vya Dar es Salaam vilionekana kuwa na uwazi zaidi wa bei za matibabu kwa asilimia 65.

Ukaguzi huu ulibaini kuwa sababu za kutoonesha bei ni utekelezaji mdogo wa kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Hospitali Binafsi ya Mwaka 1991 kinachoeleza kuwa mtu yeyote mwenye jukumu la kusimamia hospitali binafsi na kushindwa kuonesha bei atakuwa na hatia na atawajibika kulipa faini au kifungu cha miaka mitano kwa muda usiozidi miezi kumi na miwili.

Kukosekana kwa uthabiti katika kuonesha bei kunaweza kusababisha mkanganyiko na uwezekano wa kuwadhuru wagonjwa ambao hawana taarifa kamili juu ya gharama za huduma za matibabu wanazopokea.

- **Kutofanyika kwa ufuatiliaji wa bei za matibabu**

Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Afya haikufuatilia ipasavyo bei za huduma za matibabu zitolewazo na vituo binafsi na hiari vya huduma za afya, ambapo hakukuwa na ufuatiliaji kwa kipindi cha miaka kuanzia 2016/17 hadi 2021/22. Utafiti wa mwisho uliofanywa na Shirika la Afya Duniani/HAI ulijikita tu kwenye bei za dawa. Hali hii inamaanisha kwamba Wizara ya Afya haikujua bei zinazotowazwa na vituo binafsi na hiari vya afya. Zaidi ya hayo, Wizara ya Afya iliangualia tu bei zilizooneshwa kwenye mbao za matangazo na haikuthibitisha usahihi wa kiasi ambacho wagonjwa walikuwa wakitozwa kwa huduma za afya. Pia, kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Afya, lengo la ukaguzi kwenye vituo binafsi na hiari vya huduma za afya lilikuwa kujua tu iwapo vituo vya afya vinaweka wazi gharama za matibabu bila kujali usahihi wa gharama.

Sababu ya Wizara ya Afya kutothibitisha usahihi wa bei katika vituo vya kutolea huduma za afya ilikuwa kukosekana kwa kipengele katika mwongozo wa kitaifa wa usimamizi unaosaidia uhakiki wa bei za matibabu katika vituo binafsi na hiari vya afya. Hali hii inatoa nafasi kwa vituo binafsi na hiari vya afya kuwa na bei tofauti za dawa na huduma zingine za afya.

- **Kutofanyika kwa mapitio ya muundo wa bei ya huduma za matibabu**

Kwa mujibu wa Sheria ya Udhhibiti wa Hospitali Binafsi ya Mwaka 1991, Wizara ya Afya ina jukumu la kupitia upya bei za matibabu zinazotolewa na vituo binafsi na hiari vya afya.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa mapitio ya bei za huduma za afya hayakufanyika kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22. Wizara inategemea mapitio ya bei kutoka kwenye orodha ya bei za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hata hivyo, orodha hii haikuwa imehuishwa tangu mwezi Julai 2016, kinyume na Mwongozo wa Uhakiki wa Uboru wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unaotaka kamati ya huduma za afya kupitia upya vifurushi vya wanufaika wa Mfuko kila baada ya miaka mitatu. Kukosekana kwa mapitio ya muundo wa bei kunaweza kusababisha watumiaji kulipia zaidi huduma za matibabu ambazo haziakisi mienendo ya soko.

Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Afya haikuhusisha wadau wengine ili kupata njia mbadala zinazohusu namna ya udhibiti wa bei za huduma za

afya kulingana na afua ya 1 ya Lengo la 7 la Mpango wa Utekelezaji wa Sekta ya Dawa ya Wizara ya Afya wa Mwaka 2020 kwa utaratibu wa gharama za dawa kama ilivyohalalishwa kwa misingi ya afya ya umma au usawa.

(b) Ukaguzi duni wa kitabibu katika vituo binafsi na hiari vya afya

Kwa mujibu wa Mwongozo wa Taifa wa Ukaguzi wa Matibabu, Toleo Na. 1 la Mwaka 2020 na Mpango-mkakati wa Wizara ya Afya wa Mwaka 2016/17 - 2021/22, Wizara ilipanga kuhakikisha kuwa mfumo wa ukaguzi wa matibabu unaanzishwa kwa vituo vya umma na binafsi vya huduma za afya.

Ukaguzi ulibaini yafuatayo kuhusiana na utekelezaji wa ukaguzi wa matibabu katika vituo binafsi na hiari vya kutolea huduma za afya.

- **Wizara ya Afya kutofanya ukaguzi wa kitabibu kwenye vituo binafsi na hiari vya afya**

Kwa mujibu wa mpango-mkakati wa Wizara ya Afya wa mwaka 2016/2017 hadi 2021/2022, Wizara ilipanga kufanya ukaguzi wa kitabibu katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya ifikapo mwezi Juni 2022. Ukaguzi wa kitabibu hufanyika ili kujua huduma bora zinazotolewa na vituo vya afya. Wizara ya Afya ilitakiwa kufanya ukaguzi wa kitabibu katika hospitali za rufaa na hospitali zingine za ngazi za chini.

Ilibainika kuwa ukaguzi wa kitabibu haukufanyika ipasavyo kwa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya. Mapitio ya ripoti ya ukaguzi wa kitabibu kitaifa wa mwezi Julai 2022 yalionesha kuwa Wizara ya Afya ilifanya ukaguzi wa kitabibu katika vituo vya huduma za afya teule vya umma. Ukaguzi huo wa kitabibu wa Wizara ya Afya ulihusisha hospitali zote tano za taifa yaani Mloganzila, KCMC, Muhimbili, MOI na Bugando. Ukaguzi ulihusisha pia hospitali nne maalumu za taifa za Kibong'oto, Mirembe, JKCI, na Ocean Road; na hospitali 28 za rufaa za mikoa na hospitali 15 za wilaya.

Ukaguzi ulibaini kuwa kutofanyika kwa ukaguzi wa kitabibu katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya kulisababishwa na Wizara ya Afya kutokuwa na mikakati ya kufikia lengo lililotarajiwa la kuhakikisha kuwa vituo binafsi na hiari vya huduma za afya nchini vinafanyiwa ukaguzi wa kitabibu. Sababu zingine ni pamoja bajeti za idara ya tiba kwa miaka ya fedha kuanzia 2016/17 - 2021/22 kutokuwa na kipengele cha ukaguzi wa kitabibu; Wizara ya Afya kuchelewa kukamilisha Mwongozo wa Taifa wa Ukaguzi wa Kitabibu kwa Kipindi cha Miaka Miwili, Mpango-mkakati wa

Wizara ya Afya wa Kati wa Mwaka 2016/17 - 2020/21, na Mwongozo wa Taifa wa Ukaguzi wa Kliniki, ambao ulitakiwa kukamilika mwezi Juni 2018. Mwongozo huu, hata hivyo, ulikamilika na kusainiwa mwezi Novemba 2020.

Sababu nyingine ni kuchelewa kukamilika kwa mwongozo wa ukaguzi wa kliniki, ambako kuliathiri utekelezaji wa mifumo ya ukaguzi wa kitabibu. Mwongozo huo ulikuwa muhimu na chombo elekezi katika kuanzisha mfumo wa ukaguzi wa kitabibu. Sababu nyingine ilikuwa kuwapo kwa kamati ya uendeshaji ambayo haikuwahi kutekeleza mamlaka yake ya ukaguzi wa kitabibu na kushindwa kufanya mikutano miwili kulingana na mahitaji ya Mwongozo wa Ukaguzi wa Kitabibu wa Mwaka 2020.

4.6.2 Mapungufu yaliyobainika katika udhibiti wa malipo yanayofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa vituo vya huduma za afya

Kwa miaka ya hivi karibuni, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umefanya jitihada mbalimbali za kuboresha uendeshaji wake, ikiwa pamoja na kuwa na mfumo wa kielektroniki wa kuchakata madai (e-claim system) na usajili wa mtandaoni⁵. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufu kadhaa katika uchakataji wa madai kama inavyoelezwa hapa chini.

(a) Kuwapo kwa madai yasiyostahili

Ripoti za kupambana na udanganyifu na ripoti za uhakiki wa madai yaliyolipwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22 zilibainisha kuwapo kwa madai yasiyostahili yaliyoibuliwa kutoka vituo vya kutolea huduma za afya. Kwa mfano, katika kiasi cha jumla ya shilingi trilioni 1.7 zilizolipwa kwa vituo vya huduma za afya, kulikuwa na kiasi cha shilingi bilioni 14.5 zilizotokana na madai yasiyostahili. Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa kipindi kinachofanyiwa ukaguzi, kulikuwa na ongezeko la mwenendo wa madai yasiyostahili. Vilevile, madai yasiyo sahihi yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 4.3 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 4.6 mwaka 2020/21 na shilingi bilioni 5.6 mwaka 2021/22.

Malipo yasiyostahili ya madai yalibainishwa katika ngazi mbalimbali za vituo vya afya. Kwa mfano, mapitio ya ripoti za kupambana na udanganyifu na ripoti za uhakiki wa malipo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22 yalionesha kuwa kliniki maalumu, hospitali za mikoa, hospitali za wilaya, na hospitali za kanda zilikuwa na malipo yasiyostahili ya zaidi ya shilingi bilioni 2.

⁵ Ripoti ya Utendaji wa Robo ya Kwanza kwa Mwaka wa Fedha 2018-2019

Vilevile, malipo ya madai yasiyo sahihi yalibainika katika makundi mbalimbali ya umiliki wa vituo vya afya. Ukaguzi ulibaini kuwa, vituo binafsi vya huduma za afya vilikuwa na kiwango kikubwa cha madai yasiyostahili ikilinganishwa na vituo vya serikali na taasisi za kidini vya huduma za afya. Udanganyifu huo ulisababisha zaidi ya shilingi bilioni 10.4 kulipwa kwenye vituo binafsi vya afya kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22, wakati kiasi kilicholipwa kwa vituo vya Serikali vya huduma za afya ni shilingi bilioni 1.6 na kwa vituo vya taasisi za kidini vya huduma za afya kilikuwa shilingi bilioni 2.5.

Kuwapo kwa madai yasiyostahili kulihusishwa na ubadhirifu wakati wa utambuzi na usajili wa wagonjwa; huduma za kumwona daktari; vipimo; utoaji wa dawa; na kutozingatia miongozo ya matibabu ya kawaida. Kati ya kiasi cha shilingi bilioni 14.5 kilicholipwa kama madai yasiyostahili, kiasi cha shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 16 zilitokana na mapungufu wakati wa utambuzi na uhakiki wa wanufaika; kiasi cha shilingi milioni 877 sawa na 6% kilisababishwa na dosari iliyotokana na huduma ya kumuona daktari; kiasi cha shilingi bilioni 6.8 sawa na asilimia 47 kilisababishwa na mapungufu kwenye huduma za vipimo; kiasi cha shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 16 kilitokana na mapungufu wakati wa utoaji wa dawa; na kiasi cha shilingi bilioni 2 sawa na asilimia 14 kilitokana na kutozingatia mwongozo wa matibabu ya kawaida wa vituo vya huduma za afya.

Ubadhirifu unaweza kusababisha upotevu wa fedha za Mfuko. Mapitio ya ripoti za udanganyifu yalibainisha kuwa, kulikuwa na ongezeko la jumla la madai yasiyo halali kutoka shilingi bilioni 4.3 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 5.6 mwaka 2021/22. Ilibainika kuwa, kwa ujumla Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulikuwa na madai ya kiasi cha shilingi za milioni 14,464.9 kwa ajili ya malipo yasiyostahili. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ukishindwa kurejesha kiashi cha shilingi bilioni 14.5 zilizotokana na madai yasiyostahili, inaweza kusababisha hasara ya fedha kwa Mfuko.

Ukaguzi ulichambua sababu za kuwapo kwa madai na malipo yasiyo sahihi na kubaini sababu kuu zifuatazo:

- Kushindwa kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinazingatia mwongozo wa matibabu wa Wizara ya Afya pamoja na mikataba wakati wa utoaji wa huduma kwa wanufaika;
- Utaratibu wa udhibiti wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya hauhakiki madai yaliyochakatwa na kulipwa kwa vituo vya afyaili kujua iwapo

-
- ni halisi na sahihi;
 - Hatua zisizoridhisha za kurekebisha madai yasiyostahili yaliyowasilishwa na vituo vya afya; na
 - Kipimo duni cha utendaji kuhusu uchakataji wa malipo ya madai kutoka vituo vya afya.

Sababu hizi zinafafanuliwa katika sehemu zinazofuata hapa chini.

(a) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Kutohakikisha kuwa Vituo vya Afya Vinazingatia Mwongozo wa Matibabu ya Kawaida na Makubaliano ya Kimkataba wakati wa Utoaji wa Huduma za Afya kwa Walengwa

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulitekeleza jitihada mbalimbali katika kuhakikisha vituo vya afya vinazingatia mwongozo wa matibabu wa Wizara ya Afya na makubaliano ya kimkataba wakati wa utoaji wa huduma kwa walengwa. Jitihada hizo ni pamoja na mapitio ya mwongozo wa uhakiki wa ubora na madai katika mwaka wa fedha 2020/21. Kufikia mwezi Juni 2021, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulifanya ufuatiliaji wa kina wa matibabu katika hospitali 13. Pia, ili wajengea uwezo watumishi wa ofisi za mikoa na kuweka maofisa uhakiki wa ubora kwa kuongeza idadi ya madaktari ili kusaidia ufuatiliaji wa matibabu.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mapungufuyanayofafanuliwa hapa chini yaliotokana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutohakikisha vituo vya afya vinazingatia mwongozo wa matibabu ya kawaida na makubaliano ya kimkataba wakati wa utoaji wa huduma za afya kwa wanufaika wake.

- **Asilimia 100 ya vituo vya afya vilivyotembelewa havikuzingatia mwongozo wa matibabu ya kawaida na makubaliano ya kimkataba**

Ukaguzi ulibaini kuwa, kwa kipindi chote kilichofanyiwa mapitio, vituo vyote 131 vya afya vilivyotembelewa katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Dodoma havikuzingatia mwongozo wa matibabu ya kawaida kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4.4.**

Jedwali Na. 4.4: Vituo vya Afya Vilivyotembelewa Havikuzingatia Mwongozo wa Matibabu

| Mkoa | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 |
|--------|-----------|-----------|-----------|
| Dodoma | 0 | 11 | 62 |
| Mwanza | 0 | 7 | 17 |
| Mbeya | 0 | 16 | 18 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Uhakiki wa Madai baada ya Malipo ya Huduma za Afya Mwaka 2023

Jedwali Na. 4.4 linaonesha kuwa, idadi kubwa ya vituo vya afya ambavyo havikuzingatia mwongozo wa matibabu vilibainika katika mwaka wa fedha 2021/22 katika Mkoa wa Dodoma.

Hali hii ilisababishwa na uhimizaji duni wa utekelezaji wa miongozo na makubaliano ya kimkataba. Kwa mfano, ukaguzi ulibaini kutokuwapo kwa rejista ya viashiria vya hatari ili kuwa na uhakiki wenye tija na usimamizi shirikishi kulingana na matakwa ya kifungu 4.2 cha Mwongozo wa Uhakiki wa Ubora wa Mwaka 2021.

Kutozingatia mwongozo wa matibabu ya kawaida katika vituo vya afya kulisababisha hasara ya kifedha kwa Mfuko. Kwa mfano, ukaguzi ulibaini kuwa madai yasiyostahili na yasiyokuwa na dhamana yalifikia shilingi 501,378,549.36. Madai haya yalitambuliwa kupitia uhakiki uliofanyika kwenye vituo vya huduma za afya ndani ya kipindi kilichofanyiwa ukaguzi katika mikoa ya Mbeya, Mwanza na Dodoma kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4.5**

Jedwali Na. 4.5: Madai Yasiyostahili Yaliyotambuliwa kwenye Uhakiki Uliofanyika kwa Kutembelea Vituo vya Huduma za Afya

| Mkoa | Kiasi Kisichopatikana (Shilingi) |
|--------------|-----------------------------------|
| Mbeya | 280,633,999.77 |
| Mwanza | 123,346,527.00 |
| Dodoma | 97,398,022.59 |
| Jumla | 501,378,549.36 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Uhakiki wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwenye Vituo vya Huduma za Afya kwa Kipindi cha kuanzia Mwaka 2019/20 hadi 2021/22

Jedwali Na. 4.5 linaonesha kuwa Mkoa wa Mbeya ulikuwa na madai mengi yasiyostahili ambayo yalikuwa yamelipwa kwenye vituo vya huduma za afya na hayakurejeshwa kwenye Mfuko. Mapungufu haya yalisababishwa na ufuatiliaji usioridhisha wa ofisi ya mkoa husika ya Mfuko na kuhakikisha makato yanafanyika kwenye vituo vya huduma za afya husika kwa kuzingatia uhakiki uliofanywa na Mfuko.

- **Mapungufu ya Bei ya Vifurushi vya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**
Mapitio ya Utafiti wa Bei wa Mwaka 2021, viwango, na vifurushi vya nyongeza yalionesha kuwa bei zilizopo hazikufanyiwa marekebisho kwa zaidi ya miaka 6. Hali hiyo inaleta tofauti kati ya bei ya soko na bei halisi zinazotozwa na Mfuko kwa vituo vya huduma vya afya.

Ilibainika zaidi kuwa, katika mwaka wa 2021, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulifanya utafiti wa soko ambao ulilenga kupima bei za soko la dawa ili kuhuisha bei zake kulingana na bei za soko za dawa zilizochaguliwa. Hata hivyo, utafiti huo haukuhusisha huduma zingine za matibabu zilizopo kwenye vifurushi vya wanufaika vya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kama vile huduma ya kumuona daktari, huduma ya vipimo, upasuaji, na taratibu zingine. Tofauti kubwa kati ya bei ilikuwa kuanzia asilimia 25 hadi 149 kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 4. 6**

Jedwali Na. 4.6: Ulinganisho wa Bei za Rejareja na Bei za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya za mwaka 2016 za dawa 9 kati ya dawa 20 zinazotumika zaidi

| Jina la Kawaida | Nguvu (hariri lpasavyo) | Fomu ya Kipimo (Mhariri alipaswavyo) | Wastani (Rejareja) (A) | Mfuko 2016 (B) | Tofauti (Mfuko 2016/Rejareja)[$C=(A-B)/A$] |
|--|-------------------------|--------------------------------------|------------------------|----------------|--|
| Erythropoietin/Nanokine/Epo/Wapox | 4,000 IU | INJ | 26,500 | 66,000 | 149% |
| Atorvastatin Solid Oral Dosage Form | 20mg | Tabs | 500 | 800 | 60% |
| Telmisartan + Hydrochlorothiazide Solid Oral Dosage Form | 75mg | Caps | 1,000 | 1,350 | 35% |
| Telmisartan + Hydrochlorothiazide Solid Oral Dosage Form | 80mg + 12.5mg | Tabs | 975 | 1,200 | 23% |
| Metformin + Glimipride | 500mg + | Tabs | 950 | 1,000 | 5% |

| Jina la Kawaida | Nguvu (hariri lipasavyo) | Fomu ya Kipimo (Mhariri alipaswa avyo) | Wastani (Rejaraja) (A) | Mfuko 2016 (B) | Tofauti (Mfuko 2016/ Rejaraja)[C=(A-B)/A] |
|--|--------------------------|--|------------------------|----------------|--|
| Solid Oral Dosage Form | 2mg | | | | |
| Ampicillin + Cloxacillin Solid Oral Dosage Form | 250mg + 250mg | Caps | 200 | 190 | -5% |
| Cough Mixture Solution | 100ml/20 125ml | Solution | 3,000 | 2,600 | -13% |
| Vitami B1, B6, B12, Vitamin B1, B6, B12, Folic Acid Solid Oral Dosage Form | 150mg | Caps | 600 | 500 | -17% |
| Glucosamin + Chondroitin Solid Oral Dosage Form | 20mg | Caps | 1,000 | 750 | -25% |

Chanzo: Ripoti ya Utafiti wa Soko ya Mwaka 2021

Jedwali Na. 4.6 linaonesha tofauti kati ya bei za soko na bei halisi zinazotozwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwenye vituo vya afya. Tofauti hiyo ilikuwa kati ya shilingi 250 na shilingi 39,500 sawa na asilimia 25 hadi asilimia 149 ya dawa zinazotumika mara kwa mara.

Matokeo ya utafiti wa soko yalionesha kuwa, kwa kutumia bei ya mwaka 2016, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulilipa kiasi cha shilingi za kitanzania bilioni 100.79 katika mwaka wa fedha 2018/19 badala ya shilingi bilioni 93.9 kama bei za soko zilizopo zingetumika. Hali hii imepunguza gharama za vitu hivyo kwa kiasi cha shilingi bilioni 6.84 sawa na asilimia saba.

Ukaguzi ulibaini kuwa, tofauti kubwa kati ya bei za soko na bei ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni kukosekana kwa mapitio ya vifurushi ili kuakisi hali ya soko ya sasa.

Kutokana na tofauti kubwa kati ya bei za soko na bei za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya za mwaka 2016, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya hupoteza pesa ambazo husababishwa na malipo ya juu yaliyotokana na kutumia bei za Mfuko za mwaka 2016. Kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22, Mfuko ungeweza kuokoa shilingi 11,069,788,945.38 kwa madai yaliyokwisha lipwa kwenye vituo vya huduma za afya endapo bei za soko za dawa teule 20 na dawa za saratani zingepitishwa.

- Vituo vya huduma za afya kutosimamia na kutunza kumbukumbu za kweli na sahihi za wagonjwa

Katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/2022, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu za huduma zinazotolewa katika vituo vya huduma za afya. Hali hii ilibainika wakati wa uchunguzi wa udanganyifu ambao ulibaini kukosekana kwa nyaraka, utunzaji usiofaa wa kumbukumbu za maelezo ya mgonjwa, taarifa za kughushi za madai yasiyostahili, na taarifa zisizo sahihi za utoaji wa dawa. Vituo vya huduma za afya vilivyokuwa na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu za huduma vilikuwa kati ya asilimia 11 na asilimia 28 kwa mwaka kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na. 4.7**.

Jedwali 4.7: Utunzaji wa Kumbukumbu Usioridhisha Wwakati wa Utoaji wa Huduma za Afya


| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Vituo vya Huduma za Afya | Idadi ya Vituo vya Huduma za Afya Vilivyochunguzwa | Vituo vya Huduma za Afya Vilivyokuwa na Utunzaji Duni wa Kumbukumbu | Asilimia (Umri) |
|----------------|-----------------------------------|--|---|-----------------|
| 2019/20 | 8,442 | 118 | 31 | 26 |
| 2020/21 | 9,037 | 112 | 12 | 11 |
| 2021/22 | 9,556 | 65 | 18 | 28 |

Chanzo: Kanzidata ya Vituo vya Afya na Taarifa za Uchunguzi wa Udanganyifu za kuanzia Mwaka 2019/20 hadi 2021/22

Jedwali Na. 4.7 linaonesha kuwa, kulikuwa na ongezeko la asilimia ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyokuwa na utunzaji duni wa kumbukumbu kutoka asilimia 26 mwaka 2020/21 hadi asilimia 28 mwaka 2021/22.

Kwa upande wa vituo vya huduma za afya vilivyofikiwa na uchunguzi dhidi ya udanganyifu, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa utunzaji duni wa kumbukumbu za huduma za afya wa asilimia 44 wakati wa uchunguzi uliofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; asilimia 35 katika vituo vyote vya huduma (maabara na maduka ya dawa ya vituo vya afya); na asilimia 21 katika maduka ya dawa wakati wa utoaji wa dawa. Hata hivyo, uboreshaji wa utunzaji wa kumbukumbu ulibainika katika maduka ya dawa. **Kielelezo Na. 4.5** kinawasilisha uchambuzi wa utunzaji duni wa kumbukumbu kulingana na hatua ya utoaji wa huduma za afya.

Kielelezo 4.5: Utunzaji usioridhisha wa Kumbukumbu kulingana na Hatua ya Utoaji wa Huduma za Afya



Chanzo: Taarifa za Uchunguzi wa Kupambana na Udanganyifu za kuanzia Mwaka 2019/20 hadi 2021/22

Ukaguzi ulibaini kuwa, sababu za usimamizi na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu sahihi ni kukosekana kwa matokeo ya wazi ya kimkatiba kwa kutofuata matakwa ya kumbukumbu za matibabu kwa huduma zinazotolewa na vituo vya huduma za afya.

Kutopatikana kwa kumbukumbu katika hatua mbalimbali za huduma kulisababisha kutofautiana kwa taarifa kati ya madai yaliyowasilishwa kutoka vituo vya afya na huduma halisi zilizotolewa, jambo linaloweza kutoa mwanya wa malipo kwa huduma ambazo hazikutolewa.

(b) Utaratibu wa Udhhibiti wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Haukuhakikisha Madai Yaliyochakatwa na Kulipwa kwa Vituo vya Afya ni Halisi na Sahihi

Mwezi Juni 2021, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulipitia vifurushi vya wanufaika na kuwasilishwa kwa Wizara inayohusika na masuala ya afya kama jitihada za kuhakikisha kunakuwa na utaratibu wa udhibiti wa madai yaliyochakatwa. Pia, Mfuko kwa pamoja unafanya uchunguzi wa udanganyifu kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Serikali kama vile Jeshi la Polisi na TAKUKURU pale inapoonekana kuna umuhimu. Pia, ili kushughulikia mapendekezo yaliyotolewa kupitia uchunguzi wa

udanganyifu, kupitia barua zenye Kumb No. CAG.143/20191/01/259-02 na CAG.143/20191/01A/49, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulizitaka bodi za wataalamu kuchukua hatua za kikanuni kwa watumishi waliofanya ubadhirifu wakati wa kutoa huduma za afya kwa walengwa wa Mfuko. Pamoja na jitihada zilizobainishwa, ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo:


- **Uhakiki wa uanachama na idhini katika vituo vya kutolea huduma za afya haukufanyika ipasavyo**

Ilibainika kuwa uhakiki wa wanachama na idhini katika vituo vya afya haukufanyika ipasavyo kwa sababu, kwanza, vipengele vingi katika kadi za uanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya havikutosheleza kusaidia utambuzi na uhakiki wa wanufaika wakati wa utoaji wa huduma. Ukaguzi ulibaini kuwa kati ya vipengele 8 vilivyobainishwa kwenye kadi za uanachama za Mfuko, ni kipengele kimoja tu ndicho kilitosheleza utambuzi na uhakiki wa wanufaika wakati wa utoaji wa huduma za afya.

Pili, kulikuwa na wanufaika waliojipatia huduma za afya kwa kutumia saini zenye herufi za awali za majina. Uhakiki wa majalada ya madai katika ofisi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya za Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Ilala na Unguja ulibaini kuwa, baada ya kukamilika kwa huduma za afya, wanufaika 186 walisaini fomu namba 2 (a) ya Mfuko kwa kutumia herufi za awali za majina yao.

Tatu, ukaguzi ulibaini kuwa wanachama wasiostahili na wasiosajiliwa walijipata huduma za afya. Mapitio ya ripoti za kupambana na udanganyifu za kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/2022 yalibaini kuwa jumla ya shilingi milioni 3,539 zililipwa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa wanufaika wasiostahili katika mikoa ya Ilala, Mwanza na Geita kama inavyowasilishwa katika **Kielelezo Na. 4.6**.

Kielelezo 4.6: Gharama Zilizotokana na Malipo kwa Wanufaika Wasioshahidi Waliopata Huduma za Usafishaji wa Figo (kwa shilingi milioni)



Chanzo: Taarifa za Kupambana na Udanganyifu za kuanzia Mwaka 2019/20 hadi 2021/22

Kielelezo Na. 4. 6 kinaonesha kuwa gharama zilizopatikana kutokana na wanufaika wasioshahidi kupata huduma za kusafisha figo ziliendelea kuongezeka kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22.

Uhakiki duni wa uanachama katika vituo vya afya ulisababishwa na kushindwa kwa CMIS na mifumo ya taarifa za afya inayotumiwa na vituo vya huduma za afya kuchukua taarifa muhimu za mnufaika kama vile saini, alama za vidole, na picha zinazoweza kusaidia katika utambuzi wa wanufaika.

Hali hiyo ilisababishwa na udhibiti usioridhisha katika vituo vya kutolea huduma za afya hasa wakati wa usajili wa wanufaika na wakati wa kukamilisha huduma. Kwa mfano, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa kadi ya mnufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya isiyokuwa na saini. Saini ingeweza kuwasaidia watoahuduma kulinganisha saini ndani ya fomu namba 2(a) kwa lengo la kutambua wanachama halisi.


Mapungufu haya yanaweza kutoa mwanya kwa wagonjwa au watoahuduma kutumia vibaya kadi hivyo kusababisha Mfuko kulipa fedha kwa

watoahuduma kwa huduma ambazo hazikutolewa kwa walengwa hatimaye kusababisha hasara kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

▪ **Madai yaliyokaa muda mrefu zaidi**

Ripoti ya Utendaji ya Mwaka wa Fedha ya Mwaka 2021/22 ilionesha kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulirekodi wastani wa madai yaliyokaa kwa siku 62 kwa mikoa yote 30 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita ambapo wastani wa muda wa madai ulikuwa siku 57. Hali hii ina maana kwamba, idadi ya siku za kushughulikia madai iliongezeka kwa asilimia 8. Aidha, kwa mikoa iliyotembelewa, muda wa madeni kukaa ulianza siku 34 hadi 73, ambapo mikoa ya Dodoma na Mwanza ilikuwa na madai yaliyokaa muda mrefu zaidi ya lengo. **Kielelezo Na. 4.7** kinaonesha muda unaotumika kuchakata madai katika mikoa iliyotembelewa.

Kielelezo 4.7: Muda wa Kushughulikia Madai kufikia Mwezi Juni 2022



Chanzo: Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Madai Mwaka 2022

Kielelezo Na. 4.7 hapo juu kinaonesha kuwa mikoa mitatu ya Mbeya, Ilala na Zanzibar ilifikia lengo la muda uliotumika kushughulikia madai, wakati Mkoa wa Dodoma ukirekodi muda wa juu ya uli lengwa wa siku 28 na Mkoa wa Mwanza siku 22.

Kuwapo kwa madai makubwa yenye muda mrefu kulichangiwa na sababu kadhaa zikiwa pamoja na maafisa uhakiki ubora katika ofisi za mikoa

kusimamisha michakato ya madai kutokana na sababu mbalimbali; kuwapo kwa madai yenye viashiria vya udanganyifu hivyo kuchukua muda mrefu kuchakatwa na kuhakikiwa; na uhaba wa watumishi katika ofisi za mikoa huku kukiwa na ongezeko la madai yakiwemo madai ya nyongeza.

Uchakataji wa madai unaochukua muda mrefu husababisha baadhi ya vituo vya huduma za afya kushindwa kujiendesha hivyo kushindwa kutoa huduma zinazokidhi viwango vya ubora kwa wanufaika wa Mfuko.

▪ **Mfumo wa usimamizi wa taarifa za madai kutohakikisha kuwa madai yaliyochakatwa yalikuwa halisi na sahihi**

Mapitio ya CMIS yalibainisha mapungufu mbalimbali yaliyoonessa kuwa mfumo uliotumika haukuhakikisha kuwa madai yaliyochakatwa ni halisi na sahihi. Mfumo huo haukuwapa maafisa uhakiki ubora uwezekano wa kubaini ucheleweshaji wa madai yaliyowasilishwa na vituo vya kutolea huduma za afya. Matokeo yake, maafisa uhakiki ubora waliendelea kutegemea tu taarifa fupi ambazo vituo vya huduma za afya huziwasilisha katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya pale waliposhindwa kuwasilisha madai kwa wakati.

Pia, madai ya mtandaoni yaliyowasilishwa na vituo vya kutolea huduma za afya hayakuonesha matokeo ya uchunguzi wa kitabibu ambao wagonjwa hupokea kama sehemu ya huduma za afya. Madai yaliyowasilishwa yaliambatisha tu fomu namba 2 (a) na (b) na maelezo mafupi. Hayo yalibainika katika vituo vya huduma za afya vilivyotembelewa katika Hospitali ya Kamanga na Kituo cha Afya Bugando Mkoani Mwanza.

Hali hii ilisababishwa na kukosekana kwa maboresho ya mara kwa mara ya mfumo wa CMIS, hivyo kuwa vigumu kwa maafisa uhakiki wa ubora kufanya ufuatiliaji na kuhimiza utekelezaji wa masharti ya Mfuko yanayotaka vituo vya afya kuwasilisha madai kwa njia ya mtandao ndani ya saa 24 baada ya utoaji wa huduma za afya kwa walengwa wa Mfuko.

Pia, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya haikuwa na kanzidata ya kutosha kuhifadhi kiasi kikubwa cha taarifa hivyo kusababisha kuchelewa kwa uchakataji wa madai ambayo kwa upande mwingine yanaweza kuathiri utoaji wa huduma katika vituo vya afya kwa wanufaika wa Mfuko.

Aidha, dosari hii ingeweza pia kusababishwa na mfumo usio na uwezo wa kuchakata taratibu za kusimamia madeni kama vile mwongozo wa kutoa huduma za afya, mwongozo wa uhakiki wa ubora, na orodha ya watendaji wa kuhakiki madai.

-
- **Hatua zisizoridhisha zilizochukuliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhusu madai yasiyo na uhalisia yaliyowasilishwa na vituo vya afya**

Licha ya kuwapo kwa jitihada mbalimbali za kurejesha madai yasiyostahili yaliyobainika kupitia uhakiki uliofanyika kwenye vituo vya huduma za afya na uchunguzi wa udanganyifu, ukaguzi ulibaini mapungufu kuhusu hatua zilizochukuliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kurejesha fedha za madai ambayo hayakustahili kwa vituo vya huduma za afya.

Ukaguzi ulibaini kuwa urejeshaji wa madai hayo yasiyo halali haukufanyika ipasavyo. Kwa mujibu wa ripoti za utendaji wa mwaka, ripoti za kupambana na udanganyifu, na ripoti za uhakiki kwenye vituo na ratiba ya urejeshaji wa madai kufikia mwezi Juni 2022, kiasi cha shilingi 12,109,040,666.00 kilichotokana na madai yasiyostahili kilikuwa hakijarejeshwa. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa, madai yasiyo halali ya kiasi cha shilingi 804,029,589.78 yaliyotambuliwa kupitia uhakiki wa kwenye vituo yalikuwa hayajarejeshwa.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na hatua zisizoridhisha dhidi ya watumishi waliohusika na vitendo viovu. Mapungufu haya yanadhihirishwa na ukweli kuwa kulikuwa na watumishi 146 wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na wa vituo vya afya waliojijhusisha na vitendo vya udanganyifu, lakini, ili kukabiliana na watumishi hao, Kitengo cha Kupambana na Udanganyifu kiliripoti maofisa 17 tu wa Mfuko waliojijhusisha na vitendo vya udanganyifu kwa kamati za nidhamu za Mfuko kwa ajili ya hatua za kinidhamu.

Kwa upande mwingine, Kitengo hicho kiliripoti watumishi 129 kutoka vituo vya huduma za afya kwenda Wizara ya Afya na bodi za kitaaluma. Hata hivyo, hakukuwa na hatua zozote zilizochukuliwa kwa watumishi walioripotiwa kwa kamati za nidhamu, Wizara ya Afya, na bodi za kitaaluma. Mchanganuo wa idadi ya maofisa wa Mfuko na wa vituo vya afya waliojijhusisha na vitendo vya udanganyifu yanawasilishwa katika **Jedwali Na. 4.8.**

Jedwali Na. 4.8: Idadi ya Maofisa wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Vituo vya Afya Waliojikusisha na Vitendo vya Udanganyifu

| Kiashiria | Maofisa | | | |
|---|-----------|-----------|-----------|------------|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | Jumla |
| Idadi ya maofisa wa Mfuko wanaokabiliwa na mashauri ya rushwa | 17 | 1 | 1 | 19 |
| Idadi ya watumishi wa vituo vya huduma za afya wenye mashauri ya rushwa | 0 | 49 | 80 | 129 |
| Jumla | 17 | 50 | 81 | 148 |

Chanzo: Wito wa Kuhudhuria katika Kamati za Uchunguzi kuanzia Mwaka 2019/20 hadi 2021/22, Barua Na. CAG.143/191/01/263, CAG.143/191/01/259-01, CAG.143/191/01/170, na CAG.143/191/01A/33

Jedwali Na. 4.8 linaonesha kuwa, takribani asilimia 87 ya watumishi walioripotiwa kujikusisha na vitendo vya udanganyifu kwa kipindi kinachofanyiwa ukaguzi walitoka katika vituo vya huduma za afya ambapo watumishi kutoka ofisi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni asilimia 13.

Hakukuwa na hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kwa watumishi wanaojikusisha na vitendo vya udanganyifu kutoka vituo vya huduma za afya. Katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, watumishi 12 kati ya 19 wakifukuzwa kazi, wawili walipewa barua ya onyo, mmoja alisimamishwa kazi, na watumishi wanne waliobaki hakukuwa na ushahidi uliotolewa kuhusu hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi yao.

Urejeshaji usioridhisha wa madai yasiyo halali na hatua zisizoridhisha dhidi ya watumishi waliohusika na ubadhirifu ulitokana na kutofautiana katika usimamizi wa mashauri ya udanganyifu na uhakiki wa kutosha; hatua zisizoridhisha za kinidhamu zilizochukuliwa kwa watumishi waliohusika katika udanganyifu; ufuatiliaji wa mashauri yaliyobainika; na kushindwa kwa bodi za kitaaluma kuchukua hatua kwa wanachama wake waliojikusisha na vitendo vya udanganyifu hata kama matukio yaliyoripotiwa yalikuwa ndani ya mamlaka yao.

Matokeo yake, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulipoteza fedha ambazo zingeweza kuimarisha uendelevu wake.

- **Tathmini duni ya utendaji wa uchakataji na malipo ya madai kutoka vituo vya afya**

Ili kuongoza na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya shughuli zake, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Mfuko ulipanga kuandaa mfumo wa tathmini na ufuatiliaji. Katika kipindi hicho, Mfuko ulifanya ziara ya kikazi kwa kutembelea taasisi mbalimbali kwa lengo la kutafuta mbinu bora za ufuatiliaji na tathmini katika taasisi za Serikali. Ukaguzi ulibaini kuwa, tathmini ya utendaji kuhusu uchakataji na malipo ya madai kutoka vituo vya afya haikufanyika ipasavyo kutokana na mapungufu yaliyoonekana kama inavyooneshwa hapa chini.

- (i) Viashiria muhimu vya utendaji wa ufuatiliaji wa shughuli za uchakataji wa madai havikufikiwa ipasavyo**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uliweka viashiria muhimu vya utendaji ambavyo hutumika kufuatilia utendaji wa shughuli zilizopangwa kuhusiana na uchakataji wa madai kama vile kupunguza matukio ya rushwa na udanganyifu kwa wafanyakazi, na kuongeza hali ya kuridhika kwa wanufaika wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuendelea kuwapo kwa udanganyifu katika vituo vya huduma za afya.

Kwa mfano, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulifanya uchunguzi na upelelezi wa tahadhari katika vituo vya afya vilivyoshukiwa kuwa na ubadhirifu na kubaini jumla ya vituo 301 vya huduma za afya vilifanya vitendo vya udanganyifu kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wakati wa utoaji wa huduma. Kati ya hivyo, vituo 117 vya huduma za afya vilibainika mwaka wa fedha 2019/20; vituo 112 vya huduma vya afya vilibainika mwaka wa fedha 2020/21; na vituo 72 vya huduma za afya vilipatikana katika mwaka wa fedha 2021/22.

- (ii) Mifumo iliyopo haikuwa na takwimu halisi za wakati wa utoaji wa huduma za afya**

Ukaguzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Afya (HMIS) wa vituo vya afya na Mfumo wa CMIS wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya katika vituo vya afya vilivyotembelewa katika Mikoa ya Mwanza, Dodoma na Mbeya ulibaini kuwa, Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Afya unaotumiwa na vituo vya huduma za afya wakati wa utoaji wa huduma za afya kwa wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya haikuweza kutuma takwimu kwa wakati halisi kwenye Mfumo wa CMIS kwa ajili ya uchakataji wa madai.

Ukaguzi uligundua kuwa kukosekana kwa mwingiliano wa taarifa kwa wakati halisi kati ya Mfumo wa CMIS na Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya kulihusishwa na:

- Tofauti ya umiliki wa taarifa na sera za faragha kati ya wadau ambao wana jukumu la usimamizi wa mifumo ya CMIS na Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya; na
- Mfumo wa CMIS ulitengenezwa kwa malengo yanayotofautiana ambapo Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya ulikuwa na lengo la kuhifadhi kumbukumbu za afya katika vituo vya huduma za afya wakati CMIS ulitengenezwa kwa madhumuni ya usimamizi wa madai kwa huduma za afya zilizotolewa.

Kukosekana kwa mwingiliano halisi wa taarifa kati ya Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Huduma za Afya na Mfumo wa CMIS kunauzuia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kupunguza na kuzuia vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na watoahuduma za afya kwa sababu inatoa nafasi kwa vituo vya huduma za afya kubadilisha taarifa kwenye vipengele katika karatasi. Hali hii iliweka uwezekano wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wa kulipa madai yasiyo halisi.

(iii) Ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ya utendaji wa uchakataji wa malipo ya madai usioridhisha

Ukaguzi ulibaini kuwa, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulifanya uhakiki wa malipo ya awali na baada kama njia ya kufuatilia madai yaliyochakatwa na vituo vya afya. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa, uhakiki wa madai kwenye vituo vya huduma za afya haukufanyika ipasavyo ili kutathmini uhalali wa madai yaliyowasilishwa kabla ya kulipwa katika kipindi kilichofanyiwa mapitio kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4.9**.

Jedwali Na. 4.9: Hali ya Mipango na Utekelezaji wa Uhakiki wa Madai kwenye Vituo vya Huduma za Afya Uliofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

| Mwaka wa Fedha | Malengo ya Uhakiki | Uhakiki Halisi wa Madai | Tofauti | Asilimia ya Kutofanyika |
|----------------|--------------------|-------------------------|-------------|-------------------------|
| 2019/20 | 12 | Haijatolewa | Haijatolewa | - |
| 2020/21 | 20 | 13 | 7 | 65 |
| 2021/22 | 28 | 11 | 17 | 39 |

Chanzo: Taarifa za Utendaji kwa Mwaka (2019/20 - 2021/22) na Uchambuzi wa Wakaguzi

Jedwali Na. 4.9 linaonesha kuwa, kwa mwaka wa fedha 2019/20 uhakiki wa madai kwenye vituo haukufanyika kama ilivyokusudiwa. Kwa mwaka wa fedha 2020/21, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulifanya uhakiki wa madai 13 kati ya 20 sawa na asilimia 65. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Mfuko ulifanya uhakiki wa madai 11 kati ya 28 yaliyopangwa sawa na asilimia 39.

Uchambuzi zaidi ulifanyika ili kuonesha hali ya uhakiki wa madai kwenye vituo vya huduma za afya kupitia ofisi za mikoa za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya zilizotembelewa kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4.10**.

Jedwali Na. 4.10: Hali ya Uhakiki wa Vituo vya Huduma za Afya Uliopangwa na Kutekelezwa na Ofisi za Mkoa za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

| Mkoa | Mwaka wa Fedha | Mpango wa Uhakiki wa Madai | Uhakiki wa Madai Uliofanywa | Asilimia ya Utekelezaji (%) |
|--------|----------------|----------------------------|-----------------------------|-----------------------------|
| Dodoma | 2019/20 | 32 | 39 | 122 |
| | 2020/21 | 66 | 62 | 94 |
| | 2021/22 | 40 | 46 | 115 |
| Mwanza | 2019/20 | 32 | 39 | 122 |
| | 2020/21 | 20 | 27 | 135 |
| | 2021/22 | 24 | 24 | 100 |
| Mbeya | 2019/20 | 0 | 0 | 0 |
| | 2020/21 | 40 | 20 | 50 |
| | 2021/22 | 40 | 26 | 65 |
| Ilala | 2019/20 | 32 | 54 | 169 |
| | 2020/21 | 48 | 0 | 0 |
| | 2021/22 | 96 | 87 | 91 |
| Unguja | 2019/20 | 17 | 17 | 100 |
| | 2020/21 | 32 | 24 | 75 |
| | 2021/22 | 25 | 23 | 92 |

Chanzo: Mipango ya Utekelezaji ya Mwaka, Ripoti za Utekelezaji, na Uchambuzi wa Wakaguzi Mwaka 2022

Jedwali Na. 4.10 linaonesha hali nzuri ya mwenendo wa uhakiki wa madai kwenye vituo vya huduma za afya katika ofisi za kanda za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya za Dodoma, Mwanza, Ilala na Unguja. Katika mikoa hii, mwenendo wa uhakiki ulikuwa kuanzia asilimia 50 hadi 169 ikilinganishwa na idadi ya uhakiki uliopangwa kutekelezwa. Sababu ya kuvuka lengo lililowekwa la uhakiki wa madai kwa miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21

ilikuwa kuanzishwa kwa matumizi ya namba ya uhakiki kwa vituo vya afya hasa vile vilivyo chini ya serikali za mitaa. Hatua hii ilihitaji vituo kutembelewa mara kwa mara ili kuthibitisha kama wanufaika wanapata huduma za afya.

Mwenendo usiofaa wa uhakiki wa madai kwenye vituo vya huduma za afya ulihusishwa na ufinyu wa bajeti. Hali hii ilithibitishwa na matokeo ya mapitio ya Ripoti ya Utendaji wa Fedha ya Mwaka 2021/22, ambayo yalionesha kuwa changamoto ya kifedha ilikuwa kikwazo cha kufanya uhakiki wa madeni kwenye vituo vya huduma za afya.

Sababu nyingine zilizobainishwa kuhusiana na utekelezaji usioridhisha wa uhakiki wa madai kwenye vituo vya huduma za afya ilikuwa idadi ndogo ya watumishi ikilinganishwa na malengo makubwa ya uhakiki yaliyopangwa bila kuzingatia kuwapo wa rasilimali-watu.

Matokeo yake, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulifanya malipo kwa vituo vya huduma za afya kwa huduma ambazo hazikutolewa kwa wanufaika wake. Mapitio ya Ripoti ya Mkaguzi wa Ndani⁶ yalionesha kuwa, huduma za upasuaji 433 kati ya 314,399 zenye thamani ya shilingi 46,990,000 zilitolewa bila huduma hizi kufanyika.

(iv) Kukosekana kwa mfumo wa tathmini na ufuatiliaji ili kuboresha hali ya uchakataji wa madai

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini uliowekwa kusimamia shughuli za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ikiwa pamoja na uchakataji wa madai. Hata hivyo, Mfuko ulijumuisha mpango wa maandalizi na ukamilishaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kwa miaka ya fedha 2020/21 na 2021/22.

Sababu ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutotekeleza mpango wa kuandaa na kukamilisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ni kutokuwa na kipaumbele wakati wa utekelezaji wa shughuli zake zilizopangwa kwa kipindi cha miaka miwili ya fedha ya 2020/21 na 2021/22. Hali hii hatimaye ilisababisha kuingiliana kwa shughuli hivyo kutotekelezeka kwa shughuli zilizopangwa kwa miaka miwili.

⁶ Ripoti ya Ukaguzi wa Ndani kuhusu Malipo ya Madai ya Faida na Mikopo kwa Michakato ya Watoahuduma kwa Kipindi Kilichoishia Mwezi Machi 2021

Mapitio utekelezaji na ufuatiliaji wa bajeti kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22 yalibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilitumia nyaraka hizo kama mwongozo wa kufuatilia shughuli za fedha ikiwemo shughuli za kuboresha uchakataji wa madai. Kijitabu cha utekelezaji na ufuatiliaji wa bajeti kilichoandaliwa kinajumuisha mipango ya utekelezaji na malengo ya kurugenzi, vitengo, na ofisi za kanda za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Waraka huo unatumika kama kielelezo cha ufuatiliaji wa kila robo mwaka wa utendaji wa bajeti na wakati wa uandaaji wa ripoti za utendaji.


4.6.3 Mapungufu katika Udhhibiti wa Vyanzo vya Mionzi

Licha ya jitihada zilizobainika kufanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kama vile kutoa leseni kwa watumiaji wa vyanzo vya mionzi; kukagua vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi; ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kitaifa cha udhibiti wa taka za mionzi Jijini Arusha; na ujenzi wa maabara changamani. Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mapungufu yanayohusiana na udhibiti wa vyanzo vya mionzi ambao unaweza kuwa na athari kwa watumiaji, umma na mazingira kwa ujumla.

a) Wastani wa asilimia 66 ya vituo vyenye vyanzo vya mionzi vilivyosajiliwa nchini havikupewa leseni na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ya kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi

Ukaguzi ulibaini kuwa, kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2021/22, idadi ya vituo ambavyo havikupewa leseni na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania vilikuwa asilimia 68, asilimia 69, asilimia 63 na asilimia 64 mtawalia katika vituo vyote vya mionzi vilivyosajiliwa nchini. Takwimu hizi ni sawa na wastani wa asilimia 66 wa vituo vyenye vyanzo vya mionzi ambavyo havikupewa leseni na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika kipindi kilichokaguliwa cha miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi mwaka 2021/2022. Hali hii ni kinyume cha Sheria ya Nguvu za Atomiki inayoitaka Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kutoa leseni kila mwaka kwa vituo vyote vinavyotumia vyanzo vya mionzi. Asilimia ya vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi ambavyo havikupatiwa leseni kwa kila mwaka wa fedha ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 4.8**.

Kielelezo Na. 4.8: Asilimia ya Vituo vyenye Vyanzo vya Mionzi Vilivyosajiliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ambavyo Havikupatiwa Leseni ya Kumiliki na Kutumia Vyanzo vya Mionzi



Chanzo: Uchambuzi wa Leseni za Kumiliki na Kutumia Mionzi na Kanzidata ya Taasisi zote zenye Vyanzo vya Mionzi Nchini kuanzia Mwaka 2018/19 hadi 2021/22

Kielelezo Na. 4.8 kinaonesha kuwa, asilimia ya vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi visivyo na leseni viliongezeka kutoka asilimia 68 katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi asilimia 69 katika mwaka wa fedha 2019/20 lakini vilishuka hadi asilimia 63 katika mwaka wa fedha 2020/21, ingawa viliongezeka tena hadi asilimia 64 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa hatua za utekelezaji za kufungia vituo vyenye vyanzo vya mionzi vilivyobainika kutokuwa na leseni halali za umiliki na matumizi ya mionzi hazikutekelezwa ipasavyo na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, kwani asilimia 90 ya vituo visivyokuwa na leseni havikufungiwa kwa kipindi kilichokaguliwa cha miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 - 2021/22.


Kukosekana kwa mfumo sahihi wa utoaji leseni kulisababisha Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kupoteza wastani wa shilingi milioni 424.65 kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22 kwa kuttoa leseni kwa vituo 2831 vilivyosajiliwa. Makadirio hayo ya ada za leseni ambazo hazikukusanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ni kiwango cha chini ambacho kilipaswa kukusanywa kwa kiwango cha shilingi 150,000 kwa kila chanzo cha mionzi kati ya vituo 2,831 kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni za Nishati ya Nguvu za Atomiki za Mwaka 2011.

b) Uwepo wa Vyanzo Vya Mionzi Visivyotumika ambavyo havikuondolewa na Kuhifadhiwa Mahali Salama na Sahihi

Ukaguzi ulibaini kuwa kanzidata ya kutunza vyanzo vya mionzi visivyotumika na vyenye kasoro inayotunzwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ina takwimu duni za kitaifa juu ya hali halisi ya vyanzo vya mionzi visivyotumika.

Hali hii inatokana na ukweli kwamba Wakala wa Barabara Tanzania inamiliki vyanzo 15 vya mionzi vyenye kasoro⁷, huku ukiwa na vyanzo 40 vya mionzi ambavyo havitumiki (vilivyotakiwa kuondoshwa) ambavyo viko katika ofisi zake za kanda kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 4.9**. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na chanzo chochote kati ya vyanzo 55 kilichokuwa na makubaliano ya kurudi kwa mtengenezaji kwa ajili ya uhifadhi sahihi kama inavyotakiwa na Kanuni Namba 62 (1) (a) na (b) na 62 (3) za Kanuni za Nishati ya Nguvu za Atomiki (Kinga Dhidi ya Mionzi) za Mwaka 2004.

Kielelezo Na. 4.9: Kiwango cha Vyanzo vya Mionzi Visivyotumika ambavyo Havikuondoshwa katika Ofisi za Mikoa za Wakala wa Barabara Tanzania



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Hali ya Vyanzo vya Mionzi katika Ofisi za Mikoa za Wakala wa Barabara Tanzania Mwaka 2022


Kielelezo Na. 4.9 kinaonesha kuwa, vyanzo vya mionzi visivyotumika vinne (4) vilikutwa katika ofisi za mikoa za Wakala wa Barabara Tanzania zilizopo

⁷ Vyanzo vya mionzi vyenye kasoro humaanisha vyanzo vya mionzi vilivyo katika nusu ya maisha yake au katika hali ambayo haitoi tena kiasi cha mionzi inayotakiwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

kanda ya kati, vitatu (3) kanda ya ziwa, kanda ya pwani, na kanda ya nyanda za juu kusini. Pia, chanzo kimoja (1) cha mionzi kisichotumika kilikutwa katika kanda ya kusini na kanda ya kaskazini.

Hali hii ilichangiwa na ukweli kwamba, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikuwa na mfumo madhubuti wa kusimamia uingizaji wa vyanzo vya mionzi nchini. Matokeo yake, Tume ilikosa kanzidata sahihi ili kurahisisha ufuatiliaji wa vyanzo vya mionzi.


Ukaguzi ulifanya uchambuzi wa sababu za udhibiti hafifu wa vyanzo vya mionzi nchini. Sababu hizo ni pamoja na:

- Kutofanyika kwa ukaguzi wa kutosha kwenye vituo vya mionzi vilivyosajiliwa, hasa kwa vituo vya mionzi visivyo vya matibabu;
- Utaratibu usioridhisha wa utendaji kazi katika udhibiti wa vyanzo vya mionzi;
- Ufuatiliaji usioridhisha wa vyanzo vya mionzi;
- Uhaba wa vifaa vya kugundua mionzi kwa mtumiaji anayemiliki vyanzo vya mionzi;
- Uratibu usio na tija kati ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania na wadau wengine; Na 
- Ufuatiliaji na tathmini usioridhisha ya utendaji kazi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika kudhibiti vyanzo vya mionzi.

c) Asilimia 83 ya vituo vyenye vyanzo vya mionzi vilivyosajiliwa havikukaguliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 mpaka 2021/22

Ukaguzi ulibaini kuwa, ukaguzi katika vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi haukufanywa ipasavyo na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 mpaka 2021/2022. Ukaguzi katika vituo vinavyomiliki vyanzo vya mionzi ulifanyika kwa asilimia kuanzia 7 hadi 16 ya vituo vyote vilivyosajiliwa vyenye vyanzo vya mionzi nchini kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 4.10.**

Kielelezo Na. 4.10: Tathmini ya Ukaguzi Uliofanyika katika Vituo vyenye Vyanzo vya Mionzi kuanzia Mwaka 2018/19 hadi 2021/22



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Kaguzi Zilizofanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania na Kanzidata ya Taasisi zenye Vyanzo vya Mionzi kuanzia Mwaka 2018/19 - 2021/22.

Kielelezo Na. 4.10 kinaonesha kuwa, katika mwaka wa fedha 2018/19, vituo 72 kati ya 960 sawa na asilimia 7 ya vituo vyenye mionzi nchini vilikaguliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Kwa mwaka 2020/21, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilikagua vituo 463 kati ya 1,092 sawa na asilimia 42 ya vituo vyote vinavyomiliki vyanzo vya mionzi. Pia, inaonesha kuwa, kwa mwaka 2021/22, huduma za ukaguzi zilipungua hadi asilimia 16, ambapo Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilikagua vituo vyenye vyanzo 185 tu vya mionzi kati ya 1169 vilivyosajiliwa nchini. Hali hii inamaanisha kwamba, asilimia 83 ya vituo vilivyosajiliwa havikukaguliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa, ukaguzi wa vituo vya mionzi unaofanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ulifanyika kwa kiasi kikubwa kwenye vituo vya afya tofauti na sekta zingine kama vile ujenzi, utafiti, uchimbaji madini, na viwanda. Hali hii inadhihirishwa na ukweli kwamba, kwa kipindi kilichopitiwa cha miaka minne ya fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilifanya ukaguzi wa wastani wa vituo 95 kwa vituo vya afya, 6 kwa vituo vya ujenzi, tano kwa viwanda, mbili kwa vituo vya utafiti, na ukaguzi mmoja kwenye vituo vya madini.

Sababu za kaguzi kupendelea zaidi vituo vya afya kuliko maeneo mengine ni pamoja na:

- i) Kuwapo kwa idadi kubwa ya vituo vya afya ambavyo tayari vimetambuliwa na kusajiliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika kanzidata yake ya vyanzo vya mionzi. Mapitio ya kanzidata kwa mwaka wa fedha 2021/22 yalionyesha kuwa, idadi ya vituo vya afya vyenye vyanzo vya mionzi vilikuwa 798 wakati kwa maeneo mengine vilikuwa 371 tu;
- ii) Uhaba wa rasilimali-watu hasa wakaguzi wa usalama wa mionzi na wakaguzi wasaidizi wa usalama wa mionzi katika Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Ilibainika kuwa, Tume haikuwa na wakaguzi wa usalama wa mionzi na ilikuwa na upungufu wa wakaguzi wasaidizi wa usalama wa mionzi kwa asilimia 92; na
- iii) Vyanzo vya mionzi katika vituo vya afya vinatumiwa zaidi kwa binadamu, hivyo huhitaji ukaguzi kufanyika ili kuepuka matokeo hasi ambayo yanaweza kutokea kutokana na kiwango kisichotarajiwa cha mionzi kwa mwili wa binadamu kinachoweza kuleta madhara ya kiafya.

Kutofanyika kwa kiwango cha kutosha cha ukaguzi uliofanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kulichangia kuwako kwa utekelezaji usioridhisha wa mahitaji ya usalama katika vituo vyenye vyanzo vya mionzi. Hayo yalithibitishwa katika vituo vilivyotembelewa katika sekta ya ujenzi (ofisi za mikoa za Wakala wa Barabara Tanzania) ambapo, vyanzo vya mionzi vilibainika; kutunzwa vibaya bila kuwapo kwa tahadhari za mionzi; kukosekana kwa maofisa usalama waliopata mafunzo; na ubora duni wa majengo na uhifadhi duni wa vyanzo vya mionzi. Aidha, ukaguzi usioridhisha wa vituo vinavyotumia vyanzo vya mionzi nchini huongeza hatari za kiusalama kwa watumiaji wa vyanzo vya mionzi na wananchi kwa ujumla.

d) Utaratibu usioridhisha wa utendaji kazi katika udhibiti wa vyanzo vya mionzi

Ukaguzi ulibaini kuwa, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania iliandaa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Dharura za Nyuklia na Radiolojia ulioidhinishwa tarehe 11 Februari 2022. Hata hivyo, mchakato wa kuidhinishwa huo ulicheleweshwa kwa miaka miwili kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Nyaraka zote mbili zinalenga kuleta usalama katika matumizi ya vyanzo vya mionzi na kuzuia usafirishaji haramu wa vyanzo vya mionzi nchini. Pia,

ilibainika kuwa, vituo vilivyotembelewa vyenye vyanzo vya mionzi havikuwa na mpango wa dharura wa kukabiliana na radiolojia kama utaratibu wa kawaida wa uendeshaji katika ngazi ya kituo unavyotaka, kinyume na matakwa ya kanuni ya 34 (1) (V) ya Kanuni za Nishati ya Nguvu za Atomiki za Mwaka 2004.

Kutokuwapo kwa mpango wa dharura wa radiolojia na sheria na taratibu katika ngazi ya kituo, licha ya hatari zilizopo katika utunzaji duni wa vyanzo vya mionzi na kuwapo kwa vifaa vya mionzi visivyotumika kunaonesha hatari ya kutokea kwa ajali zisizodhibitiwa zinazohusisha vyanzo vya mionzi.

Aidha, ilibainika kuwa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilikuwa na uhaba wa vifaa vya ukaguzi wa kisayansi katika ofisi za kanda, mikoa, na mipakani kwa asilimia 72. Hata hivyo, Tume haikufanya uchambuzi wa mahitaji juu ya aina na idadi na kutenga bajeti sahihi inayohitajika ili kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya ukaguzi wa mionzi. Hali hii ilisababisha Tume kutokuwa na mipango na bajeti ya ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kudhibiti mionzi, hivyo kuathiri shughuli za ukaguzi kwa taasisi zenye vyanzo vya mionzi nchini.

Vilevile, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikuhakikisha vya kutosha kuwa vifaa vya kutolea mionzi vilivyopo kwenye vituo vyote vya tiba na visivyo vya tiba vinaendeshwa na wataalamu wenye sifa. Hali hii inatokana na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kutosajili ipasavyo wataalamu wote, hasa wa radiolojia, ambao wanatakiwa kupewa leseni za uendeshaji na kuzihusha kila baada ya miaka mitano. Ilibainika kuwa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilitoa leseni kwa wastani wa asilimia 67 kwa wataalamu waliosajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Radiolojia na Taswira Tanzania kwa miaka mitatu ya kalenda kuanzia mwaka 2020 hadi 2022.

Uchambuzi zaidi wa vituo visivyo vya tiba hususani Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Wakala wa Barabara Tanzania umebaini kuwa baadhi ya maafisa wanaohusika na uendeshaji wa vifaa vya mionzi hawakuwa na sifa kwa kuwa hawakuhudhuria mafunzo ya usalama wa mionzi yanayoandaliwa na kutolewa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Hali hii ilibainika katika viwanja 7 vya ndege na ofisi tano za Wakala wa Barabara Tanzania zilizotembelewa na timu ya ukaguzi.

Matokeo yake, maafisa hao walikutwa wakifanya kazi kwa kutumia vyanzo vya mionzi kama vile vifaa vya nyuklia vya kupimia udongo na skana za

mizigo kwa tahadhari za usalama wa mionzi. Kwa mfano, maofisa usalama wote wa mionzi katika ofisi tano za Wakala wa Barabara Tanzania zilizotembelewa walikuwa wakitumia vifaa vya nyuklia vya kupimia udongo bila kuchukua hatua za kutosha za tahadhari za kiusalama.

Zaidi ya hayo, Tume ilipoteza makadirio ya mapato ya kiasi cha shilingi milioni 54.4 kutokana na kutowasajili baadhi ya watu kwa kipindi kilichofanyiwa uhakiki.

Mifumo duni ya utendaji kazi wa kudhibiti vyanzo vya mionzi ilihusishwa hasa na:

- (i) Kuchelewa kuidhinishwa na kutekelezwa kwa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Dharura za Nyuklia na Radiolojia kwa miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi 2021/22;
- (ii) Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kuchelewa kutekeleza matakwa ya Sheria ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2011 za usajili wa wataalamu wenye sifa kwa kipindi cha miaka 17 tangu ilipopewa mamlaka ya kufanya hivyo kwa kifungu cha 25 (1)) cha Sheria ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003;
- (iii) Ukaguzi ulibaini kuwa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikufanya tathmini ya mahitaji juu ya aina na kiasi cha vifaa vya ukaguzi vinavyohitajika ili kurahisisha shughuli za ukaguzi. Kutokana na hali hiyo, Tume iliendelea kutoa taarifa za kuwa na upungufu wa vifaa vya ukaguzi wakati haikufanya uchambuzi wa mahitaji; Na
- (iv) Uimarishaji wa shughuli za ukaguzi katika makao makuu ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania pekee na kuziacha ofisi za kanda na za mipakani. Hali hii ilisababisha mipango ya ukaguzi na bajeti kuandaliwa na kuratibiwa kutokea makao makuu pekee.

e) Ufuatiliaji usioridhisha wa vyanzo vya mionzi

Ukaguzi ulibaini kuwa, kaguzi zilizofanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania hazikuleta tija iliyotarajiwa kwani vituo vilivyokaguliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania viliendelea kuwa na dosari zile zile. Hali hii ilithibitishwa na timu ya ukaguzi kupitia ukaguzi kwenye vituo vinane vya kitabibu na vituo 13 visivyo vya kitabibu, ambapo ukaguzi ulibaini kuwapo

kwa mapungufu yaliyobainishwa awali na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa vituo 8 kati ya 13 vya kitabibu na visivyo vya kitababu vilivyotembelewa havikuwa na vifaa vya kufuatilia mionzi (mita za uchunguzi), na ishara na alama za kutosha za tahadhari ya mionzi.

Zaidi ya hayo ilibainika kuwa, vituo vyote 21 vilivyotembelewa vilivyokuwa na vyanzo vya mionzi sawa na asilimia 100 havikuwa na mpango wa usimamizi wa taka; vituo 17 kati ya 21 sawa na asilimia 81 vilikosa mita za upimaji kwa ajili ya kufuatilia uvujaji wa mionzi kutoka kwenye vituo hivyo; na vituo 8 kati ya 21 sawa na asilimia 38 havikuwa na sheria na taratibu za usalama wa mionzi. Aidha, vituo 10 kati ya 21 sawa na asilimia 48 vilikutwa na vifaa duni vya usalama kama vile ngao za gonadi, aproni za risasi, glavu, na miwani; na vituo vinne kati ya vinane vya matibabu sawa na asilimia 50 havikuwa na eneo la kusubiri wagonjwa.

Hali hii ilichangiwa na ukosefu wa elimu ya kutosha juu ya matumizi salama ya vyanzo vya mionzi na kukosekana kwa ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania wakati wa ukaguzi wa vituo vyenye vyanzo vya mionzi. Kuwapo kwa mapungufu katika majengo yenye vyanzo vya mionzi kuna athari si tu kwa watendaji kupata dozi za juu za mionzi zaidi ya viwango vinavyopendekezwa lakini pia husababisha athari za radiolojia kwa wananchi na mazingira kwa ujumla hivyo kuchangia ongezeko la athari mbaya za kiafya kwa umma.

Mapitio ya utoaji wa huduma za mita za upimaji wa mionzi zilizotolewa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22 yalibainisha kuwa, vituo vilivyokuwa vinamiliki vyanzo vya mionzi katika nyanja mbalimbali kama vile uchunguzi wa kitabibu, uchakataji wa madini, utafiti, na ujenzi ni nadra kuwa na mita za upimaji kwa ajili ya ufuatiliaji wa mionzi katika maeneo yao. Kiwango cha vituo ambavyo havikuwa na mita za upimaji kwa ajili ya ufuatiliaji wa majengo yenye vyanzo vya mionzi kilianzia asilimia 91 hadi 100 katika sekta tofauti. Shughuli za ujenzi na vituo vya matibabu vilikuwa na upungufu wa zaidi ya asilimia 99 ya mita za uchunguzi kwa ajili ya ufuatiliaji wa vituo vyao.

Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 30 (1) na (2) cha Sheria ya Nishati ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003 ambacho kinamtaka kila mwenye leseni kuwa na vifaa vya uchunguzi wa mionzi kwa ajili ya ufuatiliaji mahali pa

kazi. Pia, kanuni inataka kupelekwa kwa vifaa hivyo kwenye maabara iliyoidhinishwa ya upimaji wa mionzi angalau mara moja kwa mwaka na kila baada ya matengenezo yake kwa ajili ya urekebishaji.

Aidha, kupitia uhakiki wa ukaguzi katika vituo 21 vilivyochaguliwa vyenye vyanzo vya mionzi, hakukuwa na kituo hata moja kati ya vituo nane vya afya na sita katika vya sekta ya ujenzi kilichokuwa na mita za upimaji wa mionzi. Kwa upande wa viwanja vya ndege vilivyotembelewa, vinne kati ya saba vilikutwa na mita za upimaji wa mionzi. Aidha, mita nne za upimaji mionzi zilizokutwa katika viwanja vya ndege vilivyotembelewa hazikupimwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania wala kuendeshwa na maofisa usalama wa mionzi wenye sifa, na hazikutumiwa kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Upungufu wa mita za upimaji kwa watumiaji wenye vyanzo vya mionzi ulichangiwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kutotimiza wajibu wake wa kisheria wa kutoa elimu kwa watumiaji wa vyanzo vya mionzi.

Vituo vyenye vyanzo vya mionzi visivyo na mita za upimaji wa mionzi vinaweza kupata athari za mionzi kutokana na hitilafu za vyanzo vya mionzi na kusababisha athari za kiafya kwa wafanyakazi na umma.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na ufuatiliaji usioridhisha wa kiwango cha mionzi kwa watumishi wanaofanya kazi kwenye mazingira yenye vyanzo vya mionzi katika sekta zisizo za afya ikiwa pamoja na sekta za usalama, madini, ujenzi na viwanda. Ilibainika zaidi kuwa, kwa kipindi cha miaka minne ya fedha kuanzia mwaka 2018/2019 hadi 2021/22, wastani wa asilimia 96.5 ya vituo visivyo vya afya nchini havikupatiwa kifaa cha kupimia mionzi yenye chaji kurekodi na kufuatilia kiwango cha mionzi ambacho mtu anayefanya kazi katika mazingira yanayohusisha matumizi ya vyanzo vya mionzi anapata.

Kutotolewa kwa vifaa vya kupimia mionzi kwa wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye mazingira yenye vyanzo vya mionzi visivyo vya kitabibu kunaweza kuhatarisha afya zao kulingana na kiwango cha mionzi wanachopata wakati wa kufanya kazi.

Kupitia ukaguzi wa kitabu cha kumbukumbu za vifaa vya kupimia mionzi vya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kwa miaka ya fedha kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22, ilibainika kuwa vituo 199 vya afya kati ya 793 sawa na asilimia 25 vilipewa vifaa vya kupimia mionzi kwa mwaka wa fedha 2021/22. Hali hii iliashiria usambazaji mdogo wa vifaa vya kupimia mionzi

kwenye vituo vya afya kwa kipindi chote cha ukaguzi huu. Kwa upande mwingine, vituo 263 kati ya 480 vya afya sawa na asilimia 55 vilipewa vifaa vya kupimia mionzi kwa mwaka 2019/20. Huu ni mwaka ambao vifaa vya kupimia mionzi vilitolewa zaidi katika kipindi cha miaka minne ya fedha iliyokaguliwa.

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania pia haikufuatilia na kusajili vyanzo 16 vya mionzi vinavyohamishika vilivyokutwa katika ofisi 7 za kanda za Wakala wa Barabara Tanzania zilizotembelewa. Hakukuwa na chanzo chochote cha mionzi kinachohamishika katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza kilichosajiliwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Hata hivyo, Mkoa wa Mtwara ulikuwa na vyanzo 4, Mkoa wa Arusha ulikuwa na vyanzo 2, na Mkoa wa Dodoma ulikuwa na 6. Katika daftari la Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kulikuwa na chanzo kimoja tu katika kila mkoa.

Chanzo cha mionzi ya simu ambacho hakijasajiliwa pia kilihifadhiwa kwa njia isiyofaa kinyume na matakwa ya kifungu cha 20 cha Sheria ya Nishati ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003.

Kukosekana kwa taarifa za uhakika za vyanzo vya mionzi inayohamishika kulitokana na ukweli kwamba Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikuwa na utaratibu mzuri wa kufuatilia mienendo ya vyanzo vya mionzi inayohamishika nchini hali iliyosababisha vyanzo kadhaa kusafirishwa ndani ya nchi, kuazimwa, au kuhamishiwa kwa watumiaji wengine bila taarifa ya mabadiliko hayo kuidhinishwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

Kushindwa kuwa na kanzidata iliyohuishwa ya vyanzo vya mionzi inayohamishika kulisababisha kuwapo kwa vyanzo vya mionzi inayohamishika vinavyosimamiwa vibaya. Usimamizi usioridhisha wa vyanzo vya mionzi inayohamishika unaweza kusababisha hatari kwa watumiaji pamoja na umma kwa kuathiriwa na mionzi inayozidi kiwango cha chini cha mionzi ambayo inaruhusiwa kwa mtu kwa mwaka.

f) Uhusiano hafifu kati ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania na Wadau wengine katika kudhibiti vyanzo vya mionzi

Ukaguzi ulibaini kuwa ushirikiano uliokuwapo kati ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania na vyuo vikuu ulihusu vyuo vikuu 3 tu kati ya 30 vilivyoidhinishwa nchini na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kufikia mwezi Mei 2022. Hali hii ilitokana na vyuo vikuu mbalimbali kutokuwa na miundombinu ya kutosha ya kujifunzia hali ambayo ingeongeza ushirikiano kati yake na

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika taaluma na utafiti. Hali hii ilizuia usambazaji wa mapema wa teknolojia za sayansi ya nyuklia kwa wasomi wengi nchini Tanzania ambayo hatimaye ingeathiri malengo ya kimkakati ya nchi ya kukuza matumizi salama ya nishati ya atomiki.⁸

Aidha, ilibainika kuwa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikuhamasisha vya kutosha watumiaji mbalimbali wa vyanzo vya mionzi kama vile sekta za tiba, viwanda, madini, na shughuli za ujenzi. Hali hii ilichangiwa na kutoingizwa kwa mafunzo na semina katika mipango yao ya mwaka wa fedha kwa miaka miwili ya fedha ya 2018/19 na 2019/20 kinyume na lengo D la mpango-mkakati wake ulioidhinishwa wa kuanzia mwaka 2018/19 hadi mwaka 2022/23. Utoaji usioridhisha wa mafunzo na uhamasishaji kwa watumiaji wa vyanzo vya mionzi unahusishwa na kukosekana kwa ujuzi wa kutosha kwa watumiaji juu ya kuzingatia viwango vya usalama wakati wa kumiliki, kutumia, au kusafirisha vyanzo vya mionzi na usalama wa vyanzo vya mionzi. Uhakiki uliofanywa na timu ya ukaguzi ulibaini kuwa, maofisa wote wanaofanya kazi kwenye mazingira yenye mionzi katika vituo visivyo vya afya vilivyotembelewa, ambavyo ni viwanja vya ndege 7 na ofisi 5 za Wakala wa Barabara Tanzania walikutwa hawajavaa vifaa vya kujikinga na mionzi kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha juu ya hatari zinazohusiana na kutofanya kazi kwa kuzingatia usalama kwa kutumia vifaa vinavyotumia mionzi.

g) Tathmini na ufuatiliaji usioridhisha wa utendaji kazi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika kudhibiti vyanzo vya mionzi

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikuwa na mpango wa kina wa ufuatiliaji na tathmini katika kukuza na kudhibiti teknolojia ya nyuklia. Mapitio ya Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Sekta ya Elimu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wa Mwaka 2015/16 - 2020/21 yalibaini kuwa Mpango huo haukujumuisha shughuli zinazohusiana na udhibiti wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia. Mpango huo ulijikita zaidi katika ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya elimu ya msingi.

Aidha, ufuatiliaji wa lengo F katika mpango-mkakati wa Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia wa kuanzia mwaka 2016/17 - 2020/21 ulibaini kuwa ni uendelezaji na udhibiti wa utekelezaji wa teknolojia za nyuklia

⁸<https://www.tcu.go.tz/sites/default/files/list%20of%20university%20institutions%20in%20tz%20as%20of%2012%20may%202022%20final.pdf>

unaotekelezwa na Wizara. Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa mpango wa ufuatiliaji usiokuwa na utaratibu na muda maalumuwa kutoa taarifa za sehemu/kitengo kinachowajibika kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya viashiria vya utendaji vilivyobainishwa.

Vilevile, mapitio ya Ripoti za Utekelezaji wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji yalibaini kuwa Wizara ilijikita zaidi katika kufuatilia wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa ambayo inatekelezwa chini ya Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania na kuweka umakini mdogo katika shughuli za udhibiti na uendelezaji kama vile utoaji leseni, ukaguzi, utafiti/uchapishaji, na usafirishaji haramu wa vyanzo vya mionzi katika vituo vya mipakani. Hali hii ilisababishwa zaidi na kuwapo kwa mipango isiyoridhisha ya Wizara, kutokana na ukweli kwamba katika kipindi chote cha ukaguzi, Wizara ilipanga kufuatilia na kutathmini miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Nishati ya Nguvu za Atomiki.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kwenye shughuli za udhibiti wa mionzi. Badala yake, mpango uliokuwapo ulihusu sekta ya elimu pekee. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pia haikuwa na viashiria na malengo ambayo yangeweza kuripotiwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ili kuiwezesha Wizara kufanya tathmini ya utendaji wa Tume. Hata hivyo, katika mpango-mkakati wake imeoneshwa wazi kwamba ufuatiliaji ulipaswa kufanywa kupitia taratibu za ndani za ukusanyaji wa data kwa utaratibu wa kutumia viashiria maalumu, data ya msingi, na viashiria vinavyolenga maadili kama ilivyooneshwa katika mpango wa ufuatiliaji.

Ufuatiliaji duni wa utendaji wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania uliofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pia ulichangiwa na ukweli kwamba shughuli nyingi za ufuatiliaji zilitegemea masuala yenye msisimko hasa ya utendaji wa bajeti, na masuala yaliyoibuliwa na Bunge na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au kutoka kwa Waziri mwenye dhamana.

Hivyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikufuatilia na kutathmini ipasavyo utendaji wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kuhusu shughuli za udhibiti na uendelezaji hivyo kuifanya Wizara kukosa taarifa za kutosha za utendaji halisi wa Tume kuhusu udhibiti na uendelezaji wa teknolojia za nyuklia.

Ufuatiliaji na tathmini duni ya utendaji kazi wa udhibiti unaofanywa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania pia ulisababisha utendaji duni katika kutekeleza majukumu ya udhibiti wa mionzi kama vile kutoa leseni kwa watumiaji wa vyanzo vya mionzi, ukaguzi wa vifaa vya mionzi, na kuhakikisha kuwa watu wanaosimamia mionzi yenye chaji wamesajiliwa.

4.7 Athari kwa Ufikiaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Dosari katika udhibiti wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya, umesababisha zaidi ya asilimia 80 ya vituo binafsi na hiari vya kutolea huduma za afya kushindwa kufikia nyota tatu katika utoaji wa huduma za afya. Jambo hili linaashiria kuwa ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo hivyo hauko katika viwango vinavyokubalika na Wizara ya Afya. Hali hii imeathiri juhudi muhimu za serikali katika sekta ya afya ambazo zinalenga kukuza na kusaidia uwekezaji wa sekta binafsi katika mnyororo wa usambazaji wa bidhaa za afya chini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26).

Udhibiti usioridhisha wa vituo binafsi vya afya pia umesababisha ubora mdogo wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi. Hali hii itasababisha kutofikiwa kwa lengo namba 3.8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalotaka kuwa na chanjo ya afya kwa wote, ulinzi wa athari za kifedha, upatikanaji wa huduma bora muhimu za afya, na upatikanaji wa dawa salama, bora, na za bei nafuu.

Mapungufu yaliyobainishwa kuhusu udhibiti wa malipo yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa vituo vya afya unaweza kusababisha hasara ya kifedha. Hasara hii inaweza kuathiri maendeleo ya Mfuko hivyo kushindwa kufikia lengo la Serikali la huduma ya bima ya afya kufikia asilimia 80 ya idadi ya watu kufikia mwaka 2025/26 kama ilivyopangwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Kwa upande mwingine, udhibiti usiojitosheleza wa vyanzo vya mionzi unaweza kuathiri maisha ya watu, hivyo kusababisha kutofikiwa kwa lengo la 3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu la kuhakikisha maisha yenye afya na kukuza ustawi kwa rika zote. Mapungufu haya yanaweza pia kuathiri mipango muhimu ya Serikali chini ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unalenga kukuza nishati ya atomiki na teknolojia za nyuklia nchini.

4.8 Hitimisho la Ukaguzi

Kwa ujumla, ukaguzi huu unahitimisha kuwa Wizara ya Afya; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haijasimamia ipasavyo utoaji wa huduma za afya kwa kuhakikisha kuwa udhibiti wa vituo vya afya unafanyika kwa mujibu wa taratibu na viwango vilivyowekwa; kuna udhibiti madhubuti katika vyanzo vya mionzi; na madai kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya yanadhibitiwa ipasavyo ili kulinda afya za watu.

Hitimisho hili linatolewa kwa sababu ingawa Wizara ya Afya ilitekeleza majukumu yake ya kudhibiti vituo binafsi na vya hiari vya huduma za afya kupitia bodi ya udhibiti wa vituo binafsi vya afya, bado kulikuwa na mapungufu katika udhibiti utoaji wa huduma za afya katika vituo binafsi na hiari vya huduma za afya kuwa wa ubora wa chini ya unaokubalika.

Pia, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uliweka udhibiti mbalimbali katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuhakikisha huduma bora za afya zinatolewa kwa walengwa wa mfuko huo. Mfuko uliweka udhibiti mbalimbali wakati wa kushughulikia madai yaliyotolewa na vituo vya afya ili kuhakikisha madai ni ya kweli. Hata hivyo, utoaji wa huduma za afya kwa vituo vya huduma za afya vilivyoidhinishwa unahusishwa na kutozingatiwa ipasavyo kwa miongozo ya kawaida ya matibabu na makubaliano ya kimkataba wakati wa utoaji wa huduma ya bima ya afya kwa walengwa wanaostahili; kushindwa kwa mifumo ya udhibiti iliyopo ndani ya Mfuko wa Bima wa Taifa kuhakikisha kwamba madai yaliyochakatwa na kulipwa ni ya kweli, sahihi na yamekamilika; kushindwa kuchukua hatua kwa wakati kurekebisha madai yasiyo ya kweli ili kupunguza hasara za kifedha; na tathmini duni ya utendaji.

Aidha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania zimechukua juhudi mbalimbali ili kuhakikisha vyanzo vya mionzi vinadhibitiwa ipasavyo. Hatua hizo ni pamoja na ujenzi wa maabara kuu Jijini Arusha na maabara zingine tano katika mikoa mitano ili kuwezesha udhibiti wa vyanzo vya mionzi. Hata hivyo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, haikudhibiti ipasavyo vyanzo vya mionzi ili kuzuia hatari za mara kwa mara kwa watumiaji, umma na mazingira. Hali hii ilisababishwa na mapungufu yaliyobainika kama vile kutotoa leseni vya kutosha kwa wataalamu wenye

sifa stahiki ambao kutokana na kazi zao hutoa mionzi kwa wagonjwa; kuwapo kwa vituo vingi vinavyofanya kazi za mionzi bila leseni halali; na kukosekana kwa vifaa vya kujikinga na mionzi. Mapungufu mengine ni kutofanyika kwa kaguzi za kutosha kwenye vituo vinavyotumia vyanzo vya mionzi; ukosefu wa mfumo thabiti wa kufuatilia vyanzo vya mionzi ambavyo havitumiki; na kukosekana kwa mpango wa dharura na maandalizi katika ngazi ya vituo vyenye vyanzo vya mionzi. Mapungufu haya yote yanahitaji juhudi zaidi kufanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania.

Mapungufu yaliyobainika katika shughuli husika za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; na Wizara ya Afya yanahitaji jitihada madhubuti ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza. Hivyo, uingiliaji kati wa jumla utaharakisha kufikiwa kwa lengo la Tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26) kuhusu kuimarisha mifumo ya usimamizi wa huduma za afya na upatikanaji na utoaji wa huduma za afya.



SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

SURA YA TANO

5



SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UBUNIFU

5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi yaliyotokana na kaguzi mbili za ufanisi ambazo ni usimamizi wa mipango na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini na usimamizi wa shughuli za utafiti na ubunifu. Sura inatoa maelezo mafupi kuhusu uhusiano kati ya sayansi, ubunifu na teknolojia na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP) na Malengo ya Maendelo Endelevu (SDGs). Inaelezea pia mikakati na juhudi za Serikali kuhusu sayansi, ubunifu na Teknolojia. Sehemu zingine za sura hii ni malengo na wigo wa ukaguzi; matokeo ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendelo Endelevu; pamoja na hitimisho la ukaguzi.

5.2 Usuli

Utafiti na ubunifu unaweza kuboresha viwango vya maisha ya watu kwa kuchochea ukuaji na kuongeza tija katika sekta muhimu za uchumi. Katika kampuni za biashara, utafiti na ubunifu unaweza kuleta ubunifu wa bidhaa mpya; uboreshaji wa bidhaa zilizopo; na kuongezeka kwa huduma, ufanisi, na utendaji kazi bora katika soko. Yote haya yanaweza kutokea iwapo utafiti unaofanywa unatokana na mahitaji ili matokeo yatumike kutatua changamoto za kijamii na za kimaendeleo ambazo ni vikwazo kwa watu.

Vilevile, matumizi ya mifumo ya TEHAMA Serikalini na ndani ya taasisi zake yamezidi kuwa muhimu katika miongo ya hivi karibuni, hasa kufuatia mabadiliko makubwa ya kompyuta, vifaa vyake, na matumizi ya mitandao ya mawasiliano. Serikali kupitia mamlaka zake zinazohusika inasonga mbele kuelekea kwenye kuhuisha shughuli za biashara kwenye mifumo kwa kusambaza na kutumia TEHAMA katika usimamizi wa wazi na kwa urahisi wa shughuli zake za kila siku za uongozi na utawala.

Pamoja na juhudi kubwa, mipango ya TEHAMA imeendelea kukabiliwa na changamoto ambazo zinahitaji ufumbuzi wa haraka na wa muda mrefu ili kuwezesha uendeshaji wa Serikali mtandao kwa njia salama. Vilevile, utafiti na ubunifu haujatimizwa kikamilifu kwa sababu ni matokeo machache tu ya utafiti na ubunifu ambayo yamebadilishwa kuwa matokeo halisi. Hali hii inaweza kuchangiwa na usimamizi duni katika utafiti na ubunifu.

5.3 Uhusiano wa Sayansi, Ubunifu na Teknolojia na Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kaguzi hizi mbili za ufanisi zina uhusiano katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Ripoti ya ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa shughuli za utafiti na ubunifu, ina uhusiano na maeneo ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yanayohusiana na kutambua uchumi jumuisi na wa ushindani, na ukuzaji wa ujuzi mablimbali. Hatua zinazochukuliwa kushughulikia maeneo hayo mawili ya kipaumbele ni pamoja na kuimarisha taasisi kwa ajili ya ushindani na kuimarisha mafunzo.

Kwa upande mwingine, ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa mipango na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini unahusishwa na maeneo mawili ya kipaumbele ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yanayolenga kufikia uchumi shirikishi na shindani pamoja na kuimarisha ukuaji wa viwanda na utoaji wa huduma. Maeneo haya mawili ya kipaumbele yanatoa tathmini ya uingiliaji kati unaohusiana na taasisi zinazosaidia kwa ushindani na sayansi, uvumbuzi na teknolojia.

Kaguzi zote mbili zinashughulikia lengo namba 9 la Ajenda ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030 linalotaka kuimarisha utafiti wa kisayansi, kuboresha uwezo wa kiteknolojia wa sekta za viwanda katika nchi zote, kuhimiza ubunifu, na kuongeza kwa kiasi kikubwa idadi ya tafiti na maendeleo. Malengo yaliyo chini ya lengo hili ni pamoja na:

- (a) Kuendeleza miundombinu iliyo bora, ya kutegemewa, endelevu, na stahimilivu ikijumuisha usafiri, maji na usafi wa mazingira, na mifumo ya nishati;
- (b) Kukuza uanzishaji wa viwanda shirikishi na endelevu na kuongeza sehemu ya viwanda katika ajira na pato la taifa;
- (c) Kuimarisha utafiti wa kisayansi na uwezo wa kiteknolojia, hasa katika nchi zinazoendelea, na kukuza ubunifu; na
- (d) Kuboresha sekta zote ili ziwe endelevu zaidi kupitia ubunifu wa kiteknolojia na kuongeza ufanisi wa rasilimali.

Zaidi ya hayo, ukaguzi huu una uhusiano wa moja kwa moja na lengo namba la 17 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa linalotaka kujenga taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika, na shirikishi katika ngazi zote. Uboreshaji wa namna Mifumo ya TEHAMA inavyojengwa itakayosababisha kupatikana kwa mifumo bora na yenye ufanisi serikalini itakuza uwajibikaji na ushirikishaji katika taasisi katika ngazi zote.

Kwa madhumuni ya kuboresha uchumi shindani, sayansi, ubunifu na teknolojia ni muhimu sana kwa sababu inakuza ujasiriamali na ubunifu katika tasnia, na kuboresha ufikiaji wa teknolojia na maarifa. Kwa kuwekeza katika utafiti na ubunifu, nchi inaweza kupata ubunifu mpya kwa changamoto zinazokabili taifa na kufikia mustakabali endelevu kwa wote.

Zaidi ya hayo, mifumo ya TEHAMA ya Serikali inachangia katika kutoa huduma za serikali kwa kutekeleza masuluhisho ya serikali kielekitroniki, na kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika utoaji huduma, jambo linaloweza kusaidia kufikia malengo ya jumla ya maendeleo ya nchi.

5.3.1 Mikakati na Juhudi za Serikali katika Sayansi, Ubunifu na Teknolojia



Serikali imechukua hatua kadhaa za kuhakikisha sayansi, teknolojia na ubunifu unaimarishwa kwa madhumuni ya kuongeza ushindani na tija katika sekta mbalimbali hususani za uzalishaji, viwanda na huduma. Zifuatazo ni hatua kuu za kimkakati za Serikali na juhudi za kuboresha sayansi, ubunifu na teknolojia:

- (a) Kuundwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia mwaka 1988 ili kuratibu na kukuza shughuli za utafiti na maendeleo ya teknolojia nchini;
- (b) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao mwaka 2019 ili kusimamia, kuratibu na kukuza uendeshaji wa huduma za serikali mtandao; na kusimamia taarifa za kielekitroniki na masuala mengine yanayohusiana na TEHAMA katika taasisi za serikali;
- (c) Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa tafiti na mawasiliano katika viwanda, elimu ya juu, na utafiti; na
- (d) Kuimarisha mifumo ya kielekitroniki ya uwasilishaji na ujenzi wa uwezo kwa ajili ya usimamizi wa taarifa kwa wafanyakazi wanaohusika na kuripoti matokeo ya utafiti katika ngazi ya taasisi.

Zaidi ya hayo, Serikali kupitia wakala zake imepanga kuboresha usimamizi wa vumbuzi na tafiti kwa kuongeza utoshelevu katika usajili wao. Pamoja

na Serikali kuwa na mpango wa kuendeleza ubunifu, pia ina mipango ya kuhakikisha asasi za maendeleo kupitia tume imara, inasaidia shughuli zinazohusiana na ubunifu kama vile kampuni ndogo na za kati, vituo, maabara, na mitandao ya uundaji shirikishi ili kuhakikisha kuna usimamizi mzuri wa utafiti na ubunifu.

Serikali imefanya jitihada kadhaa za kuboresha sayansi, ubunifu na teknolojia kupitia Mamlaka ya Serikali Mtandao katika utendaji kazi wake serikalini kwa kulenga kuwa na ubadilishanaji wa taarifa kati ya taasisi za umma ufanyike kupitia mtandao wa Serikali ulio salama au miundombinu iliyoidhinishwa na Mamlaka.

Kwa lengo la sayansi na teknolojia, Serikali kupitia taasisi zake za umma ilipanga kuendeleza na kutekeleza mfumo wa ubora wa huduma kwa wateja kwa wananchi pamoja na manufaa ya kutumia shughuli za Serikali mtandao. Hatua hii ni kiashirio cha utendaji kazi katika matumizi ya teknolojia kama vile mifumo ya akili bandia (Artificial Intelligencena TEHAMA kwa ujumla.

5.4 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha malengo na mawanda ya ukaguzi kwa Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Mandeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

5.4.1 Lengo la Ukaguzi

Ukaguzi huu ulilengakutathmini endapo sayansi, ubunifu na teknolojia nchini unasimamiwa kwa namna inayoboresha uanzishaji na matumizi yake ndani ya uchumi na jamii ili kuwezesha utoaji wa huduma na ukuaji wa uchumi wa nchi.

Malengo mahsusi yalikuwa kutathmini endapo:

- (a) Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mamlaka ya Serikali Mtandao ilisimamia ipasavyo mipango na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini nchini kwa namna ambayo inahakikisha manufaa yanayotarajiwa yanafikiwa na athari zinapunguzwa; na
- (b) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania zinasimamia ipasavyo utafiti na ubunifu ili kukuza ubunifu na teknolojia nchini.

5.4.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi huu ulihusisha taasisi kuu nne ambazo ni Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Mamlaka ya Serikali Mtandao; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Tume ya Sayansi na Teknolojia.

Lengo la ukaguzi katika kutathmini mikakati na mipango iliyoandaliwa, lilikuwa kuchunguza mipango iliyopo kuhusu majukumu ya COSTECH ya kusajili tafiti na bunifu nchini. Vilevile, ukaguzi ulijikita katika kubainisha endapo rasilimali zilizopo zimetengwa kikamilifu ili kuhakikisha kuna utekelezaji mzuri wa mipango iliyopo.

Hata hivyo, ukaguzi ulilenga kutathmini ufanisi wa Mamlaka katika kusimamia uanzishwaji wa mfumo wa TEHAMA, ukusanyaji wa mahitaji na uundaji wa vipimo, utekelezaji wa uundaji wa mifumo ya TEHAMA inayopendekezwa, upimaji na uanzishaji wa mifumo na usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini.

Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka minne ya fedha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22. Kipindi hiki kilichaguliwa mahsusi ili kuonesha mwelekeo wa utendaji wa taasisi zilizokaguliwa kwa kuzingatia maeneo ya ukaguzi yaliyobainishwa.

5.5 Matokeo ya Ukaguzi

Matokeo ya ukaguzi yamewekwa katika makundi mawili kulingana na ukaguzi husika. Kundi la kwanza ni matokeo yanayohusiana na shughuli za utafiti na ubunifu na kundi la pili ni usimamizi wa mipango na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini. Masuala haya yanafafanuliwa hapa chini.

5.5.1 Matokeo ya ukaguzi kuhusu shughuli za utafiti na ubunifu

Kiwango cha usimamizi wa shughuli za utafiti na ubunifu

Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania ilifanya mapitio ya utendaji wa utekelezaji wake wa mpango-mkakati wa miaka mitano (2016/17-2020/21) ikijumuisha utafiti na usimamizi wa ubunifu. Mapitio hayo yalibaini kufikiwa kwa mafanikio kadhaa katika utekelezaji wa malengo ya kimkakati ya Tume kama vile kutoa mafunzo ya kufanya maamuzi yanayozingatia ushahidi kwa taasisi 15 kati ya 100 zilizopangwa na kuchangia katika kuimarisha utamaduni wa kufanya maamuzi kwa kuzingatia ushahidi.

Zaidi ya hayo, dosari zifuatazo zilibainika wakati wa utekelezaji wa utafiti na ubunifu nchini.

(a) Mikakati na mipango isiyojitosheleza katika utambuzi na usajili wa shughuli za utafiti na ubunifu

Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa shughuli za utafiti na ubunifu umebaini kuwa, baadhi ya mafanikio katika utekelezaji wa malengo ya kimkakati ya tume ya sayansi na teknolojia ni kama vile kutoa uamuzi unaozingatia ushahidi; mafunzo kwa wakala 15 kati ya 100 za serikali zilizopangwa; na kutekeleza majukumu yake katika suala la kufanya usajili wa utafiti na utoaji wa vibali vya utafiti.

Hata hivyo, mapungufu yaufuatao yalibainika kuhusiana na mikakati na mipango iliyoandaliwa ya kutambua na kusajili shughuli za utafiti na ubunifu; kusimamia utafiti na ubunifu uliosajiliwa; kuratibu wadau wakuu; na ufuatiliaji. Haya yamefafanuliwa zaidi hapa chini.

(i) Utekelezaji duni wa mikakati na mipango iliyoundwa ya kutambua na kusajili tafiti na bunifu zote

Tume haikutekeleza ipasavyo mikakati na mipango yake ya kutambua na kusajili tafiti na ubunifu. Hata hivyo, iliweza kutoa mihtasari minne ya sera kati ya 15 iliyopangwa; kutoa mafunzo ya kufanya maamuzi kwa kuzingatia ushahidi kwa wizara, idara na wakala nne kati ya 100 zilizopangwa na kufanya midahalo 2 kati ya 5 iliyopangwa kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu. Hali hii ni kinyume na kifungu cha (1) cha mpango-mkakati (2016/17 hadi 2020/21) kilichopanga kufanya uchambuzi wa mahitaji ili kukabiliana na changamoto zote zilizoainishwa.

(ii) Usajili duni wa teknolojia na rasilimali za kiteknolojia za ndani na nguvukazi

Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania haikuwa imesajili Kituo cha Maendeleo na Uhamisho wa Teknolojia (CDTT) tangu kuanzishwa kwake kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania ya Mwaka 1986 inayoitaka kuunda kituo hicho kinachopaswa kutekeleza majukumu ya Tume katika masuala ya uhamisho wa teknolojia.

(iii) Utaratibu usio wazi wa kushauriana, kuratibu, na kusimamia ugawaji, mipango, na uamuzi wa fedha za shughuli za utafiti na ubunifu

Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania ilikosa mfumo wa kushauriana, kuratibu, na kusimamia shughuli zilizopangwa za utafiti na ubunifu kama inavyotakiwa kwa mujibu wa kifungu cha 5(e) cha Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania ya Mwaka 1986. Majukumu ya Tume ni kushauri, kuratibu na kusimamia uamuzi, upangaji na ugawaji wa fedha kwa taasisi za kitaifa za utafiti ili kuziwezesha kufanya utafiti wa miradi na programu ndani ya nyanja zao za utafiti. Kazi nyingine ni kuchunguza programu za utafiti na maendeleo za taasisi za utafiti za kitaifa ili kujua iwapo zimehusishwa na Tume au la na kushauri juu ya njia bora za kufikia malengo ya tafiti hizo.

(iv) Utaratibu usiotosheleza wa kutambua na kukuza ubunifu

Wizara na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania zilishindwa kubaini, kusajili na kuendeleza bunifu, vumbuzi na maarifa ya jadi kutokana na kukosekana kwa mfumo wa kufuatilia na kutambua wa bunifu. Tume ilisajili bunifu 154 sawa na asilimia 43.5 katika hatua ya maendeleo; asilimia 5.8 katika hatua ya biashara; na asilimia 13.6 katika hatua ya majaribio.

Hata hivyo, miradi ya ubunifu iliyokuwa inaendelea ambayo imesajiliwa na Tume katika taasisi zilizotembelewa ilikuwa bunifu 46 kati ya 160 sawa na asilimia 29 kutoka katika vituo vilivyotembelewa. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na uchaguzi wa kutosha wa wabunifu walioomba kupitia MAKISATU ambapo katika miaka mitatu walichaguliwa wabunifu 204 tu kati ya wawabunifu 1575 sawa na asilimia 13. Asilimia ya chini katika mwaka 2021 ikilinganishwa na miaka iliyopita inaweza kuashiria kuwa ushindani wa programu hiyo ulikuwa mkubwa zaidi na idadi kubwa ya waombaji kushindania idadi ndogo ya nafasi.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kati ya wavumbuzi 204 waliochaguliwa, 63 (asilimia 31) tu walipata msaada kutoka Tume ili kuendeleza ubunifu wao, huku wengine wakikosa. Kwa mujibu wa Ripoti ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa MAKISATU (2018/19), sababu kuu ilikuwa ukosefu wa fedha za kusaidia wavumbuzi wote waliochaguliwa hivyo kusababisha usaidizi usio endelevu kwa wavumbuzi waliochaguliwa.

Sababu zilizobainika za kuwapo kwa mikakati na mipango isiyotosheleza katika utambuzi na usajili wa shughuli za utafiti na ubunifu ni kama ifuatavyo:

- (i) Uratibu usio wazi kati ya Tume na taasisi za utafiti na maendeleo na taasisi za elimu ya juu** - Kulikuwa na mipangilio tofauti ya kitaasisi kati ya Tume na taasisi za utafiti na maendeleo na taasisi za elimu ya juu ambayo haikuhakikisha mipango yao inaendana na kuunga mkono utekelezaji wa mipango iliyotayarishwa na Tume kama inavyotakiwa na Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji wa Utafiti na Ubunifu unaokusudiwa kuhuishwa na kutekelezwa na taasisi za utafiti.
- (ii) Ukosefu wa kanuni zinazoeleweka** - Hali hii kwa kiasi fulani ilitokana na kukosekana kwa kanuni zilizoainishwa wazi za kutekeleza majukumu yake katika tathmini, usajili, na usimamizi wa mikataba ya uhamishaji wa teknolojia. Kutokana na hali hiyo, Kituo cha Maendeleo na Uhamisho wa Teknolojia kilikosa zana za kusajili na kutathmini mikataba ya uhamishaji wa teknolojia pamoja na taratibu za usajili na uendeshaji wa mikataba ya uhamishaji wa teknolojia na uwezo wa teknolojia zisizofungashwa.
- (iii) Kutokuwepo kwa miongozo** - Hali hii ilitokana na kukosekana kwa mfumo unaoisimamia Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania kushauriana, kuandaa, na kufuatilia utayarishaji na utekelezaji wa shughuli za taifa za utafiti na ubunifu. Kutokana na dosari hii, ilikuwa vigumu kupata taarifa zilizoombwa kuhusu mipango na ufadhili wa shughuli za utafiti na ubunifu kwa sababu taasisi zilikuwa na majukumu yake na ziliripoti moja kwa moja kwa wizara-mama.
- (iv) Ukosefu wa uratibu baina ya Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania na taasisi nyingine** - Moja ya sababu za msingi za tofauti hii ni kukosekana kwa uratibu kati ya Tume na vituo mbalimbali vya utafiti, maendeleo na ubunifu. Wakati wa mahojiano na wafanyakazi wa Tume, ukaguzi ulibaini kuwa Tume ilikosa kanzidata ya kufuatilia na kurekodi shughuli za ubunifu za kitaasisi zinazoendelea nchini.

Athari za mikakati na mipango isiyotosheleza katika utambuzi na usajili wa shughuli za utafiti na ubunifu

- (i) ***Tume kushindwa kuwezesha tafiti*** - Mapungufu makubwa yalikusiana na Tume kushindwa kutathmini ipasavyo kazi za utafiti zilizofanyika katika sekta; kusajili ipasavyo teknolojia na rasilimali za teknolojia ya ndani na nguvukazi; na kutambua na kusaidia Ubunifu za ndani na Ubunifukutoka nje.
- (ii) ***Kituo cha Maendeleo na Uhamisho wa Teknolojia kutokuwa na uhakika wa (CCDT) kutekeleza usajili wa teknolojia*** - Tume haikuweza kutimiza wajibu wake wa kuratibu, kufuatilia, na kuishauri serikali kuhusu namna bora ya kutumia rasilimali zilizopo za kiteknolojia na wafanyakazi kwa sababu Kituo cha Maendeleo na Uhamisho wa Teknolojia hakikuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo kuhusu uhamishaji wa teknolojia ya ndani na wafanyakazi. Hali hii inaweza pia kusababisha kushuka kwa teknolojia.
- (iii) ***Kuathiriwa kwa ukuaji wa uchumi*** - Kukosa kuwaunga mkono wavumbuzi waliochaguliwa kumekuwa na matokeo mabaya, kama vile kuu ari ya ubunifu miongoni mwa wavumbuzi wachanga ambao wanazuiwa kutumia teknolojia mpya, na humaanisha kupoteza nafasi za kazi miongoni mwa vijana. Hali hii ina inaweza kuzuia ukuaji wa uchumi wa nchi.

(b) Usimamizi duni wa shughuli za tafiti na vumbuzi zilizosajiliwa

Tume ya Sayansi na Teknolojia haikuwa na mpango wa kufuatilia shughuli zilizosajiliwa za utafiti na ubunifu kama inavyotakiwa na kifungu cha 3.9 cha Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo ya Mwaka 2000. Serikali haina budi kuimarisha kanuni na kufuatilia shughuli za utafiti nchini. Hata hivyo, mapungufuyafuatao yalibainika kuhusiana na usimamizi wa shughuli za utafiti na ubunifu zilizosajiliwa.

(i) Urasimishaji kibiashara usioridhisha wa shughuli za ubunifu unaofadhiliwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Ukaguzi ulibaini kuwa Tume ya Sayansi na Teknolojia haikuhakikisha kunafanyika urasimishaji madhubuti wa kibiashara wa shughuli za ubunifu, kinyume na Mpango-mkakati wa Tume (2016/17-2020/21) unaotaka kukuza

uchumi wa viwanda nchini. Ubunifu wa kibiashara uliofadhiliwa na Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia haukufanywa ipasavyo kuanzia mwaka 2019 hadi 2021 ambapo kati ya vumbuzi 155, ni 9 tu ndizo zilirasimshwa kibiashara.

Sababu za usimamizi duni wa shughuli za utafiti na ubunifu zilizosajiliwa

- (i) ***Ukosefu wa miundombinu ya maendeleo*** - Ili kusaidia kuendeleza ubunifu ulioanzishwa hadi kufikia hatua ya kibiashara, kuna haja ya kuwa na miundombinu inayoweza kutumika kuhakikisha maendeleo ya ubunifu ulioanzishwa.
- (ii) ***Ufuatiliaji duni wa Ubunifu uliotajwa*** - Ilibainika kuwa maendeleo ya baadhi ya ubunifu ulioanzishwa hayakufuatiliwa vya kutosha ili kutoa mrejesho juu ya maendeleo yaliyopatikana na kile ambacho kinahitajika kukamilishwa kibiashara.
- (iii) ***Uhusiano hafifu kati ya sekta ya umma na viwanda***

Licha ya jitihada mbalimbali za kuunga mkono ubunifu, ilibainika kuwa hakukuwa na mfumo mzuri wa kuwasilisha kwa ufanisi taarifa za ubunifu na maendeleo yake baina ya taasisi. Hali hii ilisababisha mtiririko mdogo wa taarifa kati ya sekta ya umma, tasnia na taasisi za elimu ya juu.

- (iv) ***Ukosefu wa maarifa ya kibiashara miongoni mwa wavumbuzi wa ndani*** - Iliripotiwa kuwa kwa baadhi ya wabunifu wa ubunifu ambao kimsingi uliendelezwa na watu binafsi katika ngazi ya kati, baadhi yao walionekana kutokuwa na uelewa wa kutosha wa hatua zinazohitajika kusogeza ubunifu huo kwenye hatua ya kibiashara.

- (c) ***Uratibu wa wahusika wakuu katika utekelezaji wa shughuli za utafiti na ubunifu***

Ukaguzi ulibaini vipengele kadhaa vya kisheria katika taasisi za utafiti vinavyoizua Tume kutekeleza kikamilifu mamlaka yake ya kisheria ya kuratibu shughuli zinazohusiana na utafiti wa kisayansi na maendeleo ya teknolojia nchini. Sehemu ifuatayo inatoa maelezo ya masuala yaliyobainishwa katika uratibu wa wahusika wakuu katika utekelezaji wa shughuli za utafiti na ubunifu.

(i) Mamlaka zinazoingiliana katika usajili wa mikataba ya uhamishaji teknolojia

Kuhusu usajili wa mikataba ya uhamishaji teknolojia, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na taasisi tatu ambazo ni Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni). Licha ya majukumu yanayojulikana ya kila chombo kuhusu mamlaka yake, hakukuwa na uratibu wa kuhakikisha utendaji kazi madhubuti kuhusu mahitaji katika usimamizi wa jumla wa masuala yanayohusiana na usajili wa uhamishaji wa teknolojia.

Mapungufu haya yaliweka mazingira magumu kwa wavumbuzi kwani walilazimika kutii mahitaji ya udhibiti wa kila taasisi kivyake hivyo kusababisha kukosekana kwa mazingira rafiki kwa Tume ya kuhakikisha kuna uratibu wa kina wa shughuli za kuhamisha na kukuza teknolojia.

(d) Ufuatiliaji duni wa utekelezaji wa shughuli za utafiti na ubunifu

Ukaguzi ulibaini kuwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21, Tume ya Sayansi na Teknolojia haikuwa na kitengo mahsusi katika ngazi ya taasisi ambacho kingewajibika kwa ufuatiliaji wa shughuli za utafiti na ubunifu. Timu ya ukaguzi haikupata ushahidi wa kuonesha kuwa ufuatiliaji ulifanyika katika kipindi kilichokaguliwa. Badala yake, ilifanywa na timu ya watu kutoka vitengo mbalimbali ambavyo viliundwa pale ufuatiliaji wa shughuli za utafiti ulipohitajika. Ukaguzi ulibaini ubunifumapungufu yafuatayo yanayohitaji kufanyiwa kazi ili.

(i) Ufuatiliaji usioridhisha wa tafiti zilizofanyika na maendeleo ya teknolojia

Ukaguzi ulibaini kuwa taasisi zinazohusika na ufuatiliaji wa ubunifu zinafahamu Mfumo wa Taifa wa Ufuatiliaji wa Utafiti na Ubunifu, lakini hazikutoa ushahidi kuonesha kwamba zinatumia kama mwongozo wakati wa kuripoti matokeo na athari. Hali hii ilitokana na kwamba hapo awali taasisi zilikuwa na mifumo yao kabla ya kuanzishwa kwa mfumo wa taifa, na mifumo hii haikuratibiwa ili kukamilishana.

Mapitio ya Taarifa ya Mwaka ya Utendaji Kazi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania ya Mwaka 2020/21), yalibaini kuwa hata Tume yenyewe haikutumia ipasavyo mfumo wa ufuatiliaji wa kazi zote za utafiti nchini.

Sababu za Ufuatiliaji duni wa utekelezaji wa shughuli za utafiti na ubunifu

- (i) ***Ukosefu wa muundo sanifu wa kuripoti*** - Ilibainika kuwa, pamoja na mfumo ulioanzishwa wa kuhakikisha muundo huo unaratibiwa kielekitroniki, hakukuwa na kumbukumbu za jitihada za muda mrefu za kuhakikisha kuwa mifumo iliyopo ya ufuatiliaji katika taasisi za utafiti na maendeleo na taasisi za elimu ya juu inahuishwa na kutumia viashiria hivyo kitaifa katika mfumo wa ufuatiliaji ili Tume iweze kufahamishwa kuhusu matokeo ya utafiti na ubunifu katika ngazi za taasisi. Kwa mujibu wa Tume, kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji wa kitaasisi kwa matokeo ya taasisi za utafiti na maendeleo kulitokana na kukosekana kwa muundo sanifu wa kuripoti ambao ungehakikisha ulinganifu wa taarifa katika sekta nzima.
- (ii) ***Viashiria muhimu vya utendaji kutowezesha ufuatiliaji wa matokeo kutoka kwenye tafiti zilizofanyika*** - Lengo la 4 la Mfumo wa Ufuatiliaji wa Utafiti linaitaka Tume kubainisha na kufafanua viashiria muhimu vinavyoweza kutumika kufuatilia na kuwasilisha kazi za utafiti. Pia, mfumo unahitaji Tume kufuatilia kwa utaratibu michakato ya utafiti iliyofanywa ili kufuatilia matokeo na athari zake. Pia, ilibainika kuwa viashiria vya ufanisi havikuwekwa ili kufuatilia ni kwa kiasi gani wadau watatumia matokeo ya tafiti zilizofanyika. Ilibainika pia kuwa ni kiashiria kimoja tu kati ya viashiria muhimu 6 vya utendaji kazi ndicho kilihusiana na malengo yaliyopangwa.

Athari kwa ufuatiliaji pungufu wa utekelezaji wa shughuli za utafiti na ubunifu

- (i) ***Ukosefu wa ufuatiliaji wa maendeleo ya teknolojia kwa kuzingatia ubunifu*** - Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania haikuweza kujulishwa kuhusu shughuli zilizoendelea za utafiti na ubunifu zilizofanywa katika ngazi za kitaasisi ambazo zingesaidea kufanya uchanganuzi na kusahihisha hali ya shughuli za taasisi za utafiti na maendeleo katika ngazi za kitaasisi pamoja na uwekaji wa kumbukumbu. Zaidi ya hayounaweza kupunguza uwezo wa kufuatilia maendeleo na kutambua maeneo ya kuboresha hivyo kusababisha

kukosa fursa za ukuaji na maendeleo katika sekta ya utafiti na ubunifu.

5.5.2 Matokeo ya Ukaguzi katika Usimamizi wa Mipango na Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini

Uanzishaji wa mifumo ya TEHAMA iyoleta manufaa yaliyotarajiwa

Taasisi za Serikali zilikuwa zikiingia gharama kununua au kuendeleza mifumo ya TEHAMA, ambayo baadhi iliachwa kutokana na sababu tofauti.

Mifumo iliyokwishajengwa iliachwa kisha kubadilishwa na mifumo mingine mipya. Katika taasisi 6 za umma zilizotembelewa zikiwemo Wizara ya Afya, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini, na Wizara ya Kilimo, jumla ya mifumo 14 ya TEHAMA yenye thamani ya shilingi billioni 4.728 ilikuwa imetelekezwa. Mambo yafuatayo yalibainika kuathiri usimamizi wa ujenzi wa mifumo ya TEHAMA.

(a) Usimamizi duni wa uanzishaji wa miradi ya TEHAMA iliyofanywa na taasisi za umma

Mapitio ya kazi ya uangalizi ya Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yamebaini kuwapo kwa mfumo usioridhisha wa ufuatiliaji na kuwapo kwa miongozo elekezi iliyopitwa na wakati kinyume na kifungu cha 4.1 cha Mkakati wa Taifa wa TEHAMA katika Serikali Mtandao wa mwaka 2013. Kifungu hicho kinaeleza kuwa Wizara inatakiwa kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaosaidia kupima na kufuatilia athari za hatua mbalimbali katika Serikali Mtandao. Mapitio ya kazi za ufuatiliaji katika Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yalibaini kuwa, Wizara haikuwa na mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera na mikakati mingine inayohusiana na TEHAMA mbayo ni pamoja na kupanga na kujenga mifumo ya TEHAMA ya Serikali.

(i) Mfumo uliogawanyika wa ufuatiliaji wa mipango na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini

Mapitio ya kazi za ufuatiliaji katika Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yaligundua kuwa kulikuwa na kukosekana kwa nyenzo za ufuatiliaji wa utekelezaji wa sera na mikakati kuhusu masuala ya

TEHAMA; utekelezaji duni wa shughuli za ufuatiliaji; na utoaji duni wa taarifa za shughuli za ufuatiliaji. Pia, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilikuwa inasimamia sera na miongozo iliyopitwa na wakati. Mapitio ya taarifa za utendaji kazi kuanzia mwaka 2017 hadi 2022 kutoka Wizarani, yalibainisha kuwa Wizara ilikuwa inategemea sera na mwongozo wa TEHAMA ambao umetumika kwa zaidi ya miaka 5 bila kufanyiwa mapitio. Mapungufu yafuatayo yalibainika.

Uhaba wa zana za kufanya ufuatiliaji

Mapitio ya shughuli za ufuatiliaji wizarani yalibaini kuwa haikuwa na vitendeakazi vinavyojitosheleza vya ufuatiliaji ambavyo vingetoa mwongozo wa aina ya takwimu zinazopaswa kukusanywa, wakati wa kukusanywa, na jinsi zinavyotakiwa kutumika. Mapungufu haya yalichangiwa na kukosekana kwa miongozo ya ufuatiliaji wa ndani na vipengele vya ufuatiliaji vilikosekana katika shughuli za ufuatiliaji za Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa vipengele vya ufuatiliaji kutoka kwenye shughuli za ufuatiliaji za Serikali Mtandao na kutotengeneza mpango wa ufuatiliaji na tathmini wakati wa utayarishaji wa zana mahususi za ufuatiliaji wa Serikali Mtandao. Ingawa ilikuwa na jukumu la kuandaa zana za ufuatiliaji, kurugenzi ya huduma za teknolojia za mawasiliano ya Serikali haikufanya juhudi za kuziandaa.

Kutokuwapo kwa zana za ufuatiliaji kulisababisha ripoti za ufuatiliaji zisizo sahihi, ambazo zilitofautiana kulingana na shughuli za ufuatiliaji wa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Dosari hii iliizuia Wizara kufanya tathmini ya kiasi ambacho mashirika na taasisi za umma zinazingatia sera za sekta ndogo za TEHAMA.

Utekelezaji usioridhisha wa shughuli za ufuatiliaji

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ilikuwa haitekelezi ipasavyo kazi zake za ufuatiliaji kwa taasisi za umma na nyinginezo. Ilielezwa kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2021/22, Wizara ilifanya ziara 2 tu za ufuatiliaji kati ya ziara 20 sawa na asilimia 10 ya ziara zilizotarajiwa.

Timu ya ukaguzi iligundua kuwa Kurugenzi ya TEHAMA katika Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora haikuwa na rasilimali-watu ya kutosha kufanya shughuli za ufuatiliaji katika taasisi na mashirika

ya umma kutokana na kukosekana kwa utaratibu uliowekwa wa watumishi watano tu wanaohusika na ufuatiliaji.

Ufuatiliaji mdogo wa Wizara ulisababisha kiwango cha chini cha utekelezaji wa sheria, miongozo, sera na viwango vya TEHAMA kwa taasisi za serikali, ambapo ni asilimia 4.25 tu ya taasisi za umma ndizo ziliandaa miongozo muhimu ya kitaasisi.

Viashiria vya utendaji visivyo sahihi

Taarifa kuu ya mkakati wa Serikali Mtandao haikuwa sahihi na haikuwakilisha taarifa za kweli zilizokusanywa kutoka kwa taasisi za umma, ambapo baadhi ya viashiria vya utendaji havikuwa na taarifa za msingi kwa ajili ya utekelezaji.

Zaidi ya hayo, ukaguzi ulibaini kuwa taasisi na mashirika ya umma hayakutumia viashiria muhimu vya utendaji kutokana na uelewa mdogo na jitihada duni za kutoa taarifa. Wizara pia ilishindwa kutoa mwongozo wa uratibu, uwianishaji, na kuhakikisha mipango ya Serikali Mtandao inaanzishwa kwa kuzingatia viwango na miongozo iliyowekwa.

(b) Usimamizi usioridhisha wa uanzishaji wa miradi ya TEHAMA


Kifungu cha 24(2a) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019 kinazitaka taasisi na mashirika ya umma yanayokusudia kutekeleza miradi ya TEHAMA kuwasilisha kwa Mamlaka kwa ushauri na kutoa maelezo ya miradi wakati wa kupanga na kupata kibali kutoka kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao kabla ya kuomba fedha hizo. Katika hatua hiyo hiyo, taasisi za umma zinatakiwa pia kuhakikisha kuwa timu zenye uwezo wa miradi zinaundwa ili kuendeleza mfumo mpya wa TEHAMA.

Mapitio ya kanzidata ya Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini (GISP) ya miradi iliyowasilishwa yaligundua kuwa nyaraka za miradi hazikuandaliwa ipasavyo na kuwasilishwa na taasisi za umma kwa Wakala wa Serikali Mtandao ambapo kinyume na kifungu cha 24(2a) cha Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019. Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo kuhusu maelezo ya dhana iliyowasilishwa.

(i) Maandalizi duni ya Nyaraka za miradi kwa taasisi za umma

Mapitio ya kanzidata ya Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini kuhusu mawasilisho ya nyaraka za miradi kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania yalionesha kuwa asilimia 86 ya nyaraka zilirejeshwa kwa taasisi za umma kwa sababu ya makosa kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 5.1** hapa chini.

Mchoro 5. 1: Kiwango cha Kurudishwa kwa Nyaraka za Uanzishaji wa Miradi kwa Mamlaka ya Serikali Mtandao



Chanzo: Uchambuzi wa Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini na Serikali Mtandao

(ii) Kuchelewa kutoa mrejesho kuhusu nyaraka zilizopitiwa kwa mashirika na taasisi za umma

Mamlaka ya Serikali Mtandao haikutoa maelezo ya ushauri kwa wakati, kinyume na kanuni ya 28 ya Kanuni Kuu za Serikali Mtandao za Mwaka 2020, inayoitaka mamlaka kuidhinisha nyaraka hizo na kuwasilisha mrejesho wa maandishi kwa taasisi husika ya umma ndani ya siku 14 za kazi. Timu ya ukaguzi ilitathmini muda ambao maelezo ya ushauri yalichukuliwa na ilibainika kuwa ni asilimia 93 ya maelezo ya ushauri yaliyowasilishwa. Mapungufu haya yalichangiwa na masuala yafuatayo:

Kukosekana kwa ujuzi wa kutosha kabla ya kuandaa nyaraka za miradi
Watumishi waliohusika katika utayarishaji wa nyaraka hawakuwa na ujuzi na uelewa juu ya orodha ya nyaraka za miradi zinazohitajika. Ilibainika kuwa ukosefu wa uelewa kwa watumishi wanaohusika katika utayarishaji wa nyaraka za miradi ulitokana na ukweli kwamba Mamlaka ya Serikali Mtandao haikuchukua hatua za kutosha ili kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kufuata taratibu wakati wa ujenzi wa mifumo mipya ya TEHAMA kwenye mashirika na taasisi za umma.

Kuchelewa kupitia mapendekezo yaliyowasilishwa - Sababu kuu ya kucheleweshwa kwa utoaji wa ushauri ilikuwa taratibu za ndani za kupitia maoni ya ujenzi wa miradi yaliyowasilishwa kwa wafanyakazi tofauti ndani ya Mamlaka ya Serikali Mtandao, ambapo ilichukua zaidi ya siku 14 kinyume na matakwa ya mkataba wa huduma kwa mteja.

Athari za utoaji duni wa maoni ni pamoja na yafuatayo:-

Uidhinishaji wa mapendekezo ya mradi kwa muda mrefu. Kwa hiyo, ucheleweshaji wa utoaji wa maelezo ya ushauri ulichelewesha kuanza kwa miradi iliyopendekezwa na hivyo kuathiri malengo yaliyokusudiwa ya miradi. Ukaguzi ulibaini kuwa miradi 601 kati ya 645 iliidhinishwa baada ya muda uliowekwa hivyo miradi hiyo kuonekana kutokuwa na umuhimu tena kulingana na wakati uidhinishaji ulipofanyika.

(a) Mahitaji ya mifumo ya TEHAMA hayakutayarishwa vya kutosha na kuwasilishwa

Mapitio ya ripoti za miradi ya TEHAMA na mipango mingine yaligundua mapungufu yanayohusiana na utayarishaji wa mahitaji ya mfumo kama vile ushirikishaji duni wa wadau na ukusanyaji duni wa mahitaji na maelezo ya mtumiaji kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 2.3.3 cha Mkakati wa Mamlaka wa Kielekitroniki wa Mwaka 2021/22. Kifungu hicho kinataka Wakala wa Serikali Mtandao kuhakikisha mipango inajibu mahitaji na matarajio ya wadau mbalimbali. Mapungufu yafuatayo yalibainika:

(i) Ushirikishaji duni wa wadau katika kukusanya mahitaji

Mashirika na taasisi za umma hazikushirikisha wadau katika kukusanya mahitaji ya mtumiaji na utendaji kazi kabla ya kuunda viwango vya mahitaji

ya mifumo kama vile idara husika, wafanyakazi wa kiufundi wa TEHAMA, raia na walipakodi, na mashirika mengine ya umma kama inavyotakiwa na Mpango-mkakati wa Serikali Mtandao wa kuanzia Mwaka 2021/2022 - 2025/26.

Mapitio ya nyaraka za uanzishaji wa Mfumo wa TEHAMA yalionesha kutoshirikishwa ipasavyo kwa wadau kama vile Wizara ya Afya, Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Dodoma Mjini, Mamlaka ya Udhambi wa Huduma za Nishati na Maji, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wakala Wa Huduma za Manunuzi Serikalini, na Wizara ya Kilimo. Ushirikiano bora wa wadau ulibainika kwa Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini iliyokuwa na asilimia 80 huku ushiriki mdogo zaidi ulibainika katika Wizara ya Kilimo iliyokuwa na asilimia 33, ambapo wastani wa ushirikishaji wa wadau ulibainika kuwa asilimia 59 katika taasisi zilizotembelewa na timu ya ukaguzi.

Sababu zilizochangia ushirikishaji duni wa wadau ni kama zifuatazo:

Kukosa maarifa - Mahojiano na maafisa kutoka taasisi za umma yalibaini kuwa ushirikishaji duni wa wadau ulisababishwa na uelewa mdogo wa taratibu za utayarishaji wa mifumo na miongozo. Dosari hii ilisababisha mambo yafuatayo:

Usanifu upya wa mifumo - Kutoshirikishwa kwa wadau kulisababisha uundaji upya wa mifumo na kuanzishwa kwa moduli mpya za mifumo baada ya kuzinduliwa kwa mifumo ili kukidhi mahitaji ya watumiaji ambayo hatimaye ilishughulikia lengo na faida zilizokusudiwa za kupata mifumo. Kwa mfano, mifumo 13 ya TEHAMA kutoka taasisi za umma zilizotembelewa ilikuwa imeundwa upya ili kukidhi mahitaji mapya ya watumiaji. Wadau walishirikishwa kwa kiasi ili kutoa mahitaji ya sehemu moja ya biashara au moduli huku wakishiriki kikamilifu kutoa michango kwa michakato yote ya biashara wakati wa kukusanya mahitaji.

(c) Usimamizi usioridhisha wa uendelezaji na Mpangilio wa mifumo ya TEHAMA

Sheria ya Serikali Mtandao inaitaka Mamlaka ya Serikali Mtandao kuhakikisha kuwa mifumo inayopatikana au kujengwa na taasisi za umma inakuwa ya ubora wa juu na inayokidhi matakwa ya taasisi. Upungufu uliobainika ni pamoja na udhibiti na uhakiki ubora usioridhisha; ushirikiano mdogo wa

mifumo; mifumo isiyo mizuri; udhibiti hafifu wa teknolojia; ujenzi wa mifumo bila idhini ya Mamlaka ya Serikali Mtandao; uwezo duni wa ndani wa kuunda mifumo, uaminifu hafifu; na maendeleo yasiyoridhisha ya biashara.

Kwa mujibu wa kanzidata ya mali zilizosajiliwa za TEHAMA katika tovuti ya huduma za TEHAMA Serikalini, jumla ya miradi 421 ya TEHAMA ilianzishwa na kukamilika katika kipindi husika. Kati ya hiyo, ni miradi 17 tu sawa na asilimia 4 ndiyo iliidhinishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao huku miradi 404 iliyobaki ikiwa bado haijaidhinishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao. wakati wa ukaguzi, mambo yafuatayo yalibainishwa:

(i) Udhibiti usiotosheleza wakati wa uanzishaji wa mifumo ya TEHAMA

Mapitio ya mawasiliano kati ya taasisi za umma na Mamlaka ya Serikali Mtandao yalionesha kuwa kulikuwa na kutowasilishwa kwa taarifa za undani za miradi na hatua muhimu wakati wa mchakato wa kujenga mifumo ya TEHAMA kinyume na kifungu cha 2.3.3 (vii) cha Viwango na Miongozo ya Utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA Serikalini.

Mamlaka ya Serikali Mtandao ilikuwa na udhibiti mdogo katika awamu muhimu za uanzishaji wa miradi, isipokuwa kwa awamu za awali za uanzishaji wa miradi, ambapo udhibiti ulikuwa na nguvu zaidi. Hata hivyo, kwa hatua zilizobaki, ukaguzi ulibaini upungufu katika udhibiti wa hatua za ununuzi, ukandarasi, uendelezaji, upimaji, kukabidhi, na ufungaji. Zaidi ya hayo, Mamlaka haikutoa ukumbusho wa kuwasilisha vitu vinavyopaswa kuwasilishwa katika kila hatua ya ujenzi wa mifumo. Upungufu huu ulisababishwa na udhibiti duni wa mifumo ya TEHAMA.

Ukosefu wa uelewa - Uwasilishaji duni wa hatua muhimu na zinazoweza kufikiwa kwa miradi iliyopatikana ya TEHAMA ulitokana na ukosefu wa uelewa juu ya mahitaji. Taasisi za umma zilifahamu hitaji la kuomba idhini kabla ya shughuli za ununuzi, lakini hazikujumuisha uwasilishaji wa vitu vinavyoweza kuwasilishwa katika kila hatua.

(ii) Uhakiki Ubora usioridhisha kwa Mifumo ya TEHAMA iliyoanzishwa

Ukaguzi ulibaini kuwa hakukuwa na shughuli za uhakiki ubora zilizofanywa kwenye mifumo iliyojengwa na taasisi au iliyoundwa kwa ajili ya matumizi katika taasisi husika. Kazi pekee ya udhibiti ubora ilikuwa upimaji wa kukubalika kwa mfumo kwa mtumiaji. Ukaguzi wa uhakiki wa ubora haukufanyika kabla au baada ya kukamilika kwa mifumo.

Kukosekana kwa uhakiki wa ubora wa mifumo ya TEHAMA iliyoanzishwa ulisababisha mapungufu ya mara kwa mara, hitilafu, kupunguza kasi ya utendaji kazi wa mifumo na kusababisha kutopatikana kwa mtandao mara kwa mara. Udhibiti duni wa ubora wa mifumo ya TEHAMA ulisababisha mambo yafuatayo:

Makosa ya kimfumo wakati wa matumizi

Wakati wa majadiliano na maafisa wenye dhamana kwenye taasisi zilizotembelewa ilibainika kuwa makosa na changamoto katika mifumo ni matokeo ya makosa ambayo hayakupitiwa na ambayo hayakusahihishwa wakati wa utayarishaji. Makosa yaliyobainika ni uundaji upya wa kanuni na maoni hasi yaliripotiwa katika asilimia 18 ya taarifa zilizotathminiwa. Wakati huohuo, ni asilimia 11 tu ya mifumo ya serikali iliyoachwa. Masuala haya yalisababishwa na mapungufu katika kudhibiti ubora wa mifumo ya TEHAMA iliyoundwa.

(iii) Udhibiti usiotosheleza wa Teknolojia ya mbele (front-end) na ya nyuma (back-end) wakati wa uundaji wa TEHAMA

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa taasisi za umma zilikuwa zikitengeneza maombi ya biashara kwa kutumia teknolojia ya programu inayotambulika, ambapo michakato 30 kati ya 593 ya ndani ya mifumo (back-end) na ya matokeo ya upande wa mtumiaji, (front-end) 27 kati ya 521 hazikuwa za bure na zilikuwa na programu ndogo kinyume na matakwa ya Sera ya Taifa ya TEHAMA na Sheria ya Serikali ya Kielekitroniki ya Mwaka 2019. Programu za kawaida zinazotumika ni pamoja na fomu za tovuti za .NET, Oracle DBMS, ABAP, Aheeva, na DELPHI.

(iv) Muunganiko na mwingiliano mdogo wa mifumo iliyoanzishwa ya TEHAMA iliyoanzishwa

Mapitio ya mifumo ya TEHAMA ya Serikali kutoka taasisi za serikali zilizotembelewa ilionesha kuwa mifumo mingi iliyoanzishwa ilikuwa inafanya kazi peke yake na haikuwa na uwezo wa kuwasiliana na mifumo mingine ndani au nje ya taasisi. Kwa mujibu wa mapitio ya mifumo ya TEHAMA wakati wa ziara ya ukaguzi katika taasisi za umma, takribani mifumo 42 kati ya 79 ya TEHAMA sawa na asilimia 53 ya mifumo ya TEHAMA iliyokuwa inatumiwa na taasisi za umma haikuwa inawasiliana na mifumo mingine, na mifumo 47 iliyobaki haikuwa na mawasiliano kirahisi na mifumo mingine.


Hali hii ilisababishwa na mwingiliano mdogo kutokana na mkabala wa kupata programu ambapo mifumo mingi ya TEHAMA inayotegemea wauzazi ilitengenezwa bila kuwa na dirisha kuu la kuruhusu mawasiliano na kubadilishana data kati ya mifumo miwili.

Zaidi ya hayo, kanzidata za baadhi ya mifumo iliyopatikana ya TEHAMA hazikuweza kunyumbuka na hivyo kutoruhusu kwa urahisi kuongeza au kupunguza watumiaji wakati mahitaji mapya ya rasilimali yalipoombwa. Mifumo iliyotengenezwa iliruhusu mawasiliano tu na mifumo iliyo na lugha sawa au lugha ya kanzidata au ufafanuzi wa lugha ambayo iliweza kubadilishana taarifa na mifumo mingine ndani ya mfumo huohuo.

(v) Uanzishaji wa mifumo ya TEHAMA bila idhini ya Mamlaka ya Serikali Mtandao

Mapitio ya miradi iliyoibuliwa kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2021/2022 yalibaini kuwa baadhi ya miradi ya TEHAMA ambayo ilinunuliwa na taasisi za umma haikuidhinishwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Serikali Mtandao kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 5.2** hapa chini.

Kielelezo Na. 5. 2: Hali ya Uidhinishaji wa Mifumo ya TEHAMA Iliyopatikana kuanzia Mwaka 2017 hadi 2022




Chanzo: Taarifa kutoka Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini kuanzia Mwaka 2017-2022



Mamlaka ya Serikali Mtandao haikuwa na nguvu za kisheria za kutosha za kutekeleza miongozo ya usajili, hivyo kusababisha taasisi nyingi za umma kutozingatia matakwa ya kupata kibali. Timu ya ukaguzi iligundua kuwa kiwango cha uzingatiaji katika kuomba vibali kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao kiliendelea kuwa chini licha ya kupitishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kiwango cha uzingatiaji wa mahitaji ya idhini kilikuwa cha chini zaidi ikilinganishwa na wale ambao walikuwa hawazingatii matakwa kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 5.3**.

Kielelezo Na.5. 3: Kiwango cha Uzingatiaji wa Masharti ya Kuidhinishwa baada ya Kupitishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Mwaka 2019




Chanzo: Taarifa kutoka Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini kuanzia Mwaka 2017-2022



(vi) Uwezo usioridhisha wa kujenga mifumo ya TEHAMA

Mapitio ya mikataba ya kuendeleza mifumo ya TEHAMA kutoka kwa taasisi za umma zilizotembelewa yameonesha kuwa taasisi za umma zilikuwa na uwezo mdogo wa ndani wa kutengeneza mifumo ya TEHAMA iliyokusudiwa kurahisisha michakato yao ya kibiashara. Taasisi za umma zilikuwa zikitumia wataalamu wengi wa TEHAMA wa nje kuliko watumishi wa ndani kutokana na kukosekana kwa wataalamu wenye sifa za kutengeneza mifumo ya TEHAMA kinyume na kifungu 1(f) cha Mwongozo wa Serikali Mtandao unaozitaka taasisi za umma kutengeneza zenyewe mifumo ya TEHAMA. **Kielelezo Na. 5.4** hapa chini kinaonesha muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mifumo ya TEHAMA.

Kielelezo 5. 4: Muhtasari wa Hali ya Utekelezaji wa Mifumo ya TEHAMA (Mali za Programu) Iliyoanzishwa kuanzia Mwaka 2017 - 2022



Chanzo: Kanzidata ya Usajili wa Mali katika Mamlaka ya Serikali Mtandao na Tovuti ya Huduma za TEHAMA Serikalini kuanzia Mwaka 2017-2022

Kielelezo Na. 5.4 kinaonesha kuwa asilimia 58 ya miradi ya TEHAMA katika taasisi za serikali ilinunuliwa kutoka nje ya taasisi za umma, huku asilimia 42 ikitekelezwa na watumishi wa ndani wa TEHAMA.

(d) Upimaji na Ukabidhi usio na tija wa mifumo ya TEHAMA

Mapitio ya matokeo ya majaribio sambamba na ripoti za mifumo ya TEHAMA iliyoanzishwa yalibaini mapungufu yaliyofanya shughuli za upimaji kutokuwa na ufanisi kinyume na kifungu cha 2.3.4 (iv) cha Viwango na Miongozo ya Utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA Serikalini. Yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyobainika wakati wa ukaguzi:

(i) Kukosekana kwa majaribio ya kuunganisha mifumo iliyoanzishwa

Timu ya ukaguzi ilipitia nyaraka za miradi ya TEHAMA na kubaini kuwa kati ya mifumo 64 ya TEHAMA, 13 pekee ndiyo ilinunuliwa na taasisi za Serikali. Majaribio ya mtumiaji yalifanyika lakini ni taasisi mbili tu za umma zilizofanya majaribio ya ujumuishaji kwa mifumo iliyopatikana kinyume na kifungu cha 2.1 cha Viwango na Miongozo ya Mifumo ya Ushirikiano wa Serikali Mtandao.

Kutokuwapo kwa majaribio ya ushirikishaji wa mifumo ni changamoto kwa taasisi za umma wakati wa kuunganisha mchakato mmoja wa biashara na mwingine. Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa changamoto za mifumo wakati wa ubadilishanaji wa taarifa kwenye moduli ndani ya baadhi ya mifumo kama vile ripoti za mara kwa mara za makosa.

5.6 Mchango wa Ukaguzi katika kufikia Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Ukaguzi wa usimamizi wa shughuli za utafiti na ubunifu ulilenga kukagua uandaaji wa mikakati na mipango, usimamizi wa utafiti na ubunifu uliosajiliwa, uratibu wa wahusika, na ufuatiliaji.

Usimamizi wa mifumo ya TEHAMA serikalini ulikagua uanzishaji wa mifumo ya TEHAMA, ukusanyaji wa mahitaji na uundaji wa vigezo, utekelezaji wa maendeleo ya Mifumo ya TEHAMA inayopendekezwa, upimaji na uagizaji na uangalizi wa mipango ya mifumo, na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kuhusu malengo unaeleza kuwa, Serikali inatambua umuhimu wa matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu, uboreshaji wa kidigitali, ukuzaji wa ujuzi wa watumishi, uwezo wa ubunifu, na matumizi ya masuala ya kidigitali.

Malengo haya ya ukaguzi yalipimwa ili kufikia lengo la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Tatu wa Miaka Mitano. Zaidi ya hayo, lengo la 9 la Malengo ya Maendeleo Endelevu na lengo dogo la 9.5 linataka kuwapo kwa miongozo ya viwanda, ubunifu na miundombinu kwa ajili ya kujenga miundombinu thabiti, kukuza uchumi endelevu wa viwanda, na kukuza ubunifu. Hviyo, mapungufu katika usimamizi wa utafiti, ubunifu, usimamizi wa mipango, na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA Serikalini yanaathiri kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa yaliyotajwa.

5.7 Hitimisho la Ukaguzi

Inahitimishwa kuwa usimamizi wa utafiti na ubunifu unaotekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania na usimamizi wa uanzishaji wa mifumo ya TEHAMA inayotekelezwa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora haikutekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania haikuhakikisha kuwapo kwa uratibu wa kutosha katika utekelezaji wa shughuli zinazolenga kukuza utafiti, teknolojia, na ubunifu nchini. Utekelezaji wa mikakati iliyoanzishwa ya utafiti na ubunifu ulikuwa hafifu kutokana na kukosekana kwa uratibu baina ya mashirika ya utafiti.

Usimamizi wa upangaji na ujenzi wa mifumo ya TEHAMA katika taasisi za umma haukufanyika ipasavyo na ulihitaji hatua madhubuti za kuongeza udhibiti kwa taasisi za umma zinazopata mifumo ya TEHAMA. Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora haikuweza kutekeleza kikamilifu kazi yake ya uangalizi katika kupanga na kupata mifumo ya TEHAMA, na hivyo kusababisha utekelezaji mdogo wa sheria, kanuni na miongozo mingine ya serikali mtandao. Hatua madhubuti zinahitajika ili kuongeza udhibiti kwa taasisi za umma zinazojenga mifumo ya TEHAMA.



MAZINGIRA NA USALAMA WA CHAKULA

SURA YA SITA

6



MAZINGIRA NA USALAMA WA CHAKULA

6.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa kaguzi mbili za ufanisi zilizofanywa kuhusu masuala ya mazingira na usalama wa chakula kama inavyohusishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Ukaguzi wa kwanza ni juu ya usimamizi wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu, wakati ukaguzi mwingine ulihusu usimamizi wa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo. Sura hii inaangazia pia uhusiano wa mazingira na usalama wa chakula katika Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, mikakati na juhudi za Serikali katika kuhakikisha kuwapo kwa usimamizi wa kutosha wa mazingira, na usalama wa chakula. Sura inaelezea zaidi juu ya malengo, mawanda, matokeo, hitimisho na mapendekezo ya kaguzi hizi za ufanisi.

6.2 Usuli kuhusu Mazingira na Usalama Wwa Chakula

Maendeleo ya Tanzania kwa kiasi kikubwa yanategemea matumizi ya maliasili zake kwa huduma za mifumo ya ikolojia. Kwa mfano, maisha ya takribani asilimia 80 ya wakazi wa vijijini hutegemea ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013, uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa unategemea kilimo, ambacho kinachangia takribani asilimia 24.1 ya pato la taifa, asilimia 30 ya mapato ya nje, na kuajiri takribani asilimia 77.5 ya watu wote nchini.

Mazingira na usalama wa chakula ndio misingi ya maendeleo endelevu. Ili kuhakikisha kuna usimamizi mzuri wa mazingira na usalama wa chakula, matumizi endelevu, ulinzi na ustawi wa wanyamapori, misitu, ardhi pamoja na makazi haviepukiki. Aidha, jamii inahimizwa kuongeza uzalishaji wa chakula na virutubisho ili kupunguza kuenea kwa matatizo ya kiafya yatokanayo na ukosefu wa chakula cha kutosha.

Maendeleo ya Tanzania yanategemea sana kilimo, lakini nchi ipo katika athari kubwa ya uvamizi wa viumbe vamizi katika mazingira yake. Mara nyingi viumbe vamizi huathiri ikolojia na utoaji wa huduma za kimazingira kwa kubadilisha virutubisho, vimelea haidrolojia, pamoja na kuathiri makazi ya viumbe kwa ujumla wake.

Usindikaji wa mazao ya kilimo na usimamizi bora wa mavuno ni miongoni mwa masuala yanayotoa hakikisha usalama wa chakula nchini. Masuala haya ni muhimu katika kubadilisha bidhaa za kilimo kuwa bidhaa za msingi kwa kupunguza upotevu wa mavuno, na kuongeza muda wa watumizi ya bidhaa hizo hivyo kuboresha upatikanaji, utimilivu, na utoshelvu wa chakula nchini. Matokeo ya usimamizi mzuri wa usindikaji wa mazao ya kilimo ni upunguzaji wa upotevu wa chakula, usalama wa chakula na lishe, pamoja na kuongezeka kwa fursa za kiuchumi.

6.2.1 Uhusiano kati ya Mazingira na Usalama wa Chakula na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Sehemu hii inatoa taarifa juu ya uhusiano kati ya mazingira na uhakika wa chakula pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

(a) Uhusiano wa mazingira na usalama wa chakula na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, inawajibika kufuata Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu. Ili kushughulikia masuala yanayohusiana na usimamizi wa mazingira, ukaguzi wa ufanisi ulifanyika kuangalia usimaizi wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu. Ukaguzi huu unahusiana moja kwa moja na Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa sababu lengo la 15 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linahimiza kuimarisha utunzaji, urejeshaji, na uendelezaji wa matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya ardhi, pamoja na usimamizi endelevu wa misitu na kusitisha upotevu wa viumbe hai.

Masuala haya yanapaswa kufanywa kwa kuanzisha hatua za kuzuia uingiaji wa viumbe vamizi na kupunguza athari zao kwenye mazingira ya nchikavu na majini.

Mikakati ya usalama wa chakula nchini iliangaliwa kupitia ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo nchini. Ukaguzi huu unahusishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa maana kwamba, lengo Na. 2 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linahimiza

kutokomeza njaa, kuwa na usalama wa chakula, kuboresha lishe, na kuhamasisha kilimo endelevu. Aidha, lengo Na. 12.3 linataka kupunguza nusu ya uharibifu wa chakula duniani pamoja na kupunguza upotevu katika mnyororo wa uzaliashaji na usambazaji wa mazao ya chakula.

Ili kuongeza tija katika kilimo, pamoja na uwekezaji katika tafiti za kilimo na huduma za ugani, maendeleo ya teknolojia, suala la kutunza vinasaba vya mimea na mifugo linapaswa kutiliwa mkazo. Hali hii inapaswa kufanywa kwa kuzingatia hatua za kuhakikisha utendaji sahihi wa masoko ya bidhaa za chakula na kuwezesha upatikanaji kwa wakati wa taarifa za masoko, ikiwa pamoja na akiba ya chakula ili kusaidia kupunguza kupanda kwa bei za chakula.

(b) Uhusiano wa mazingira na usalama wa chakula na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Usimamizi wa masuala ya mazingira uliangaliwa kupitia ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa viumbe vumizi katika mazingira ya nchikavu. Ukaguzi huu ulihusiana na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Kifungu cha 4.2.6 cha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2015/16 - 2020/21) kinasisitiza usimamizi wa maliasili, mazingira, na mabadiliko ya tabianchi.

Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika sehemu hii ni:

- (i) Kulinda, kurejesha, na kukuza matumizi endelevu ya mifumo ya ikolojia ya ardhi; kusimamia misitu kwa uendelevu; na kusitisha upotevu wa viumbe hai;
- (ii) Utekelezaji wa tathmini ya athari za mazingira, tathmini ya athari za kimkakati za mazingira; na sheria nyingine za mazingira; na
- (iii) Kuunganisha na kuratibu sera na mikakati endelevu ya mazingira ili kuhakikisha kuna ukuaji katika sekta muhimu, ikiwa pamoja na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo, inatarajiwa kuwa ukaguzi huu utasaidia au kuwezesha uboreshaji wa michakato na taratibu za utekelezaji wa malengo haya ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Kifungu cha 5.3.5 cha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/25) kinaangazia usimamizi wa mazingira na maliasili. Katika kufanikisha suala hili, mambo muhimu yaliyopangwa kufanyika ni pamoja na:

- (i) Utekelezaji na ufuatiliaji wa mikakati ya kukabiliana na viumbe vamizi ifikapo mwezi Juni 2026 ili kupunguza upotevu wa viumbe hai kutoka asilimia 16 mwaka 2019/20 hadi asilimia 14 mwaka 2025/26.
- (ii) Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kwa kutunga Kanuni za Tathmini ya Athari za Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira za Mwaka 2005 kama ilivyorekebishwa mwaka 2018; na
- (iii) Uboreshaji wa uratibu wa taasisi kwa kuzingatia na kuimarisha usimamizi wa mazingira katika mamlaka 186 za serikali za mitaa na wizara 13 za kisekta ifikapo mwezi Juni 2026.

Ukaguzi huu unatarajiwa utasaidia kuboresha hatua za usimamizi wa mazingira nchini.

Masuala ya usalama wa chakula yaliangaliwa kwa kufanya ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo. Ukaguzi huu ulihusiana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa namna ifuatayo:

Kifungu cha 4.2.6 cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa Tatu wa wa Miaka Mitano kinasisitiza usimamizi wa usalama wa chakula na lishe. Ili kufanikisha suala hili, hatua muhimu za kuzingatia ni pamoja na:

- (i) Kukuza uwekezaji katika uzalishaji na matumizi ya vyakula mbalimbali vyenye virutubisho; na
- (ii) Kuongeza uzalishaji, usambazaji, na matumizi ya chakula kinachozalishwa nchini.

Ukaguzi huu wa usimamizi wa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya chakula unatarajiwa kuwa utasaidia kuboresha usimamizi wa usalama wa chakula na lishe nchini.

6.2.2 Mikakati na juhudi za serikali katika usimamizi wa mazingira na uhakika wa chakula

Katika kuhakikisha Serikali inaimarisha usimamizi wa mazingira na usalama wa chakula nchini, mikakati na juhudi zifuatazo zilifanyika:

(a) Mikakati na jitihada za serikali katika usimamizi wa viumbe vamizi nchini

Ili kuhakikisha utoshelevu katika usimamizi wa viumbe vamizi nchini, nchi imepitisha mikakati na mikataba mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kama inavyofafanuliwa hapa chini.

(i) Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Viumbe Vamizi wa Mwaka 2019 - 2029

Katika mkakati huu, nchi ililenga kupunguza athari za viumbe vamizi kwa kuanzisha mfumo bora na madhubuti wa kisheria na kitaasisi; mawasiliano na elimu; mfumo wa uhamasishaji wa umma; na teknolojia za kuzuia, kutokomeza, na kudhibiti viumbe vamizi.

(ii) Mkakati na Mpangokazi wa Taifa wa Bayoanuai wa Mwaka 2015-2020

Huu ni mkakati wa kitaifa ambao lengo lake lilikuwa kuhifadhi viumbe hai. Katika mkakati huu, nchi ililenga kupitia na kutekeleza sheria zinazosimamia matumizi ya rasilimali za majini na nchikavu. Aidha, mkakati huu ulilenga kutambua vipaumbele katika usimamizi wa viumbe vamizi kwa kuzingatia udhibiti au utokomezaji wa viumbe hawa.

(iii) Mpango Kabambe wa Taifa wa Mazingira wa Mwaka 2022 - 2032

Mpango huu unataja suala la viumbe vamizi kama moja ya maeneo ya vipaumbele vya mazingira. Mpango umeweka baadhi ya mikakati ya kukabiliana na suala la viumbe vamizi, kwa kuimarisha utunzaji wa bayoanuai katika uingiaji, ueneaji, pamoja na athari za viumbe vamizi katika mazingira.

(b) Mikakati na jitihada za serikali juu ya usimamizi wa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo

Zifuatazo ni jitihada na mikakati iliyoandaliwa na Serikali ili kushughulikia masuala yote yanayohusu usimamizi wa usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo nchini.

(i) Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Mpango huu ulijumuisha kukuza viwanda kwa ajili ya mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya jamii kupitia maeneo makuu manne yaliyopewa kipaumbele. Usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo ulionekana kwenye maeneo ya kipaumbele cha kwanza na cha pili, ambapo maeneo hayo yalilenga katika ukuaji wa uchumi na viwanda na kuboresha mazingira ya maendeleo ya biashara.

(ii) Mkakati Jumuisi wa Maendeleo ya Viwanda wa Mwaka 2021-2025

Mkakati huu unatarajiwa kuboresha shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo na viwanda vinavyosaidia shughuli za kilimo. Ifikapo mwaka 2025, eneo la kanda maalumu za kiuchumi za kilimo zinapaswa kuanzishwa ili kuhudumia kila aina ya viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo na viwanda vinavyosaidia kilimo ambavyo vinatarajiwa kuanzishwa.

(iii) Mkakati wa Pili wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo wa Mwaka 2015/16 - 2024/25

Mkakati huu unaongoza utekelezaji wa sera za sekta ya kilimo kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2024/25. Mkakati unalenga kuleta mabadiliko ya sekta ya kilimo ili iwe ya kisasa, ya kibiashara, yenye tija, stahimilivu na yenye ushindani.

(iv) Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Mavuno wa Mwaka 2019-2029

Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Mavuno unatekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi ukilenga mazao ya chakula hasa nafaka, kunde, matunda na mbogamboga, na mizizi na mazao yanayotoa mafuta ya kupikia. Mkakati huu unatarajia kuweka hatua kubwa za kupunguza hasara baada ya mavuno na uwezekano wa kukabiliana na upungufu wa chakula.

(v) Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Maendeleo ya Kilimo cha Mazao ya Bustani wa Mwaka 2021-2031

Mkakati huu unashughulikia maeneo mapana ya hatua zinazohusiana na uzalishaji, usindikaji, na utafutaji wa masoko ya mazao ya bustani. Mkakati huu unahamasisha kuwapo kwa uratibu, rasilimali, pamoja na mpango wa utekelezaji. Masuala haya yanalenga kuboresha hatua ya msingi ya kushughulikia na kusindika bidhaa za kilimo cha mazao ya bustani ili kupunguza upotevu wa mazao, kuongeza kiwango cha uzalishaji, na kupata malighafi za viwandani kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi.

6.3 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha malengo na mawanda ya ukaguzi kwa Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano:

6.3.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo wizara zenye dhamana zimesimamia ipasavyo mipango ya utunzaji wa mazingira na usalama wa chakula nchini ili kuimarisha maendeleo ya jamii kupitia utunzaji wa viumbe hai na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno ili kuongeza usalama wa chakula nchini.

Lengo hili lilifanyiwa kazi kwa kuzingatia malengo mahususi yafuatayo:

- (a) Kubaini iwapo Ofisi ya Makamu wa Rais- - Mazingira imesimamia ipasavyo viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu ili kuzuia na kudhibiti athari kwa viumbe hai, mazingira, na hasara za kiuchumi nchini zitokanazo na viumbe hawa; na
- (b) Kutathmini iwapo Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo zinasimamia ipasavyo shughuli za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo ili kupunguza hasara baada ya mavuno na kuongeza ubora na hivyo kuimarisha usalama wa chakula kitaifa na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa.

6.3.2 Mawanda ya Ukaguzi

Kuhusu usimamizi wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu, mkaguliwa alikuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa kuwa ni mwangalizi wa jumla wa masuala ya mazingira, ikiwa pamoja na usimamizi wa viumbe vamizi nchini.

Ukaguzi ulitathmini kiwango ambacho Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira imesimamia ipasavyo viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu ili kupunguza uingiaji, ukuaji, ueneaji, pamoja na athari za viumbe vamizi kwa viumbe hai na mazingira. Vipengele vilivyofanyiwa kazi katika ukaguzi huu ni pamoja na hatua za kuzuia, hatua za kudhibiti, uratibu, na ufuatiliaji na tathmini ya masuala yanayohusiana na usimamizi wa viumbe vamizi.

Ukaguzi huu uliangalia utendaji wa miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2021/22. Kipindi hiki kilichaguliwa kwa sababu serikali iliweka mikakati mbalimbali ya kudhibiti viumbe vamizi hususani Mkakati na Mpangokazi wa Taifa wa Viumbe Vamizi wa Mwaka 2019-2029. Aidha, kipindi hiki kilichaguliwa ili kuiwezesha timu ya ukaguzi kufanya uchambuzi mzuri kwa lengo la kupata hitimisho kwa kuunganisha na mwenendo wa utendaji wa kila mwaka katika usimamizi wa viumbe vamizi.

Kuhusu usimamizi wa Usindikaji na Uongezaji Thamani ya Mazao ya Kilimo, wakaguliwa wakuu walikuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Kilimo. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ina jukumu la usimamizi wa shughuli za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo. Wakati huohuo, Wizara ya Kilimo ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

Ukaguzi uliangazia tathmini ya kiwango ambacho Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inasimamia shughuli za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo. Vilevile, ukaguzi ulijikita katika kuangalia upatikanaji wa teknolojia za kutosha za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, masoko, ufuatiliaji, na uratibu wa shughuli za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo.

Ukaguzi huu uliangazia kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2021/22. Kipindi hiki kilichaguliwa kwa sababu serikali iliweka

mkazo mkubwa katika mipango ya viwanda kupitia Mpango wa Maendeleo wa Pili wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21.

6.4 Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo ya kaguzi mbili za ufanisi zilizofanyika katika masuala ya mazingira na usalama wa chakula. Ukaguzi wa kwanza ulihusu usimamizi wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu na ukaguzi wa pili ulihusu usimamizi wa usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo. Maelezo ya kina ya matokeo ya kaguzi hizi yanatolewa hapa chini.

6.4.1 Matokeo ya ukaguzi wa ufanisi kwenye usimamizi wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu

Uchambuzi uliofanywa na timu ya wakaguzi kutoka katika taarifa zilizowasilishwa katika Mkakati na Mpangokazi wa Taifa wa Viumbe Vamizi wa Mwaka 2019-2029 unaonesha kuwa, Tanzania ilikuwa na aina 220 za viumbe vamizi waliotambuliwa. Asilimia 92 ya viumbe hawa ni wa kigeni wakati asilimia 8 ni viumbe vamizi wa asili. Ilibainika kuwa aina hizi za viumbe zilivamia maeneo mbalimbali nchini. Kwa mfano, hifadhi za taifa zilikuwa zimevamiwa na aina 70 za mimea vamizi inayokadiriwa kusambaa kwenye eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 541.94 ambazo ni sawa na asilimia 0.52 ya eneo lote la hifadhi zote za taifa nchini. Aidha, misitu ilikuwa imevamiwa na aina tofauti za mimea uvamizi ambapo kilomita za mraba 21.32 kati ya kilomita za mraba 286.8 za hifadhi za misitu zilibainika kuvamiwa.

Hali hii ilitokana na kuzuia na kudhibiti kusikojitosheleza kwa uingiaji, ueneaaji na ukuaji wa viumbe vamizi nchini. Pia, ilitokana na uratibu na ufuatiliaji na tathmini duni ya mikakati ya kusimamia viumbe vamizi. Maelezo ya ziada juu ya changamoto zilizobainika wakati wa ukaguzi huu yanatolewa hapa chini.

(a) Uzuiaji wa viumbe vamizi Usiojitosheleza

Ukaguzi ulibaini kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa kushirikiana na wizara za kisekta haikuhakikisha uzuiaji madhubuti wa viumbe vamizi nchini. Upungufu huu ulidhihirishwa na mambo yafuatayo:

(i) Utambuzi na usimamizi Usiojitosheleza wa njia zinatumiwa kuingia na kusambaa kwa viumbe vamizi

Lengo la 1, hatua ya 1.1.1 ya Mkakati na Mpango-kazi wa Taifa wa Viumbe Vamizi wa Mwaka 2019-2029 unazielekeza Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, Wizara za Kisekta, taasisi za utafiti na maendeleo na taasisi za elimu ya juu kuweka malengo ya utambuzi na usimamizi wa njia zinatotumiwa na viumbe vamizi kuingia, kukua na kusambaa katika mazingira ya nchikavu.

Mapitio ya taarifa za utendaji pamoja na taarifa za utafiti kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira yalionesha kuwa, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maliasili na Utalii hazikufanya uchambuzi wa kina wa njia mabalimbali zinazoweza kusababisha uingiaji na usambaaaji wa viumbe vamizi nchini.

Hali hii ilisababishwa na utafiti usioridhisha uliofanywa na taasisi za elimu ya juu na taasisi za utafiti na maendeleo kama vile Taasisi ya Utafiti wa Wanyapori Tanzania (TAWIRI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) kwenye maeneo ya njia za uingiaji na ueneaji wa viumbe vamizi nchini. Vilevile, kulikuwa na utegemezi wa kanzidata ya viumbe vamizi ya kidunia na si ya nchini Tanzania. Hata hivyo, taasisi hizi hazikuwa na bajeti zinazotosha kufanya tafiti, hali iliyozuia utoaji taarifa juu ya njia sahihi za kuzuia uingiaji na ueneaji wa viumbe vamizi kupitia utambuzi wa njia kuu zinatotumiwa na viumbe vamizi hawa wakati wa uvamizi. Aidha, hali hii ilizulia utambuzi wa uhusiano wa kisekta kati ya njia za uingiaji na ueneaji wa viumbe vamizi, na hivyo kuathiri uanadaaji wa mikakati ya usimamizi wa viumbe hawa nchini.⁹

(ii) Uzuiaji wa viumbe vamizi usiotosheleza katika maeneo ya kuingilia nchini

Ilibainika kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania, haikusimamia na kuratibu ipasanvyo uzuiaji wa kuingia kwa viumbe vamizi kupitia maeneneo ya kuingilia nchini kama vile kwenye mipaka ya nchi. Upungufu huu ulitokana na ukaguzi usioridhisha wa viumbe vamizi katika maeneno hayo ya nchi.

⁹ *Kundi la Wataalamu wa Viumbe Vamizi (ISSG-IUCN) (2018).*

Mambo yaliyochangia uzuiaji usiojitosheleza wa viumbe vamizi katika maeneo hayo kuingia nchini yameelezwa hapa chini.

Idadi ndogo ya wakaguzi katika maeneo ya kuingilia nchini - Timu ya wakaguzi ilitembelea makundi matatu ya maeneo ya kuingilia nchini ambayo ni viwanja vya ndege, bandari, pamoja na mipaka ya nchi na kubaini kuwa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania ilikuwa na upungufu wa wakaguzi 9 (31 kati ya 40 wanaohitajika) sawa na asilimia 23 ya idadi ya wakaguzi inayohitajika.

Upungufu wa wakaguzi kulisababisha uzuiaji hafifu wa uingiaji wa viumbe vamizi kupitia maeneo mbalimbali ya kuingilia nchini.

Upungufu wa vifaa vya ukaguzi katika maeneno ya kuingilia nchini - Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa, maeneo ya kuingilia nchini ya Namanga, Sirari, Kasumulo, na uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro hayakuwa na vifaa vya kutosha vya ukaguzi wa viumbe vamizi. **Jedwali Na. 6.1.** linaonesha hali ya upungufu wa vifaa vya ukaguzi wa viumbe vamizi katika maeneo ya kuingilia nchini.

Jedwali Na. 6.1: Hali ya Upungufu wa Vifaa katika Maeneno ya Kuingilia Nchini

| Aina ya Vifaa | Idadi ya Vifaa Inayohitajika | Idadi ya Vifaa Iliyopo | | | |
|-------------------|------------------------------|------------------------|-----|---------|----------|
| | | Sirari | KIA | Namanga | Kasumulo |
| Vifaa vya Kinga | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 |
| Vifaa vya Maabara | 20 | 13 | 10 | 9 | 0 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Idadi ya Vifaa Vilivyopo katika Maeneno ya Kuingilia Nchini Mwaka 2022

Kwa mujibu wa mahojiano na watumishi wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania, ukosefu wa vifaa vya ukaguzi katika maeneo ya kuingilia nchini unasababishwa na uhaba wa fedha za kukidhi mahitaji hayo. Serikali haikutoa fedha za kutosha kuwezesha ununuzi wa vifaa vya ukaguzi katika maeneno hayo.

(iii) Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Wizara ya Kilimo hazikufanya tathmini ya hatari na athari za kimazingira za viumbe vamizi

Mapitio ya taarifa za utekelezaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na Wizara ya Kilimo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hadi 2022 yalibainisha kuwa, hakukuwa na jitihada mahususi za kufanya tathmini ya hatari na athari za kimazingira za viumbe vamizi wanaoweza kuingia nchini. Ilielezwa kuwa aina hizi za viumbe vamizi huletwa nchini kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na wataalamu wa kigeni ambao huagiza vifaa kutoka nchi za nje. Hali hii inaongeza uwezekano wa kuingia na kuenea kwa viumbe vamizi nchini.

Mapungufu haya yalitokana na kukosekana kwa mkakati na mipango ya utekelezaji wa athari na hatari ya viumbe vamizi. Kuwapo kwa mkakati huu kungeongoza jinsi ya kufanya tathmini ya hatari na athari za kimazingira za viumbe vamizi.

Kwa namna hiyo, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira pamoja na wizara za kisekta hazikuweza kutabiri ni aina za viumbe vamizi zilizokuwa na uwezekano mkubwa wa kuletwa nchini kupitia miradi ya maendeleo. Hali hii pia ina athari za kiuchumi pamoja na usumbufu katika mazingira ya nchikavu na majini.

(b) Udhhibiti wa viumbe vamizi Usiojitosheleza katika mazingira ya ardhi ya Nchikavu

Kwa ujumla, timu ya wakaguzi iligundua kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na wizara za kisekta, haikuhakikisha udhibiti mzuri wa viumbe vamizi nchini. Hali hii ilidhihirishwa na mambo yafuatayo:

(i) Kukosekana kwa kanzidata ya taifa ya viumbe vamizi

Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na wizara yenye dhamana ya wanyamapori, uvuvi, misitu, Tume ya Sayansi na Teknolojia, taasisi za utafiti na maendeleo, taasisi za elimu ya juu, sekta binafsi, pamoja na mashirika yasiyo ya Kiserikali, haikuandaa kanzidata ya taifa ya viumbe vamizi.

Kanzidata hii ingesaidia kutoa taarifa juu ya aina za viumbe vamizi vinavyopaswa kupewa kipaumbele, kiwango cha uvamizi nchini, na maeneo

yaliyovamiwa na yaliyo katika hatari ya uvamizi wa viumbe hao. Taarifa kutoka katika kanzidata hiyo zingeweza kutumika kama chanzo cha kufuatilia matukio ya uingiaji na ueneaji wa viumbe hao. Kanzidata hii pia ingeweza kutumika katika kutoa fursa za utambuzi wa upungufu katika usimamizi wa viumbe vamizi nchini.

Kutokana na kosekana kwa kanzidata hiyo, nchi inakosa taarifa za kisasa kuhusu viumbe vamizi ambao wamejipenyeza katika sekta mbalimbali. Kwa hivyo, nchi inakabiliwa na hatari ya namna bora ya ufuatiliaji wa kuingia, kukua na kuenea kwa viumbe vamizi. Kukosekana kwa kanzidata ya taifa ya viumbe vamizi kulitokana na mambo yafuatayo:

Utafiti wa viumbe vamizi Usiojitosheleza: - Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa katika Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029, hadi kufikia mwaka 2019 kulikuwa na miradi 20 tu ya utafiti iliyofanywa kuhusu usimamizi wa viumbe vamizi. Vilevile, hakukuwa na utaratibu wa kutekeleza mwenendo na usambazaji wa matokeo ya tafiti hizi kwa wadau wote wenye dhamana ya usimamizi wa viumbe vamizi ili kuboresha hatua za kudhibiti viumbe hao.

Ukosefu wa kipaumbele toshelevu katika mipango na bajeti ya usimamizi wa viumbe wavamizi- Mapitio ya mipango ya utekelezaji wa mwaka kutoka mamlaka za serikali za mitaa ulionyesha kwamba, usimamizi wa viumbe vamizi haukujumuishwa katika mipango ya utekelezaji wa kila mwaka pamoja na bajeti za mamlaka hizo. Kati ya sekretarieti za mikoa pamoja na halmashauri za wilaya nane zilizotembelewa, ni halmashauri moja tu ndiyo ilijumuisha mipango na kutenga mfuko wa kupambana na athari za viumbe vamizi.

Usambazaji usioridhisha wa taarifa za aina ya viumbe vamizi - Wakati wa mahojiano na maofisa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, ilibainika kuwa kulikuwa na mapungufu katika kupeanataarifa kuhusu utafiti wa viumbe vamizi. Kwa mfano, matokeo ya tafiti kuhusu magugu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa zilizofanywa na taasisi za utafiti kama vile Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2021/22, hayakuwasilishwa.

Aidha, ilibainika kuwa hakukuwa na wajibu au matakwa ya kisheria yanayolazimisha usambazaji wa taarifa kwa wadau wote wanaohusika katika

usimamizi wa viumbe vamizi. Aidha, kwa sababu utafiti ulifanywa kwa msingi wa kitaaluma, mtafiti alikuwa huru kusambaza au kutosambaza taarifa za utafiti, kwa kuwa utafiti ulifanywa kwa gharama ya mtafiti.

(ii) Mipango na utekelezaji wa kampeni za kujijengea uwezo isiyokidhi mahitaji

Mapitio ya mipango ya utekelezaji wa kila mwaka na taarifa za utekelezaji wake kutoka katika wizara, taasisi na mamlaka za serikali za mitaa kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2012/22, yaligundua kuwa mipango ya kujenga uwezo juu ya usimamizi wa viumbe vamizi haikufanyika ipasavyo. Kati ya taasisi 15 za Serikali zilizotembelewa na wakaguzi, hakukuwa na taasisi hata moja iliyokuwa na mipango ya kujenga uwezo kuhusu udhibiti wa viumbe vamizi nchini. Zaidi ya hayo, mahojiano yaliyofanywa kwa maafisa kutoka mamlaka za serikali za mitaa yalibaini kuwa, wafanyakazi hawakupewa mafunzo ya aina yoyote juu ya usimamizi wa viumbe vamizi nchini.

Kupita mahojiano yaliyofanywa kwa maafisa kutoka mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa, ilibainika kuwa wengi wa maafisa hao hawakuwa na maarifa juu ya uingiaji, ukuaji na ueneaji wa viumbe vamizi nchini.

Timu ya ukaguzi pia ilibaini kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikuratibu utekelezaji wa mipango ya elimu na uhamasishaji wa jamii juu ya usimamizi wa viumbe vamizi kinyume na maelekezo na Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029.

Ukosefu wa mipango ya kuongeza uwezo wa udhibiti madhubuti wa viumbe vamizi ulitokana na sababu zifuatazo:

Utaalamu usiotosheleza juu ya udhibiti wa viumbe vamizi - Ilibainika kuwa kulikuwa na idadi ndogo ya watumishi ambao wamepata ujuzi au wamekamilisha utaalamu katika usimamizi wa viumbe vamizi. Timu ya ukaguzi iligundua kuwa usimamizi wa viumbe vamizi uliratibiwa na wataalamu kutoka vitengo vya mazingira katika wizara na taasisi nyingi za Serikali, na hakukuwa na watumishi kama vile wataalamu wa magugu, wataalamu wa wadudu, wataalamu wa uhusiano wa viumbe hai (wanaikolojia), na wataalamu wa afya ya binadamu (wataalamu wa

patholojia), ambao wangehusika moja kwa moja na kutoa maarifa yenye ufasaha juu ya usimamizi wa viumbe vamizi katika mazingira.

Tafiti za kubainisha hatua madhubuti za kudhibiti viumbe vamizi - zisizojitoshesha. Ilibainika kuwa tafiti juu ya njia sahihi za kudhibiti uingiaji, kuenea, na athari za viumbe vamizi hazikufanywa vizuri. Hali hii ilitokana na ukosefu wa utaalumu, teknolojia, na fedha za kuwezesha tafiti hizo. Kwa kuongezea, mipango ya kuwezesha kampeni za kujenga uwezo katika taasisi zinazoshughulika na usimamizi wa viumbe vamizi haikuandaliwa vya kutosha.

(iii) Mbinu za kudhibiti athari za viumbe vamizi zisizokua na tija

Mapitio ya taarifa za tafiti juu ya usimamizi wa viumbe vamizi zilizofanywa na Mwalongo, Notkery na Andrew (2020) na ule uliofanywa na Ngondya na wenzake (2016) yalifafanua kwamba, hatua zinazotumiwa kudhibiti viumbe vamizi nchini hazikuwa na ufanisi. **Jedwali Na. 6.2** linafafanua hali ya hatua za usimamizi wa viumbe vamizi nchini.

Jedwali Na 6.2: Hali ya Hatua za Udhibiti wa Viumbe Vamizi Nchini

| Eneo la Utafiti | Mbinu za Udhibiti Zilizopendekezwa | Maoni ya Jumla | Maoni ya Wakaguzi |
|---|--|---|---|
| Kuboresha Uzalishaji wa Mazao kupitia Usimamizi Jumuishi wa Magugu Wilayani Kongwa Mwaka 2020 ¹⁰ | Mbinu za kienyeji kama vile kung'oa au kufyeka | Ni ghali na zinahitaji nguvukazi kubwa | Ni njia isiyo na tija na inahitaji mtaji na nguvukazi kubwa. |
| Mimea vamizi, athari za kiikolojia, hali, changamoto za usimamizi nchini Tanzania na namna ya | Matumizi ya kemikali (dawa) za kuulia wadudu | Matumizi yasiyofaa ya dawa za kuulia wadudu yamechangia kuwapo kwa viumbe vamizi sugu | Haifai kwani inaweza kusababisha usugu kwa viumbe vamizi wakati wa kuwadhibiti. |
| | Matumizi ya kemikali | Magugu kuwa sugu, gharama kubwa ya kutumia dawa za kuua magugu | |
| | Mbinu za kawaida kama vile kung'oa na kukata | Huchochea uotaji wa magugu yasiyotakiwa | Haifai kwa kuwa inahusishwa na uotaji wa magugu |

¹⁰ Mwalongo, Notkery Andrew (2020)

| Eneo la Utafiti | Mbinu za Udhhibiti Zilizopendekezwa | Maoni ya Jumla | Maoni ya Wakaguzi |
|---|--|--|--|
| kuzitatua, 2017 ¹¹ | | kutokana na utifuaji wa udongo wakati wa kung'oa. | yasiyohitajika. |
| Kuongeza na Kutathmini ufanisi wa mbinu za Kudhibiti na kurejesha maeneo yaliyovamiwa mimea vamizi kama <i>Tagetes Minuta</i> , <i>Bidens Schimperii</i> na <i>Gutenbergia Cordifolia</i> katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), 2020 | Matumizi ya kemikali | Husababisha usugu wa magugu vamizi, uchafuzi wa mazingira, na gharama kubwa zinazohusiana na ununuzi wa dawa za kua viumbe vamizi. | Ukosefu wa tija kwani huweza kusababisha uchafuzi wa mazingira na gharama kubwa. |
| | Njia za kienyeji (kufyeka, kuchoma na kung'oa) | Ufanisi mkubwa, rafiki wa mazingira, na njia rahisi za usimamizi wa udhibiti wa viumbe vamizi | Kutokuwa na ufanisi kwani hutumia muda mwingi hasa pale kunapokuwa na uvamizi mkubwa wa viumbe vamizi. |
| Mbinu ya asili ya kusimamia magugu vamizi aina ya <i>Gutenbergia cordifolia</i> , 2016 ¹² | Njia ya kemikali kwa kutumia dawa za kuulia wadudu | Haishauriwi kutumika katika mazingira ya asili, na hasa katika maeneo ya hifadhi. | Haifai kwa kuwa huleta mwingilano wa kiikolojia. |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa kutoka kwenye Tafiti kuhusu Usimamizi wa Aina za Wageni Vamizi, 2022

Aidha, mapitio ya Mpango wa Usimamizi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili ya Mlima Rungwe (2016/17 - 2020/21) yamebaini idadi isiyotosheleza ya vifaa vinavyohitajika kudhibiti wingi na kuenea kwa viumbe vamizi katika hifadhi za misitu nchini. **Jedwali Na. 6.3** linaonesha hali ya upatikanaji wa zana zinazohitajika kudhibiti viumbe vamizi katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Rungwe.

¹¹ Ngondya, Issakwisa, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela (2017)

¹² Issakwisa Bernard Ngondya, Linus K. Munishi, Anna C. Treydte na Patrick A. Ndakidemi (2016)

Jedwali Na.6.3: Hali ya Vifaa vya Kudhibiti Viumbe Vamizi katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Rungwe

| Jina la vifaa | Namba Inayotakiwa | Namba Inapatikana |
|----------------------|--------------------------|--------------------------|
| Msumeno | 1 | 0 |
| Koleo | 100 | 0 |
| Majembe | 100 | 0 |
| Shoka | 50 | 0 |
| Mapanga | 100 | 0 |
| Reki | 30 | 0 |
| Kamba | 150 | 0 |
| Viatu vya Mvua | 50 | 0 |
| Glavu | 50 | 0 |
| Kofia ngumu | 50 | 0 |
| Mifuko | 200 | 0 |
| Ova Roli | 50 | 0 |

Chanzo: Mpango wa Usimamizi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili ya Mlima Rungwe (2016/17 - 2020/21)

Mambo yafuatayo yalisabisha upungufu ulioonekana katika hatua za kudhibiti uingiaji, kuenea, na athari za spishi za viumbe vamizi:

Gharama kubwa za utekelezaji wa hatua za udhibiti wa viumbe vamizi - Ukaguzi uligundua kuwa gharama za kutekeleza hatua za udhibiti wa viumbe vamizi ni kubwa. Kwa mujibu wa kifungu cha 2.0 cha taarifa ya kiwango cha uvamizi wa viumbe vamizi katika hifadhi za taifa iliyoandaliwa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) mwaka 2022, kuanzia mwaka huo, jumla ya gharama za kudhibiti na kutokomeza aina mbalimbali za viumbe vamizi katika hifadhi za taifa kwa miaka 25 ijayo inakadiriwa kuwa shilingi 34,430,750,000.

Kukosekana kwa mkakati wa kitaifa wa udhibiti wa viumbe vamizi - Timu ya Ukaguzi ilibaini kuwa nchi haikuwa na mkakati wa taifa wa kudhibiti viumbe vamizi, ambao ungeainisha maeneo ya udhibiti, mbinu za kudhibiti, bajeti, muda uliopangwa, na mahitaji katika ufuatiliaji wa mbinu hizo. Aidha, mapitio ya taarifa ya mwezi Februari 2019 ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kuhusu viumbe vamizi ilibainisha kuwa hakukuwa na mfumo wa taifa wa kudhibiti viumbe vamizi. Mapungufu hayo yalisababisha kuruhusu mimea vamizi kuendelea kuingia na kuenea katika hifadhi za taifa.

Ukosefu wa miongozo ya ugawaji rasilimali kwa ajili ya kusimamia viumbe vamizi - Kuwapo kwa miongozo hii kungetoa muhtasari wa maelekezo jumuisi ya uwekezaji wenye msingi wa usimamizi wa viumbe vamizi ikiwa pamoja na uwekezaji wa kifedha na rasilimali-watu, pamoja na mipango ya kudhibiti uingiaji, kuenea, na athari za viumbe vamizi.

Kukosekana kwa mfumo wa kitaifa wa kukabiliana na dharura za kudhibiti uingiaji, kuenea na athari za viumbe vamizi - Kama ilivyopendekezwa katika Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029, mfumo wa kukabiliana na dharura unapaswa kuanzishwa ili kuhakikisha fedha na rasilimali-watu zinapatikana kwa urahisi na kwa haraka kwa ajili ya kukabiliana na viumbe vamizi wapya. Hata hivyo, timu ya ukaguzi haikuona mfumo wowote ulioandaliwa kwa ajili ya kukabiliana na athari za viumbe vamizi nchini.

Udhibiti usiofaa wa viumbe vamizi huongeza hatari ya kuenea kwao kwa wingi. Hali hii inaweza kuleta athari kwa mifumo ya ikolojia kwani inaweza kubadilisha mfumo wa haidrolojia na makazi ya viumbe wa asili, hivyo kusababisha upotevu wa viumbe hai.

**(c) Uratibu Usiojitosheleza wa wadau katika kuhakikisha ufanisi wa kuzuia na kudhibiti viumbe vamizi nchini**

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kulikuwa na uratibu mdogo kati ya wadau muhimu katika kuhakikisha ufanisi wa kuzuia na kudhibiti viumbe vamizi. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira pamoja na wizara za kisekta hazikufanya ufuatiliaji na tathmini ya kutosha ili kufuatilia kiwango cha maendeleo na mafanikio yaliyopatikana katika usimamizi wa viumbe vamizi nchini. Upungufu huu ulitokana na:

(i) Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikuwezesha uratibu wa kutosha kati ya wadau muhimu katika usimamizi wa viumbe vamizi

Ilibainika kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikuwahakikisha uratibu mzuri kati ya watendaji muhimu ili kuwezesha usimamizi mzuri wa viumbe vamizi nchini. Hali hii ilidhihirishwa na mambo yafuatayo:

Ufanyikaji wa vikao usioridhisha: Mahojiano yaliyofanywa kati ya timu ya ukaguzi na maafisa wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, Wizara ya

Maliasili na Utalii, na Wizara ya Kilimo yalibainisha kuwa mikutano ya Idara ndani ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, mikutano ya wakurugenzi wa sekta, mikutano ya kamati ya kitaifa ya uendeshaji, mikutano ya mawaziri wa sekta, na mikutano ya wadau haikufanyika kama ilivyopangwa. Badala yake, mikutano hiyo ilifanyika kupitia kikosikazi cha kitaifa kilichoanzishwa wakati wa kukabiliana na hali mbaya ya uvamizi wa viumbe vamizi.

Kukosekana kwa hatua shirikishi za kuzuia na kudhibiti viumbe vamizi nchini - Mapitio ya taarifa za utendaji (2018/19-2021/2022) kutoka wizara tatu zilizokaguliwa yalibaini kuwa, usimamizi wa viumbe vamizi haukuwa shirikishi. Kila sekta ilikuwa ikitekeleza usimamizi kwa maslahi na namna yake. Kwa mfano, kila wizara ilikuwa ikifanya utafiti na usimamizi wa viumbe vamizi kwa uwezo wake na kutumia taarifa kwa sekta yake, licha ya ukweli kwamba suala la usimamizi wa viumbe vamizi ni mtambuka na linagusa sekta mbalimbali za uchumi.

Kukosekana kwa uratibu mtambuka wa sekta mbalimbali nchi nzima kumekwamisha mafanikio ya wadau mbalimbali katika kudhibiti viumbe vamizi nchini. Kwa mfano, katika sekta ya wanyamapori, taasisi kama Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCAA) zimefanya kazi kubwa katika kusimamia viumbe vamizi, na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kudhibiti na kufuatilia viumbe hao katika maeneo yao. Hata hivyo, bado zinakabiliwa na changamoto kadhaa kwa sababu baadhi ya viumbe vamizi huletwa mbugani kutoka nje, ambako hakuna hatua za kudhibiti wa uingiaji na ueneaji wa viumbe hawa.

(ii) Upashanaji duni wa taarifa za viumbe vamizi katika sekta husika

Mapitio ya taarifa za utendaji kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha kuanzia 2018/19 hadi 2021/22 yalibainisha kuwa wizara hazikupeana taarifa kuhusu usimamizi wa viumbe vamizi wa kigeni katika maeneo yao. Wakaguzi walibaini kuwa kulikuwa na shughuli kadhaa ambazo zilifanywa na sekta katika kusimamia viumbe vamizi. Kwa mfano, mapitio ya mipango na bajeti (2018/19-2021/22) za Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) pamoja na Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCAA) yalionesha kuwa mamlaka hizo zilitenga fedha kwa ajili ya kusimamia viumbe vamizi katika maeneo yake. Pamoja na jitihada hizo zilizofanywa na mamlaka hizi, ukaguzi ulibaini kuwa

hazikuwahi kuwasilisha taarifa za hali ya utekelezaji katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na zizara zingine kama inavyosisitizwa na Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029.

Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Mwaka 2019 ilionesha kuwa, kukosekana kwa ushirikiano wa kitaarifa kulichangiwa na kutofuata utaratibu uliowekwa na Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029 ili kuhakikisha ushirikiano na uratibu mzuri wa usimamizi wa viumbe vamizi nchini.

Kukosekana kwa ushirikiano wa kutosha katika utoaji wa taarifa na ushirikiano miongoni mwa sekta husika kulisababisha kuendeleza tatizo la uvamizi wa viumbe vamizi nchini. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kongwa, magugu vamizi yanayojulikana kitaalam kama *Astripomoea Hyoscyamoides* yalienea zaidi kuliko ilivyodhaniwa hapo awali. Aina hii magugu imevamia eneo la Kongwa na kusababisha kushuka kwa rutuba ya ardhi hivyo kuathiri mazao na malisho. Mbali na Wilaya ya Kongwa, magugu hayo yameripotiwa kuenea katika maeneo mengine kama vile Handeni, Kiteto, Singida, Kondo, Chamwino, Bahi, Gairo, Morogoro, Korogwe, Mwanga, Manyoni, Pwani-Ruvu, na Nkasi¹³.

(iii) Ushirikiano Usioridhisha kati ya Tanzania na nchi jirani katika maeneo ya mipakani

Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Mwaka 2019, viumbe vamizi waliingia nchini kupitia njia tofauti kutoka nchi jirani. Taarifa hiyo inafichua kuwa viumbe hawa walikuwa maarufu zaidi katika maeneo ya mipakani. Hali hii inaashiria umuhimu wa kuwapo kwa juhudi za pamoja za kuimarisha ushirikiano katika utekelezaji wa makubaliano ya kikanda ya ulinzi na udhibiti wa viumbe vamizi katika maeneo ya mipakani.

Hata hivyo, ilibainika kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikuchukua hatua kama vile kuanzisha utaratibu wa uratibu na mawasiliano kwa ajili ya usimamizi mzuri wa viumbe vamizi kwa wadau wote husika na kuimarisha ushirikiano wa mipaka katika usimamizi wa viumbe vamizi.

¹³Utafiti wa *Kuimarisha Uzalishaji wa Masafa na Maisha ya Jamii kupitia Usimamizi Jumuishi wa Magugu Yasiyo na Tija katika Wilaya ya Kongwa, SUA (2019)*

Upungufu huu unaleta hatari kubwa ya viumbe vamizi kutoka nchi za kigeni kuendelea kuvamia nchini kupitia njia tofauti kama vile usafiri, ushoroba na nyinginezo. Aidha, kutokuwa na upashanaji madhubuti wa taarifa za kutosha kulikwamisha maendeleo ya utambuzi na kuzuia uingiaji wa viumbe vamizi nchini.

(d) Ufuatiliaji na tathmini isiyojitosheleza kuhusu hatua za kuzuia na kudhibiti viumbe vamizi

Ilibainika kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikufanya ufuatiliaji na tathmini madhubuti ya masuala yanayohusiana na usimamizi wa viumbe vamizi. Upungufu huu ulithibitishwa na mambo yafuatayo:

(i) Kukosekana kwa mpango wa mwaka wa ufuatiliaji na tathmini ya viumbe vamizi

Mahojiano na maafisa kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, yalibainisha kuwa, ofisi hii haikuwa na mpango wowote wa ufuatiliaji na tathmini ya masuala yanayohusiana na usimamizi wa viumbe vamizi. Kukosekana kwa mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya kila mwaka kulichangiwa na masuala ya ufuatiliaji na tathmini katika usimamizi wa viumbe vamizi kutopewa kipaumbele cha kutosha.

Ukosefu wa mpango wa ufuatiliaji na tathmini unainyima fursa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kufanya ufuatiliaji ili kutathmini kiwango cha maendeleo katika utekelezaji wa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini 2019-2029. Pia, kukosekana kwa mpango wa ufuatiliaji na tathmini kumesababisha kutopatikana kwa taarifa za utendaji wa wizara za kisekta katika utekelezaji wa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini 2019-2029.

(ii) Mifumo isiyo na tija ya utoaji taarifa za viumbe vamizi

Mifumo ya utoaji taarifa haikufanya kazi ipasavyo ili kuimarisha kuwezesha usimamizi wa viumbe vamizi nchini kama ilivyoelezwa hapa chini.

Kukosekana kwa taarifa za utekelezaji wa usimamizi wa viumbe vamizi kutoka wizara za kisekta na mamlaka za serikali za mitaa kwenda Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira

Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikupokea taarifa yoyote kutoka wizara za kisekta na mamlaka za serikali za mitaa zinazoonesha maendeleo katika utekelezaji wa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029.

Ukaguzi huu ulibaini kuwa kutowasilishwa kwa taarifa kutoka wizara za kisekta kwenda Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kulichangiwa na uwajibikaji usiojitosheleza wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira katika kuratibu uwasilishaji wa taarifa hizo kutoka katika wizara na taasisi hizo za serikali kama kifungu cha 36 (3) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa viumbe vamizi nchini 2019-2029 unavyotaka. Kutotoa taarifa za viumbe vamizi katika maeneo mbalimbali kunaikosesha Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira taarifa kamili muhimu za hali ya usimamizi wa viumbe vamizi nchini.

Aidha, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa taarifa za viumbe vamizi zinawasilishwa mara kwa mara kulingana na maelekezo ya Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029 . Kuanzia mwaka 2019 hadi wakati wa ukaguzi huu, ni mara moja tu (mwaka 2021) ndipo Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira iliandika barua kwa wizara za kisekta na taasisi za serikali kuzikumbusha kuwasilisha mipango na taarifa za kila mwaka zinazoonesha hali ya utekelezaji wa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi wa Viumbe Vamizi Nchini wa Mwaka 2019-2029.

(iii) Kukosekana kwa vikao vya kupitia hali ya utendaji

Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa hakukuwa na kumbukumbu za kuwapo kwa vikao vilivyofanyika kuhusu usimamizi wa viumbe vamizi nchini. **Majedwali Na 6.4** pamoja na **6.5** yanaonesha mahitaji ya vikao vya mapitio ya utendaji katika usimamizi wa viumbe vamizi nchini.

Jedwali Na. 6.4: Idadi ya Vikao Vilivyopangwa dhidi ya Vilivyofanyika

| Aina ya Kikao | 2019/20 | | 2020/21 | | 2021/22 | |
|---------------------|------------------|------------------|------------------|-----------------|------------------|------------------|
| | Vilivyohi tajika | Vilivy ofanyi ka | Vilivyohi tajika | Vilivyo fanyika | Vilivyohi tajika | Vilivy ofanyi ka |
| Vikao vya Divisheni | 4 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 |

| Aina ya Kikao | 2019/20 | | 2020/21 | | 2021/22 | |
|--------------------------------|------------------|------------------|------------------|-----------------|------------------|------------------|
| | Vilivyohi tajika | Vilivy ofanyi ka | Vilivyohi tajika | Vilivyo fanyika | Vilivyohi tajika | Vilivy ofanyi ka |
| Vikao vya Wakurugenzi wa Sekta | 4 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Mawasiliano (Majalada ya Kilimo) kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira Mwaka 2023

Jedwali Na. 6.5: Vikao vya Nusu Mwaka na Mwisho wa Mwaka

| Aina ya Kikao | Muda wa Kikao | 2019/20 | | 2020/21 | | 2021/22 | |
|--------------------------------|-----------------|------------------|-----------------|-------------------|-----------------|-------------------|-----------------|
| | | Vilivyo hitajika | Vilivyo fanyika | Vilivyohi itajika | Vilivyo fanyika | Vilivyohi itajika | Vilivyo fanyika |
| Vikao vya Divisheni | Nusu-Mwaka | 2 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 |
| Vikao vya Wakurugenzi wa Sekta | Mwisho wa Mwaka | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| Vikao vya Wadau | Mwisho wa | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa za Mawasiliano (Majalada ya Kilimo) kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ya Mwaka 2023

Upungufu huu ulisababisha kushindwa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuwa na taarifa mpya za maendeleo yaliyofanywa dhidi ya malengo ya kitaifa ya kuzuia na kudhibiti viumbe vamizi nchini.

6.4.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Usimamizi wa Usindikaji na Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo

Kwa ujumla, kiwango cha ukuaji wa shughuli za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo kilikuwa hafifu. Hali hii ilibainishwa na usimamizi wa usindikaji na uongezaji duni wa thamani wa mazao ya kilimo kutokana na uhaba wa teknolojia, masoko ya mazao, na ukosefu wa fedha za kukidhi shughuli za uchakataji na uongezaji thamani. Aidha, kulikuwa na utekelezaji duni wa mikakati mbalimbali inayohusiana na usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo. Dosari hizi zilisababisha kutofikiwa kikamilifu kwa malengo mbalimbali yaliyowekwa. Maelezo zaidi yametolewa hapa chini.

(a) Usimamizi wa Usiojitosheleza wa usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo

Usindikaji wa mazao ya kilimo una umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya taifa kwa kuwa unahusisha na kushirikisha nguzo mbili za uchumi, ambazo ni viwanda na kilimo. Pamoja na faida hizo hapo juu, ukaguzi ulibaini kuwa kiwango cha ukuaji wa shughuli za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo ulikua na mapungufu kama yalivyoainishwa hapo chini:

(i) Kutotekelezwa kwa asilimia 75 ya sera, mikakati na malengo yanayohusiana na usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo

Mapitio ya sera ya biashara ndogo na za kati pamoja na taarifa za tathmini ya viwanda endelevu yalibainisha kuwa, sera zinazoongoza usimamizi wa shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo zilitekelezwa kwa asilimia 25 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na 6.6** hapa chini.

Jedwali Na. 6.6: Muhtasari wa Utekelezaji wa Mikakati ya Usindikaji na Uongezaji wa Thamani ya Mazao ya Kilimo kuanzia Mwaka 2017/18-2021/22

| Sera | Asilimia ya Mikakati Iliyotekelezwa |
|--|-------------------------------------|
| Sera ya Biashara Ndogo na za Kati ya Mwaka 2003 | 14 |
| Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 1996-2020 | 36 |
| Wastani | 25 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kwa Kutumia Ripoti za Tathmini ya Sera za Biashara Ndogo na za Kati wa Mwaka 2022

Jedwali Na. 6.6 hapo juu linaonesha kuwa, malengo ya sera ya biashara ndogo na za kati na sera ya maendeleo ya viwanda yalitekelezwa kwa wastani wa asilimia 25. Hali hii ina maana kwamba asilimia 75 ya mikakati haikutekelezwa. Mikakati ambayo haikutekelezwa ilihusiana na upatikanaji bora wa fedha na kuimarisha utamaduni wa ujasiriamali na masoko ili kuchochea maendeleo endelevu na sekta binafsi iliyoimarishwa ili kufikia utekelezaji mzuri wa biashara ndogo na za kati pamoja na mipango na hatua zinazohusiana na kuimarisha viwanda vijijini.

Vilevile, taarifa ya tathmini ya sera ya biashara ndogo na za kati ya mwaka 2017 ilibainisha kuwa utekelezaji wa jumla wa malengo na viashiria vya

ukuaji wa usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo ulifikiwa kwa asilimia 12.5 na asilimia 14 mtawalia.

Mahojiano yaliyofanywa kati ya timu ya ukaguzi na watumishi mbalimbali pamoja na ziara ya wakaguzi iliyofanywa katika mikoa ilionesha kuwa, mifumo ya ulipaji fedha ilikuwa haujitoshelezi; hakukuwa na teknolojia sahihi za usindikaji wa mazao ya kilimo; na kulikuwa na uhusiano usioridhisha wa masoko ya bidhaa za kilimo zilizosindikwa. Masuala haya yalitokana na utekelezaji hafifu wa mikakati ya biashara ndogo na za kati pamoja na sera ya maendeleo endelevu ya viwanda.

(ii) Kupungua kwa mwenendo wa mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa

Kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, wizara zenye dhamana ya kilimo zilitakiwa kuhakikisha kuwa mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa unaongezeka hadi asilimia 29.4 ifikapo mwaka 2020 huku makadirio yakiwa asilimia 32 ifikapo mwaka 2025 kupitia uboreshaji wa uzalishaji katika shughuli za kilimo.

Hata hivyo, ukaguzi huu ulibaini kuwa mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa ulikuwa ukishuka kwa miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2017 hadi 2021 kutoka asilimia 29.7 hadi asilimia 26.6, ambayo ni chini ya lengo la asilimia 29.4 la kufikia mwaka 2020. Aidha, ukaguzi ulibaini kuendelea kupungua kwa mwenendo wa mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa kutoka mwaka wa Fedha 2017/18 hadi Mwaka wa Fedha 2019/20, kutoka asilimia 28.8 hadi asilimia 26.6, ambayo ilikuwa chini ya asilimia 29.4 iliyolengwa hadi mwaka 2019/20, naongezeko dogo la hadi asilimia 29.7 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Mchango mdogo wa sekta ya kilimo katika pato la taifa ulitokana na usimamizi usioridhisha wa shughuli za kilimo, kama vile kutegemea zaidi mvua za msimu, matumizi ya mbegu zisizo na ubora, na kufanya kilimo cha kujikimu. Hali hii ilisababishwa pia na usimamizi duni wa shughuli za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo, kwa sababu mazao mengi ya kilimo bado yalikuwa yakiuzwa bila kuchakatwa. Changanoto nyingine ilikuwa kukosekana kwa mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ili kuimarisha uzalishaji na kuongeza mchango katika pato la taifa.

(iii) Kasi ndogo ya ukuaji wa utendaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo nchini

Ukaguzi ulibaini kasi ndogo ya ukuaji wa utendaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo kama inavyothibitishwa na changamoto zifuatazo:

Kufungwa kwa Asilimia 42 ya viwanda vya kusindika mafuta ya alizeti kutokana na uhaba wa malighafi

Ukaguzi huo ulibaini kuwa viwanda vitano kati ya 12 (sawa na asilimia 42) vya kusindika mafuta ya alizeti vilifungwa kutokana na uhaba wa malighafi. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa viwanda vilivyokaguliwa vilionekana kufanya kazi chini ya uwezo wake kwa asilimia 77.4. Hali hii ilimaanisha kuwa, viwanda havikuweza kufanya kazi kwa uwezo wake wa tani 1,724 kwa mwaka badala yake, vilichakata tani 540 tu kwa mwaka.

Vilevile, taarifa ya sekta ya mafuta ya kula ya mwezi Novemba 2022 iliripoti kuwa, viwanda 12 vya kusindika mafuta ya alizeti vilikuwa na upungufu wa malighafi wa takribani tani 1,334. Taarifa hiyo ilionesha zaidi kuwa, asilimia 25 ya malighafi zinazohitajika zilizalishwa ndani ya nchi huku asilimia 75 ziliagizwa kutoka nchi za nje.

Kutokana na hali hiyo, Serikali imetumia jumla ya shilingi trilioni 2.6 ndani ya miaka mitano kuanzia mwaka 2015/16-2019/20 kuagiza mafuta ghafi kwa ajili ya kukabiliana na uhaba wa mafuta. Uhaba pamoja na ubora duni wa mafuta ulisababisha ulisababishwa na kuwapo kwa kilimo cha kujikimu, ujuzi mdogo wa viwango vya ubora wa mafuta, na kutotumika kwa kilimo cha vitalu, hivyo kuzalisha malighafi pungufu na zisizo na ubora wa kutosha.

(b) Uwezeshaji usioridhisha wa upatikanaji wa teknolojia za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo

Taarifa ya utafiti kutoka Chama cha Mazao ya Bustani Tanzania (TAHA) ilieleza kuwa mashine za usindikaji na ujuzi wa uendeshaji wa mashine hizo ulipata matokeo ya asilimia 50 kati ya mahitaji makuu saba ya wasindikaji wa mazao katika mnyororo wa thamani wa usindikaji wa mazao ya kilimo.

Hata hivyo, pamoja na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kupewa mamlaka ya kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia za usindikaji wa mazao ya kilimo, ukaguzi ulibaini kuwa upatikanaji wa teknolojia ulikuwa bado

kikwazo kikubwa kilichoathiri viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo nchini. Dozasri hii ilidhihirishwa na mapungufu yafuatayo:

Teknolojia zote zinazohitajika za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo hazikupatikana

Kulikuwa na upungufu wa kiteknolojia katika mashine zilizopo kwa ajili ya usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo nchini. Kwa ujumla, katika ngazi ya taifa, teknolojia zilizokosekana ni pamoja na teknolojia za utengenezaji wa mashine ndogo na zana zake; teknolojia za umaliziaji wa mashine ili kupata mwonekano mzuri; teknolojia za utengenezaji wa mashine za vifungashio na mashine za uchambuzi wa unyevu katika mazao; na teknolojia za kuchakata mabaki ya mazao ya chakula (*briquetting technologies*) kama nyongeza ya teknolojia maalumu za mazao ya kilimo. Hali hii ilikuwa kinyume na kifungu cha 5(a) cha Sheria ya Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), ya Mwaka 1975, inayoitaka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo, kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia kulingana na mahitaji ya biashara ndogo na za kati ili kuwezesha shughuli za kuongeza thamani kulingana na rasilimali zilizopo ndani ya nchi.



Ukaguzi ulibaini mapungufu mbalimbali ya kiteknolojia katika usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo ambayo yalitakiwa kufanyiwa kazi ipasavyo. Mathalani, ilibainika kuwa, Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo halikuwahi kutengeneza teknolojia yoyote ya kuongeza virutubisho kwenye mazao ya chakula. Matokeo yake, uongezaji wa thamani kwa mazao mengi haukufanyika. Kwa mfano, mafuta yote ya alizeti yaliyosindikwa na wasindikaji nchini yalikuwa mafuta ghafi, kwa sababu hakukuwa na teknolojia ya kuyasafisha.

Pamoja na mapungufu hayo, uchambuzi wa ukaguzi wa mapungufu ya kiteknolojia ulibaini mambo yafuatayo:

(i) Uwezo duni wa teknolojia zilizopo kuwezesha usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo

Katika vituo vyote vitatu vya maendeleo ya teknolojia, teknolojia zilizopatikana hazikuwa sahihi kwani hazikujumuisha hatua zote za michakato yote ya mnyororo wa thamani ya mazao. Mara nyingi teknolojia

zilizopo zilikuwa za kawaida kwa kuwa hazikuhusisha mchakato wa moja kwa moja na badala yake kila hatua ya usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo ulikuwa na mashine yake peke yake. Majibu 15 kati ya 16 ambayo ni sawa na asilimia 94 ya wasindikaji wa kilimo waliohojiwa yalionesha kutokuwa na ufanisi wa mashine za kusindika mazao ya kilimo. Kwa mfano, ilibainika kuwa, mashine zilizopo kwa ajili ya usindikaji wa mafuta ya alizeti zilisababisha upotevu wa mazao kwa asilimia 75.

Vilevile, mapitio ya Mkakati wa Alizeti wa Mwaka 2017 yalionesha kuwa mashine zilizopo za kuchakata mafuta ya alizeti kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo na watengenezaji wengine binafsi wa ndani hazikuwa na uwezo wa kuchakata mbegu za alizeti ili kuhakikisha kuwa mafuta yote yanavunwa. Hali hii ilitokana na kuwapo kwa mafuta baada ya kurudia kuchakata mbegu ya alizeti iliyokwishachakatwa na mashine hizo.

(ii) Matumizi ya mashine na teknolojia za kizamani kwa ajili ya usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo

Mapitio ya nyaraka¹⁴ yalibaini kuwa, teknolojia nyingi zilizokuwa zinatumika katika viwanda vya ndani kwa ajili ya usindikaji wa mazao ya kilimo zilipitwa na wakati kiasi cha kufanya iwe vigumu kupata vipuri wakati wa matengenezo.. Suala la kuwapo kwa mashine zenye teknolojia za kizamani lilithibitika pia wakati wa ziara zilizofanywa na wakaguzi. **Kielelezo Na. 6.1** na **Kielelezo Na. 6.2** vinaonesha mashine mbili za kizamani zilizokutwa katika mikoa ya Mbeya na Kigoma.

¹⁴ Ripoti za Tathmini ya (wajasiliamali wadogo na wakati) SME,2017,



Kielelezo Na. 6.1: Mashine ya zamani kama iliyokutwa katika Kituo cha Teknolojia Kigoma. Picha imechukuliwa na wakaguzi tarehe 30 Septemba 2022.



Kielelezo Na. 6.2: Mashine ya zamani kama iliyokutwa katika Kituo cha Teknolojia Mbeya. Picha imechukuliwa na wakaguzi tarehe 30 Septemba 2022.

Picha Na. 6.1 na **6.2** zinaonesha mashine mbalimbali za zamani kati ya mashine 19 zilizokutwa katika mikoa ya Mbeya na Kigoma. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa, mashine hizo zilinunuliwa na kuletwa katika vituo vya teknolojia mwaka 1975.

Ilielezwa zaidi kuwa, wataalamu wa ndani wa teknolojia walikabiliwa na ushindani mkubwa kutoka teknolojia za nje. Bei ya teknolojia za nje ilikuwa nafuu ikilinganishwa na bei ya teknolojia za ndani. Hali hii ilitokana na bei ya teknolojia ya nje kuwa na gharama ndogo za matengenezo kutokana na kutofautiana kwa kiwango cha uchumi kati ya Tanzania na nchi zinazotengeneza teknolojia hizo. Kwa sababu hii, vituo vinavyohusika na maendeleo ya teknolojia vinakosa uwezo wa kushindana na teknolojia za nje.

(c) Upatikanaji wa teknolojia za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo Usiojitosheleza

Kwa mujibu wa kifungu cha 4.1(1) cha Sera ya Taifa ya Masoko ya Kilimo ya Mwaka 2008, shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo na uongezaji thamani zinapaswa kuendelezwa na kuimarishwa. Aidha, sehemu Na. 4.4.5 ya Mpango-mkakati wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo wa Mwaka

2016/17-2020/21 ulilenga kuhakikisha uwezesaji wa ushirikishaji wa teknolojia kwa wadau. Mkakati huu ulilenga pia kuanzisha mitandao ya ushirikiano ya watengenezaji wa teknolojia na taasisi za utafiti na maendeleo, kuanzisha vituo vya teknolojia, na kuimarisha uwezo uliopo wa vituo hivyo. Mambo yafuatayo yalibainika wakati wa ukaguzi.

(i) Teknolojia za ndani za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo kuwa za gharama kubwa ikilinganishwa na teknolojia za nje ya nchi

Tathmini ya upatikanaji wa teknolojia za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo iliyofanyika kwa kupima bei na upatikanaji wake ilibaini kuwa, teknolojia za kisasa hazikupatikana kwa urahisi kwa wasindikaji wengi wa kilimo nchini. Vilevile, mashine za kusindika mazao ya kilimo zilizotengenezwa nchini zilikuwa za gharama kubwa ikilinganishwa na zilizotengenezwa nje ya nchi. Gharama za teknolojia za usindikaji wa mazao ya kilimo za ndani ya nchi zilikuwa juu kuliko za nje ya nchi kwa asilimia kuanzia 8 hadi 76.


Ilielezwa zaidi kuwa wavumbuzi wa teknolojia za ndani wanakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka teknolojia za nje ya nchi. Bei ya teknolojia za nje ya nchi zilikuwa ndogo na nafuu ikilinganishwa na bei ya teknolojia za ndani ya nchi. Mathalani, bei ya mashine ya kusaga mahindi iliyotengenezwa ndani ya nchi yenye uwezo wa kuzalisha kilo 300 hadi 1,000 kwa saa ni kati ya shilingi milioni 7.5 na 10.5. Wakati bei ya mashine iliyoagizwa nje ya nchi yenye uwezo huo inauzwa kwa shilingi milioni 4.5. Kwa hiyo, vituo vya teknolojia nchini havikuwa na uwezo wa kuendeleza teknolojia za ndani kutokana na ushindani mkubwa kutoka teknolojia za nje ya nchi. Hali hii pia inaweza kusababishwa na ukosefu wa malighafi kwani mara nyingi malighafi zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Vilevile, bei ya teknolojia za nje ilikuwa nafuu ikilinganishwa na za ndani ya nchi kutokana na gharama ndogo za uzalishaji wa vifaa. Pia, vifaa vinavyotumika katika utengenezaji wa mashine za ndani ya nchi huagizwa kutoka nje na kupatikana kwa bei ya juu. Hali hii ilichangia teknolojia za ndani kupatikana kwa gharama kubwa.

(ii) Ushirishaji wa teknolojia kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo Usiojitosheleza

Ukaguzi ulibaini kuwa, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo halikushirikisha ipasavyo teknolojia zake kwa wadau mbalimbali. Ilibainika kuwa, asilimia 42 ya teknolojia zote zilizobuniwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo hazikushirikishwa kwa wadau ndani ya miaka mitano. Ukaguzi ulibaini pia kuwa hakukuwa na mwaka wa fedha ambapo Shirika lilishirikisha teknolojia zote (kwa asilimia 100) ilizobuni. Hali hii ni kinyume na matakwa ya lengo la 5 (5.1) la Mpango-mkakati wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo ambao linataka Shirika kuhakikisha teknolojia za kuongeza thamani zinafanywa kibiashara kila mwaka. Asilimia ya teknolojia zilizobuniwa na kushirikishwa kwa wadau zimeoneshwa katika **Kielelezo Na. 6.1**.

Kielelezo Na. 6.1: Teknolojia Zilizobuniwa na Kushirikishwa kwa Wadau kwa Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2017/18 hadi 2021/22



Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha kwamba, idadi ya teknolojia zilizobuniwa na kushirikishwa kwa wadau katika miaka mitano ya fedha zilitofautiana. Teknolojia zilizohamishwa zilionekana kuwa juu zaidi kwa mwaka wa fedha 2019/20, ambapo asilimia 42 ya teknolojia zote zilishirikishwa kwa wadau. Teknolojia zilizoshirikishwa kwa wadau ni kati ya asilimia 31 hadi 42 ya teknolojia zote zilizobuniwa. Hali hii inamaanisha kuwa teknolojia

zilizobuniwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo zilikuwa haziwafikii ipasavyo wasindikaji wa mazao ya kilimo. Kutokana na hali hiyo, ukaguzi ulibaini kuwa wasindikaji wa mazao ya kilimo walikuwa wanatumia mashine za kizamani ambazo zilikuwa na ufanisi mdogo na zilisababisha hasara na upotevu wa mavuno na kuharibika kwa ubora wa bidhaa za kilimo wakati wa usindikaji.

Miongoni mwa sababu za uhaba wa teknolojia ni kukosekana kwa kipaumbele cha kutosha kwa maendeleo mbalimbali ya kiteknolojia hasa yale yanayotoka katika vituo vya maendeleo ya teknolojia nchini.

(d) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kutohakikisha upatikanaji wa masoko ya kutosha ya bidhaa zilizosindikwa

Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo yanayohusiana na upatikanaji wa masoko ya uhakika ya bidhaa za kilimo zilizosindikwa:

(i) Ukosefu wa mazingira yanayosaidia kukuza soko la bidhaa zinazozalishwa kwa watumiaji wa ndani na nje ya nchi

Kulikuwa na uwezesaji usioridhisha wa mazingira ya kukuza bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi kwa watumiaji wa ndani na nje ya nchi. Hali hii ilisababishwa na ushirikiano duni wa wadau mbalimbali zikiwemo wizara husika. Hakukuwa na uratibu mzuri miongoni mwa wadau ili kuweka mazingira mazuri ya uendelezaji wa masoko ya bidhaa za mazao. Kwa mfano, wakulima walihitaji taarifa kwa wakati juu ya aina na ubora wa mazao au malighafi, ambazo zinahitajika kwenye masoko ya nje na ndani ya nchi, ingawa hali halisi haikuwa hivyo. Kutokana na hali hiyo, wakulima walizalisha malighafi kwa ajili ya usindikaji wa mazao ya kilimo ambazo hayakukidhi ubora na wingi unaotakiwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Hali hii ilisababisha kukosa soko kwa mazao na hatimaye kuchangia ongezeko la hasara baada ya mavuno.

(ii) Uhusianisho duni wa masoko pamoja na bidhaa za kilimo zilizosindikwa

Wakati matumizi ya maonesho ya biashara yakitajwa kuwa miongoni mwa njia za kuboresha uunganishaji wa soko, tathmini iliyofanywa na ukaguzi ilibaini kuwa uhusiano wa soko ulikuwa wa kutosha lakini uliathiriwa na mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni kwamba, njia

zilizotumika katika maonesho ya kibiashara hazikuwa sahihi. Ukaguzi ulibaini kuwa, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo halikufanikiwa kufanya maonesho matano kwa mwaka kama ilivyopangwa. Mahojiano yaliyofanywa kati ya timu ya ukaguzi na maafisa wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo yalibainisha kuwa upungufu huo ulisababishwa na uhaba wa rasilimali kwani Shirika lilitegemea vyanzo vyake vya mapato vilivyopatikana kutoka katika ofisi za mikoa na za kanda.

(iii) Ufungashaji Usioridhisha wa bidhaa zitokanazo na shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo

Taarifa ya Sensa ya Taifa ya Viwanda ya Mwaka 2022 ilibainisha kuwa asilimia 80 ya wasaga nafaka hawakufungasha bidhaa zao. Asilimia 20 iliyobaki ya wasaga nafaka wakubwa na wa kati walifungasha bidhaa zao. Taarifa hiyo inaonesha zaidi kuwa asilimia 64 ya wamiliki wa viwanda vidogo vya kusaga nafaka hawakufungasha bidhaa zao na ni asilimia 36 tu kati yao ndiyo walikuwa na vifungashio vya bidhaa zao. Viwanda vidogo vya kusaga nafaka hawakutoa vifungashio kwa sababu mara nyingi wateja huja na vifungashio vyao wenyewe na wengine walidai kuwa hawakuwa na uwezo wa kununua vifungashio hivyo.



(e) Upatikanaji wa huduma za fedha kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo usioridhisha

Wasindikaji wa mazao ya kilimo walibainisha kuwa walikumkana na matatizo ya kifedha katika utekelezaji wa shughuli zao. Vilivile, ilibainika kuwa upatikanaji wa fedha haukuwa wa kutosha kwani wasindikaji wa mazao ya kilimo hawakuweza kupata fedha kwa wakati na wakati mwingine walipata fedha zisizotosheleza kufanya shughuli zao.

Taarifa zilizotolewa na Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali na Mpango wa Dhamana ya Mikopo zilionyesha kuwa, wastani wa msaada wa kifedha kwa biashara ndogo na za kati kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2021/22 ulikuwa Shilingi. 2,059,036.31 na Shilingi. 31,611,274.51 mtawalia. Pia, ilibainika kuwa kiasi kilichotolewa na Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali kilikuwa hakitoshelezi kuendeleza shughuli za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo. Pamoja na kiasi kilichotolewa na Mpango wa Dhamana ya Mikopo kuwa cha kujitosheleza, ni waombaji wachache tu ndio walipata mkopo huo kwa sababu ya masharti ya mkopo kuwa magumu.

Asilimia ya mikopo inayotolewa kila mwaka ni asilimia 49 kwa mwaka wa fedha 2018/19 na asilimia 51 kwa mwaka wa fedha 2021/22. Waombaji waliopokea mikopo ya Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali walikuwa wakipungua kila mwaka.

Aidha, tathmini iliyofanywa na timu ya ukaguzi juu ya mpango wa ufadhili wa Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali ilibainisha kuwa, mpango huo ulitoa fedha zinazoweza kutosheleza shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo. Wastani wa chini wa mkopo uliotolewa kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo ulikuwa Shilingi. 26,250,000.00 wakati kiwango cha juu cha mkopo kilikuwa Shilingi. 31,611,274.51. Pamoja na kiasi cha ombi la mkopo kilichofadhiliwa chini ya mpango huu kuwa kikubwa ikilinganishwa na kile kilichofadhiliwa na Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali, bado kulikuwa na waombaji wachache kutokana na ugumu wa ufuataji wa masharti ya kupata mkopo huo.

(f) Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara haikufuatilia ipasavyo utendaji wa usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo

Ili kufuatilia kwa ufanisi utendaji wa usindikaji wa mazao ya kilimo, Wizara ilitarajiwa kuwa na msingi wa takwimu na nyenzo za kufuatilia. Hata hivyo, ilibainika kuwa wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo haikuwa na kanzidata ya wasindikaji wa mazao ya kilimo, viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, maeneo yao ya kazi, pamoja na anwani zao ya kudumu. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa idara inayohusika na maendeleo ya viwanda ilikosa taarifa endelevu kuhusu idadi ya viwanda vilivyopo nchini.

Maofisa kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara walionesha kuwa, kukosekana kwa kanzidata ya viwanda vya uchakataji kulisababishwa na utekelezaji duni wa mpango kwa kuwa sekta ya usindikaji wa mazao ya kilimo ilipewa kipaumbele kidogo.

Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ulionesha kuwa, utoaji wa fedha kwa Idara ya Maendeleo ya Viwanda ulikuwa zaidi ya asilimia 80 kwa miaka minne iliyopita (2017/18, 2019/20 pamoja na 2021/22), isipokuwa Mwaka wa Fedha 2020/21 ambapo utoaji huo ulibainika kuwa asilimia 41.

Ukaguzi ulibaini kuwa shughuli za utambuzi na usajili zilianza katika mwaka wa fedha 2020/21 na zilitarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2021/22. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi huu, shughuli hizo zilikuwa bado zinaendelea na mafanikio yaliyopatikana ni kwa mikoa mitatu tu kati ya 26 ya Tanzania Bara sawa na asilimia 12.

(g) Uratibu Usioridhisha kati ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo katika kusimamia shughuli za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo

Ukaguzi ulibaini mapungufu yafuatayo katika kuhakikisha uratibu mzuri wa shughuli za usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo:

(i) Mwingiliano wa kazi za kusimamia usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo kati ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo

Ukaguzi huu ulibaini uratibu usioridhisha kama inavyohibitishwa na kuwapo kwa mwingiliano wa majukumu kati ya idara zenye dhamana ya kusimamia usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo zilizo chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Kilimo. Vilevile, ilibainika kuwa wizara zote mbili zilikuwa na idara inayohusika na masoko, ikiwa na majukumu ya kutafuta masoko ndani na nje ya nchi. Pia, ilibainika kuwa sheria za uanzishaji wa wizara hizi mbili hazikuonesha tofauti ya kimajukumu kati yake kuhusu masoko ya bidhaa za kilimo zilizosindikwa.

Vilevile, baadhi ya majukumu kati ya wizara hizi mbili yaliingiliana. Kwa mfano, katika Wizara ya Kilimo, shughuli za uchakataji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo zilifanyika katika Idara ya Kilimo, wakati shughuli hizohizo pia zilifanyika katika Idara ya Biashara Ndogo na za Kati na ile ya Viwanda na Maendeleo katika Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Licha ya kuwapo kwa mwingiliano katika majukumu, ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara hazikuwa na utaratibu rasmi wa kubadilishana taarifa za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo.

(ii) Kukosekana kwa uratibu kati ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo na mashirika mengine ya utafiti wa teknolojia

Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa uratibu usioridhisha kati ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo na mashirika mengine kama vile Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo na Shirika la Maendeleo na Utafiti wa Viwanda Tanzania ili kuliwezesha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo kuendeleza utafiti wa teknolojia. Pamoja na hayo, ilibainika kuwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo halikubadilishana teknolojia na taasisi hizi za kitaalamu kutokana na kukosekana kwa uratibu. Pia, ilibainika kuwa taasisi hizi zilikuwa zikifanya kazi kwa kujitenga na hakukuwa na mipango ya kushirikishana maarifa na teknolojia.

Kukosekana kwa uratibu kati ya taasisi za utafiti pamoja na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo kulisababishwa na mawazo ya asili ya uzalishaji wa mazao. Kutokana na hali hiyo, kila taasisi ilificha teknolojia yake kwa kuhofia kunakiliwa na taasisi nyingine licha ya kwamba zote ziko chini ya wizara moja.

6.5 Mchango wa Kaguzi katika Kufikia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sehemu hii inatoa ufafanuzi wa mchango wa kaguzi zilizofanyika katika usimamizi wa viumbe vamizi pamoja na usimamizi wa usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo nchini katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mipango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maelezo zaidi ya mchango wa kaguzi hizi yametolewa hapa chini.

Serikali imehakikisha ulinzi wa mazingira na uhakika wa chakula nchini kwa kubuni mikakati na jitihada mbalimbali. Hata hivyo, kupitia kaguzi za ufanisi zilizofanyika, ilibainika kuwa utekelezaji wa mikakati na jitihada hizo haukufanyika kwa ufanisi na utoshelevu.

Ili kusimamia viumbe vamizi, lengo la 15.8 la Malengo ya Maendeleo Endelevu lilielekezwa kuanzisha hatua za kuzuia na kupunguza kwa kiasi kikubwa athari za viumbe vamizi kwenye mazingira ya ardhi na maji na kuangalia namna ya kudhibiti au kutokomeza viumbe hawa. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unasisitiza juu ya kuongeza ufuatiliaji wa mikakati ya usimamizi wa viumbe vamizi ifikapo mwezi Juni

2026 ili kupunguza upotevu wa viumbe hai kutoka asilimia 16 mwaka 2019/20 hadi asilimia 14 mwaka 2025/26.

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na utekelezaji usioridhisha wa hatua za kuzuia, kudhibiti na kupunguza athari za viumbe vamizi. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa rasilimali na ujuzi wa kitaalamu kuhusu viumbe hawa. Aidha, hakukuwa na tafiti za kina ili kuthibitisha uingiaji, ukuaji na ueneaaji wa viumbe vamizi nchini.

Kwa upande wa usimamizi wa uchakataji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo nchini, lengo la 2.3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linaekeza kuongeza maradufu uzalishaji wa mazao ya kilimo na kipato cha wazalishaji wadogo wa chakula, hususani wanawake, wazawa, wafugaji, na wavuvi, ikiwa pamoja na usawa na upatikanaji wa ardhi, rasilimali zingine za uzalishaji mali, na pembejeo. Vilevile, lengo hili linaekeza kuongeza maarifa, huduma za kifedha, masoko, na fursa za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unasisitiza kukuza uwekezaji katika uzalishaji na matumizi ya vyakula mbalimbali vyenye virutubisho pamoja na kuongeza uzalishaji, usambazaji na matumizi ya chakula nchini.



Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na utekelezaji duni wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kutokana na uhaba wa teknolojia zilizopo ili kuwezesha usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo. Aidha, ilibainika kuwa asilimia 75 ya sera, mikakati na malengo yanayohusiana na usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya chakula hayakutekelezwa. Ukaguzi huu pia ulibaini kuwa kulikuwa na matumizi ya mashine za teknolojia za kizamani katika usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo. Aidha, teknolojia ya usindikaji ya ndani ya nchi ilikuwa na gharama kubwa ikilinganishwa na teknolojia kutoka nje ya nchi.

6.6 Hitimisho la Ukaguzi

Sehemu hii inatoa maelezo juu ya hitimisho la ukaguzi kulingana na matokeo yaliyotokana na malengo ya jumla na mahususi ya kaguzi hizi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

6.6.1 Hitimisho la Ujumla

Timu ya ukaguzi inatambua juhudi zilizooneshwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; na Wizara ya Kilimo katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa mazingira na uhakika wa chakula nchini.

Hata hivyo, mapungufu kadhaa yalibainishwa na hivyo yanahitaji maboresho. Hali hii inatokana na Wizara kutosimamia ipasavyo viumbe vamizi pamoja na usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo. Hali hii iliongeza hatari ya kuwapo kwa maendeleo duni ya kijamii kupitia utunzaji wa viumbe hai na kupunguza hasara baada ya mavuno ya mazao ya kilimo.



6.6.2 Hitimisho Maalumu

Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira haikusimamia ipasavyo viumbe vamizi nchini katika mazingira ya nchikavu na hivyo kuongeza hatari ya athari za viumbe hawa katika bayoanuai pamoja na mifumo ya ikolojia nchini. Hali hii ilidhihirishwa na mambo yafuatayo:

Uzuiaji wa viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu ulibainika kuwa na mapungufu. Hali hii ilidhihirishwa na ukweli kwamba, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na wizara za kisekta, haikutambua na kuainisha njia mbalimbali zilizotumiwa na viumbe vamizi kuenena. Vilevile, kulikuwa na uzuiaji usiojitosheleza wa viumbe vamizi katika sehemu za kuingilia nchini. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na wizara za kisekta haikukufanya tathmini ya hatari na athari za kimazingira zinazolenga kutambua viumbe vamizi katika mazingira.

Vilevile, kulikuwa na changamoto katika hatua zilizotumiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na wizara za na kisekta katika kudhibiti viumbe vamizi nchini. Hali hii ilidhihirishwa na kukosekana kwa kanzidata ya kitaifa

ya aina mbalimbali za viumbe vamizi na utafiti duni wa viumbe hawa. Pia, ilibainika kulikuwa na matumizi ya chini ya rasilimali katika kudhibiti viumbe vamizi na athari zake katika mazingira.

Ilibainika zaidi kuwa, hakukuwa na juhudi na uratibu wa pamoja wa kuhakikisha usimamizi wa kutosha wa viumbe vamizi nchini. Hali hii ilidhihirishwa na kukosekana kwa juhudi za pamoja za utekelezaji wa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa Taifa wa Viumbe Vamizi wa Mwaka 2019-2029; ushirikishaji duni wa taarifa katika sekta nzima na wadau wote; pamoja na ushirikiano hafifu katika mipaka ya nchi jirani.

Ufuatiliaji na tathmini ya usimamizi wa viumbe vamizi nchini haukufanyika ipasavyo. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa mpango wa kila mwaka wa ufuatiliaji na tathmini; na mfumo usiofaa wa utoaji taarifa na vikao vya mapitio ya utendaji ili kubaini hali ya utekelezaji wa mipango ya kusimamia viumbe vamizi.

Kwa upande mwingine, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Kilimo hazikusimamia ipasavyo shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo na uongezaji wa thamani ya mazao ili kupunguza hasara baada ya mavuno, kuboresha uchumi wa wakulima, na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa.

Wizara husika hazikuweka mazingira rafiki kwa wasindikaji wa mazao ya kilimo. Teknolojia za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo hazikufikiwa kwa urahisi na wasindikaji wengi wa mazao ya kilimo kutokana na gharama kubwa ya kupata teknolojia hizo.

Matokeo yake, kumekuwa na uboreshaji usiotosheleza katika upotevu wa mavuno ya mazao ya kilimo kwa kuwa wastani wa asilimia 40 ya mazao yote yaliyovunwa yalikuwa na ubora usioridhisha na hivyo kukosa ushindani katika soko la nje. Utaratibu duni wa upatikanaji wa teknolojia zinazohitajika za usindikaji na uongezaji thamani, uratibu usiojitosheleza, na ufuatiliaji usioridhisha ndio sababu kuu za utendaji hafifu katika shughuli za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo.

Aidha, ongezeko la upotevu wa mavuno ya mazao ya kilimo ulisababisha uhaba wa malighafi kwa ajili ya uendeshaji wenye ufanisi wa viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo pamoja na kuongeza hatari kwa uhakika wa

chakula nchini kutokana na kuwapo kwa viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo ambavyo havifanyi kazi. Vilevile, kukosekana kwa utaratibu madhubuti wa ufadhili na utekelezaji wa mikakati iliyopo, kulisababisha kuwapo kwa usimamizi duni wa usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo .



USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA NA UWEKEZAJI WA MALI ZA SERIKALI

SURA YA SABA

7



USIMAMIZI WA MALI ZA UMMA NA UWEKEZAJI WA MALI ZA SERIKALI

7.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa kaguzi mbili za ufanisi wa utawala bora na utawala wa sheria, hifadhi ya jamii, na masuala ya mageuzi ya mazingira ya biashara na uwekezaji yanayounganishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpangano wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Ukaguzi huu wa ufanisi unajumuisha ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uondoshaji wa magari ya serikali; na ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa uwekezaji wa mali zisizohamishika unaotekelezwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Sura hii inaangazia uhusiano wa utawala bora na utawala wa sheria, ulinzi wa jamii, na uimarishaji wa mageuzi ya mazingira ya biashara na uwekezaji kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpangano wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa malengo na juhudi za serikali katika kuhakikisha uondoshaji wa magari ya serikali na uwekezaji wa mali za serikali. Sura hii pia inawasilisha malengo na mawanda ya kaguzi pamoja na matokeo, hitimisho na mapendekezo ya ukaguzi.



7.2 Usuli kuhusu Usimamizi wa Uondoshaji wa Magari ya Serikali na Uwekezaji wa Mali za Serikali.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 1994 - 1995, serikali ya Tanzania iliamua kuondoa magari yote kwa wafanyakazi wa umma na kuweka kikomo kwa kila taasisi kuwa na magari mawili ili kupunguza matumizi makubwa na gharama zitokanazo na idadi kubwa ya magari. Mfanyakazi wa umma aliyekuwa anatumia gari husika alipewa kipaumbele cha kuuziwa gari hilo na magari yaliyobaki yalipigwa mnada.

Tofauti na sasa, Serikali inatumia kiasi kikubwa cha fedha (takribani Shilingi bilioni 500) katika ununuzi wa magari, matengenezo ya magari na ununuzi wa mafuta ya kuendesha magari ya serikali. Mwaka 2009 Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitoa mwongozo wa uendelezaji wa maboresho ya magari ya serikali kwa wafanyakazi wa umma. Miongozo iliyotolewa ilikusudia kusawazisha taratibu za uondoshaji wa magari ya Serikali katika taasisi za umma nchini.

Tanzania ina mifuko mikuu miwili ya hifadhi za jamii ambayo ni Mfuko wa

Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii unahusika na waajiri na wafanyakazi kutoka sekta binafsi zikiwemo kampuni, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kidini, huku Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ukishuhusika na watumishi wa umma. Mifuko yote miwili inahusisha usajili wa wanachama, ukusanyaji wa michango, uwekezaji wa michango iliyokusanywa, na ulipaji wa mafao kwa wanachama wanaositaili.

Serikali ilifanya jitihada za kujenga mazingira bora ya uwekezaji na uendeshaji ambayo yanatoa nafasi ya uchumi kukua hadi wastani wa asilimia 7 kwa mwaka. Kwa hiyo, wastani wa ukuaji wa mapato ya kila mwaka ya uwekezaji unaofanywa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii unatarajiwa kupata na kuendelea kutoa faida zaidi kwa mfuko na juu ya mtaji uliowekezwa.

7.2.1 Usimamizi wa uwekezaji na mali za serikali unavyohusishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Maeneo mawili yaliyokaguliwa yanahushishwa na utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Kwa mfano, menejimenti ya uondoshaji wa magari ya serikali imetekeleza maboresha ya utawala bora na utawala wa sheria. M, huku menejimenti ya uwekezaji wa mali za serikali imetekeleza maboresho ya hifadhi ya jamii, uimarishaji, na mageuzi ya mazingira bora ya biashara na uwekezaji.

Usimamizi wa uwekezaji na mali za serikali unavyohusishwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi zilizotia saina Ajenda ya Mwaka 2030 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu imechukua hatua za kuunganisha ajenda hiyo katika muktadha wa kitaifa. Kwa hiyo, utekelezaji wa ukaguzi wa ufanisi katika uwekezaji wa mali za umma una umuhimu mkubwa kwa kuwa ukaguzi huo unahusishwa moja kwa moja na Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030. Uhusiano uliopo ni kwamba lengo la namba 1 lengo dogo namba 1.3 linahitaji uwiano wa idadi ya watu waliohusishwa na hifadhi ya jamii kijinsia, watu wasio na ajira, watoto waliotengwa, wazee, watu wenye ulemavu, wajawazito, watoto

wachanga, watu walioumia kazini, maskini, na watu walio katika mazingira magumu.

Zaidi ya hayo, lengo namba 5 lengo dogo namba 5.4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linatambua na kuthamini matunzo yasiyolipiwa na kazi za nyumbani kupitia utoaji wa huduma za umma, miundombinu, na sera ya hifadhi za jamii na kukuza uwajibikaji wa pamoja ndani ya kaya na familia kama inavyotakiwa kitaifa.

Ukaguzi wa ufanisi wa usimamizi wa mali za serikali na uwekezaji unashughulikia kipengele cha hifadhi ya jamii cha Malengo ya Maendeleo Endelevu kwani usimamizi mzuri wa uwekezaji wa Mfuko utahakikisha malipo endelevu ya wanufaika.

Hivyo, utekelezaji wa mapendekezo yanayotokana na ukaguzi wa ufanisi wa mali za serikali na uwekezaji utaimarisha kufikiwa kwa malengo ya 1 na 5 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Usimamizi wa uwekezaji na mali za serikali unavyohusishwa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano



Mkakati namba 5.5.4 wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaeleza kuwa mifuko ya hifadhi ya jamii kihistoria imekuwa wawekezaji wa kutegemewa katika maeneo mbalimbali kwa kutumia fedha zinazokusanywa ndani ya nchi kwa njia ya michango ya wanachama wa mifuko hiyo.

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2015 uliotolewa na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, mifuko itashiriki kikamilifu katika fursa zilizopo za kuwekeza katika viwanda vilivyopo na vipya kupitia mikopo iliyunganishwa; dhamana za mifuko; au fedha za ndani. Mifumo ya Hifadhi ya Jamii itafanya kazi kwa karibu na taasisi zingine zinazohusika zikiwemo Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana; Benki ya Taifa ya Uwekezaji - Maendeleo; Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania; na Shirika la Maendeleo la Taifa.

Vilevile, kaguzi zilizofanyika katika sura hii zilijikita katika tathmini ya mali zilizowekezwa na mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

7.2.2 Mikakati na juhudi za Serikali katika usimamizi wa mali na uwekezaji wa Serikali

Mikakati na juhudi za Serikali zilizohusika katika ukaguzi huu ni uondoshaji wa magari ya Serikali; na uwekezaji wa miradi kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Juhudi katika eneo la uondoshaji wa magari ya Serikali

Wizara ya Fedha na Mipango iliandaa mpango-mkakati wake wa kwanza wa mwaka 2012/13-2016/17 kama nyenzo ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Mwaka 2011/12 - 2015/16 na Mpango-mkakati wa Pili wa Mwaka 2017/18 - 2021/22. Mipango hii ilikusudiwa kufikia usimamizi wa fedha na uwajibikaji, haswa usimamizi wa magari kuanzia wakati wa ununuzi hadi uondoshaji.

Mkakati mkuu kuhusu uondoshaji wa magari ya Serikali ni pamoja na kuimarisha usimamizi na uratibu wa uondoshaji magari yasiyoweza kukarabatiwa na Serikali kutoka wizara, idara na wakala; ofisi za mikoa; na halmashauri yaondoshwe ifikapo mwezi Juni 2022 kwa mtiririko huo.

Juhudi kwenye eneo la uwekezaji wa miradi

Hizi ni juhudi za Serikali katika kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji wa miradi ili kukuza uchumi wa nchi. Mazingira yanayotarajiwa ya uwekezaji na uendeshaji yangetoa nafasi kwa uchumi kukua hadi wastani wa asilimia 7 kwa mwaka. Wastani wa ukuaji wa pato la kila mwaka katika uwekezaji unatarajiwa kuendelea kutoa na kuongeza mapato ya mifuko.

Serikali pia ilidhamiria kuongeza ajira ili kuongeza mchango katika mifuko ya hifadhi ya jamii. Kwa mfano, kati ya mwaka 2016/17 na 2018/19 nafasi za ajira zilizotengenezwa zilikuwa 1,167,988. Hali hii ilikuza michango iliyokusanywa na mifuko ya hifadhi za jamii. Kwa kuzingatia kifungu cha 4.3.7 na 5.5.4 cha Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Benki Kuu ya Tanzania iliazimia kuendelea kuandaa mwongozo wa kimkakati kuhusu mbinu za uwekezaji zinazolenga kuhakikisha mifuko inakuwa imara na uendelevu.

7.3 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha malengo na mawanda ya ukaguzi kwa Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Mandeleo wa Taifa wa Miaka Mitano:

7.3.1 Malengo ya Ukaguzi

Lengo kuu lilikuwa kutathmini iwapo wizara zinazohusika zimesimamia ipasavyo mali zinazomilikiwa au kusimamiwa na Serikali. Malengo mahususi ya ukaguzi yalikuwa kutathmini iwapo:

- (i) Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilisimamia ipasavyo uondoshaji wa magari ya Serikali kwa wakati na kwa thamani inanyotakiwa; na
- (ii) Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma imesimamia kwa ufanisi na tija uwekezaji wa mali zake (majengo,viwanja na daraja).



7.3.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulihusisha taasisi kuu tatu zilizokaguliwa ambazo ni Wizara ya Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma.

Kuhusu usimamizi wa uondoshaji wa magari ya serikali, ukaguzi ulihusisha maeneo makuu manne ambayo ni utambuzi, uthamini, idhini ya uondoshaji, na ufuatiliaji wa uondoaji wa magari ya Serikali. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2021/22.

Katika usimamizi wa uwekezaji wa mali za serikali (majengo,viwanja na daraja) taasisi kuu zilizokaguliwa zilikuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii.

Ukaguzi ulitathmini mipango ya uwekezaji wa mali, uendeshaji wa mali zilizowekezwa, matengenezo ya mali zilizowekezawa, na utoshlevu wa

ufuatiliaji na tathmini juu ya usimamizi wa mali zisizohamishika. Ukaguzi ulilenga zaidi uwekezaji wa mali zisizohamishika (majengo ya biashara, nyumba za kuishi, viwanja na daraja) chini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii. Hususani, ukaguzi ulitathmini mipango, matengenezo, ufuatiliaji na tathmini za mali zisizohamishika. Ukaguzi ulihusisha kipindi chote ambacho uwekezaji wa majengo ulifanyika, ambacho ni kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011 hadi mwezi Juni 2022.

7.4 Matokeo Makuu ya Ukaguzi

Matokeo makuu ya ukaguzi yamegawanywa katika vipengele viwili kulingana na ukaguzi. Katika suala hili, sura hii inawasilisha matokeo yanayohusiana na usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali na matokeo yanayohusiana na usimamizi wa uwekezaji wa mali zisizohamishika. Kasoro zilizobainika wakati wa ukaguzi zimewasilishwa hapa chini kama ifuatavyo:

7.4.1 Matokeo ya usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali

Matokeo yanayohusiana na sehemu hii yalihusu usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali unaofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama ilivyoelezwa hapa chini.

a) Magari mabovu 547 ya Serikali kutotumika muda mrefu

Utumiaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali hutoa uhakika kwamba mali za serikali si tu zinatunzwa na kuboreshwa bali pia zinakuwa imara na endelevu kwa muda mrefu. Kulingana na kiwango cha ISO 55001, ilitarajiwa kwamba magari ya Serikali yaliyo katika taasisi zake tofauti yawe yanatumika chini ya utaratibu maalumu wa matengenezo au uondoshaji.

Kutokana na mapitio ya ripoti mbalimbali, ukaguzi ulibaini kuwa hadi mwezi Septemba 2022, magari 547 ya Serikali yaliwekwa katika karakana za Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) na katika baadhi ya taasisi za Serikali. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa magari mabovu ambayo yamewekwa na hayatumiki hayakuwa na mpango wa matengenezo wala uondoshaji. **Jedwali Na. 7.1** linaonesha idadi ya magari mabovu ambayo yamehifadhiwa

na hayatumiki katika baadhi ya taasisi za Serikali na Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania.

Jedwali Na. 7.1: Magari Mabovu ambayo Yameegeshwa na Hayatumiki kufikia Mwezi Septemba 2022

| Aina ya Taasisi/Wakala | Jina la Taasisi/ Wakala | Idadi ya Magari Mabovu |
|---|---|------------------------|
| Mashirika ya Umma na Taasisi Zingine | Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) | 86 |
| | Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) | 19 |
| Wizara | Wizara ya Fedha na Mipango | 51 |
| | Wizara ya Mambo ya Nje | 39 |
| | Wizara ya Afya | 14 |
| Wakala na Taasisi Mbalibali chini ya Wizara | Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) | 176 |
| | Wakala wa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) | 44 |
| | Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | 37 |
| Mamlaka za Serikali za Mitaa | Halmashauri ya Jiji la Tanga | 18 |
| | Halmashauri ya Wilaya ya Meatu | 15 |
| | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | 13 |
| | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa | 12 |
| Taasisi Zinazojitegemea | Mahakama ya Tanzania | 23 |
| Jumla | | 547 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi kuhusu Magari Mabovu Yamehifadhiwa na Hayatumiki kwa Muda Mrefu Mwaka 2022

Jedwali Na. 7.1 linaonesha kuwa takribani magari mabovu 547 ya Serikali ambayo yalikuwa yamehifadhiwa na hayatumiki katika taasisi zilizotembelewa. Ikumbukwe kuwa idadi kubwa ya magari mabovu ambayo yamehifadhiwa na hayatumiki ilikuwa katika Wakala wa Ufundi na Umeme iliyokuwa na magari 176 ikifuatiwa na Kampuni ya Simu Tanzania iliyokuwa na magari 86. Katika taasisi zilizokaguliwa, idadi ndogo kabisa ya magari mabovu ilikuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa iliyokuwa na magari 12.

Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya magari hayakuwa na mipango ya matengenezo wala uondoshaji. Magari hayo hayakuwa yakitumika kwa sababu mbalimbali kama vile ajali, kutofanyiwa matengenezo, kuegeshwa, na kusubiri vibali vya uondoshwaji. Sababu nyingine ni pamoja na tathmini duni ya magari yanayotakiwa kuondoshwa, kukosekana kwa uwazi wa magari yaliyoondoshwa mapema kwa watumishi, na usajili duni wa magari ya Serikali katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali. Pia, ukaguzi ulibaini kuwa magari ya Serikali yanayowekwa kwenye karakana za Wkala wa Ufundi na Umeme na vituo vingine vya serikali yalikusishwa na uhakiki na ukaguzi hafifu wa kipindi kirefu cha magari unaofanywa na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM).

Kuwapo kwa magari mabovu ya Serikali ambayo yamehifadhiwa na hayatumiki kwa muda mrefu bila uondoshaji kulikuwa na athari zifuatazo:

- (i) Magari mabovu yaliyohifadhiwa na hayatumiki kwa muda mrefu huchakaa na huharibika zaidi na kwa kasi na hivyo kupungua kwa kasi thamani yake, hata wakati Serikali inapoamua kuyaondoa;
- (ii) Madhumuni ya ununuzi wa magari hayafikiwi ipasavyo kwa vile magari hayafanyi kazi kulingana na madhumuni yaliyokusudiwa;
- (iii) Kuongezeka kwa gharama za matengenezo kutokana na uchakavu wa magari mabovu ambayo yamehifadhiwa na hayatumiki kwa muda mrefu; na
- (iv) Upotevu wa rasilimali-fedha za umma

b) Tathmini isiyotosheleza ya magari ya takayoondoshwa

Kifungu cha 16 cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma cha Mwaka 2019 kinamtaka afisa masuuli kuhesabu na kubainisha mali zisizo na manufaa zinazopaswa kuondolewa kila mwaka. Aidha, afisa masuuli analazimika kuteua bodi ya ukaguzi ili kukagua na kuandaa ripoti ambayo itatumika kuandaa mpango mbadala.

Ukaguzi ulibaini kuwa utambuzi wa magari haukufanyika ipasavyo kwa sababu taasisi hazikuwa na bodi za tathmini ya kufanya shughuli hiyo. Timu ya ukaguzi ilibaini kuwa katika taasisi 9 kati ya 10 zilizotembelewa, maafisa masuuli hawakuunda bodi za ukaguzi ili kutathmini na kubainisha magari ya kuondolewa au kubadilishwa. **Jedwali Na. 7.2** linaonesha hali ya uundaji wa bodi za ukaguzi lilizopaswa kuundwa na maafisa masuuli katika taasisi za serikali zilizotembelewa.

Jedwali Na. 7.2: Hali ya Uundaji wa Bodi za Utafiti

| Taasisi Inayotakiwa Kuondosha Magari | Hali Halisi |
|--|------------------|
| Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa | Bodi haikuundwa. |
| Halmashauri ya Jiji la Tanga | Bodi haikuundwa. |
| Halmashauri ya Wilaya ya Njombe | Bodi haikuundwa. |
| Mahakama ya Tanzania - Fungu 40 | Bodi haikuundwa. |
| Wizara ya Afya | Bodi haikuundwa. |
| Wizara ya Fedha na Mipango | Bodi haikuundwa. |
| Wizara ya Mambo ya Nje | Bodi haikuundwa. |
| Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | Bodi haikuundwa. |
| Shirika la Simu Tanzania (TTCL) | Bodi haikuundwa. |
| Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) | Bodi haikuundwa. |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Taasisi Zilizotembelewa Mwaka 2022

Jedwali Na. 7.2 linaonesha kuwa taasisi zote zilizotembelewa hazikuunda bodi za ukaguzi ili kuhesabu na kutathmini magari yatakayoondoshwa kila mwaka. Hali hii inatia shaka kuhusu uamuzi wa uondoshaji wa magari uliofanyika kipindi cha nyuma.

Kwa magari yaliyotakiwa kupewa wafanyakazi, ukaguzi ulibaini uwezekano wa muda wa magari hayo kuegeshwa ili yaonekane kuhitaji matengenezo makubwa hivyo kupunguza thamani ya magari hayo. Ukaguzi ulibaini pia kuwa vibali vya uondoshaji wa magari kwa wafanyakazi haukuzingatia uundaji na maamuzi ya bodi za uchunguzi. Hali hii ilikuwa kinyume na matakwa ya aya ya 16 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa Mwaka 2019.

Maafisa masuuli kutounda bodi za ukaguzi kulichangiwa na kutozingatia miongozo ya usimamizi wa mali za serikali na uhakiki usiotosheleza wa mali za serikali unaofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango.

c) Usajili usioridhisha wa Magari ya Serikali katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)

Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2021/22 kuhusu usimamizi wa mali za umma kupitia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS), uliotolewa tarehe 15 Julai 2021 ulizitaka taasisi zote za umma kusajili mali zao, yakiwemo magari katika mfumo huo ifikapo tarehe 31 Agosti 2021 ili kuwa na taarifa za mali zote na hali zake. **Jedwali Na. 7.3** linaonesha hali ya taasisi zilizosajiliwa katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali.

Jendwali Na. 7.3: Hali ya Mali za Taasisi Zilizosajiliwa katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS)

| Taasisi | Hali Halisi ya Usajili katika GAMIS |
|--|-------------------------------------|
| Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa | ✓ |
| Mahakama ya Tanzania - Fungu 40 | ✓ |
| Wizara ya Afya | ✓ |
| Wizara ya Mambo ya Nje | ✓ |
| Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | ✓ |
| Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) | ✓ |
| Halmashauri ya Jiji la Tanga | x |
| Halmashauri ya Wilaya ya Njombe | x |
| Wizara ya Fedha na Mipango | x |
| Kampuni ya Simu TTCL | x |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali Mwaka 2022

Ufunguo

X = Haijasajiliwa

✓ = Imesajiliwa



Jedwali Na. 7.3 linaonesha kwamba hadi tarehe 30 Septemba 2022, taasisi 6 kati ya 10 zilizochaguliwa zilikuwa na mali zilizosajiliwa katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali. Taasisi hizo ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Mahakama ya Tanzania - Fungu 40, Wizara ya Afya, Wizara ya Mambo ya Nje, TANROADS na TBC. Taasisi ambazo hazijasajiliwa ni Halmashauri ya jiji la Tanga, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Wizara ya Fedha na Mipango na TTCL.

Ukaguzi ulibaini sababu tofautitofauti za kutosajili magari katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali. Kwa mfano, Kampuni ya Simu TTCL ilisema kuwa daftari lao la mali za kudumu halikidhi mahitaji ya mfumo. Mfumo uliokuwapo wa Kampuni ya Simu haukuwa na taarifa muhimu kama vile sehemu zilizopo mali na hali ya mali husika. Kwa hiyo, Kampuni ya Simu imekuwa ikiifanyia kazi kwa kufanya uhakiki wa moja kwa moja ambao taarifa zake zitawekwa kwenye mifumo badaye. Kwa upande mwingine, Halmashauri ya Wilaya ya Tanga na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe hazikutoa sababu za wazi za kutosajili mali zao kwenye Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali licha ya kupewa mafunzo kufanya hivyo.

Ukaguzi ulilinganisha idadi ya magari yaliyosajiliwa kwenye Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali na idadi ya magari yanayomilikiwa na taasisi za serikali. **Jedwali Na. 7.4** linaonesha hali halisi ya idadi ya magari yaliyopo na idadi iliyorekodiwa kwenye mfumo.

Jedwali Na. 7.4: Hali Halisi ya Magari Yaliyosajiliwa katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali dhidi ya Idadi Halisi ya Magari Yanayomilikiwa na Taasisi za Umma

| Taasisi | Idadi ya Magari Yaliyo sajiliwa kwenye GAMIS | Idadi Kamili ya Magari Iliyopo | Tofauti |
|--|--|--------------------------------|---------|
| Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) | 411 | 567 | 156 |
| Mahakama ya Tanzania - Fungu 40 | 353 | 443 | 90 |
| Wizara ya Fedha na Mipango | 196 | 147 | 49 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa | 25 | 27 | 2 |
| Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) | 68 | 68 | 0 |
| Wizara ya Mambo ya Nje | 101 | 83 | 18 |
| Wizara ya Afya | 198 | 83 | 103 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa kwenye Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali Mwaka 2022

Jedwali Na. 7.4 linaonesha kuwa kulikuwa na kutolingana kwa takwimu katika Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali na idadi halisi ya magari yanayopatikana kwenye taasisi husika. Ukaguzi ulibaini kuwa kwa Wakala wa Barabara Tanzania, tofauti ni magari 156 ambayo ndiyo idadi ya juu zaidi, wakati katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, tofauti ni magari 2 ambayo ni taasisi ya chini zaidi kati ya taasisi vilizotembelewa. Shirika la Utangazaji Tanzania ndiyo taasisi pekee ambayo haikuwa na tatizo hilo. Hali hii inaonesha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango haina usajili wa wazi na halisi wa magari ya serikali na kujua hali zake.

Kupitia mahojiano na maafisa wa Wizara ya Fedha na Mipango, ilibainika kuwa taasisi za umma hazikuweka na kuidhinisha kwa wakati taarifa mpya katika mfumo licha ya jitihada za Wizara ya Fedha na Mipango katika

kuwajengea uwezo wa kutumia mfumo wa Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali katika taasisi zote zilizotembelewa.

Ukaguzi ulibaini kuwa kukosekana kwa takwimu za kutosha za magari na hali zake kulichangiwa na kushindwa kufanyika kwa kaguzi za mali za serikali na ni vipengele vitatu tu kati ya tisa vilivyopo kwenye Mfumo wa Taarifa wa Usimamizi wa Mali za Serikali ndizo zilizofanyiwa kazi.

d) Uthaminishaji Usioridhisha wa magari ya Serikali yanayouzwa kwa watumishi.

Agizo Na 13 (3) (b) la Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Tangazo la Serikali Na. 493 la Mwaka 2009 linataka bei ya ununuzi wa gari kutoka Serikalini, mamlaka za serikali za mitaa, mashirika ya umma, au kupitia chanzo kingine chochote ikokotolewe kutokana na gharama halisi kwa kuzingatia uchakavu wa gari. Ili kuthibitisha ufanisi wa uthamini uliofanywa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ukaguzi ulikokotoa tena thamani ya magari 500 yaliyotolewa ambapo miongoni mwa magari yaliunzwa kwa watumishi wa umma kuanzia mwaka wa fedha 2016/17- 2021/22.

Ukaguzi ulibaini tofauti kati ya takwimu zilizowekwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na zilizoandaliwa na timu ya ukaguzi. **Jedwali Na. 7.5** linaonesha tofauti ya takwimu zilizotengenezwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na iliyoandaliwa na timu ya ukaguzi kwa asilimia 36 na 836 mtawalia.

Jedwali Na. 7.5: Tofauti ya Takwimu kati ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Timu ya Ukaguzi

| Tofauti ya Takwimu katika Asilimia (%) | Idadi ya Magari | Asilimia ya Magari |
|--|-----------------|--------------------|
| -36-0 | 11 | 2 |
| <10 | 14 | 3 |
| 10-100 | 296 | 59 |
| 101-200 | 148 | 30 |
| 201-836 | 34 | 7 |

Chanzo: Mchanganuo wa Wakaguzi wa Taarifa za Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wa Mwaka 2016/17 hadi 2021/22

Jedwali Na. 7.5 linaonesha kuwa kulikuwa na magari matano yaliyotathminiwa kwa thamani ya juu kupita kiasi; magari matatu yalikuwa na thamani sahihi, na magari 482 sawa na asilimia 96.4 yalitathminiwa kwa thamani ya chini. Tofauti hizi zinaonesha thamani ya magari 500 miongoni mwa magari yaliyochanguliwa yalitathminiwa kwa thamani ya chini sawa na Shilingi bilioni 2.7.

e) Upungufu wakati wa kutathmini thamani za magari

Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu (IAS 16) na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta za Umma (IPSAS 17), gharama za mali, mitambo na vifaa pamoja na gharama zilizotumika awali kupata mitambo na vifaa na gharama zilizotumika baadaye kuongeza, hubadilisha sehemu ya mali hizo au kuzifanyia matengenezo yeyote mali hizo. Gharama ya kupata bidhaa inajumuisha (a) bei yake ya ununuzi, ikijumuisha ushuru wa bidhaa na kodi zisizorejeshwa za ununuzi, baada ya kutoa punguzo la biashara na makato yote; (b) gharama zozote zinazohusishwa moja kwa moja za kuifikisha mali hadi mahali inapotakiwa na ikiwa katika hali nzuri ili ifanye kazi iliyokusudiwa na watumiaji wake; na baadaye, gharama inayojumuisha ukarabati na matengenezo makubwa tu na si ya mara kwa mara.

Mapitio ya ripoti za uthamini zilizofanywa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilionesha kuwa uthamini ulizingatia tu bei ya ununuzi na gharama za bima. Gharama zingine za awali kama vile kodi, ushuru wa bidhaa na gharama za kibali hazikuzingatiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wakati wa uthamini. Kwa hiyo, thamani ya mali ilikuwa chini ikilinganishwa na thamani yake halisi, ambayo ina athari kubwa kwa thamani ya gari lililoondoshwa.

Kutojumuishwa kwa gharama zingine kulisababisha uondoshaji wa magari kuwa wa thamani ndogo. Wakati wa uhakiki, timu ya ukaguzi ilibaini kuwa kulikuwa na tofauti ya asilimia 83 ya thamani ya mali ikiwa na gharama za uagizaji pekee na zile zilizojumuishwa gharama zote za ununuzi kama zilivyokokotolewa na wakaguzi. **Jedwali Na. 7.6** linalinganisha thamani halisi pamoja na gharama za ununuzi na bima pekee katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Jedwali Na. 7.6: Thamani ya Awali ya Magari Ikilinganishwa na Gharama Zote za Ununuzi na Bima Pekee katika Wizara ya Fedha na Mipango

| Taasisi | Idadi ya Magari | Gharama za Awali pamoja na Ununuzi (Shilingi) | Gharama ya Ununuzi na Bima Pekee (Shilingi) | Tofauti | |
|----------------------------|-----------------|---|---|----------------|--------------|
| | | | | Kiasi | Asilimia (%) |
| Wizara ya Fedha na Mipango | 27 | 1,159,502,326.65 | 202,727,796.75 | 956,774,529.90 | 83 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti za Uthamini Mwaka 2022

Jedwali Na. 7.6 linaonesha kuwa kuna gharama ambazo hazikuwekwa katika kubainisha gharama za magari wakati wa uthamini wa magari 27 yaliyoondoshwa katika Wizara ya Fedha na Mipango. Hali hii ilipunguza thamani ya magari na kusababisha hasara ya Shilingi 956,774,529.90.

f) Idhini ya uondoshaji wa magari kwa njia ya mnada kuchukua muda mrefu

Ukaguzi ulifanya mapitio ya maombi 2,226 ya uondoshaji wa magari kutoka taasisi mbalimbali kwenda Wizara ya Fedha na Mipango kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2021/22 na kuchambua muda uliochukuliwa ili kuidhinishwa. **Jedwali Na. 7.7** linaonesha muda uliochukuliwa kutoa vibali vya kuidhinisha uondoshaji wa magari. Ukaguzi ulibaini kuwa utoaji wa vibali ulitofautiana kwa kiasi kikubwa kuanzia mwezi 0 - 72.

Jedwali Na. 7.7: Muda Uliotumika Kutoa Vibali vya Uondoshaji wa Magari ya Serikali

| Muda katika Miezi | Idadi ya Magari | Asilimia ya Magari (%) |
|-------------------|-----------------|------------------------|
| 37-72 | 1070 | 48 |
| 25-36 | 340 | 15 |
| 7-12 | 278 | 13 |
| 0-6 | 77 | 4 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Maombi na Kibali Kilichotolewa kuanzia mwaka 2016/16-2021/22

Jedwali Na. 7.7 linaonesha kuwa asilimia 48 ya vibali vya uondoshaji wa magari vilitoletwa kati ya miezi 37-72; asilimia 22 ya vibali vilitolewa baada ya miezi 13-24; asilimia 15 ya vibali vilitolewa kati ya miezi 25-36; asilimia

13 vilitolewa kati ya miezi 7-12; wakati asilimia 4 tu vilitolewa kati ya miezi 0-6.

Ukaguzi uligundua kuwa kuwapo kwa muda tofauti katika kufanya maamuzi ya uondoshaji wa magari kulitokana na kuchelewa kuwasilishwa kwa ripoti ya mchanganuo wa waombaji, mwingiliano wa shughuli kati ya ACGEN na GAMD. Pia, ukaguzi ulibaini kuwa urasimu uliokuwapo katika shughuli za uondoshaji wa magari ulisababisha mchakato wa uondoaji kuwa wa muda mrefu. Mara baada ya ripoti ya mchanganuo wa waombaji kuwasilishwa kwa ACGEN, ripoti hizo zilielekezwa kwa Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za Serikali ambaye alitakiwa kuipitia na kuikusanya ili kuomba idhini ya uondoshwaji wa magari kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mahojiano zaidi kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Wizara ya Fedha na Mipango yalibaini kuwa wizara hiyo ilikuwa katika mchakato wa kurekebisha sheria ambapo Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mali za Serikali atapewa mamlaka ya kuteua bodi ya uamuzi na kupitia ripoti zake na kuzikusanya. Hatua hii itafupisha mchakato wa kutoa taarifa za mchakato wa uondoshaji wa magari.

g) Ukopeshaji Usiofaa wa Magari kwa Wafanyakazi wa Umma

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Fedha, Shirika la Utangazaji Tanzania na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ziliunda kamati kwa ajili ya kutathmini maombi ya uondoshaji wa magari kwa watumishi wa umma. Ukaguzi ulibaini kuwa kamati hizo ziliunda vigezo na moja ya vigezo vilivyotumika kutathmini ni mtu wa kwanza kuomba ndiye atakayekuwa wa kwanza kuzingatiwa.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa uamuzi wa Mahakama ya Tanzania wa kuondosha magari hayo kwa watumishi wake katika ngazi ya taasisi ulizingatia tu uamuzi wa ofisa masuuli na si kwa kuzingatia uamuzi wa bodi ya ukaguzi. Hali hii ilitokana na kutoundwa kwa bodi ya ukaguzi ili kubaini magari ya kuondoshwa. Ukaguzi unahitimisha kuwa hakukuwa na vigezo vilivyoundwa ili kutathmini maombi ya mfanyakazi kabla ya kuondoshwa magari hayo kwa mkopo nafuu.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa afisa masuuli wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa aliidhinisha gari aina ya Toyota Land Cruiser GX V8 kwa mtumishi bila kushirikisha timu ya menejimenti ya halmashauri au baraza kamili.

Kutokana na hali hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa iligoma kukabidhi gari hilo kwa mtumishi huyo ingawa malipo yalikuwa yameshafanyika.

Ukaguzi ulibaini kuwa hali hiyo ilisababishwa na kukosekana kwa vigezo vya kuidhinisha maombi na ugawaji wa magari na kukosekana kwa sharti la lazima kwa maafisa masuuli kufuata kabla ya kufanya maamuzi kuhusu uondoshaji wa mali ya serikali.

Hivyo, kumekuwa na fursa isiyo sawa kwa watumishi kufaidika na uondoshwaji wa magari ya serikali kupitia njia ya mkopo au mauzo ya bei nafuu. Baadhi ya watumishi walipata magari zaidi ya moja ndani ya muda mfupi.

7.4.2 Matokeo kuhusu Usimamizi wa Uwekezaji wa Mali Zisizohamishika

Ukaguzi ulihusisha uwekezaji wa mali zisizohamishika unaosimamiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii. Mali hizo zisizohamishika zilikuwa majengo ya biashara, nyumba za kuishi, viwanja, na daraja chini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii. Wakati wa ukaguzi, miradi 69 ilihusika, ambapo kati ya miradi 37 ilitokelezwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na miradi 32 ilitokelezwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii. Yafuatayo ni matokeo ya msingi kuhusu usimamizi wa uwekezaji wa mali hizo kama inavyotekelezwa na mifuko ya hifadhi ya jamii.

a) Kuwapo kwa Majengo ya uwekezaji yenye hali isiyoridhisha

Kifungu cha 14 cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mali wa Mwaka 2019 kinamtaka kila afisa masuuli kuhakikisha kuwa mpango wa matengenezo ya mali unatayarishwa na kuzingatiwa. Madhumuni ya mpango wa matengenezo ni kuhakikisha kuwa mali inabaki kuwa muhimu kwa madhumuni yaliyokusudiwa, utoaji wa huduma, na kutumika kiuchumi ili kuongeza faida kwa shirika.

Ukaguzi ulibaini kuwapo kwa majengo chakavu na yaliyokuwa katika hali mbaya yanayomilikiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), dosari zilizobainika ni pamoja na nyufa kwenye sakafu na kuta, dari mbovu, fangasi ukutani na rangi za ukutani kung'olewa, paa kuvuja na kuvunjwa kwa

madirisha, madoa kwenye mbao za dari, vyoo na milango mibovu, kuharibika kwa milango.

Kwa upande wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), kasoro zilizobainika ni nyufa, kuchubuka kwa rangi kwenye kuta, kuvuja kwa paa, kupasuka na kuchakaa kwa sakafu, kutu kwenye mabati, mfumo mbovu wa majitaka, ubovu wa lifti na uchakavu wa nyaya za umeme. Ukaguzi pia ulibaini kulikuwa na majengo yenye hali chakavu ambayo yalitelezwa kama vile Mradi wa Nyumba za Makazi Dege na Mradi wa Nyumba Kijichi.

Hali mbaya ya majengo ilichangiwa na ufinyu wa bajeti na kutoendeshwa kwa shughuli za matengenezo hali iliyosababisha kutofanyika kwa matengenezo ya kutosha kwa majengo hayo.

Majengo yaliyochakaa yalisababisha idadi ndogo ya watu kukaa au kutokaliwa kwa majengo hayo hivyo kusababisha kushuka kwa kiwango cha mapato. Kwa mfano, kwa miradi iliyo chini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, kulikuwa na kushuka kwa viwango vya mapato hadi asilimia 81 kutoka asilimia 96 katika mwaka wa fedha 2017/18, na hadi asilimia 15 kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwa Jengo la Water Front, huku Julius Nyerere Pension Tower mapato yakishuka hadi asilimia 75 kutoka asilimia 95 mwaka wa fedha 2017/18; na hadi asilimia 20 kwa mwaka wa fedha 2021/22. Kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, kiwango cha cha mapato kilibainika kushuka kutoka asilimia 28 katika mwaka wa fedha 2017/18 hadi asilimia 21 katika mwaka wa fedha 2021/22.

b) Utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa mali zisizohamishika bila upembuzi yakinifu

Ukaguzi ulibaini kuwa, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma haikuwa na mipango madhubuti ya mali zilizowekezwa. Ukaguzi ulibaini kulikuwa na utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa majengo bila upembuzi yakinifu. Kwa miradi iliyotekelezwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko ulifanya upembuzi yakinifu kwa miradi miwili (2) kati ya 34 iliyowekezwa. Hii ina maana kuwa asilimia 94 ya mali zake za uwekezaji ziliwekezwa bila upembuzi yakinifu. Vilevile, miradi 9 kati 46 ya

miradi ya majengo iliyowekezwa katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii haikufanyiwa upembuzi yakinifu.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulitekeleza uwekezaji wa mali kabla ya upembuzi yakinifu au pendekezo la mradi kwa sababu haikuwa na sera na miongozo ya uwekezaji. Kwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii sababu ilikuwa kukosekana kwa taratibu za uwekezaji zilizoainishwa vizuri; na utekelezaji usiojitosheleza wa sera na mwongozo za uwekezaji.

Kutokuwapo kwa upembuzi yakinifu kulisababisha ugumu katika kutathmini utendaji wa miradi. Kwa mfano, mapato ya uwekezaji na kipindi cha malipo hakijawahi kutathminiwa na kukaguliwa kwa baadhi ya miradi ya mali isiyohamishika.

c) Baadhi ya uwekezaji wa mali zisizohamishika kutozalisha faida kwa mifuko

Ukaguzi ulibaini kuwa, baadhi ya uwekezaji wa mali za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) haukuwa na faida. Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulifanya uwekezaji wa mali usio na faida, ambapo kwa jumla ya shilingi 323,566,201. Sambamba na hilo, kulikuwa na miradi 10 ya uwekezaji wa majengo ambayo haikukamilika kwa matumizi na baadhi kutelekezwa.

Vilevile, kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), jumla ya shilingi 3,305,397,599 zilibainiwa kuwa uwekezaji usio na faida. Miradi hiyo ni pamoja na kiwanja cha biashara na makazi cha Ununio jijini Dar es Salaam, nyumba za makazi Njedengwa Jijini Dodoma. Sababu za kutofanikiwa kwa miradi hiyo ni mipango duni ya miradi na kushindwa kukamilika ndani ya muda uliopangwa hali iliyosababisha mabadiliko ya mwelekeo wa uwekezaji kutoleta mapato kwa mifuko.

Kadhalika, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na kiwango kidogo cha mapato kurudisha faida kwenye uwekezaji wa mali zisizohamishika. Ufanisi wa mapato kurudisha faida kwenye uwekezaji wa mali isiyohamishika kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulifikia asilimia 70.43 katika mwaka wa fedha 2019/2020 kisha hadi asilimia 21.90 katika mwaka wa fedha 2021/2022. Kushuka kwa mapato kulifikia asilimia 48.53 kwa miaka mitatu ya fedha iliyopita.

Mapato hayo yalishuka kwa kasi kutoka asilimia 70.43 mwaka 2019/20 hadi asilimia 17.76 mwaka wa fedha 2020/21 sawa na asilimia 52.67. Vilevile, kwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, mapato yatokanayo na uwekezaji wa majengo yalikuwa ya wastani wa asilimia 1.83 kwa miaka minne iliyopita ambayo ni chini ya asilimia 9 ya uwekezaji kwenye dhamana za Serikali, ambayo ina asilimia 10.83 kama faida ya wastani ya uwekezaji.

Sababu zingine za kushuka kwa mapato ni uchakavu wa majengo uliosababishwa na kutofanyika matengenezo ya kutosha; kiwango cha chini cha umiliki; utunzaji duni wa kumbukumbu kwa uwekezaji uliofanywa; na kutokuwa na ufatiliaji wa mradi ili kujua iwapo unarudisha gharama za uwekezaji na faida yake.

Sababu za mali za uwekezaji kuwa chakavu ni:

- (i) Ukusanyaji duni wa malipo ya huduma za makazi;
- (ii) Mipango duni ya kurejesha faida ya uwekezaji kwa mali iliyowekezwa;
- (iii) Utendaji duni wa ukarabati wa mali zilizowekezwa;
- (iv) Mfumo usiofaa wa ukusanyaji wa mapato kutoka kwa mali zilizowekezwa;
- (v) Mali za uwekezaji kutoleta mapato yaliyokusudiwa;
- (vi) Kushindwa kuhakikisha kuwa mali zilizowekezwa zinasimamiwa na wasimamizi huru; na
- (vii) Utekelezaji duni wa shughuli za ufatiliaji wa mali zilizowekezwa.


Sababu hizi zinafafanuliwa kwa kina hapa chini.

Ukusanyaji wa gharama za huduma kwenye Majengo yaliyowekezwa kuwa chini ya gharama za uendeshaji wa majengo husika

Mapitio ya Taarifa za Usimamizi wa Miliki kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22 yalionesha kuwa, makusanyo ya tozo za huduma za uendeshaji mali zilizowekezwa katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii yalikuwa hayatoshi kwani yalikuwa Shilingi.353, 386,033.36 wakati malipo ya huduma na malimbikizo yaliyokuwa hayajalipwa yalifikia Shilingi 357,169,633.63. Kwa upande mwingine, Ripoti za Usimamizi wa Miliki za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma za mwaka wa fedha 2021/22, zilionesha kuwa, gharama za uendeshaji wa majengo ya uwekezaji zilikuwa juu zaidi ikilinganishwa na tozo ya huduma iliyokusanywa. Gharama za huduma zilizokusanywa hazikutosha ikilinganishwa na gharama za

uendeshaji wa majengo kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 7.1** hapa chini.

Keilelezo Na. 7.1: Ukusanyaji wa Gharama za Huduma na Matumizi ya Uendeshaji wa Majengo Aprili - Juni 2022



Chanzo: Ripoti ya Robo ya Nne ya Usimamizi wa Mali ya Mwaka wa Fedha Uliomalizika Mwezi Juni 2021/22

Kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 7.1**, Jengo la Golden Jubilee lilitumia kiasi cha Shilingi milioni 226.97 kama gharama za uendeshaji huku makusanyo ya ada ya huduma yakiwa shilingi milioni 196.73. Jengo la Twin Tower la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma lilitumia kiasi cha Shilingi milioni 245.65 kama gharama za uendeshaji, huku makusanyo yatokanayo na ada ya huduma yakiwa Shilingi milioni 96.81. Ongezeko la gharama za uendeshaji wa majengo zilisababishwa na ukusanyaji usioridhisha wa ada za huduma na kupungua kwa idadi ya wapangaji katika majengo.

Ukusanyaji usioridhisha wa ada za huduma ya upangaji na uwekezaji wa majengo ulisababisha kutopatikana kwa baadhi ya huduma. Kwa mfano, ukaguzi ulibaini utoaji usioridhisha wa huduma na mwenendo wa

matengenezo ambayo ni pamoja na uchakavu wa lifti, jenereta, mfumo wa viyoyozi, na mifumo ya ulinzi wa moto.

Mipango isiyoridhisha ya kurejesha gharama za uwekezaji pamoja na upatikanaji wa faida

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma haukuwa na mipango madhubuti inayohakikisha faida ya kutosha ya uwekezaji kutoka mali zilizowekezwa. Isipokuwa Ripoti ya Utendaji ya Mwaka 2021/22, ripoti zingine hazikujumuisha uchanganuzi wa mapato kwenye uwekezaji. Ingawa Ripoti ya Utendaji ya Mwaka 2021/22 ilionesha kulikuwa na asilimia 3 ya faida kwenye uwekezaji wa majengo, ukaguzi ulibaini kuwa ripoti hiyo haikuwa na maelezo ya msingi kama vile kipindi ambacho kila mradi ungeweza kurejesha gharama za uwekezaji na haikuwa na maelezo ya kina juu ya asilimia ya mapato kutoka kwenye kila uwekezaji uliofanyika.

Ilibainika zaidi kuwa, tathmini ya kurejesha gharama za uwekezaji ilifanywa kwa uwekezaji mmoja tu. Mapitio ya taarifa mbili za upembuzi yakinifu mahsusi wa mwezi Machi 2020 kwa ajili ya Jengo la Twin Towers kwenye Kiwanja Na.120/121 katika Mtaa wa Sokoine na upembuzi yakinifu wa Jengo la PPF Tower wa mwezi Agosti 1997 yalibaini kuwa Ripoti ya Upembuzi Yakinifu ya PPF Tower pekee ndiyo ilikuwa na taarifa za msingi kuhusu muda wa kurejesha gharama za uwekezaji. Taarifa hiyo ilionesha kipindi cha kurejesha gharama za mradi ni miaka 8, kiwango cha kurejesha gharama za mradi cha asilimia 11.98, na kiwango cha marejesho ya kiuchumi cha asilimia 12.66.

Hivyo, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma haukuwa na kiwango bayana na takwimu za namna gharama za uwekezaji zitakavyorejeshwa katika uwekezaji wa mali isiyohamishika hasa kwa kila jengo. Athari za kutopanga kurejeshwa kwa gharama za uwekezaji wa mali zilizowekezwa ni kwamba, gharama inayopatikana wakati wa uwekezaji inaweza kuwa kubwa kuliko mapato yanayotarajiwa kwenye uwekezaji.

Vilevile, mapitio ya taarifa za utendaji wa uwekezaji wa mwaka za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa miaka ya fedha 2020/21, 2019/20 na 2018/19 yalionesha kuwa, mapato yatokanayo na uwekezaji wa majengo yalikuwa chini ya yale ya uwekezaji wa dhamana za Serikali kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.7.8.**

Jedwali Na 7.8: Mali Zisizohamishika dhidi ya Uwekezaji wa Dhamana za Kiserikali

| Mwaka wa Fedha | Jumla ya Uwekezaji kwenye Mali Zisizohamishika (Shilingi) | Mapato Yatokanayo na Mali Zisizohamishika (Shilingi) | Faida Itokanayo na Mali Isiyohamishika (%) | Asilimia ya Dhamana za Serikali | Asilimia ya Jumla ya Mapato kwa Mwaka |
|----------------|---|--|--|---------------------------------|---------------------------------------|
| 2021/22 | 783,850,538.00 | 3,119,092.88 | 1.59 | 10.87 | 5.93 |
| 2020/21 | 572,540,792.36 | 3,107,106.83 | 2.17 | 11.21 | 4.77 |
| 2019/20 | 582,532.73 | 10,872.88 | 1.87 | 10.40 | 3.32 |
| 2018/19 | 707,354.29 | 20,138.98 | 1.70 | 7.30 | 4.82 |
| Average | | | 1.83 | 10.83 | 4.71 |

Chanzo: Taarifa za Uwekezaji wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kuanzia Mwaka wa Fedha 2018/19 hadi 2021/22


Jedwali Na. 7.8 linaonesha mapato yatokanayo na uwekezaji wa majengo kwa wastani wa asilimia 1.83 kwa miaka minne iliyopita ya fedha ambayo ni asilimia 9 chini ya pato la asilimia 10.8 la uwekezaji wa dhamana za Serikali. Zaidi ya hayo, marejesho ya uwekezaji wa mali isiyohamishika yalifikia thamani ya chini kabisa ya asilimia 1.59 kwa mwaka wa fedha 2021/22 ikilinganishwa na asilimia 1.83. Pia, ilibainika kuwa mapato ya mali isiyohamishika hayakufikia kiwango kamili cha mapato cha angalau asilimia 2.5 kwa mwaka kwenye jalada la jumla la uwekezaji.

Mwenendo usioridhisha wa ukarabati wa Majengo yaliyowekezwa

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulikuwa na mipango duni ya ukarabati ambayo ilishughulikia baadhi ya majengo chini ya mamlaka yao, kama vile majengo ya biashara, makazi na ofisi, lakini si mali zote zilizojumuishwa kwenye mipango hiyo. Mfuko una mali zisizohamishika 49 katika uwekezaji, lakini mpango wao wa ukarabati kuanzia mwaka wa fedha 2020/21-2024/25 haukujumuisha mali zote. Ilibainika kuwa jumla ya mali zisizohamishika 35 kati ya 49 zilikuwa zikifanyiwa matengenezo.

Mapitio zaidi ya bajeti za mwaka zilizotumika kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2020/2021 yalibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulipanga bajeti ya ukarabati na uhuishaji wa majengo kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 7.2.**

Kielelezo Na 7.2: Bajeti Zilizowekwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya Ukarabati na Uhuishaji wa Majengo



Chanzo: Bajeti za Mwaka kuanzia Mwaka Fedha 2017/18-2021/22

Kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 7.2**, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2021/22, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulitenga kiasi cha Shilingi milioni 2,444, Shilingii milioni 3,670, na Shilingi milioni 1,520 mtawalia kwa ajili ya ukarabati wa majengo. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19 hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya matengenezo ya Majengo.

Aidha, kupitia mapitio ya Bajeti za Mwaka wa fedha 2019/2020-2021/22, Ukaguzi ulibaini kuwa bajeti iliyopangwa haitoshelezi kugharamia majengo yote yanayohitaji matengenezo. Kutokana na hali hiyo, majengo mengine yalichukua muda mrefu kukarabatiwa jambo ambalo lilisababisha kuchakaa na kuhitaji fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo yake. Kwa mfano, jengo la Water Front lilipangwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa bajeti ya Shilingi milioni 2,150 ambayo ilikuwa karibu asilimia 88 ya bajeti yote iliyowekwa kwa shughuli za matengenezo kwa mwaka huo.

Aidha ilibainika kuwa, licha ya kutenga bajeti ya shughuli za ukarabati, utekelezaji wake haukufanyika ipasavyo. Kwa mfano, wakati timu ya ukaguzi ilipotembelea Jengo la Water Front tarehe 5 Oktoba 2022, hakukuwa na ukarabati uliofanyika licha ya kuwa na bajeti ya Shilingi bilioni 2.15 katika mwaka wa fedha 2019/20.

Hali hii ilisababisha uchakavu zaidi wa mali hivyo kusababisha kuwa na kiwango cha chini cha thamani ya uwekezaji na kupungua kwa mapato.

Ukaguzi ulibaini pia kuwa, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii haukuwa na ripoti za utafiti wa hali ya majengo kabla ya utekelezaji wa ukarabati. Sababu zilizotolewa na maofisa wa Mfuko ni kwamba, shughuli hizo hazikupangiwa bajeti kutokana na mabadiliko ya kanuni katika mwelekeo wa uwekezaji. Hali hii ilisababisha uchakavu zaidi wa mali isiyohamishika ambapo majengo yalionekana kuwa katika hali mbaya.

Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma haukuwa na utaratibu wa kuhakikisha uendeshaji madhubuti wa miradi iliyowekezwa. Mapitio ya mpango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa miaka mitatu ya fedha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22 ulibaini kuwa, mipango hiyo haikujumuisha ukarabati wa mali zilizowekezwa. Vilevile, mapitio ya Mpango wa Uwekezaji wa Mwaka 2022 yalionesha kuwa mipango hiyo ilihusu miradi ya ujenzi inayoendelea na si shughuli za ukarabati wa mali zilizowekezwa.


Hali hii ilisababisha ukarabati hafifu wa majengo na kusababisha uchakavu zaidi. Pia, ilisababisha mrundikano wa kazi za ukarabati na kutokamilika kwa wakati kwa kazi za ukarabati zilizotekelezwa.

Mifumo usiojitosheleza wa ukusanyaji wa mapato kutoka kwa majengo yaliyowekezwa

Ukaguzi wa taarifa za wateja kwa kipindi cha kuanzia mwezi Machi 2019 hadi Juni 2021 ulibaini hali isiyoridhisha ya ufuatiliaji wa wapangaji walioshindwa kulipa kodi ya pango. Ripoti hiyo ilionesha kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ulitoa ankara zenye thamani ya kiasi cha Shilingi 82,343,154,285.31. Kati ya ankara hizo, fedha zilizokusanywa ni Shilingi 19,146,902,626.1 (asilimia 23) na ambazo hazikuweza kukusanywa ni Shilingi 63,404,228,799.69 sawa na asilimia 77.

Hali hii ilibainishwa pia katika Ripoti za Wasimamizi wa Miliki kuanzia Mwaka wa Fedha 2017/18 hadi 2021/22 ambazo zilionesha kuwapo kwa madai ya malipo ya kodi yanayoashiria kutofuatilia vizuri kodi kwa wapangaji walioshindwa kulipa. Ripoti zilionesha kodi ambayo haikulipwa ilikuwa kati ya Shilingi bilioni 14 kwa mwaka wa fedha 2017/18 na Shilingi bilioni 36 kwa mwaka 2018/19 kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 7.3**.

Kielelezo Na. 7.3: Kiwango cha Kodi Inayodaiwa Kwa Miaka Mitano Iliyopita ya Fedha 2021/22



Chanzo: Ripoti ya Wasimamizi Miliki 2017/18-2021/22 na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Taarifa za Miaka ya Fedha 2017/18-2021/22

Kielelezo Na. 7.3 kinaonesha kuwapo kwa kodi isiyolipwa ambayo ilikuwa inabadilikabadilika. Kwa mfano, kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2018/19 kiasi cha kodi kiliongezeka kutoka Shilingi bilioni 31.843 hadi Shilingi bilioni 36.272; kisha ilipungua hadi Shilingi bilioni 31.836 katika mwaka wa fedha 2019/20 na hadi Shilingi bilioni 14.067 mwaka wa fedha 2020/21; lakini iliongezeka tena hadi Shilingi bilioni 23.004 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Zaidi ya hayo, ukaguzi ulipitia kumbukumbu za malipo ya wapangaji na kubaini deni la pango la muda mrefu. Kwa mfano, katika Mafao House Mkoani Arusha ni wapangaji 10 tu kati ya 51 ndio walilipa kodi kwa wakati kulingana na mikataba ya upangaji wakati Kaloleni Plaza, ni wapangaji watatu tu kati ya 19 ndio walilipa kodi kwa wakati kulingana na mikataba yao ya upangaji.

Vilevile, katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, ukaguzi ulibaini tofauti katika ankara iliyotolewa ikilinganishwa na fedha taslimu iliyopokelewa. Ukaguzi ulibaini kuwa upungufu ulikuwa kati ya asilimia 56 hadi asilimia 93 ambayo uliotokana na kutolinganishwa kwa ankara iliyotolewa kwa wapangaji na deni walilodaiwa kutokana na utaratibu wao wa kulipa malipo ya kodi ya pango.

Ukaguzi ulibaini mapungufu katika udhibiti wa ndani wa ukusanyaji wa mapato ya mali zilizowekezwa katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii ambao ni pamoja na kutowekwa sawa kati ya akaunti ya malipo ya huduma za jengo,

kutopitia kwa wakati mikataba na utiaji saini wa mikataba ya wapangaji, ufuatiliaji usioridhisha wa waliokiuka taratibu za upangaji na ufuatiliaji usioridhisha wa mikataba kabla ya kumalizika muda wake.


Mifumo isiyoridhisha ya ukusanyaji wa mapato ilisababisha ukusanyaji wa mapato wa muda mrefu na wenye madeni ambayo hayajalipwa. Kwa mfano, mapatio ya ankara zilizotolewa na ukusanyaji halisi wa kodi kutokana na uendeshaji wa mali ya uwekezaji katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma yalibaini kuwa, kodi ambazo hazijalipwa ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 27.4 mwaka 2018/19 hadi Shilingi bilioni 36.3 mwaka 2020/21.

Mali zilizowekezwa bila kuzalisha mapato yaliyokusudiwa

Kifungu cha 9(1) cha Mwongozo wa Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wa Mwaka 2015 kinaitaka bodi ya wadhamini ya kila mfuko kuhakikisha uwekezaji wowote tofauti na ule wa hazina uwe na marejesho ambayo ni zaidi ya ule wa hazina na dhamana za hazina wakati wa kuwekeza kulingana na ukubwa wa uwekezaji huo.

Ukaguzi ulichambua katika mwaka wa fedha wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2020/21 na ulibaini kuwa uwekezaji wa majengo ulikuwa na wastani wa faida ya chini katika uwekezaji kwa asilimia 2.66 ikilinganishwa na asilimia 2.67 ya uwekezaji katika hisa na asilimia 9.28 ya Soko la Fedha kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 7.4.**

Kielelezo Na. 7.4: Wastani wa Marejesho wa Mapato kwenye Uwekezaji wa Kipindi cha kuanzia Mwaka 2018/19 hadi 2020/21



Chanzo: Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali Mwaka 2022

Kielelezo Na. 7.4 hapo juu kinaonesha kuwa uwekezaji wa mali zisizohamishika ulikuwa na asilimia 3 kwenye marejesho ya uwekezaji ikilinganishwa na kile kinachopatikana katika soko la fedha.

Mapato yaliyokusanywa chini ya kitengo cha uwekezaji wa mali yalionesha ongezeko. Ukaguzi ulibaini kuwa, kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21, mapato yaliyokusanywa yaliongezeka kutoka Shilingi bilioni 28 hadi Shilingi bilioni 33.

Kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, ukaguzi ulibaini kuwa, miradi ya Kinyerezi na Kijichi haikuwa na mapato yaliyokusanywa kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2020/21. Kadhalika, mradi wa mauzo ya nyumba na viwanja ulikuwa na makusanyo yasiyoridhisha kwani yaliuingizia Mfuko hasara.

Utendaji hafifu wa makusanyo ya mapato ulisababishwa zaidi na udhibiti duni wa ndani wa ukusanyaji wa mapato na ufuatiliaji duni wa mikataba ya upangaji kwa vile haikuhuishwa kwa wakati na ufuatiliaji duni wa mali zilizowekezwa.

Kutozingatia mwongozo unaotaka mali zilizowekezwa kusimamiwa na meneja miliki huru anayejitegemea



Kifungu cha 13 cha Miongozo ya Uwekezaji ya Mifumo ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2015 inaitaka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha kuwa mali zote za uwekezaji zinasimamiwa na wasimamizi huru wa mali, na ujenzi wa majengo unafanywa na watu wengine huru waliosajiliwa na mamlaka husika.

Mapitio ya mafaili ya Wasimamizi wa Miliki na Orodha ya Uwekezaji wa Mali ya Mwaka 2021/22 kutoka Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii yalibaini kuwa, majengo 8 kati ya 46 yaliyowekezwa sawa na asilimia 17 hayakusimamiwa na meneja miliki huru. Hali hii ilibainika kusababishwa na uzembe wa Mfuko kutozingatia matakwa yaliyotolewa licha ya kuwa na taarifa za kutosha juu yake. Kutokuwapo kwa wasimamizi huru wa miliki kwenye majengo hayo yaliyowekezwa kunamaanisha kuwa, Mfuko haikupata taarifa juu ya hali ya majengo kwa sababu mameneja miliki huru wana jukumu la kuwasilisha ripoti za maendeleo kwa Mfuko kila robo mwaka.

Kwa upande wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, ukaguzi ulibaini kuwa, majengo 22 kati ya 48 yaliyowekezwa sawa na 54% hayakusimamiwa na wasimamizi huru. Hali hii ilibainika kusababishwa na

idadi ndogo ya wasimamizi wa mali. Mapitio ya orodha ya wasimamizi wa uwekezaji wa mali yalionesha kuwa, kulikuwa na wasimamizi 5 kati ya 48 wanaohitajika.

Idadi duni ya wasimamizi wa mali zilizowekezwa ilisababisha usimamizi duni wa majengo. Pia, kutokuwapo kwa wasimamizi wa miliki kulimaanisha hali na huduma za mali zilizowekezwa haikuboreshwa. Vilevile, ukaguzi ulibaini kuwa majengo ambayo hayakuwa na wasimamizi yalikuwa duni kwa sababu mifuko haikupata taarifa za maendeleo ya kila robo mwaka kutoka kwa wasimamizi hao.

Utekelezaji duni katika ufuatiliaji wa mali zilizowekezwa

Kifungu cha 5 (2) (i), Sehemu ya II ya Miongozo ya Uwekezaji ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2015 inazitaka bodi za mifuko ya hifadhi ya jamii kuhakikisha kuwa sera za uwekezaji zinajumuisha taratibu za ufuatiliaji na tathmini ya uwekezaji.

Ukaguzi umebaini kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu haikutekeleza ipasavyo mpango-kazi wa ufuatiliaji wa shughuli za uwekezaji zinazofanywa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii. Imebainika kuwa, kwa mwaka wa fedha 2019/20, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu iliweza kufanya ukaguzi na uchunguzi kwa Mifuko yote miwili ya hifadhi ya jamii. Kwa mwaka wa fedha 2020/21 ukaguzi na uchunguzi ulifanyika kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma peke yake.

Kwa mwaka wa fedha 2021/22 hakukuwa na ukaguzi wala uchunguzi uliofanyika. Kadhalika, ukaguzi umebaini kuwa uhakiki ulifanyika mara moja tu kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2021/22. Zaidi ya hapo, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu haikuweza kutekeleza shughuli za ufuatiliaji kama inavyopaswa kwa kipindi kilichokaguliwa kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 mpaka 2021/22

Sababu iliyotolewa ya kutofanya shughuli za ufuatiliaji ipasavyo ni kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu ilianza jukumu la shughuli za ufuatiliaji kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii katika mwaka

wa fedha 2019/20 baada ya mabadiliko ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii namba 6 ya mwaka 2019. Mabadiliko ya Sheria hii yaliamishia majukumu ya iliyokuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Jamii kwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu. Kadhalika, divisheni ya Hifadhi ya Jamii ya Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu iliundwa rasmi mwezi Septemba 2019 na kuanza kutekeleza majikumu ya ufuatiliaji mwaka huo.

Mapitio ya taarifa za utekelezaji kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22, yamebaini kuwa, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu haikufuatilia mapendekezo yaliyotolewa kwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii wakati wa ukaguzi ili kuhakikisha kuwa Mfuko unatekeleza ipasavyo mapendekezo yaliyotolewa. Kukosa kufuatilia mapendekezo yaliyotolewa kunamaanisha kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu haina uhakika kama uboreshaji wa mapungufu yaliobainika ulifanyiwa kazi kama inavyohitajika.

Utekelezaji duni wa ufuatiliaji uliopangwa unaweza kusababisha kutofuatwa kwa miongozo, sera na kanuni za uwekezaji hali inayoweza kusababisha Mfuko kuwekeza katika miradi isiyo na faida kama vile Mradi wa Kijiji cha Dege ECO na nyumba za gharama nafuu za Kijichi chini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na mradi wa nyumba za gharama nafuu.

7.5 Athari za kutofikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Athari za kutofikiwa kwa Malengo ya Maendeleo Endelevu

Mapungufu katika usimamizi wa uwekezaji wa mali kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii yamechangia kutofikiwa kwa lengo la kwanza, lengo dogo la 1.3 katika Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo linahitaji kutekeleza mifumo na hatua zinazofaa za kitaifa katika hifadhi za kijamii kwa wote, ikiwa ni sehemu muhimu ya mpango wa kufikia Ajenda ya Mwaka 2030 katika kutokomeza umaskini na watu wanaoishi katika mazingira magumu.

Vilevile, usimamizi usio na tija wa uwekezaji wa mali hautachangia kufikiwa kwa lengo namba 1, lengo dogo namba 5.4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalotambua na kuthamini huduma zinazotolewa na umma bila malipo na utoaji wa huduma za umma katika familia, miundombinu, sera za

usalama wa jamii, na kukuza uwajibikaji wa pamoja ndani ya kaya na familia kama inavyofaa kitaifa.

Athari za kutofikiwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Ukaguzi wa usimamizi wa mali na uwekezaji wa mali za Serikali ulikusudiwa kuboresha utendaji wa mali na maeneo ya uwekezaji ya Serikali yanayoendana moja kwa moja na mkakati namba 5.5.4. wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Hivyo, dosari katika usimamizi wa mali na maeneo ya uwekezaji ya Serikali unakwamisha juhudi za nchi kufikia malengo maalumu ya mkakati wa 5.5.4 wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao unatambua mifuko ya hifadhi ya jamii kihistoria imekuwa wawekezaji wa kutegemewa katika maeneo mbalimbali, kwa kutumia fedha za ndani zitokanazo na makusanyo ya michango ya wanachama.

Mapungufu katika usimamizi wa mali za uwekezaji katika mifuko unasababisha kupungua kwa fursa zingine ambazo mifuko ingepata katika uwekezaji wake, kwa mfano katika viwanda vilivyopo na vipya kwa njia ya mikopo iliyunganishwa dhamana kutoka taasisi zingine.

7.6 Hitimisho la Ukaguzi

Ukaguzi unatambua juhudi zilizofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma katika kuboresha usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali na uwekezaji wa rasilimali za serikali. Hata hivyo, hatua zaidi zinahitajika ili kuhakikisha usimamizi madhubuti wa uondoshwaji wa magari ya Serikali na uwekezaji wa rasilimali za serikali unafanyika ipasavyo.

Kwa kuzingatia matokeo kama yalivyojadiliwa kuhusiana na malengo ya kaguzi hizi mbili za ufanisi, inahitimishwa kama kwamba Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na hazijasimamia ipasavyo uondoshwaji wa Magari ya Serikali. Pamoja na kutambua juhudi zinazofanywa na serikali kama vile kutengeneza Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali, utoaji wa umiliki wa mali unaotokana na Waraka wa Miradi ya Serikali Na. 7 na Mwongozo wa

Usimamizi wa Mali, ukaguzi huu unahitimisha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora hazijasimamia ipasavyo uondoshaji wa magari ya Serikali.

Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa hatua zaidi bado zinahitajika ili kuboresha zaidi usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali nchini kwa sababu utambuzi wa magari yaliyoondoshwa kwa njia ya mnada kwa watumishi wa umma haukufanywa vizuri. Vilevile, utoaji wa idhini ya magari ya Serikali kuondoshwa haujafanyika kwa wakati. Uamuzi wa kuondosha magari ya Serikali kwa njia ya minada huchukua muda mrefu bila sababu za msingi; hauna ufanisi wala uwazi; na haufanywi mara kwa mara. Hivyo, magari ya Serikali yanachukua muda mrefu yakiwa yamehifadhiwa pasipo kuondoshwa, jambo linalosababisha kushuka kwa thamani ya magari hayo.

Aidha, matokeo ya ukaguzi wa usimamizi wa uwekezaji wa mali zisizohamishika yanasababisha hitimisho kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa taifa wa Hifadhi ya Jamii haijasimamia ipasavyo shughuli za uwekezaji wa mali zisizohamishika ili kuhakikisha malengo ya Mifuko yanafikiwa ambayo ni kuongeza mapato ya uwekezaji unaofanyika kwa lengo la kukua kiuchumi na kijamii.

Dosari hizo zimesababishwa zaidi na mpango usioridhisha wa uwekezaji wa mali zisizohamishika; utunzaji duni wa mali za uwekezaji; kushindwa kuendesha ipasavyo mali za uwekezaji; na ufuatiliaji wa mali za uwekezaji usio na tija.

MIPANGO MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI YA WATU

SURA YA NANE

8



MIPANGO MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI YA WATU

8.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo na hitimisho linalotokana na taarifa ya ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa urasimishaji wa makazi holela. Sura hii pia inaelezea uhusiano uliopo kati ya eneo hili la ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mipango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ikijikita katika mpango wa pili na wa tatu.

8.2 Usuli kuhusu Urasimishaji wa Makazi Holela

Urasimishaji wa makazi holela ni mchakato ambao mamlaka za upangaji hubainisha viwanja ambavyo havijapangwa katika maeneo ya mijini na kupitia mchakato wa urasimishaji wa viwanja hivi. Mchakato pia unahusisha kupanga, kupima, na kupewa hatimiliki kwa wamiliki wa viwanja vilivyorasimishwa. Kupitia urasimishaji, maeneo yasiyopangwa huboreshwa na kuyafanya yafikike kwa ajili ya huduma za msingi kama vile barabara, maji na umeme kwa jamii zinazohusika.¹⁵ Utaratibu wa urasimishaji umetolewa katika Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 na katika Sheria ya Mipango-miji ya Mwaka 2007. Jambo la muhimu zaidi ni kwamba haki za umiliki wa ardhi katika makazi holela huimarishwa kwa njia ya hatimiliki.

Makazi yasiyopangwa nchini yanachukua zaidi ya asilimia 70 ya makazi ya mijini. Hali hii inaonesha kuwa watu wengi wanaishi katika makazi yasiyo rasmi na hawana utambuzi wa kisheria wa ardhi/mali zao. Kutokana na hali hiyo, Serikali imefanya jitihada mbalimbali za kushughulika na ongezeko la makazi yasiyo rasmi. Moja ya jitihada hizo ni urasimishaji wa makazi holela, ambayo hushughulikia kuongeza usalama wa umiliki kwa wakazi wa maeneo husika.

¹⁵Magina, F.B., Kyessi, A.G., & Kombe, J.W. (2020). Nexus ya Ardhi ya Mijini - Changamoto na Fursa za Kudhibiti Makazi Yasiyo Rasmi: Uchunguzi wa Kesi za Dar es Salaam na Mwanza nchini Tanzania. Jarida la Utafiti wa Mali Isiyohamishika ya Kiafrika, 5(1), uk.32-54

8.3 Uhusiano kati ya Mipango miji na Maendeleo ya Makazi, na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Uhusiano kati ya mipango miji na maendeleo ya makazi, na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Tanzania ikiwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa inawajibika kufuata Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo la 11, lengo dogo 11.3 linalenga kuhakikisha kuwa miji na makazi ya binadamu yanakuwa jumuisi ifikapo mwaka 2030. Shabaha hii itafikiwa endapo tu kutakuwa na miji jumuisi na mipango endelevu ya makazi ya binadamu katika nchi zote.

Hivyo, usimamizi makini wa urasimishaji wa makazi yasiyopangwa utaimarisha mipango ya Serikali kuelekea kufikia shabaha Na. 11.3 ya lengo Na. 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Uhusiano kati ya Mipango-miji na Maendeleo ya Makazi, na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa Pili uliweka lengo la kupunguza makazi holela kutoka asilimia 66 mwaka 2015/16 hadi asilimia 50 mwaka 2021. Vilevile, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unatambua kuwa ardhi yenye makazi holela kwa mwaka 2019/20 ilikuwa asilimia 70 na makazi rasmi yalikuwa 1,496,357. Mpango huu umelenga kurasimisha makazi holela hadi kufikia makazi 2,496,357 ifikapo mwaka 2025/26. Kazi hii ilipangwa kufanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama wizara ekelezi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Hivyo, ukaguzi huu ulilenga kuangalia kiwango ambacho Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinatekeleza shughuli za urasimishaji wa makazi holela nchini ili kufikia Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

8.3.1 Mikakati na juhudi za Serikali katika mipango-miji na maendeleo ya makazi

Kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, mikakati iliyowekwa kwa ajili ya kuboresha mipango-miji na maendeleo ya makazi mahususi kwa ajili ya urasimishaji wa makazi holela ni pamoja na:

- Kufanya kampeni za uhamasishaji wa urasimishaji katika ngazi zote za mamlaka ya serikali za mitaa;
- Kutambua na kuweka alama viwanja 1,200,000 katika makazi holela; na
- Kuandaa mipango ya urasimishaji wa makazi yote holela.

Jitihada zilizofanywa na Serikali katika udhibiti wa makazi holela ni pamoja na kuanzishwa kwa kurugenzi saidizi yenye dhamana ya kushughulikia urasimishaji wa makazi holela; uandaaji wa miongozo ya urasimishaji; na utambuzi wa viwanja 2,348,324 kwa ajili ya urasimishaji katika mikoa 24 nchini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022.

8.4 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

8.4.1 Malengo ya Ukaguzi



Lengo la ukaguzi huu lilikuwa kuangalia namna ambavyo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilisimamia kwa ufanisi urasimishaji wa makazi holela ili kuhakikisha kuwa makazi hayo yanaboreshwa. Ili kutekeleza lengo la ukaguzi, malengo mahususi manne yafuatayo yalitumika. Malengo hayo yalikuwa kutathmini iwapo:

- a) Halmashauri zinapanga bajeti ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji;
- b) Halmashauri zinahakikisha utekelezaji mzuri wa utambuzi, upangaji, upimaji na utoaji wa hatimiliki katika urasimishaji wa makazi holela;
- c) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinaratibu ipasavyo shughuli za upangaji na upimaji zinazotekelezwa na halmashauri, kampuni binafsi, ofisi za ardhi za mikoa, na wadau wengine; na

-
- d) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinafuatilia na kutathmini kwa ufanisi shughuli za upangaji na upimaji wa makazi.

8.4.2 Mawanda ya Ukaguzi

Taasisi kuu zilizokaguliwa zilikuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilichaguliwa kwa kuwa inahusika na ugawaji wa ardhi, uandaaji wa nyaraka zinazohusiana na haki za umiliki, utatuzi wa migogoro ya ardhi, kusimamia masuala yote yanayohusu usimamizi wa ardhi, na kutoa utaalumu na huduma katika utoaji wa chati za upimaji, mipango na ramani. Kwa upande mwingine, OR-TAMISEMI, kupitia halmashauri husika, ina jukumu la kuidhinisha michoro ya urasimishaji wa ardhi iliyoandaliwa na kampuni binafsi na kuiwasilisha katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kuidhinishwa na kusimamia utekelezaji wa urasimishaji wa viwanja kama mamlaka ya upangaji.

Ukaguzi huu ulijikita zaidi katika upangaji, utekelezaji, ufuatiliaji na uratibu wa shughuli za urasimishaji wa makazi zinazotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia halmashauri katika kupanga, kupima na kutoa hatimiliki ya viwanja. Kwa upekee, ukaguzi ulitathmini hatua zilizopo katika uandaaji wa mipango kwa kuzingatia rasilimali-watu na fedha, utambuzi wa maeneo kwa ajili ya urasimishaji, mipango ya uhamasishaji, na ununuzi wa kampuni binafsi zitakazohusika katika shughuli za urasimishaji.

Ukaguzi huu ulihusisha kipindi cha miaka mitano ya fedha kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2021/22. Kipindi hicho kilichaguliwa kwa sababu ndicho kipindi serikali ilishirikisha kampuni binafsi kufanya urasimishaji wa viwanja ambapo miradi mbalimbali ilitekelezwa nchini.

Ukaguzi huo uligusa nchi nzima lakini taarifa zilikusanywa katika mikoa mitano ambayo ilichaguliwa kwa kuzingatia uwakilishi wa kijiografia na idadi ya viwanja vilivyotambuliwa kwa ajili ya urasimishaji.

8.5 Matokeo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi juu ya usimamizi wa urasimishaji wa makazi yasiyopangwa nchini. Matokeo hayo yanajikita katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa ujumla, katika kipindi cha miaka minane kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2021/22, ukaguzi ulibaini kasi ndogo ya kupunguza ukubwa wa makazi holela.

Kwa mujibu wa takwimu za tarehe 30 Juni 2022, ukaguzi ulibaini kuwa, kuanzia mwaka 2013/14 wakati shughuli za urasimishaji zilipoanza kulikuwa na viwanja 2,348,324 vilivyotambuliwa, kati ya hivyo, viwanja 171,210 vilikamilisha mchakato wa urasimishaji na wamiliki kupewa hatimiliki, sawa na asilimia 7 ya viwanja vilivyotambuliwa. Hii inamaanisha kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilifanikiwa kupunguza wingi wa makazi holela kwa asilimia saba ya maeneo holela yaliyotambuliwa kwa kipindi cha miaka minane.

Pia, ukaguzi huu ulibaini kuwa, kwa miaka minane iliyopita (2013/14 hadi 2021/22), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hakukuwa na mkoa wowote ulioweza kufanya shughuli za urasimishaji kwa zaidi ya asilimia 10 ya viwanja vilivyotambuliwa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8.1**.

Jedwali Na. 8.1: Hali ya Urasimishaji wa Makazi kuanzia Mwaka 2013/14 hadi 2021/22

| Mkoa | Idadi ya Viwanja Vilivyotambuliwa kwa Urasimishaji (n) | Idadi ya Viwanja ambavyo Hati Zimetolewa (n) | % ya Viwanja Vilivyorasimishwa na Hati Kutolewa |
|---------------|--|--|---|
| Songwe | 19,227 | 1,298 | 7 |
| Kigoma | 39,379 | 2,864 | 7 |
| Dar es Salaam | 604,571 | 22,104 | 4 |
| Mbeya | 149,839 | 5,763 | 4 |
| Dodoma | 390,360 | 8,144 | 2 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Mpango-mkakati wa Urasimishaji wa Mwaka 2015 na Takwimu za Urasimishaji hadi kufikia Tarehe 30 Juni 2022

Jedwali Na. 8.1 linaonesha kuwa Songwe na Kigoma ndiyo mikoa pekee iliyokuwa na utendaji wa hali ya juu wa asilimia ya viwanja

vilivyotambuliwa, kukamilika na kutolewa hatimiliki. Mikoa mingine kama vile Dar es Salaam na Mbeya ilikuwa na 4% tu ya viwanja vilivyotambuliwa ambavyo vilitolewa hatimiliki ilhali Mkoa wa Dodoma ulikuwa na 2% tu ya viwanja vilivyotambuliwa na kutolewa hatimiliki. Kasi ndogo ya urasimishaji wa makazi holela ilisababishwa na mambo yalivyoelezwa hapo chini.

8.5.1 Wizara, ofisi za ardhi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kutounganisha ipasavyo shughuli za urasimishaji katika mipango yao ya kimkakati na mipango yao ya mwaka

Mapitio ya mipango-mkakati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yalibaini kuwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika bajeti yake ya jumla kwa ajili ya kupata maeneo ya kupanga, kupima, na kumilikisha iliidhinisha kiwango cha juu cha asilimia mbili ya kiasi cha bajeti kwa ajili ya urasimishaji wa makazi holela. Kiwango cha juu kilichotengwa kilibainika katika mwaka wa fedha 2020/21 ambazo ni shilingi milioni 80. Aidha, kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2018/19, hakuna bajeti iliyotengwa kwa ajili ya shughuli za urasimishaji. Mchanganuo wa bajeti iliyotengwa kwa kipindi cha miaka mitano ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 8.2:

Jedwali Na. 8.2: Mchanganuo wa Bajeti kwa ajili Urasimishaji katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

| Mwaka wa Fedha | Bajeti kwa ajili ya Kupata Maeneo ya Kupanga, Kupima, na Kumilikisha (Shilingi milioni) ¹⁶ | Bajeti Iliyotengwa kwa ajili ya Urasimishaji (Shilingi Milioni) | % ya Kiasi Kilichotengwa kwa Ajili ya Urasimishaji (Shilingi Bilioni) |
|----------------|---|---|---|
| 2017/18 | 0 | 0 | 0 |
| 2018/19 | 0 | 0 | 0 |
| 2019/20 | 4,240 | 70 | 2 |
| 2020/21 | 10,030 | 80 | 1 |
| 2021/22 | 28,380 | 10 | 1 |

Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa Zilizotolewa katika Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mipango ya kuanzia Mwaka 2017/18 hadi 2021/22

¹⁶Hali hii inajumuisha Idara ya Maendeleo ya Makazi ya Binadamu (Mipango), Idara ya Utafiti na Ramani, na Utawala wa Ardhi (Titling).

Kwa upande mwingine, mapitio ya mpango-mkakati wa OR-TAMISEMI wa kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 - 2020/21 na 2021/22 - 2025/26 ulionyesha kuwa, OR-TAMISEMI haikutenga fedha katika bajeti yake ya kuwezesha shughuli za urasimishaji katika mamlaka za serikali za mitaa kwa miaka mitano iliyopita (2017/18 hadi 2021/22). Aidha, mapitio ya mpango wa matumizi wa nusu muhula kwa kipindi cha kuazia mwaka 2015/16 hadi 2017/18 na mwaka 2018/19 hadi 2020/21 yalionyesha OR-TAMISEMI haikutenga fedha kwa ajili ya shughuli za urasimishaji wa ardhi.

Ukaguzi ulibaini kuwa kutoingizwa kwa shughuli za urasimishaji katika mipango-mkakati na mipango ya mwaka kulitokana na kutoweka kipaumbele kwenye shughuli za urasimishaji. Hali hii inathibitishwa na ukosefu wa bajeti maalumu kwa ajili ya shughuli za utambuzi, upangaji, upimaji na utoaji wa hatimiliki zinazotokana na urasimishaji.

Kutokana na hali hiyo, serikali haiwezi kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ifikapo mwaka 2025/26 na lengo la 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusu maendeleo ya makazi ya binadamu. Matokeo yake, makazi hayo hayatapangwa hivyo kufanya iwe vigumu kujenga barabara za kuwafikia wananchi wote kwani kila mmoja ataendelea kujenga makazi mapya kiholela.

8.5.2 Upungufu wa rasilimali-watu katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ofisi za ardhi za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya urasimishaji

Kupitia taarifa ya maendeleo ya mwaka, ukaguzi huu ulibaini kuwa, hadi tarehe 30 Juni 2021, makao makuu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na ofisi za mikoa zilikuwa na watumishi 2,139 wakati idadi iliyokuwa inatakiwa ni watumishi 5,234 hivyo kuwa na upungufu wa watumishi 2,895¹⁷. Ukaguzi ulifanya uchambuzi zaidi wa watumishi katika taaluma tatu muhimu kwenye urasimishaji katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri, ambazo ni wapangamiji, wapimaardhi na maofisa ardhi. Uchambuzi wa mchanganuo wa watumishi katika mamlaka ya serikali za mitaa na ofisi za ardhi za mikoa nchi nzima umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 8.3.**

¹⁷Ripoti ya Maendeleo ya Mwaka ya MLHSD kwa Mwaka 2020/21

Jedwali Na. 8.3: Upungufu wa Watumishi wa Kufanya Shughuli za Urasimishaji katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa


| Kada | Watumishi Wanaohitajika (a) | Watumishi Waliopo (b) | Mahitaji ya Watumishi (c)=a-b | Asilimia ya Mapungufu ya Watumishi (%) (c/a)*100 |
|---------------|-----------------------------|-----------------------|-------------------------------|--|
| Wapangamiji | 786 | 175 | 611 | 77.7 |
| Wapimaardhi | 1,018 | 145 | 873 | 85.8 |
| Maofisa Ardhi | 1,206 | 605 | 601 | 49.8 |
| Jumla | 3,010 | 925 | 2085 | |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu za Rasilimali-watu kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mwaka 2022

Jedwali Na. 8. 3 linaonesha utofauti katika uhitaji wa watumishi ambao ulianza asilimia 49.8 hadi asilimia 85.8. Hali hii inaonesha kuwa, kulikuwa na upungufu mkubwa wa wapangamiji na wapimaardhi kwa asilimia 77.7 na asilimia 85.8 mtawalia. Upungufu mdogo ulikuwa kwa mahitaji ya maofisa ardhi ambao ulikuwa asilimia kwa 49.8.

Kwa upande mwingine, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa watumishi katika ofisi za ardhi za mikoa zilizotembelewa kwa kada ya sekta ya ardhi. **Kielelezo Na. 8.1** kinaonesha watumishi wanaotakiwa na upungufu uliopo.

Kielelezo Na. 8.1: Idadi ya Watumishi katika Ofisi za Ardhi za Mikoa Zilizotembelewa



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Uanzishaji wa Watumishi Mwaka 2022

Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha kuwa kulikuwa na pengo kubwa la watumishi katika ofisi za ardhi za mikoa katika mikoa iliyotembelewa. Uchambuzi wa kina ulionesha kuwa kada iliyokuwa na mapungufu makubwa ya watumishi ni wasanifu ramani ambapo upungufu katika Mkoa wa Dodoma ulikuwa asilimia 80, Mbeya asilimia 94, Kigoma asilimia 96, na Songwe asilimia 100. Kada zilizokuwa na upungufu mdogo zilikuwa mipango-miji ambao ulikuwa kati ya asilimia 61 na 81; wasanifu-ramani ulikuwa kati ya asilimia 33 na 72, na maafisa ardhi ulikuwa kati ya asilimia 24 na 80.

Hata hivyo, katika Mkoa wa Dar es Salaam hali ilikuwa tofauti ambapo taaluma za mipango-miji, wasanifu-ramani, na maafisa ardhi walizidi kiwango cha watumishi wanaotakiwa kwa asilimia 14, asilimia 67 na asilimia 94 mtawalia. Kwa upande mwingine, kwa kada ya wapima-ardhi kulikuwa na upungufu wa asilimia 53.

Kutokana na upungufu huu wa watumishi wanaohusika na urasimishaji wa ardhi, kukamilika kwa shughuli za urasimishaji kuliathirika.

8.5.3 Upimaji usioridhisha wa makazi yaliyopangwa

Shughuli za urasimishaji hupitia hatua nne, ambapo hatua ya kwanza ni utambuzi wa viwanja, hatua ya pili ni upangaji wa viwanja vilivyotambuliwa, hatua ya tatu ni kupima viwanja vilivyopangwa, na mwisho ni utoaji wa tatimiliki ya viwanja vilivyopimwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa, idadi ya viwanja vya ardhi vilivyotambuliwa kwa ajili ya urasimishaji havikupimwa. Mapitio ya takwimu za urasimishaji zilizotolewa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yalibaini kuwa hadi mwishoni wa mwaka wa fedha 2021/22, viwanja 2,315,170 kati ya 2,348,324 vilivyobainishwa kwa ajili ya urasimishaji vilipangwa sawa na asilimia 98 ya viwanja vyote vilivyobainishwa. Hata hivyo, kati ya viwanja 2,315,170 vilivyopangwa ni viwanja 1,137,437 tu ndivyo vilipimwa sawa na asilimia 49 ya viwanja vilivyopangwa. Kutopimwa kwa viwanja vyote vilivyopangwa kulisababishwa na:

(a) Malipo hafifu ya fedha za urasimishaji kutoka kwa wananchi

Ukaguzi ulibaini malipo hafifu ya kugharamia urasimishaji kutoka kwa wananchi kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 8.4** kulingana na takwimu zilizokusanywa kutoka mamlaka za serikali za mitaa zilizotembelewa.

Jedwali Na. 8.4: Asilimia ya Jamii/Kaya Zilizolipa Gharama za Urasimishaji

| Halmashauri | Idadi ya Jamii/Kaya Zilizotambuliwa | Idadi ya Kaya Zilizolipa Gharama za Urasimishaji | Asilimia ya Kaya Zilizotambuliwa Zilizolipa Gharama za Urasimishaji (%) |
|--------------------------------|-------------------------------------|--|---|
| Jiji la Dodoma | 300,445 | 7,054 | 2 |
| Jiji la Mbeya | 42,746 | 3,372 | 8 |
| Halmashauri ya Mji wa Tunduma | 6,423 | 693 | 11 |
| Halmashauri ya Mji wa Kibaigwa | 6,304 | 70 | 1 |

| Halmashauri | Idadi ya Jamii/Kaya Zilizotambuliwa | Idadi ya Kaya Zilizolipia Gharama za Urasimishaji | Asilimia ya Kaya Zilizotambuliwa Zilizolipia Gharama za Urasimishaji (%) |
|----------------------------------|-------------------------------------|---|--|
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali | 68,733 | 1,884 | 3 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe | 2,357 | 0 | 0 |
| Manispaa ya Ilala | 182,339 | 4,307 | 2 |
| Manispaa ya Kigoma Ujiji | 14,578 | 2,604 | 18 |

Chanzo: Taarifa za Urasimishaji Mwaka 2022

Jedwali Na. 8.2 linaonesha kuwa kaya zilizolipia gharama za urasimishaji zilikuwa chini ya asilimia 20 katika halmashauri zote nane. Kiwango cha chini kilikuwa katika Halmashauri ya Mji wa Kibaigwa uliokuwa na asilimia 1, na kiwango cha juu kilikuwa katika Manispaa ya Kigoma Ujiji kikiwa na asilimia 18 ya wamiliki wote wa viwanja vilivyotambuliwa ambao walilipia gharama za urasimishaji. Kwa upande mwingine, wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe hawakulipa chochote kwa ajili ya urasimishaji.

Upimaji uliweza kuathirika kwa sababu ulilazimika kufanyika kidogokidogo wakati upangaji hauruhusu kufanyika kidogokidogo. Hii ndiyo sababu baada ya kukamilika kwa upangaji wa maeneo ya urasimishaji, kampuni binafsi za urasimishaji zilianza kupima tu kwa wale ambao wamekamilisha malipo kwa ajili ya urasimishaji.

Kutolipia gharama za urasimishaji kulizichelewesha kampuni binafsi kuendelea na michakato ya upimaji na kukamilika kwa shughuli za urasimishaji. Ucheleweshaji wa kukamilika kwa urasimishaji ulichangia Serikali kupoteza mapato ambayo yangeweza kutozwa kutokana na kodi ya ardhi iliyorasimishwa.

(b) Mipango isiyojitosheleza ya kufanya kampeni kwa jamii juu ya shughuli za urasimishaji

Kifungu cha 3(vii) cha Waraka Na. 1 wa Mwaka 2019 kuhusu Urasimishaji wa Makazi Holela nchini kinawataka maafisa wa halmashauri (wataalamu mipango miji na upimaji wa ardhi) kuandaa mikutano ya hadhara kwa ajili ya uhamasishaji wa masuala ya urasimishaji wa ardhi holela.

Ukaguzi ulibaini kuwa, halmashauri hazikujumuisha kampeni za uhamasishaji katika mipango yake ya kazi na bajeti ya kila mwaka. Aidha, halmashauri zote zilizotembelewa hazikuwa zikitoa taarifa juu ya uhamasishaji uliofanyika na kwa mazingira hayo hazikuwa na kumbukumbu za shughuli za uhamasishaji zilizofanyika.

Hiali hii ilithibitishwa kupitia mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa halmashauri tano zilizotembelewa, ambapo ilibainika kuwa kulikuwa na kampeni urasimishaji zisizojitosheleza kwa jamii kuanzia ngazi ya kata hadi mitaa. Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa masuala ya kampeni za urasimishaji katika mipango na bajeti za halmashauri nchini. Kutokana na hali hiyo, wananchi walikosa hamasa ya kulipia gharama za urasimishaji na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa kukamilisha mchakato wa urasimishaji.

8.5.4 Uratibu Usioridhisha kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, OR-TAMISEMI, ofisi za ardhi za mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kifungu cha 5.5 cha Mwongozo wa Maandalizi ya Mipango ya Jumla na Miradi ya Kina ya Maeneo Mapya, Uhuishaji wa Miji na Urasimishaji wa Mwaka 2007 kinaitaka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI kupitia halmashauri kuratibu shughuli za urasimishaji zinazotekelezwa katika maeneo yao ya utawala.

Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI hazikuwa na utaratibu rasmi wa kuhakikisha kuwa shughuli zote za urasimishaji zinazotekelezwa na halmashauri zinaratibiwa na kutolewa taarifa kupitia njia husika kama vile wakurugenzi wa halmashauri husika (kwa upande wa halmashauri) na makamishna wasaidizi wa ardhi (kwa upande wa ofisi za ardhi za mikoa).

Ukaguzi ulibaini zaidi kuwa, maofisa waliokuwa wakifanya kazi chini ya mwamvuli wa halmashauri kama vile maofisa mipango-miji, wapimaardhi, maofisa ardhi na wathamini hawakuwa na utaratibu maalumu wa kutoa taarifa za moja kwa moja kwa wakurugenzi husika wa mamlaka ya serikali za mitaa au makatibu tawala wa mikoa bali walitoa taarifa moja kwa moja kwa makamishna wasaidizi wa ardhi.

Hali hii ilidhoofisha utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa katika michakato ya urasimishaji kutokana na wakurugenzi wa mamlashauri kutowasimamia moja kwa moja maofisa hao. Wakurugenzi wa halmashauri hawakuweza kuwaadhibu maofisa hao endapo kungekuwa na utovu wa nidhamu au kutofanya kazi kwa sababu hawakuwa na mamlaka ya kinidhamu juu watumishi wa ardhi ambao ndio watekelezaji wakuu wa shughuli za urasimishaji wa makazi.

Athari ya suala hili ni kwamba OR-TAMISEMI na sekretarieti za mikoa hazikupokea taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji. Kutokana na hali hiyo, wakurugenzi wa halmashauri hawakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya kuboresha utendaji wa utekelezaji wa shughuli za urasimishaji kutokana na kukosa taarifa za utekelezaji kutoka katika sekretarieti za mikoa na OR-TAMISEMI.

Hali hii ilisababisha OR-TAMISEMI kukosa taarifa za urasimishaji wa makazi na hivyo ilikuwa vigumu kwa OR-TAMISEMI kuchukua hatua yoyote katika shughuli zinazoendelea za urasimishaji katika halmashauri mbalimbali nchini.

8.5.5 Ufuatiliaji usiotosheleza wa shughuli za urasimishaji unaofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI

Aya ya 4(ii) ya Mwongozo wa Urasimishaji wa Makazi Holela wa Mwaka 2021 inaitaka OR-TAMISEMI kufuatilia utekelezaji wa shughuli za urasimishaji katika mamlaka zote za upangaji (halmashauri). Pia, kifungu cha 6(ix) cha Mwongozo huu kinataka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kufanya ufuatiliaji, usimamizi na tathmini shirikishi ya urasimishaji katika ngazi zote za utekelezaji.

Ukaguzi ulibaini ufuatiliaji usioridhisha wa shughuli za urasimishaji nchini kutokana na kukosekana kwa ripoti za ufuatiliaji zilizofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na OR-TAMISEMI katika kutathmini kazi ziliyofanywa na ofisi za ardhi za mikoa na mamlaka za upangaji. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilikuwa ikipokea taarifa za shughuli za urasimishaji kutoka ofisi za ardhi za mikoa tu. Kupitia mahojiano kati ya timu ya ukaguzi na maofisa wa Wizara wanaohusika na urasimishaji ilibainika kuwa walifanya tathmini mwaka 2020 kuhusu changamoto

zinazokabili shughuli za urasimishaji nchini na kutoa mapendekezo. Hata hivyo, taarifa ya tathmini hiyo ilikuwa haijakamilika.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa OR-TAMISEMI mbali na kutofanya ufuatiliaji wa shughuli za urasimishaji haikupokea taarifa yeyote ya urasimishaji kutoka sekretarieti za mikoa na mamlaka ya serikali za mitaa. Hali hii ilifanya OR-TAMISEMI kutokuwa na taarifa yoyote juu ya shughuli za urasimishaji nchini na hivyo haikuweza kutoa mapendekezo ya kuboresha utendaji wa sekretarieti za mikoa au mamlaka za serikali za mitaa katika shughuli za urasimishaji.

8.6 Mchango katika Kufikia Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sehemu hii inatoa maelezo juu ya matokeo ya changamoto zilizobainishwa katika usimamizi wa urasimishaji wa makazi holela katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Lengo la 11, lengo dogo la 11.3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linataka kuhakikisha kuwa miji na makazi ya watu yanakuwa jumuishi ifikapo mwaka 2030 na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unalenga kupunguza idadi ya makazi holela.

Kwa ujumla, lengo la 11, lengo dogo la 11.3 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linashabihiana na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaosisitiza kuhakikisha makazi yote holela yanarasimishwa. Serikali, katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, kupitia Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iliweka mikakati ya kupunguza wingi wa makazi holela kutoka asilimia 66 hadi asilimia 50 ifikapo mwaka 2021/22.

Hata hivyo, ukaguzi huu ulibaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2022, kulikuwa na viwanja 2,348,324 vilivyobainishwa kwa ajili ya urasimishaji, kati ya hivyo, viwanja 171,210 vilikamilisha mchakato wa urasimishaji hadi wamiliki kupewa hatimiliki. Hali hii inaonesha kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI ziliweza kupunguza wingi wa makazi holela kwa asilimia 7 ya viwanja vilivyotambuliwa. Hali hii ilisababishwa na ujumuishaji hafifu wa shughuli za urasimishaji katika mipango-mkakati yao na mipango ya kila mwaka; utekelezaji hafifu wa kampeni za uhamasishaji wa shughuli za urasimishaji; na upungufu wa rasilimali-watu katika ofisi za ardhi za mikoa na mamlaka

za serikali za mitaa kwa ajili ya zoezi la Urasimishaji. Dosari nyingine ni uratibu hafifu kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, OR-TAMISEMI, ofisi za ardhi za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na ufuatiliaji hafifu wa shughuli za urasimishaji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI.

Kwa kuwa ni mwaka mmoja tu tangu utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano uanze, kama changamoto hizi hazitatatuliwa kulingana na mapendekezo yaliyotolewa, Serikali haitaweza kupunguza makazi 2,496,357 ambayo hayajapangwa kufikia mwaka 2025/26 ambao ni mwisho wa utekelezaji wa mpango. Kwa sababu kuanzia mwaka 2017/18 hadi 2021/22, ni asilimia 7 tu ya viwanja vilivyobainishwa kwa ajili ya urasimishaji vilirasimishwa.

8.7 Hitimisho la Ukaguzi

Ukaguzi unatambua jitihada zinazofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI katika kuwezesha shughuli za urasimishaji na kuongeza kasi ya upatikanaji wa hatimiliki na kupunguza makazi holela. Ukaguzi unahitimisha kuwa mchakato wa urasimishaji haukusimamiwa ipasavyo ili kuwezesha kupunguza makazi holela nchini.

Hali hii ilidhihirishwa na ukweli kwamba, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR-TAMISEMI kwa muda wa miaka 8 kuanzia mwaka wa fedha 2013/14 hadi 2021/22 ziliweza kubainisha jumla ya viwanja 2,348,324, ambapo kati ya hivyo ni viwanja 171,210 tu vilikamilika mchakato wa urasimishaji na hatimiliki kutolewa, sawa na asilimia 7 ya viwanja vilivyotambuliwa. Kasi hii haiwezi kupunguza kwa haraka makazi holela.

Hali hii ilisababishwa na wizara, ofisi za ardhi za mikoa, na halmashauri kutokutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli za urasimishaji na uendeshaji wa kampeni za uhamasishaji jamii na wananchi kutolipia gharama urasimishaji. Kwa mfano, katika halmashauri 8 zilizotembelewa, halmashauri iliyofanya vizuri kuliko zingine, asilimia 18 ya wananchi walimaliza kulipia viwanja vyao vilivyotambuliwa, halmashauri zingine zote zilikuwa chini ya hapo. Pia, kulikuwa na upungufu wa asilimia 69 ya watumishi wanaohitajika hasa wa kada ya mipango-miji, wapima-ardhi na maofisa ardhi.

Zaidi, ukaguzi ulibaini kuwa ucheleweshaji wa urasimishaji ulichangiwa na uratibu usioridhisha kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, OR-TAMISEMI, Ofisi za Ardhi za Mikoa na mamlaka za serikali za mitaa. Hali hii ni kwa sababu maofisa waliokuwa wakifanya kazi chini ya mwamvuli wa halmashauri kama vile maofisa mipango-miji, wapima-ardhi, maofisa ardhi na wathamini walikuwa hawatoi taarifa za utendaji moja kwa moja kwa wakurugenzi husika wa mamlaka za serikali za mitaa au makatibu tawala wa mikoa bali walitoa taarifa moja kwa moja kwa kamishna msaidizi wa ardhi ambaye yuko chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hali hii ilisababisha OR-TAMISEMI kutokuwa na taarifa za uhakika kuhusu urasimishaji na kufanya OR-TAMISEMI isiweze kuchukua hatua zozote za kukuza shughuli za urasimishaji.



USAMBAZAJI WA MAJI

SURA YA TISA

9



USAMBAZAJI WA MAJI

9.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo na hitimisho linalotokana na taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji wa maji. Sura hii pia inaelezea uhusiano uliopo kati ya eneo la ukaguzi na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

9.2 Usuli wa Uendeshaji na Ukarabati wa Miundombinu ya Usambazaji wa Maji

Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali ya Tanzania imeweka kipaumbele zaidi katika upanuzi wa miundombinu ya miradi ya maji. Pia, Serikali imeongeza uwekezaji katika sekta ya maji kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita kutoka shilingi bilioni 563.1 katika mwaka wa fedha 2011/12 hadi shilingi bilioni 705 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21. Pamoja na kwamba fedha zimeongezeka, msisitizo umebaki katika kuongeza miundombinu ya usambazaji zaidi huku utunzaji wa miundombinu hiyo haujapewa kipaumbele.



Kutokana na ukarabati duni, hali ya miundombinu ya maji huchakaa haraka, na hivyo maisha ya usanifu wa miundombinu hayawezi kufikiwa matokeo yake ni kuongeza gharama za kuijenga upya. Kwa mujibu wa taarifa ya hali ya maji iliyotolewa na Wizara ya Maji Mwaka 2020, takribani asilimia 30 ya vituo vya maji vilivyojengwa nchini Tanzania (42,035 kati ya 138,987) havikufanya kazi kuanzia mwaka 2014 hadi 2019. Hali hii inaashiria hasara kwa uwekezaji wa Serikali katika huduma za usambazaji maji na kuleta changamoto katika kusimamia shughuli za ukarabati. Matokeo yake, upatikanaji wa huduma ya maji unakuwa hatarini.

Katika nchi yetu, miradi ya usambazaji wa maji na usafi wa mazingira inasimamiwa na mamlaka za usambazaji maji mijini na usafi wa mazingira (UWSSAs) na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), zote zikiwa chini ya Wizara ya Maji.

9.3 Uhusiano wa Usambazaji Maji na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Uhusiano wa usambazaji maji na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Tanzania ikiwa mwanachama wa Umoja wa Mataifa inawajibika kufuata Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo 6, lengo dogo Na. 6.4 linataka kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji katika sekta zote na kuhakikisha usambazaji uendelevu wa maji safi ili kukabiliana na uhaba wa maji na kupunguza idadi ya watu wanaosumbuliwa na uhaba wa maji ifikapo mwaka 2030.

Kwa hiyo, usimamizi mzuri wa uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji utaisaidia kutekeleza mipango iliyowekwa kufikia shabaha lengo Na 6, lengo dogo Na. 6.4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Uhusiano kati ya Usambazaji Maji na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umeweka lengo la kupunguza maji yasiyo ya mapato kutoka asilimia 47 hadi asilimia 30 kwa Jiji la Dar es Salaam; ukarabati wa vituo 19,889 vya maji visivyofanya kazi ili kurejesha huduma ya usambazaji maji kufikia vituo vya maji 4,972,250; na kuboresha miundombinu ya usambazaji maji na kupunguza maji yasiyo ya mapato katika makao makuu ya mikoa ifikapo mwaka 2020/2021.

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unalenga kupunguza maji yasiyo ya mapato kutoka asilimia 35 hadi asilimia 20 Jijini Dar es Salaam na kutoka asilimia 30 hadi 20 katika makao makuu mikoa ifikapo mwaka 2025/26.

Hivyo, ukaguzi huu ulilenga kuangalia ni kwa kiwango gani Serikali kupitia Wizara ya Maji imetekeleza shughuli za kuboresha miundombinu ya usambazaji maji na kupunguza maji yasiyo ya mapato nchini katika Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira.

9.4 Mikakati na Jitihada za Serikali kuhusu Upatikanaji wa Maji

Kwa mujibu wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Serikali iliweka mikakati ya kupunguza maji yasiyo ya mapato ifikapo mwaka 2020 na kutenga kiasi cha shilingi milioni 900 kutekeleza mkakati huo. Jitihada zilizofanywa na Serikali katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji ni pamoja na kuanzisha na kuingiza masuala ya uendeshaji na ukarabati katika Mwongozo wa Usanifu, Usimamizi wa Ujenzi, Uendeshaji na Ukarabati wa Mwaka 2020 katika Wizara ya Maji.

9.5 Malengo na Mawanda ya Ukaguzi

9.5.1 Lengo la Ukaguzi

Lengo kuu la ukaguzi huu lilikuwa kutathmini iwapo Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira inaendesha kwa ufanisi miradi ya usambazaji maji ili kuhakikisha inakuwa endelevu. Ili kukamilisha lengo kuu, ukaguzi ulikuwa na malengo matatu mahsusi ambayo ni kutathmini iwapo:

- a) Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira zinaendesha ipasavyo miradi ya usambazaji maji iliyoanzishwa nchini;
- b) Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira zinatunza ipasavyo miradi ya usambazaji maji iliyoanzishwa nchini; na
- c) Wizara ya Maji inafuatilia ipasavyo utendaji wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira katika kuendesha na kukarabati miradi ya maji nchini.

9.5.2 Mawanda ya Ukaguzi

Mkaguliwa mkuu alikuwa Wizara ya Maji. Wizara hii ina jukumu la kutunga sera, miongozo na mikakati ya huduma za usambazaji maji na usafi wa mazingira nchini. Pia, Wizara ina jukumu la kutoa ushauri wa kitaalamu, kufuatilia utendaji wa mamlaka za maji, kuratibu na kufuatilia mikakati na mipango ya mamlaka za maji.

Ukaguzi huu ulijikita zaidi katika uendeshaji na ukarabati wa miundombinu

ya usambazaji maji nchini. Ukaguzi uliangalia kipekee ufanisi katika uendeshaji wa miradi ya usambazaji maji; ufanisi katika ukarabati wa miradi ya maji nchini; na ufanisi katika kufuatilia utendaji wa jumuiya za watumiaji maji vijijini, mamlaka za maji na usafi wa mazingira, na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira vijijini unaofanywa na Wizara ya Maji.

Kuhusu ufuatiliaji wa jumuiya za watumiaji maji vijijini, mamlaka za maji na usafi wa mazingira, na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira vijijini unaofanywa na Wizara ya Maji, lengo lilikuwa kuangalia mipango na mikakati ya ufuatiliaji; idadi ya shughuli za ufuatiliaji; utaratibu wa utoaji taarifa; na faini zilizotozwa kwa walioshindwa kukidhi matakwa ya utendaji kazi yaliyowekwa.

Ukaguzi huu uliangalia kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Kipindi hicho kilichaguliwa ili kuaangalia mwenendo wa utendaji kazi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, mamlaka za maji na usafi wa mazingira na jumuiya za watumiaji maji vijijini katika uendeshaji na utunzaji wa miradi ya usambazaji maji. Pia, kipindi hiki kilichaguliwa ili kutoa nafasi mahususi kwa ajili ya tathmini ya utendaji wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini tangu ilipoanzishwa mwaka 2019.

Ukaguzi ulitathmini utoshelevu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira katika kuhakikisha huduma za kutibu maji, utoaji ankara na mita za maji kwa wateja, na upangaji wa rasilimali kwa ajili ya shughuli za usambazaji maji nchini. Aidha, ukaguzi ulitathmini utoshelevu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira katika uandaaji na utekelezaji wa mipango ya ukarabati, ukaguzi wa miundombinu ya maji na uchukuaaji wa hatua stahiki kwa mapungufu yaliyobainishwa, na utaratibu uliowekwa wa kuratibu ukarabati wa miundombinu ya maji iliyoanzishwa.

9.6 Matokeo ya Ukaguzi kuhusu Uendeshaji na Ukarabati wa Miundombinu ya Usambazaji Maji

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi kuhusu uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji nchini. Matokeo yanahusu Wizara ya Maji, mamlaka za maji na usafi wa mazingira, na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira. Matokeo ya ukaguzi huu yamegawanya katika makundi mawili

ambayo ni uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji katika maeneo ya mijini na vijijini kama ilivyoelezwa hapa chini.

9.6.1 Uendeshaji Usiotosheleza wa Miundombinu ya Usambazaji Maji

Utoshelevu wa viawango vya utekelezaji wa uendeshaji wa miundombinu ya usambazaji maji ni muhimu ili kuwa na uendeshaji wenye tija na uendelevu wa miundombinu ya maji iliyojengwa¹⁸. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini mambo yafuatayo:


(a) Miundombinu ya maji iliyojengwa kutumika chini ya uwezo wake

Uchambuzi wa taarifa ya mapitio ya utendaji wa huduma za maji ya EWURA ya mwaka 2022 ulibaini kuwa, kwa miaka mitatu mfululizo ya fedha, uzalishaji wa maji kwa mwaka ulikuwa mdogo kuliko uwezo wa miundombinu ya usambazaji maji iliyojengwa licha ya kuwa mahitaji ya maji hayakufikiwa. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha , Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba ilitakiwa kuzalisha mita za ujazo 13,871, na ilikuwa na uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha mita za Ujazo 18,000 lakini uzalishaji halisi ulikuwa mita za ujazo 7,041 tu. 🌧️

Pia, ilibainika katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi, mahitaji yalikuwa mita za ujazo 53,296, wakati miundombinu iliyowekwa ilikuwa na uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 57,038 lakini uzalishaji halisi wa maji ulikuwa mita za ujazo 33,507 tu. Kwa ujumla, katika mamlaka 8 za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa, jumla ya uzalishaji wa maji ya kila siku ilibainika kuwa chini ya uwezo wa miundombinu iliyowekwa kama ilivyoelezwa katika **Kielelezo Na. 9.1**.

¹⁸ Mwongozo wa Ubunifu, Usimamizi, Uendeshaji na Ukarabati wa Mwaka 2020

Kielelezo Na.9.1: Asilimia ya Matumizi ya Miundombinu Kulingana na Uwezo wa Miundombinu



Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa kutoka Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Zilizotembelewa Uliofanywa na Wakaguzi Mwaka 2023

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha kuwa kati ya mamlaka 8 za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa, ni moja tu ndiyo ilitumia uwezo asilimia 100 wa miundombinu yake. Mamlaka 5 kati ya 8 zilizotembelewa ambazo ni Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama, na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi zilibainika kuwa na kiwango kidogo cha matumizi ya miundombinu cha asilimia 60. Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi ilibainika kuwa na uwezo mdogo zaidi wa matumizi kati ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa ambapo uwezo wake ulikuwa asilimia 22.6 tu.

Zaidi, ukaguzi ulibaini kuwa mamlaka 3 za maji na usafi wa mazingira kati ya 8 zilizotembelewa, zilikuwa na miundombinu ya usambazaji maji isiyofanya kazi, zikiwemo pampu na visima.

(b) Kuwapo kwa miundombinu ya usambazaji maji isiyofanya kazi

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na miundombinu kadhaa isiyofanya kazi katika mamlaka 5 kati ya 8 iliyotembelewa, hali iliyopunguza uzalishaji wa maji. **Jedwali Na. 9.1** linaonesha miundombinu isiyofanya kazi katika miradi ya usambazaji maji .

Jedwali Na. 9.1: Miundombinu ya Usambazaji Maji Isiyofanya Kazi katika Miradi ya Usambazaji Maji Iliyotembelewa

| Mamlaka ya Maji Iliyotembelewa | Jina la Mradi | Muundombinu Usiofanya Kazi | Maoni ya Mkguzi |
|--|---------------------------------|---|---|
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi (LUWASA) | Mradi wa Usambazaji Maji Ng'apa | Kisima Kirefu | Visima vinne kati ya nane vilikuwa havifanyi kazi. Hali hii ilisababisha mita za ujazo 5,712 za maji kutozalishwa na kuifikia jamii kwa siku. Visima visivyofanya kazi vilipunguza uzalishaji wa maji kwa hivyo kutofikia uwezo kamili wa uzalishaji wa maji. |
| | | Mfumo wa kutibu maji ulikuwa umezimwa | Mchakato wa kutibu maji haukufanyika ipasavyo. |
| | | Mfumo wa uwekaji dawa ya klorini haukuwa ukifanya kazi kwa sababu ya kuzibwa na krolini katika mfumo. Kwa hiyo dawa ya krolini haikuwekwa. | Uwekaji dawa ya klorini ulifanywa kwa mikono jambo linalohatarisha uwezekano wa kuzidisha au kupunguza kiwango cha dawa. |
| | | Mfumo wa Udhhibiti wa Usimamizi na Ukusanyaji wa Data kwa ajili ya ufuatiliaji wa utendaji kazi wa mtambo wa kutibu maji haukuwa ukifanya kazi vizuri. Matokeo yake, walihamia kwenye mfumo wa kienyeji wa kutibu kwa mikono. | Kiwango cha maji katika machujio kilifuatiliwa bila kutumia mfumo. Pia, waendeshaaji hawakuweza kufuatilia kwa wakati kiwango cha maji kwenye visima vilivyokuwa vikisambaza maji kwenye mtambo wa kutibu. |
| Mamlaka ya | Mradi wa | Pampu | Pampu moja ya dharura |

| Mamlaka ya Maji Iliyotembelewa | Jina la Mradi | Muundombinu Usiofanya Kazi | Maoni ya Mkaguzi |
|--|---------------------------------|---|--|
| Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Usambazaji Maji wa Ruvu Juu | | katika mtambo wa zamani wa kutibu maji kutoka kwenye chanzo cha maji haikuwa ikifanya kazi. |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba | Mradi wa Usambazaji Maji Bunena | Pampu | Wakati wa ziara, pampu moja kati ya tatu zilizopo kwenye chanzo cha maji ilikuwa haifanyi kazi kutokana na kuharibika kwa takribani wiki mbili. |
| | | Mita ya kisasa ya kupima kiwango cha tope kwenye maji ilikuwa haifanyi kazi kutokana na kuharibika kwa taa yake. Fundi mchundo alikuwa akitumia mita ya zamani kupima tope kwenye maji ambayo haikuwa na ufanisi mkubwa. | Hatari ya kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa sababu mita ya kisasa ya kupima tope ilikuwa na ufanisi mkubwa kuliko mita ya zamani. |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza | Kapripoint | Mfumo wa Udhibiti wa Usimamizi na Ukusanyaji wa Data kwa ajili ya ufuatiliaji wa uendeshaji wa miundombinu uliowekwa katika mtambo wa kutibu maji haukuwa ikifanya kazi vizuri. Matokeo yake, walihamia kwenye mfumo wa kufanya kwa mikono. | Waendeshaji wa mtambo wa kutibu maji hawakuweza kupata taarifa sahihi kwa ajili ya kufuatilia miundombinu ya kutibu maji ikiwa pamoja na kuwekea dawa, chujio, kiwango cha maji kwenye tanki, na ubora wa maji yanayoingia na kutoka kwenye mtambo wa kutibu maji. |

| Mamlaka ya Maji Iliyotembelewa | Jina la Mradi | Muundombinu Usiofanya Kazi | Maoni ya Mkguzi |
|---|----------------------------|--|---|
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | Chamchem ya Shiri na Nsere | Pampu ya dharura kwa ajili ya kuweka klorini katika chemchemi ya Nsere na Shiri ilikuwa haifanyi kazi. | Hatari ya kutotibu maji ikitokea pampu inayofanya kazi ikaharibika. |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu na Uhakiki w Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Zilizotembelewa Mwaka 2023

Jedwali Na. 9.1 linaonesha kuwa mamlaka za maji na usafi wa mazingira tano kati ya nane zilizotembelewa zilikuwa na miundombinu ya usambazaji maji ambayo ilikuwa haifanyi kazi kama ilivyokusudiwa.

Visima vinne vilikuwa havifanyi kazi kutokana na kuharibika kwa transfoma za visima viwili na kusababisha kuacha kutumia maji kutoka kwenye kisima kimoja ambacho kilikuwa na kiwango kikubwa cha tope na hivyo kuwapo na haja ya kufanya ukarabati wa kisima kimoja ili kiendelea kufanya kazi.

Kutofanya kazi kwa visima vinne katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi kulisababisha mita za ujazo 5,712 za maji kutokuzalishwa kwa siku na kusababisha wananchi kukosa maji yaliyokusudiwa. Aidha, kuharibika kwa pampu moja katika Chanzo cha Maji Bunena katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA) kulisababisha kukosekana kwa pampu ya dharura jambo linalohatarisha upatikanaji wa maji endapo pampu moja kati ya hizo mbili ikiharibika.

Jedwali Na 9.1 linaonesha kuwa kutofanya kazi kwa vituo vya kutibu maji kulitokea katika mamlaka 4 kati ya 8 za maji zilizotembelewa. Hali hii ilipunguza ufanisi wa kufuatilia ubora wa maji. Mapungufu haya yalisababishwa na masuala yafuatayo kama yalivyoenezwa hapa chini.

(i) Mipango ya uendeshaji na ukaguzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji isiyojitosheleza

Mwongozo wa Uendeshaji na Ukarabati wa Miundombinu ya Maji wa Wizara ya Maji wa Mwaka 2020 unazitaka mamlaka za maji kuandaa mipango, na taratibu za uendeshaji wa kila kifaa kikubwa, na mradi mzima kwa ujumla.

Ukaguzi ulitembelea mamlaka 8 za maji na usafi wa mazingira na kubaini kuwa mamlaka zote hazikuwa na mipango na taratibu kutoshelevu ya uendeshaji wa miradi yao ya usambazaji maji pamoja na vifaa vikubwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na 9. 2** hapa chini.

Jedwali Na. 9.2: Hali ya Uandaaji wa Mipango, Ratiba na Taratibu za Uendeshaji

| Jina la Mamlaka ya Maji | Jina la Mradi wa Usambazaji Maji | Kuwapo kwa Mipango ya Jumla | Mpango wa Uendeshaji wa Vifaa Vikubwa | Ratiba ya Ukaguzi | | | |
|---|--|-----------------------------|---------------------------------------|-------------------|----------|-----------|-----------|
| | | | | kwa Siku | Kwa Wiki | Kwa Mwezi | Kwa Mwaka |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) | Mradi wa Usambazaji wa Maji wa Kapri Point | ✓ | ✓ | x | X | x | x |
| KUWASA | Mpango wa Usambazaji wa Maji Kigoma | X | x | x | x | X | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma | Mradi wa Usambazaji wa Maji Mzakwe | X | x | x | x | X | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba | Mradi wa Usambazaji wa Maji Bunena | ✓ | ✓ | x | x | X | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Mradi wa Usambazaji Maji Ruvu Juu | ✓ | ✓ | x | x | X | x |

| Jina la Mamlaka ya Maji | Jina la Mradi wa Usambazaji Maji | Kuwapo kwa Mipango ya Jumla | Mpango wa Uendeshaji wa Vifaa Vikubwa | Ratiba ya Ukaguzi | | | |
|---|-------------------------------------|-----------------------------|---------------------------------------|-------------------|-----------|----------|---------|
| | | | | kwa Wiki | Kwa Mwezi | Kwa Mwak | Ukaguzi |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi | Mradi wa Usambazaji Maji wa N'gapa | X | x | x | x | X | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | Chemchem ya Maji Nsere | ✓ | ✓ | x | x | X | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida | Mradi wa Usambazaji wa Maji Majengo | ✓ | ✓ | x | x | X | x |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Data kutoka Uthibitisho wa Eneo la Mradi Jumuiya za Watumiaji wa Maji Zilizotembelewa mwaka 2023

Jedwali Na. 9.2 hapo juu linaonesha kwamba, kwa mamlaka 8 za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa, mamlaka tatu zilifanya kazi bila kuwa na taratibu rasmi za uendeshaji ambazo zinatakiwa kufuatwa na wafanyakazi wote. Mamlaka 5 zilikuwa na mipango ya jumla pamoja na mipango ya uendeshaji wa vifaa vikubwa lakini hazikuwa na ratiba ya ukaguzi. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa mwongozo na mpango wa uhamasishaji kutoka Wizara ya Maji kwa wafanyakazi wanaosimamia uendeshaji na matengenezo juu ya umuhimu wa kuwa na mipango ya uendeshaji kwa kila kifaa kikubwa kilichowekwa katika miradi ya usambazaji maji.

Aidha, katika jumuiya 19 za kijamii za utoaji wa huduma za maji zilizotembelewa ambazo zilikuwa zikiendesha miradi ya usambazaji maji vijijini chini ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini hazikuwa na mipango na taratibu za uendeshaji wa miradi ya maji. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa uelewa miongoni mwa watoahuduma kuhusu mahitaji ya kuwa na mipango na taratibu za uendeshaji; na kukosekana kwa mafunzo ya

kuhakikisha kuwa timu za usimamizi zinakuwa na uwezo wa kuandaa na kutumia mipango na taratibu za uendeshaji.


Kukosekana kwa mipango na taratibu za uendeshaji wa miradi ya maji kumesababisha shughuli za uendeshaji kufanywa kwa kutumia uzoefu na mitazamo ya mtu kibinafsi, ambayo inaweza kusababisha uendeshaji kuwa kinyume na maelekezo ya mtengenezaji hatimaye kusababisha kifaa kuharibika au kushindwa kufanya kazi.

(ii) Ukusanyaji hafifu wa ankara za maji kutoka kwa wateja

Mamlaka za maji na usafi wa mazingira (WSSAs) zina jukumu la kuhakikisha kuwa wateja wote waliopatiwa huduma za maji wanatozwa ankara na kuhakikisha kuwa kiasi kinachostahili kulipwa kinakusanywa kwa ufanisi. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na madeni makubwa kutoka kwa wateja ambao walipewa huduma za maji.

Ukaguzi ulibaini kuwa, madeni katika mamlaka nane za maji zilizotembelewa kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2021/22 ni kati ya shilingi milioni 119 hadi milioni 11,309. **Kielelezo Na. 9.2** kinaonesha kiasi cha madeni kwa mwaka kwa kila mamlaka ya maji iliyotembelewa.

Kielelezo Na.9.2: Kiasi cha Madeni katika Mamlaka za Maji Zilizotembelewa kuanzia Mwaka 2019/20 hadi 2021/22



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu kutoka Mamlaka za Maji Zilizotembelewa Mwaka 2023

Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni 31.676 ni deni la ankara za maji ambazo hazikulipwa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka

2019/20 hadi 2021/22. Deni la juu zaidi lilikuwa katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam ambapo deni lake lilikuwa wastani wa shilingi bilioni 11.309 kwa mwaka wakati kiwango cha chini cha deni kilikuwa katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi ambayo ilikuwa na deni la kiasi cha shilingi milioni 119.

Jitihada za Wizara ya Maji zisizoridhisha katika kusaidia ukusanyaji wa madeni ya wateja zinahatarisha uwezekano wa kurejesha madeni hayo. Aidha, mamlaka za maji huenda zikashindwa kufikia lengo la kujiendeleza kupitia mapato yatokanayo na ankara za maji na kupunguza utegemezi kwa Serikali na kufanya uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya maji kwa kutumia mfuko wao wenyewe.

(iii) Mipango duni ya vipuri na vifaa kwa ajili ya uendeshaji, ukaguzi wa maji na udhibiti wa uvujaji na mipango ya matumizi bora ya nishati ya umeme

Kwa mujibu wa kifungu cha 4.2 cha Mwongozo wa Uendeshaji na Ukarabati wa Wizara ya Maji, mamlaka za maji zinatakiwa kuandaa mpango wa utoaji wa vipuri na vifaa kwa ajili ya uendeshaji; kuwa na mpango wa ukaguzi wa maji na udhibiti wa uvujaji; na kuwa na mpango wa matumizi bora ya nishati ya umeme.

Hata hivyo, mapitio ya taarifa za utendaji ya kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22 kutoka mamlaka nane za maji zilizotembelewa yalionesha kuwa, mamlaka hazikuandaa mpango wa utoaji wa vipuri na vifaa; hazikuwa na mpango wa ukaguzi wa maji na udhibiti wa uvujaji; na hazikuwa na mpango wa matumizi bora ya umeme. Maelezo ya kina kuhusu mamlaka za maji zilizotembelewa yanatolewa katika **Jedwali Na. 9.3**.

Jedwali Na. 9.3: Hali ya Upatikanaji wa Mipango Mbalimbali katika Mamlaka za Maji Zilizotembelewa

| Jina la Mamlaka ya Maji | Mipango ya Kujengewa ya Uwezo | Mipango ya Vipuri na Utoaji wa Vifaa | Mipango ya Ukaguzi wa Maji na Udhibiti wa Uvujaji wa Maji | Mipango ya Matumizi Bora ya Umeme |
|--|-------------------------------|--------------------------------------|---|-----------------------------------|
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza | ✓ | x | x | x |
| Mamlaka ya Maji | ✓ | x | x | x |

| Jina la Mamlaka ya Maji | Mipango ya Kujengewa ya Uwezo | Mipango ya Vipuri na Utoaji wa Vifaa | Mipango ya Ukaguzi wa Maji na Udhhibiti wa Uvujaji wa Maji | Mipango ya Matumizi Bora ya Umeme |
|---|-------------------------------|--------------------------------------|--|-----------------------------------|
| na Usafi wa Mazingira Kahama | | | | |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | ✓ | x | x | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba | ✓ | x | x | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | ✓ | x | x | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi | ✓ | x | x | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | ✓ | x | x | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida | ✓ | x | x | x |


Chanzo: Programu ya Mafunzo kutoka WSSAs na Miradi ya Usambazaji Maji Iliyotembelewa Mwaka 2023

Jedwali Na. 9.3 linaonesha kuwa mamlaka zote 8 zilizotembelewa zilikuwa na mipango ya kujengea uwezo watumishi wanaohusika na uendeshaji wa miradi ya maji. Hata hivyo, hazikuwa na mipango ya vipuri na zana za uendeshaji, mipango ya ukaguzi wa maji na udhibiti wa uvujaji, na mipango ya matumizi bora ya nishati ya umeme. Dosari hii ilichangia ongezeko la asilimia ya maji yasiyo ya mapato.

Aidha, kukosekana kwa mipango yenye ufanisi katika matumizi ya nishati kumesababisha kiasi kikubwa cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya uendeshaji na ukarabati kutumika kulipia ankara za umeme. **Jedwali Na. 9.2** linaonesha ukosefu wa ufanisi katika matumizi ya nishati ya umeme na kusababisha matumizi makubwa katika kuendesha miradi ya usambazaji maji. Kwa upande mwingine, mapungufu haya yalisababisha kiasi kikubwa cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya uendeshaji na ukarabati kutumika

kugharamia ankara za umeme. Uchambuzi wa asilimia ya bajeti ya uendeshaji na ukarabati iliyotumika kwa ajili ya kulipa ankara za umeme unaoneshwa katika Kielelezo Na. 9.3.

Kielelezo 9.3: Asilimia ya Bajeti ya Uendeshaji na Ukarakabati Inayolipwa kama Ankara za Umeme katika Mamlaka za Maji



Chanzo: Uchambuzi wa Takwimu wa Wakaguzi kutoka Mamlaka za Maji Zilizotembelewa Mwaka 2023

Kielelezo Na. 9.3 kinaonesha kuwa mamlaka 2 za maji kati ya 8 zilizotembelewa zilikuwa na zaidi ya asilimia 50 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya uendeshaji na ukarabati iliyokuwa inatumika kulipia ankara za umeme. Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama ilitumia karibu asilimia 100 ya bajeti ya uendeshaji na ukarabati katika miaka yote mitatu kulipia ankara za umeme.

9.6.2 Ukarakabati hafifu wa miundombinu ya usambazaji wa maji

Mwongozo wa Usanifu, Usimamizi wa Ujenzi, Uendeshaji na Ukarakabati wa Mwaka 2020 wa Wizara ya Maji unazitaka mamlaka za maji na usafi wa mazingira na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kufanya

ukarabati wa mitandao ya miundombinu ya usambazaji wa maji iliyojengwa ili ifanye kazi kulingana na muda wa usanifu wake. Ukaguzi ulibaini kuwa miundombinu mbalimbali ya maji haifanyi kazi kama ilivyosanifiwa kutokana na sababu mbalimbali kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

Ukosefu wa mipango ya ukarabati wa kinga

Kifungu cha 4.2 cha Mwongozo wa Uendeshaji na Ukarabati kinazitaka mamlaka za usambazaji maji kuandaa mipango ya uendeshaji na ukarabati kwa kila kifaa kikubwa na mtandao wa usambazaji wa maji kwa ujumla. Mpango wa uendeshaji na ukarabati kwa ujumla unapaswa kuwa kwa mradi mahususi ili kukidhi mahitaji ya miundombinu mbalimbali iliyowekwa.


Ukaguzi ulibaini kuwa, katika mamlaka 8 zote za maji na usafi wa mazingira na jumuiya 19 za utoaji wa huduma za maji zilizotembelewa hazikuwa na mipango ya ukarabati wa kila mwaka/mara kwa mara. Kuwapo kwa mipango hii ingehakikisha ukarabati endelevu wa miundombinu iliyowekwa katika miradi ya usambazaji wa maji kwa sababu bila mipango, kipaumbele huwekwa katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia 100 na si shughuli za ukarabati ya kinga.

Kumbukumbu duni za ukarabati wa miradi ya usambazaji wa maji

Mwongozo wa uendeshaji na ukarabati wa miradi ya maji unaelekeza kwamba, shughuli zote za ukarabati ziandikwe kwenye kumbukumbu za ukarabati. Aidha, kumbukumbu za kila ukarabati au kazi za matengenezo katika mfumo wa usambazaji wa maji pamoja na gharama za vifaa, kazi na tarehe ambayo ukarabati umefanyika vinatakiwa kutunzwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa, katika mamlaka za maji na usafi wa mazingira 5 kati ya 8 zilizotembelewa, hakukuwa na kumbukumbu za kutosha za ukarabati huku mamlaka 3 zikiwa hazina kabisa kumbukumbu za ukarabati kama inavyotakiwa na mwongozo wa uendeshaji na matengenezo wa miradi ya maji. Maelezo ya kina kuhusu mamlaka husika za maji na usafi wa mazingira ni kama zilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 9.4.**

Jedwali Na. 9.4: Hali ya Utunzaji wa Kumbukumbu za Ukarabati wa Miradi ya Usambazaji wa Maji

| Jina la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira | Uwasilishaji wa Kumbukumbu za Matengenezo | |
|---|---|----------------------------------|
| | Kumbukumbu duni za ukarabati | Kukosekana kabisa kwa kumbukumbu |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma | ✓ | |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza | ✓ | |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | ✓ | |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi | | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba | ✓ | |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama | ✓ | |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | | x |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida |  | x |

Chanzo: Uchambuzi wa Takwimu za Wakaguzi kutoka Jumuiya za Watumiaji wa Maji Zilizotembelewa Mwaka 2023

Jedwali Na. 9.4 linaonesha kuwa kati ya mamlaka 8 za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa, 5 zilikuwa na kumbukumbu duni za ukarabati wa miundombinu ya usambazaji wa maji wakati 3 hazikuwa na kumbukumbu kabisa. Mamlaka 5 zilizokuwa na kumbukumbu, kumbukumbu hizo zilihusu shughuli za kila siku za uendeshaji wa pampu za maji ambazo ni pamoja na jina la fundi mchundo, saa za uendeshaji wa pampu na kuwashwa na kuzimwa hakukuwa na kumbukumbu yoyote ya ukarabati mkubwa.

Ufuatiliaji na ukaguzi hafifu wa mitandao ya usambazaji maji

Wafanyakazi kutoka Idara ya Uendeshaji na Ukarabati katika mamlaka za maji na usafi wa mazingira wanatakiwa kufanya ufuatiliaji katika mitandao ya usambazaji maji ili kubaini uharibifu, au uchakavu kwenye mtandao na kuchua hatua stahiki¹⁹. Pia, pampu za maji zinatakiwa kukaguliwa angalau

¹⁹ Kifungu cha 7.5.1(c), na 9.4 cha Wizara ya Maji O&M Mwongozo

mara moja kwa mwaka na waendeshaji au wahandisi wenye sifa.²⁰

Ukaguzi ulibaini kuwa, mamlaka za maji na usafi wa mazingira hazikufanya ufuatiliaji wa mitandao ya miundombinu ya usambazaji wa maji. Badala yake, maofisa kutoka mamlaka za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa walisema kwamba, mara zote wanafanya ukaguzi usiokuwa na mpangilio kulingana na taarifa ya hitilafu ya miundombinu ya maji inavyotolewa. Hata katika mazingira hayo, ukaguzi haufanyiki kwa mpangilio na hakuna taarifa yoyote inavyotolewa katika mamlaka zote saba za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa.

Ni Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Moshi pekee ndiyo iliweza kuandaa taarifa. Mapitio ya taarifa hiyo yalionesha kuwa sababu kuu za matatizo hayo ni kukosekana kwa ukarabati wa sehemu muhimu za miradi ya usambazaji maji ikiwa pamoja na chemba na valvu, kukosekana kwa ratiba za ukarabati wa sehemu muhimu za miradi ya usambazaji maji, kukosekana kwa ukarabati wa marekebisho ya miundombinu muhimu ya maji, na kukosekana kwa alama kuonesha mabomba yalimopita.

Ukarabati duni kutokana na kasoro zinazobainika katika mfumo wa usambazaji wa maji

Mamlaka za maji na usafi wa mazingira zinatakiwa kuweka utaratibu wa ukarabati wenye tija na kwa wakati wa uvujaji wa maji²¹. Ukaguzi ulibaini kasoro katika mifumo ya usambazaji maji ambazo hazikurekebishwa ipasavyo kama inavyoelezwa katika **Jedwali Na. 9.5**.

Jedwali Na. 9.5: Kasoro za Miundombinu ambazo Hazikurekebishwa katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Zilizotembelewa

| Jina la Mtandao wa Usambazaji Maji | Jina la Mtandao wa Usambazaji Maji | Kasoro zilizobainika na Hazikurekebishwa. |
|--|---|--|
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma | Mradi wa Maji ya Visima Mzakwe | <ul style="list-style-type: none">Mfumo wa Udhhibiti wa Usimamizi na Ukusanyaji wa Data hautoi tena taarifa kuhusu utendaji wa baadhi ya visima kwenye kituo cha ufuatiliaji katika Ofisi ya Mzakwe. |

²⁰ Pg 91 ya Mwongozo wa Uendeshaji na Matengenezo ya Miradi ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, Toleo la Nne 2020

²¹ Pg 79 ya Mwongozo wa Uendeshaji na Matengenezo ya Miradi ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, 2020 *Toleo la Nne*

| Jina la Mtandao wa Usambazaji Maji | Jina la Mtandao wa Usambazaji Maji | Kasoro zilizobainika na Hazikurekebishwa. |
|--|---|--|
| | | <ul style="list-style-type: none"> Hata hivyo, maofisa waliokuwa wanaendesha visima katika eneo la Mzakwe waliondolewa baada ya mashine kufungwa na wakati huo ilikuwa ikifanya kazi vizuri. Wakati wa ukaguzi huu, mfumo ulikuwa haufanyi kazi na waendeshaji hawakurudishwa kufuatilia uendeshaji wa visima badala yake wanategemea walinzi ambao hawana kabisa ujuzi wa kiufundi. Mfumo huo ulihitaji kufanyiwa maboresho lakini Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma haikuwa na wataalamu wa kuutengeneza au kuuhuisha ili kurekebisha kasoro zilizobainika. |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza | Mtambo wa kutibu maji wa Capri Point | <ul style="list-style-type: none"> Mamlaka ilikuwa na mfumo wa <i>kielekituroniki</i> wa kusoma hali ya uendeshaji wa kituo katika mtambo ya kutibu maji. Wakati wa ukaguzi huu, mfumo ulikuwa haufanyi kazi. Maofisa ubora wa maji walisema walikuwa wanafuatilia uendeshaji wa mtambo wa kutibu maji kwa kuangalia kwa macho, hawakuwa na uwezo wa kuurejesha mfumo wa <i>kioleturoniki</i> ambao ulikuwa na kasoro. |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi | Visima 4 kati ya 8 vilivyoanzishwa vilikuwa havifanyi kazi. Visima ambavyo havifanyi kazi ni namba 9, 11, 13 na 14. | <ul style="list-style-type: none"> Kisima kimoja kilikuwa na kiwango kikubwa cha tope na kusababisha kifungwe. Hali hii ilisababisha utafiti usiotosheleza wa kuhakikisha maji yanayopatikana yatafikia viwango vinavyotakiwa kabla ya kuaza uchimbaji Visima viwili vilikuwa havifanyi kazi kwa sababu ya kuharibika kwa mota. |

| Jina la Mtandao wa Usambazaji Maji | Jina la Mtandao wa Usambazaji Maji | Kasoro zilizobainika na Hazikurekebishwa. |
|--|------------------------------------|---|
| | | <ul style="list-style-type: none"> • Kisima kimoja kilihitaji matengenezo ili kiweze kufanya kazi. • Mfumo wa Udhibiti wa Usimamizi na Ukusanyaji wa Data uliowekwa kwenye mtambo wa kutibu maji haukuwa unafanya kazi hivyo kushindwa kutoa taarifa za uendeshaji kama vile visima na chujio, na hawakuweza kurekebisha mfumo huo kutokana na kukosa utaalumu. |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba | Mradi wa Usambazaji Maji wa Bunena | <ul style="list-style-type: none"> • Pampu moja kati ya tatu kwenye chazo cha maji ilikuwa haifanyi kazi kwa sababu mota ilikuwa imeharibika. • Mita ya 'morden turbidity' ilikuwa haifanyi kazi kutokana na taa yake kuharibika. Fundi mchundo alikuwa akitumia mita ya zamani kupima tope kwenye maji ambayo ufanisi wake ulikuwa mdogo ikilinganishwa na mita ya kisasa. |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | Chanzo cha Maji cha Shiri na Nsere | <ul style="list-style-type: none"> • Pampu ya dharura kwa ajili ya kuwekea dawa ya klorini katika chanzo cha maji Nsere na Shiri ilikuwa haifanyi kazi kwa sababu mota ilikuwa imeharibika. |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa Zilizokusanywa Walipotembelea Mradi wakati wa Ukaguzi Mwaka 2023

Jedwali Na. 9.5 linaonesha kasoro zilizobainishwa katika miradi ya usambazaji maji iliyotembelewa katika mamlaka tano za maji na usafi wa mazingira ambazo zilikuwa hazijarekebishwa. Sababu kuu za kutorekebishwa kwa kasoro zilizobainishwa ni pamoja na:

- (i) Uwezo mdogo wa uendeshaji wa mifumo ya kujiendesha yenyewe katika kuendesha mitandao/mfumo wa usambazaji maji.

(ii) Mafunzo duni kwa maofisa wanaoendesha miradi wakati wa ufungaji na kukabidhi mifumo iliyowekwa na kampuni zilizopewa zabuni.


Athari za ukarabati hafifu kwa miundombinu ya usambazaji maji

(i) Kutofikiwa kiwango cha asilimia 20 cha huduma cha maji yasiyo ya mapato katika maeneo ya mijini

Wizara ya Maji imepanga kupunguza asilimia ya maji yasiyo ya mapato kutoka wastani wa kitaifa wa asilimia 36 mwezi Julai 2014 hadi asilimia 25 ifikapo Juni 2024. Pia, Wizara ilipanga kufikia asilimia 28 ya maji yasiyo ya mapato ifikapo mwaka 2022. Aidha, kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji, kiwango cha huduma kinachotakiwa cha maji yasiyo ya mapato (upotevu wa maji) ni si zaidi ya asilimia 20 ya maji yanayozalishwa²²

Katika mamlaka 8 za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa, ni mamlaka moja tu ilipata kiwango cha huduma kilichopendekezwa cha maji yasiyo ya mapato yaani kiwango kisichozidi asilimia 20. **Kielelezo Na. 9.4** kinawasilisha muhtasari wa taarifa kuhusu hali ya maji yasiyo ya mapato katika mamlaka zilizotembelewa.

Kielelezo Na. 9.4: Hali ya Maji Yasiyo ya Mapato katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Zilizotembelewa



Chanzo: Uchambuzi wa Takwimu za Wakaguzi kutoka EWURA Mwaka 2022

²² Pumri wa Miaka 52 na 108 Mtawalia wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati wa Miaka Mitano wa MoW 2019/20 - 2023/24

Kielelezo Na. 9.4 kinaonesha kuwa, kwa miaka ya fedha 2019/20, 2020/21 na 2021/22, kati ya mamlaka nane za maji na usafi wa mazingira zilizotembelewa ni mamlaka moja tu ambayo ni Moshi ndiyo iliweza kufikia kiwango kilichopendekezwa cha asilimia 20 ya maji yasiyo ya mapato kwa mwaka 2020/21. Kiwango cha juu cha maji yasiyo ya mapato kilishuhudiwa katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba kwa asilimia 42, 45 na 44 mwaka 2019/20, 2020/21 na 2021/22 mtawalia. Kati ya mamlaka nane zilizotembelewa, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi ilifanya vizuri kwa kipindi chote cha miaka mitatu ikilinganishwa na mamlaka zingine zilizotembelewa. Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi ilikuwa na kiwango cha maji yasiyo ya mapato kwa asilimia 22, 20 na 27 kwa miaka ya 2019/20, 2020/21 na 2021/22 mtawalia.

Miongoni mwa sababu za kutofikia kiwango kinachotakiwa cha maji yasiyo ya mapato zilikuwa:

- (i) Upotevu wa maji kutokana na kupasuka kwa mfumo wa mabomba kutokana na matengenezo yasiyo na mpangilio ya mtandao wa miundombinu ya usambazaji maji;
- (ii) Uharibifu wa mabomba kutokana na uratibu duni wa wakala za serikali wakati wa uanzishaji wa miradi ya usambazaji maji kama vile Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini Tanzania na Wakala wa Barabara Tanzania wakati wa kujenga mtandao wa barabara ambao hukata mabomba wakati wa ujenzi; na
- (iii) Ukosefu wa mita za kupima upotevu wa maji na kuwapo kwa mita za maji zisizofanya kazi. Katika mamlaka 8 zilizotembelewa, kulikuwa na jumla ya mita 15,180 za maji zisizofanya kazi ambazo zilisababisha kutojua sawasawa kiasi cha maji kinachotumiwa na wateja.

Kutokana na asilimia kubwa ya maji yasiyo ya mapato, maji yaliyozalishwa hayakuwafikia wananchi waliokusudiwa na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali. Kiasi cha mapato kinachopotea kutokana na maji yasiyo ya mapato kwa miaka ya fedha 2020/21 na 2019/20 kimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 9.6.**

Jedwali Na. 9.6: Mapato ya Mwaka Yanayopotea kutokana na Maji Yasiyo ya Mapato kwa Miaka ya Fedha 2019/20 na 2020/21

| Mamlaka za Maji Zilizotembelewa | Upotevu wa Maji Juu ya Kikomo Kinachotakiwa cha Asilimia 20 ya Maji Yanayozalishwa | Bei ya Mita Moja ya Ujazo (shilingi) | Upotevu wa Mapato ya Mwaka kutokana na Upotevu wa Maji Juu ya Kiwango Kinachotakiwa (Shilingi Billioni) |
|---|--|---|--|
| Mwaka wa Fedha 2020/21 | | | |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba | 556,559.30 | 1,888 | 1.05 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 27,718,687.89 | 1,663 | 46.10 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma | 2,704,252.80 | 1,397 | 3.78 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama | 460,281.90 | 1,400 | 0.64 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi | 144,417.55 | 1,800 | 0.26 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | - | 900 | 0.00 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza | 4,694,382.24 | 1,873 | 8.79 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida | 296,953.20 | 937 | 0.28 |
| Jumla ndogo | | | 60.90 |
| Mwaka wa Fedha 2019/20 | | | |
| WSSAs | Upotevu wa Maji Juu ya Kikomo Kinachoruhusiwa - 20% (M ³) | Ushuru wa Wastani - Shilingi kwa M ³ | Upotevu wa mapato ya mwaka kutokana na upotevu wa maji juu ya kiwango kinachoruhusiwa (shilingi bilioni) |

| Mamlaka za Maji Zilizotembelewa | Upotevu wa Maji Juu ya Kikomo Kinachotakiwa cha Asilimia 20 ya Maji Yanayozalishwa | Bei ya Mita Moja ya Ujazo (shilingi) | Upotevu wa Mapato ya Mwaka kutokana na Upotevu wa Maji Juu ya Kiwango Kinachotakiwa (Shilingi Billioni) |
|---|--|--------------------------------------|---|
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba | 501,152.30 | 1,888 | 0.95 |
| Dar es Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Salaam | 29,467,180.00 | 1,663 | 49.00 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma | 1,625,031.10 | 1,397 | 2.27 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama | 292,562.10 | 1,400 | 0.41 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Lindi | 113,776.52 | 1,700 | 0.19 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | 235,848.40 | 800 | 0.19 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza | 3,586,563.00 | 1,060 | 3.80 |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Singida | 341,807.90 | 1,231 | 0.42 |
| Jumla ndogo | | | 57.23 |
| Hasara ya Jumla kwa Miaka ya Fedha Miwili | | | 118.13 |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Utendaji wa WSSAs kwa Miaka ya Fedha 2020/21, 2023

Jedwali Na. 9.6 zaidi inaonesha kuwa, katika mamlaka 8 zilizotembelewa, serikali ilipoteza jumla ya shilingi bilioni 118.13 kutokana na kuwapo kwa maji yasiyo ya mapato juu ya kiwango kinachotakiwa kwa miaka ya fedha

2020/21 na 2019/20. Takwimu za mwaka wa fedha 2021/22 hazikuchambuliwa kwa kuwa bado hazijatolewa na EWURA.


Ukaguzi ulibaini pia kuwa, Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini haikuwa na utaratibu wa kuhakikisha kuwa takwimu za maji yasiyo ya mapato zinachuliwa kutoka jumuiya za utoaji wa huduma ya maji ngazi ya jamii na kuzifanya ziwe zinapatikana katika makao makuu ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Hali hii ilitokana na kukosekana kwa mita za kusoma kiasi cha maji kinachozalishwa na kutumika katika miradi ya usambazaji maji ili kuhakikisha kiasi cha maji yanayozalishwa, kusambazwa na kutolewa kwa mteja kinapimwa ili kujua kiasi cha maji yaliyozalishwa na kiasi cha maji yaliyotumika. Matokeo yake, kulikuwa na hatari ya kutofikia lengo lililowekwa la maji yasiyo ya mapato kwa kiwango cha asilimia 28 kufikia mwaka 2022.

Sababu za kiwango kikubwa cha maji yasiyo ya mapato ni kama ifuatavyo:

- **Kuwapo kwa mita za maji zisizofanya kazi**

Kwa kawaida, mita zilizowekwa kwa wateja wa huduma za maji zinatakiwa kubadilishwa ndani ya miaka mitano. Aidha, mita zote za maji zenye kasoro zinatakiwa kubadilishwa ili kufikia huduma za maji zilizokusudiwa. Hali ya mita za maji zisizofanya kazi katika mamlaka za maji zilizotembelewa ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na.9.5**.

Kielelezo Na.9.5: Hali ya mita za maji zisizofanya kazi



Chanzo: Uchambuzi wa data kutoka Mamlaka za Maji Zilizotembelewa, 2022


Kielelezo Na. 9.5 kinaonesha kuwa idadi kubwa ya mita za maji zenye kasoro ilibainika katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam iliyokuwa na mita za maji 48,547 zisizofanya kazi wakati kiwango cha chini kilikuwa kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Bukoba iliyokuwa na mita za maji 16 zisizofanya kazi.

Kuwapo kwa mita zisizofanya kazi kulisababishwa na ukosefu wa ukarabati wa mara kwa mara wa mita zenye kasoro na upimaji wa mita wa mara kwa mara ili kutathmini utendaji wake na kuchukua hatua stahiki pale mapungufu yanapobainika. Hali hii ilileta hatari ya kuwapa wateja ankara zisizoendana na kiwango cha maji walichotumia.

- **Uwekaji hafifu wa mita za maji kwenye miradi ya usambazaji maji vijijini**

Ukaguzi ulibaini kukosekana kwa mita za kutosha za wateja kwa ajili ya miradi ya usambazaji maji katika maeneo ya vijijini jambo lililofanya iwe vigumu kujua wingi wa maji yanayotolewa kwa wateja. Asilimia ya wateja ambao hawajafungiwa mita 19 za maji katika jumuiya za utoaji wa huduma za maji vilivyotembelewa imeoneshwa katika **Kielelezo Na. 9.6**.

Kielelezo Na. 9.6: Asilimia ya Wateja Wasio na Mita kutoka katika Jumuiya za Utoaji wa Huduma za Maji Zilizotembelewa



Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Takwimu kutoka Jamii za Utoaji Huduma za Maji Zilizotembelewa Mwaka 2023

Kielelezo Na. 9.6 kinaonesha kuwa jumuiya 19 za utoaji huduma za maji ngazi ya jamii zilizotembelewa, 11 vilikuwa na asilimia 50 au zaidi ya wateja wao ambao hawana mita wakati katika jumuiya tatu walikuwa na asilimia 100 ya wateja wao ambao hawakuwa na mita kabisa.

Matokeo yake, ilikuwa vigumu kujua kiasi cha maji kinachotumika na kiasi cha mapato kinachotarajiwa. Pia, ilikuwa vigumu kutathmini kiwango cha maji yasiyo ya mapato au maji yaliyokuwa yanazalishwa lakini yanapotea katika maeneo ya vijijini kwa kuwa hawawezi kufuatilia kiasi cha maji yanayotolewa kwa jamii kutokana na kukosekana kwa mita. Aidha, hakukuwa na makadirio ya kiasi cha maji kinachosambazwa kwa jamii kutokana na kukosekana kwa mita.

(i) Hatari ya kupungua kwa maeneo yanayopata huduma za maji

Ikiwa utunzaji wa miundombinu ya maji hautakuwa wa ufanisi kwa kuchukua hatua stahiki juu ya kasoro zilizobainishwa, miundombinu ya maji haitadumu kulingana na muda iliyosanifiwa. Hii ni kwa sababu miundombinu ya usambazaji wa maji haitatumika kulingana na uwezo wake wa juu iliyosanifiwa kwa hivyo haitaweza kuzalisha kiwango kinachotakiwa cha maji na mahitaji ya maji yaliyokudiwa hayatafikiwa.

(ii) Kupungua kwa uendeleu wa miradi ya usambazaji maji

Utendaji wa mitandao ya usambazaji maji hautaweza kutathminiwa kwa ufasaha ili kubaini uendeleu wake na kuchukua hatua stahiki za kurekebisha. Aidha, kumbukumbu za ukarabati zinaweza kusaidia kuunda programu maalumu za ukarabati na kutumika kuzuia gharama kubwa za ukarabati kutokea. Katika hali hii, miundombinu ya usambazaji maji bila kumbukumbu za ukarabati inakuwa katika hatari ya kuharibika.

9.6.3 Ufuatiliaji hafifu wa utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira

Wizara ya Maji ilikuwa na jukumu la kufuatilia shughuli zinazofanywa na mamlaka za maji na usafi wa mazingira. Hata hivyo, mapitio ya ufuatiliaji uliofanywa kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22 yalibaini kuwa, badala ya kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kuhusu shughuli na kazi za matengenezo za mamlaka za maji na usafi wa mazingira, Wizara ya Maji

ilitegemea sana taarifa zilizowasilishwa na mamlaka za maji kwa njia ya mtandao na kufanya ufuatiliaji bila kuwa na ratiba maalumu. Pia, ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ilifanya ufuatiliaji baada ya kutokea tatizo kama ilivyoelezwa kwenye **Jedwali Na. 9.7.**

Jedwali Na. 9.7: Ufuatilia Uliofanyika kwa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira

| Jina la Mamlaka | Sababu ya Kufanya Ufuatiliaji Kulingana na Ripoti Iliyowasilishwa |
|---|---|
| Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Arusha | Wizara ya Maji ilikuwa na mpango wa kuendesha mafunzo ya uendeshaji na ukarabati wa mradi ya maji kwa wahandisi na mafundi wa mamlaka za maji. Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Arusha na Moshi zilichaguliwa kama mamlaka za majaribio ambapo shughuli zao za uendeshaji na ukarabati zilipimwa ili kutumia changamoto katika kupanga mafunzo ya baadaye. |
| Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi | |
| Mradi wa Maji Makonde | Ukaguzi ulifanywa na watumishi mafundi kutoka Wizara ya Maji baada ya kupata taarifa kutoka kwa Meneja wa Mamlaka ya Maji Makonde kuhusu kupungua kwa utendaji wa pampu kutoka mita za ujazo 344,000 hadi 120,000 kwa mwezi |

Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Ufuatiliaji kutoka Wizara ya Maji Mwaka 2023

Kulingana na maelezo kutoka kwa maafisa wa Wizara ya Maji, fedha kwa ajili ya ufuatiliaji ilikuwa changamoto kwa sababu Wizara ya Maji haikuipa kipaumbele bajeti ya ufuatiliaji wa shughuli za uendeshaji na ukarabati katika mamlaka za maji na usafi wa mazingira. Badala yake, Wizara ya Maji iliweka kipaumbele katika ufadhili wa miradi inayoendelea na mipya ya usambazaji wa maji.

Kutokana na hali hiyo, Wizara kama mwangalizi haikuteteleza majukumu yake kwa ufanisi. Zaidi ya hayo, Wizara ya Maji haikuhakikisha kuwa hatua za kurekebisha zilichukuliwa haraka iwezekanavyo juu ya dosari iliyobainika katika uendeshaji na ukarabati wa miradi ya usambazaji wa maji. Katika suala hili, miradi iliyoanzishwa ya usambazaji wa maji ilikabiliwa na hatari ya kutokuwa endelevu kwa sababu ya kuchelewa kutambuliwa kwa kasoro na kuchukua hatua husika za kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa.

9.7 Athari katika Kufikia Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano na Malengo ya Maendeleo Endelevu

Sehemu hii inatoa maelezo juu ya mchango wa matokeo ya ukaguzi katika usimamizi wa jumla wa uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya usambazaji wa maji katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Lengo la 6 na lengo dogo la 6.4 la Mpango wa Maendeleo Endelevu linataka kuhakikisha ufanisi wa matumizi ya maji katika sekta zote na kuhakikisha uvunaji endelevu na usambazaji wa maji safi ili kukabiliana na uhaba wa maji na kupunguza idadi ya watu wanaoathirika na uhaba wa maji ifikapo mwaka 2030. Mpango wa Pili na wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unalenga kupunguza maji yasiyo ya mapato nchini kwa kuboresha miundombinu ya usambazaji maji. Kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam lililenga kupunguza maji yasiyo ya mapato kutoka asilimia 47 hadi asilimia 30 ifikapo mwaka 2021/22. Pia, utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ulikuwa na lengo la kupunguza maji yasiyo ya mapato kutoka asilimia 35 hadi asilimia 20 Jijini Dar es Salaam na kutoka asilimia 30 hadi 20 kwenye makao makuu ya mikoa ifikapo mwaka 2025/26.

Kwa ujumla, kufanikiwa kwa lengo la 6 na lengo dogo la 6.4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linaonekana pia katika Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kunakolenga kuhakikisha uboreshaji wa miundombinu ya usambazaji maji na kupunguza maji yasiyo ya mapato katika vituo vyote vya Mkoa ikiwemo Dar es Salaam hakujaifikiwa katika mikoa yote.

Ukaguzi ulibaini kuwa mpango umefanikiwa katika mamlaka mbili tu kati ya nane za maji zilizotembelewa ambazo ni Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Moshi katika makao makuu ya Mkoa wa Kilimanjaro na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Kahama iliyopo katika makao makuu ya Wilaya ya Kahama kwa mwaka wa fedha 2021/22 ambayo asilimia ya maji yasiyo ya mapato haikuzidi asilimia 30 ya maji yanayozalishwa. Kwa miradi ya maji vijijini iliyopo chini ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, hakukuwa na kumbukumbu zozote kuhusu maji yasiyo ya mapato.

Ukaguzi ulibaini kuwa moja ya sababu za kutofikia lengo la maji yasiyo ya mapato yasiyozidi asilimia 30 ya maji yanayozalishwa ifikapo mwaka

2021/22 kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni ukarabati usiojitosheleza wa miundombinu ya maji kama vile mita za maji na mitandao ya mabomba kutokana na kutokuwapo kwa mipango ya ukarabati wa kinga na utengaji wa bajeti inayojitosheleza kutokana na makusanyo yasiyojitosheleza ya mapato ya maji.

Kwa kuwa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano una mwaka mmoja tu tangu uanze, ukaguzi una maoni kwamba kama changamoto hizi zilizobainika hazitatatuliwa kwa kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hii, lengo la kupunguza maji yasiyo ya mapato ifikapo mwaka 2025/26 unaweza usifanikiwe.

9.8 Hitimisho la Ukaguzi

Kwa kuzingatia taaarifa zilizokusanywa na kuchambuliwa, imebainika kuwa, Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira, haifanyi kazi kwa ufanisi ya kuendesha na kukarabati miradi ya usambazaji wa maji ili kuhakikisha kuwa miradi inakuwa endelevu.

Hali hii ilitokana na uendeshaji duni wa miundombinu ya usambazaji maji kutokana na kutoandaa ratiba ya ukaguzi wa kila siku, wiki, mwezi na mwaka kwa vifaa vikubwa vya maji kama vile pampu na transfoma; ukusanyaji hafifu wa ankaru za maji kutoka kwa wateja wanaopata huduma ya maji ambapo katika mamlaka za maji 8 zilizotembelewa, jumla ya shilingi bilioni 31.676 hazikukusanywa kutoka kwa wateja kwa miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22. Kiasi hiki cha fedha kingeweza kutumika kwa ajili uendeshaji wa shughuli za usambazaji maji.

Aidha, ukaguzi ulibaini utunzaji duni wa miundombinu ya usambazaji maji kutokana na kukosekana kwa mipango ya ukarabati wa kinga. Kutokana na hali hiyo, ilibainika kuwa jumla ya mita 63,727 za maji zilikuwa hazifanyi kazi; kupasuka kwa mabomba ambayo hayakukarabatiwa; na kuwa na pampu za maji zisizofanya kazi. Kutokana na kukosekana kwa mpango wa ukarabati wa kinga, ukaguzi ulibaini kuwa mamlaka karibu zote za maji hazikufanikiwa kufikia kiwango kinachotakiwa cha maji yasiyo ya mapato yasiyozidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa. Kwa mwaka 2020/21, ni mamlaka ya maji moja tu ya Moshi kati ya 8 za maji zilizotembelewa ndiyo ilifikia lengo. Kwa miaka ya fedha 2019/20 na 2021/22 katika mamlaka zote

nane za maji zilizotembelewa hakuna mamlaka hata moja iliyofikia lengo la maji yasiyo ya mapato yasiyozidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa. Kiasi cha mapato kinachopotea kutokana na maji yasiyo ya mapato juu ya kiwango kinachotakiwa katika miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21 kilikuwa shilingi bilioni 57.23 na shilingi bilioni 60.96 mtawalia



HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

SURA YA KUMI

10



HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

10.1 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho lililotokana na mapitio na uchambuzi wa matokeo ya ripoti 12 za ukaguzi wa ufanisi zilizofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Pia inatoa mapendekezo ambayo yanaelekezwa kwa vyombo husika vilivyokaguliwa.

10.2 Hitimisho la Ukaguzi la Ujumla

Ukaguzi unatambua juhudi za taasisi zilizokaguliwa katika kuboresha utendaji wao ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambayo dhima yake kuu ilikuwa mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanywa katika maeneo tajwa hapo juu ulihitimisha kwamba, licha ya juhudi zilizofanywa na taasisi zilizokaguliwa katika kuhakikisha kuwa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unafikiwa, bado kulikuwa na changamoto za kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kuna mapungufu katika utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini; usimamizi wa mifumo ya utoaji wa huduma za afya, sayansi, teknolojia na uvumbuzi, mazingira na uhakika wa chakula; usimamizi wa mali na uwekezaji wa Serikali; na mipango-miji na maendeleo ya makazi ya watu pamoja na usimamizi wa usambazaji wa maji nchini. Mapungufu haya yanahitaji hatua za haraka ili kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali katika kufikia mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya binadamu kulingana na Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yanafikiwa. Maelezo ya hitimisho yanafafanuliwa zaidi kulingana na ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi.

10.3 Hitimisho Mahususi

Hitimisho mahususi la taarifa hii ni kama ilivyofafanuliwa hapa chini.

10.3.1 utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu nchini

Ukaguzi huu ulihitimisha kuwa, licha ya kujumuisha Malengo ya Maendeleo Endelevu katika muktadha wa kitaifa na uanzishaji wa vyanzo vingine vya ukusanyaji wa rasilimali-fedha, Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hazijasimamia ipasavyo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu kuanzia muktadha wa mipango ya kitaifa hadi utekelezaji katika ngazi za chini za Serikali. Hali hii ni kutokana na Wizara ya Fedha na Mipango kutosimamia ufuatiliaji na tathmini ya taarifa za utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Pia, Wizara ya Fedha na Mipango haikuweza kuoanisha taasisi muhimu za utekelezaji wa malengo na taasisi zisizo za kiserikali katika kuhakikisha ushirikiano ili kufikia maeneo ya kipaumbele katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Maika Mitano ili kuhakikisha utekelezaji wa Maelengo ya Maendeleo Endelevu unazingatia kanuni za ufanisi, tija na wekevu.

Pia, OR-TAMISEMI haijaweza kutekeleza uratibu, ushirikiano na mawasiliano ya kutosha baina ya wadau wa utekelezaji na kuongoza uhuishaji wa taarifa na utekelezaji wa malengo ya maendeleo endelevu katika ngazi za chini za serikali za mitaa ili kuhakikisha ufikiaji wa malengo yaliyowekwa na "kutomwacha mtu nyuma" katika ngazi zote za utekelezaji.

10.3.2 Usimamizi wa mifumo ya utoaji wa huduma za afya

Ukaguzi unahitimisha kuwa usimamizi wa mfumo wa utoaji wa huduma za afya haukufanyika ipasavyo kwa sababu udhibiti wa vituo binafsi vya afya, udhibiti wa malipo kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwenda kwa watoa huduma za afya na udhibiti wa vyanzo vya mionzi haukusimamiwa ipasavyo.

Wizara ya Afya haikuwa na utaratibu wenye tija na ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa utoaji wa huduma za afya zinazotolewa na vituo binafsi na hiari nchini, ambapo usimamizi na ukaguzi katika vituo binafsi na hiari vya afya haukufanyika kwa kiwango kinachoridhisha.

Pia, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya haukuweka utaratibu wa kutosha wa udhibiti wa malipo ya madai kutoka katika vituo vya afya ili kuhakikisha kuwa madai hayo ni halisi, sahihi na kamili kwa sababu Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya haukuhakikisha kuwa vituo vya afya vinazingatia miongozo ya matibabu na makubaliano ya kimkataba wakati wa utoaji wa huduma za bima ya afya kwa walengwa.

Pia, taratibu zilizopo za udhibiti wa madai ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yaliyochakatwa na kulipwa zilikuwa sahihi na kamilifu vya kutosha na hatua za kurekebisha zilichukuliwa kwa wakati kwa madai yasiyo ya kweli ili kupunguza upotevu wa fedha. Tathmini ya utendaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwenye uchakataji wa malipo ya madai kutoka kwenye vituo vya huduma za afya haikufanyika mara kwa mara.

Pia, mifumo ya udhibiti iliyopo katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilishindwa kuhakikisha kwamba madai yaliyochakatwa na kulipwa yalikuwa ya kweli, sahihi na yamekamilika. Mfuko ulishindwa kuchukua kwa wakati hatua za kurekebisha madai yasiyo ya kweli ili kupunguza hasara za kifedha. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilifanya tathmini duni ya utendaji wake.

Zaidi ya hayo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, haikuhakikisha kunakuwa na udhibiti wa kutosha wa vyanzo vya mionzi nchini ili kupunguza hatari kwa watumiaji, umma na mazingira. Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikuwa na mbinu bora za udhibiti na usalama kwa vyanzo vya mionzi. Pia, Tume haifuatilia vya kutosha vyanzo vya mionzi ili kuhakikisha usalama kwa wafanyakazi wanaofanya kazi na vyanzo vya mionzi, umma na mazingira. Pia, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia haikufuatilia na kutathmini mara kwa mara utendaji kazi wake na ule wa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kuhusu udhibiti wa vyanzo vya mionzi nchini.

10.3.3 Sayansi, ubunifu na teknolojia

Hitimisho kuu la ukaguzi huu ni kwamba shughuli za utafiti na uvumbuzi hazikusimamiwa ipasavyo kwa sababu Serikali haikuweza kusimamia ipasavyo utekelezaji wa mikakati na mipango iliyoandaliwa ya kuibua na kusajili shughuli za tafiti na bunifu kwa kuhakikisha kunakuwapo uratibu madhubuti katika utekelezaji wa shughuli zinazolenga kukuza utafiti, teknolojia na ubunifui nchini; na ni taasisi chache zilizokuwa na uhusiano kama inavyotakiwa na kanuni.

Vilevile, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania hazikusimamia ipasavyo tafiti na bunifu ili kukuza uvumbuzi na teknolojia nchini kwa sababu hazikuhakikisha kuwapo kwa mikakati na mipango iliyoandaliwa ya kuibua na kusajili shughuli zote za utafiti na uvumbuzi; kusimamia shughuli za utafiti na uvumbuzi zilizosajiliwa; kuratibu wahusika wakuu katika utekelezaji wa shughuli za utafiti na uvumbuzi; na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za utafiti na uvumbuzi.

Vivyo hivyo, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mamlaka ya Serikali Mtandao haikusimamia ipasavyo upangaji na upatikanaji wa mifumo ya TEHAMA ya Serikali kwa sababu haikuhakikisha kuwa taasisi za umma zinapata mifumo ya TEHAMA kwa namna ambayo itachangia kufikia manufaa yaliyotarajiwa.

Zaidi ya hayo, Mamlaka ya Serikali Mtandao haikuhakikisha kwamba uanzishaji wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini umepangwa na kuanzishwa ipasavyo; na kuwapo kwa utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba mahitaji ya mifumo ya TEHAMA yanatayarishwa vya kutosha na kuwasilishwa kwa wadau wote husika kabla ya kupata mifumo ya TEHAMA Serikalini. Ilibainika kuwa taasisi za Serikali zilitengeneza mifumo ya TEHAMA ambayo inasaidia vyema michakato yao ya biashara na upimaji na ukabidhi wa mifumo iliyopatikana ya TEHAMA.

10.3.4 Mazingira na uhakika wa chakula

Ukaguzi unatambua juhudi zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa mazingira na uhakika wa chakula nchini. Hata hivyo, ukaguzi unatimisha kuwa serikali haijasimamia ipasavyo mipango ya ulinzi wa mazingira na uhakika wa chakula ili kuimarisha maendeleo ya binadamu kupitia ulinzi wa viumbe hai na kupunguza hasara baada ya mavuno ili kuongeza uhakika wa chakula nchini.

Ofisi ya Makamu wa Rais haikusimamia ipasavyo viumbe vamizi katika mazingira ya nchikavu hivyo kuongeza hatari ya athari mbaya kwa viumbe hai na mifumo ya ikolojia nchini. Hali hii ilidhihirishwa na ukweli kwamba, kulikuwa na hatua duni za kuzuia mazalia, ukuaji na kuenea kwa viumbe vamizi nchini. Hatua zilizotumika kudhibiti viumbe vamizi zilibainishwa

kuwa hazina ufanisi. Aidha, kulikuwa na uratibu hafifu miongoni mwa wadau muhimu katika kuhakikisha usimamizi wa viumbe vamizi nchini. Vilevile, ufuatiliaji na tathmini ya mikakati, mipango na ubunifu katika kusimamia viumbe vamizi ilibainika kuwa na mapungufu.

Kwa upande mwingine, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, na Wizara ya Kilimo hazikusimamia ipasavyo shughuli za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo. Hali hii ilithibitishwa na kuwapo kwa mazingira yasiyofaa kwa wasindikaji wa kilimo. Aidha, teknolojia zinazohitajika za usindikaji na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo hazikufikiwa kwa urahisi na wasindikaji wengi wa mazao ya kilimo wadogo na wa kati kutokana na gharama kubwa. Kukosekana kwa utaratibu madhubuti wa ufadhili na utekelezaji wa mikakati iliyopo ni miongoni mwa sababu za usimamizi usiofaa wa usindikaji na uongezaji thamani ya mazao ya kilimo nchini.

10.3.5 Usimamizi wa mali za umma na uwekezaji wa mali za Serikali

Ukaguzi unatambua juhudi zilizofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma katika kuboresha usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali na uwekezaji wa rasilimali za serikali. Hata hivyo, hatua zaidi bado zinahitajika ili kuhakikisha usimamizi madhubuti wa uondoshaji wa magari ya Serikali na uwekezaji wa rasilimali za Serikari unafanyika ipasavyo.

Kwa kuzingatia matokeo kama yalivyojadiliwa kuhusiana na malengo ya kaguzi hizi mbili za ufanisi hususani kuhusu ukaguzi wa usimamizi wa uondoshaji wa magari ya Serikali, inahitimishwa kuwa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora hazikusimamia ipasavyo utaratibu huu. Pamoja na kutambua juhudi zinazofanywa na Serikali kama vile kuunda Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS), utoaji wa umiliki wa mali unaotokana na Waraka wa Miradi ya Serikali Na. 7 na Mwongozo wa Usimamizi wa Mali, ukaguzi huu unahitimisha kuwa Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora hazikusimamia ipasavyo uondoshaji wa magari ya Serikali.

Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa hatua zaidi bado zinahitajika ili kuboresha usimamizi wa uondoshaji wa magari ya serikali nchini Tanzania.

Hali hii ni kwa sababu utambuzi wa magari yaliyoondoshwa kwa njia ya mnada kwa wafanyakazi wa umma haukufanywa vizuri. Vilevile, kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa utoaji wa idhini ya kuondoshwa kwa magari ya serikali. Uamuzi wa kuondosha magari ya serikali kwa njia ya mnada huchukua muda mrefu bila sababu ya msingi. Aidha, utaratibu huu hauna ufanisi wala uwazi, na haufanywi mara kwa mara. Kwa hivyo, magari ya Serikali yanachukua muda mrefu yakiwa yamehifadhiwa tu pasipo kuondoshwa, hivyo kusababisha kushuka kwa thamani ya magari hayo.

Aidha, kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi wa usimamizi wa uwekezaji wa mali zisizohamishika, ukaguzi unahitimisha kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii haikusimamia ipasavyo shughuli za uwekezaji wa mali zisizohamishika ili kuhakikisha malengo ya Mifuko yanafikiwa ambayo ni kuongeza mapato ya uwekezaji kwa lengo la kukua kiuchumi na kijamii.

Hali hii ilisababishwa zaidi na mpango usioridhisha wa uwekezaji wa mali zisizohamishika; utunzaji duni wa mali za uwekezaji; kushindwa kuendesha mali za uwekezaji ipasavyo; na ufuatiliaji wa mali za uwekezaji usio na tija.



10.3.6 Usimamizi wa urasimishaji wa makazi holela

Ukaguzi unatambua juhudi zinazofanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuwezesha shughuli za urasimishaji na kuongeza kasi ya upatikanaji wa hatimiliki na kupunguza makazi holela. Ukaguzi unahitimisha kuwa mchakato wa urasimishaji haujasimamiwa ipasavyo ili kuwezesha kupunguza makazi holela nchini.

Hali iko hivi kutokana na kwamba, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa miaka minane kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2021/22 ziliweza kutambua jumla ya viwanja 2,348,324, ambapo kati ya hivyo, ni viwanja 171,210 pekee vilikamilisha mchakato wa urasimishaji hadi kupata hatimiliki sawa na asilimia saba ya viwanja vilivyotambuliwa. Hii inamaanisha kuwa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zilipunguza ukubwa wa makazi holela kwa asilimia saba tu ya viwanja vilivyotambuliwa kwa ajili ya urasimishaji kwa kipindi cha miaka nane. Hali hii ilisababishwa na OR-TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ofisi za ardhi

za mikoa, na halmashauri kutokuwa na bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli za urasimishaji ufanyakaji wa kampeni kwa ajili ya uhamasishaji wa wananchi ili kuongeza ari ya wananchi kuchangia gharama za urasimishaji; na upungufu wa watumishi kwa asilimia 69 hasa katika kada ya mipango-miji, wapima ardhi na maofisa ardhi.

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa, ucheleweshaji wa urasimishaji ulichangiwa na uratibu hafifu kati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, OR-TAMISEMI, ofisi za ardhi za mikoa, na mamlaka za serikali za mitaa. Hali hii ilitokana na maofisa waliokuwa wakifanya kazi chini ya halmashauri kama vile maofisa mipango-miji, wapima-ardhi, maofisa ardhi, na wathamini wa ardhi waliokuwapo katika ofisi za halmashauri kutotoa taarifa kwa wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa husika au makatibu tawala wa mikoa na badala yake waliripoti moja kwa moja kwa kamishna msaidizi wa ardhi wa mkoa ambaye yuko chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hali hii ilisababisha OR-TAMISEMI kutokuwa na taarifa za urasimishaji wa makazi holela nchini ili kuweza kuchukua hatua za kuongeza kasi ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji.

10.3.7 Usambazaji wa maji



Kwa kuzingatia taaarifa zilizokusanywa na kuchambuliwa, imebainika kuwa, Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini na mamlaka za maji na usafi wa mazingira, haiKUfanya kazi ya kuendesha na kukarabati miradi ya usambazaji maji kwa ufanisi ili kuhakikisha kuwa miradi inakuwa endelevu.

Hali hii ilitokana na uendeshaji usiojitosheleza wa miundombinu ya usambazaji maji kutokana na kutoandaa ratiba ya ukaguzi wa kila siku, wiki, mwezi na mwaka kwa vifaa vikubwa vya maji kama vile pampu na transfoma. Sababu nyingine ni ukusanyaji usiojitosheleza wa ankara za maji kutoka kwa wateja wanaopata huduma ya maji, ambapo katika mamlaka za maji 8 zilizotembelewa, jumla ya shilingi bilioni 31.676 hazikukusanywa kutoka kwa wateja kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2019/20 mpaka 2021/22. Kiasi hiki cha fedha kingeweza kutumika kwa ajili uendeshaji wa shughuli za usambazaji maji.

Aidha, ukaguzi ulibaini utunzaji usioridhisha wa miundombinu ya usambazaji maji kutokana na kukosekana kwa mipango ya ukarabati wa kinga. Kutokana

na hali hiyo, ilibainika kuwa jumla ya mita za maji 63,727 zilikuwa hazifanyi kazi; kupasuka kwa mabomba ambayo hayakukarabatiwa; na kuwapo kwa pampu za maji zisizofanya kazi. Kutokana na kukosekana kwa mpango wa ukarabati wa kinga, ukaguzi ulibaini kuwa mamlaka za maji hazikufanikiwa kufikia kiwango kinachotakiwa cha maji yasiyo ya mapato yasiyozidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa. Kwa mwaka 2020/2021 ni mamlaka ya maji moja tu ya Moshi kati ya mamlaka nane za maji zilizotembelewa ndiyo ilifikia lengo. Kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22 mamlaka zote nane za maji zilizotembelewa hakukuwa na mamlaka hata moja iliyofikia lengo la maji yasiyo ya mapato yasiyozidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa. Kiasi cha mapato kinachopotea kutokana na maji yasiyo ya mapato juu ya kiwango kinatakiwa katika miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21 kilikuwa shilingi bilioni 57.23 na shilingi bilioni 60.96 mtawalia.

10.4 Mapendekezo ya Ukaguzi

Sehemu hii inawasilisha mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi wa changamoto zilizobainishwa kwenye ripoti hii. Ili kufanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa katika kufikia maendeleo ya binadamu na mabadiliko ya kiuchumi muhimu kwa ajili ya kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, taasisi zilizokaguliwa zinashauriwa kutekeleza mapendekezo ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Ili kuhakikisha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu na Mpango wa Pili na Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unafanikiwa kwa tija na ufanisi ndani ya kipindi kilichopangwa:

Wizara ya Fedha na Mipango inashauriwa:

- Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu unawiana vizuri na kuratibiwa katika ngazi zote za utekelezaji kwa madhumuni ya kuzingatia muda uliyowekwa hadi mwaka 2030. Kadhalika, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imehimizwa kuimarisha uratibu na mwongozo kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kutosha wa mipango-mkakati kwa kushirikisha na kujumuisha vikundi vilivyvo katika mazingira hatarishi.

Wizara ya Afya inahimizwa:

- Kukagua utendaji kazi wake (kuhusu michakato ya usajili wa vituo, ukaguzi wa vituo, ukaguzi wa kitbibu na upangaji wa bei za huduma za afya) na iandae mifumo ya udhibiti na mikakati itakayohakikisha kuwa Vituo Binafsi vya Afya vinatoa huduma za afya bora na kwa bei nafuu.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unahimizwa:

- Kuendeleza udhibiti thabiti (ikiwemo ya mifumo ya Tehama na Miongozo) katika vituo vya afya na wakati wa uchakataji wa madai katika ofisi za NHIF ili kuhakikisha madai yatakayolipwa ni sahihi na ya kweli kwa huduma zote za afya; na
- Kufanya mapitio ya mara kwa mara katika vifurushi vya wanufaika ili kuhakikisha bei za bidhaa zote zinaendana na hali halisi ya soko.

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania inahimizwa:

- Kuimarisha mifumo ya udhibiti wa vyanzo vya mionzi, ili kuhakikisha vyanzo vya mionzi havidhuru watumiaji, umma na mazingira kwa ujumla.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania inahimizwa:

- Kuendeleza na kutekeleza mfumo wa kina wa usimamizi wa utafiti na uvumbuzi, mfumo huu unapaswa kujumuisha michakato ya kutambua, kufuatilia, na kutathmini shughuli zote za utafiti na uvumbuzi. Inapaswa pia kutoa miongozo iliyo wazi kwa watafiti na wadau wengine kuhusu jinsi ya kushiriki katika shughuli hizi na jinsi ya kuripoti matokeo yao.

Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mamlaka ya Serikali Mtandao zinahimizwa:

- Kufanya tathmini ya kina ya mahitaji kabla ya kutekeleza mfumo wowote wa TEHAMA ili kubaini mahitaji mahususi ya shirika. Pia, kuhakikisha kuwapo kwa mafunzo na usaidizi wa kutosha; kuhakikisha matumizi bora ya mifumo ya TEHAMA; na kutoa mafunzo ya kutosha na

usaidizi kwa watumiaji wa mwisho. Hatua hizi ziwezeshe kwa kufuatilia na kutathmini utekelezaji ili kubaini masuala au maeneo yoyote ya kuboresha.

Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, kwa kushirikiana na wizara za kisekta, zinazohusika inasisitizwa:

- Kuwezesha usimamizi wa viumbe vamizi nchini na kuhakikisha kuna hatua madhubuti za kuzuia na kudhibiti viumbe hawa. Hatua hii iambatane na uratibu na ufuatiliaji na tathmini ya kutosha ya hatua zote zinazochukuliwa ili kukabiliana na athari za viumbe vigeni vamizi nchini.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Kilimo zinahimizwa:

- Kuhakikisha usimamizi madhubuti wa shughuli za usindikaji na uongezaji thamani wa mazao ya kilimo kwa kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi kwa kufanikisha upatikanaji wa teknolojia za kutosha za usindikaji wa mazao ya kilimo na uongezaji thamani wa mazao pamoja na upatikanaji wa masoko. Hatua hizi ziwezeshe kupitia uratibu na ufuatiliaji na tathmini madhubuti ya shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo nchini.

Wizara ya Fedha na Mipango inahimizwa:

- Kuandaa mwongozo na mfumo wa uondoshaji wa magari utakaoeleza mchakato mzima wa uondoshaji au mzunguko na hatua muhimu kwa kila hatua ili kuepusha ucheleweshaji wa uondoshaji wa magari ya Serikali.

Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inahimizwa.

- Inasisitizwa kuweka utaratibu wa kuhakikisha uwazi na haki wakati wa mchakato wa uondoshaji wa magari ya Serikali kwa watumishi wa umma.

Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Serikali na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii inahimizwa:

- Kuandaa mpango wa uwekezaji wa mali, utunzaji wa mali za uwekezaji kwa kufanya matengenezo, uendeshaji wa mali za uwekezaji, na ufuatiliaji wa uendeshaji wa mali za uwekezaji.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inapaswa:

- Kuandaa uangalizi wa kina ili kuwezesha usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa udhibiti wa makazi holela nchini. Hatua hizo ni pamoja na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli za udhibiti, kuongeza mafungu kwa ajili ya kampeni ya uhamasishaji jamii ambayo italenga kuongeza ari ya jamii kuchangia mfuko kwa ajili ya shughuli za udhibiti, na kuboresha uratibu wa shughuli za udhibiti miongoni mwa wadau muhimu ili kukuza shughuli za udhibiti nchini.

Wizara ya Maji inapaswa:



- Kuandaa mikakati ya kina ili kuwezesha miradi madhubuti ya uendeshaji na ukarabati wa mifumo ya miundombinu ya usambazaji wa maji ili kuhakikisha kuwa inakuwa endelevu nchini. Hatua hizo zinapaswa kuhakikisha upunguzaji wa maji yasiyo ya mapato na uendelevu wa usambazaji wa maji katika miundombinu yote ya maji iliyojengwa nchini.

MAREJELEO

1. Association of Private Healthcare Facilities in Tanzania (APHFTA) (2016). *End evaluation of five-year strategic plan for 2016-2020*, Tanzania
2. Association of Private Healthcare facilities in Tanzania (APHFTA) (2021). *Development of five-year new strategic plan for 2021-2025*, Tanzania
3. Commission for Science and Technology (2010). *National Research and Development Policy*: Tanzania
4. Commission for Science and Technology (2016). *Strategic Plan (2016-2021)*: Tanzania
5. Commission for Science and Technology (2018). *National Research Registration and Clearance Guidelines*: Tanzania
6. Commission for Science and Technology (2018). *Research and Innovation Impact Bulletin, Vol 1*: Tanzania
7. Commission for Science and Technology (2020). *National Research and Innovation Monitoring Framework*: Tanzania
8. Commission for Science and Technology (2020). *Report of the Stakeholders' Meeting on Coordination of Research Registration and Permits*: Tanzania
9. Commission for Science and Technology (2020). *STI Indicator Report*: Tanzania
10. Commission for Science and Technology (2020). *The Global Innovation Index (GII) Report*: Tanzania
11. Commission for Science and Technology (2021). *Field Monitoring Report*: Tanzania
12. Commission for Science and Technology (2021). *Fostering Innovation for Sustainable Socio-economic Development - Innovative Cluster Subprogram Field Monitoring Report*: Tanzania
13. Commission for Science and Technology (2021). *Repository Project Report*: Tanzania

-
14. Commission for Science and Technology (2021). *Research and Innovation Impact Bulletin, Vol 2: Tanzania*
 15. Commission for Science and Technology (2021). *Research and Innovation Impact Bulletins, Vol 3: Tanzania*
 16. Commission for Science and Technology (2022). *National Research Registration and Clearance Guidelines: Tanzania*
 17. Energy and Water Utility Regulatory Authority (EWURA) (2022), *Districts and Township Water Utilities Performance Report: Tanzania*
 18. International Atomic Energy Agency (IAEA) (2007). *Identification of Radioactive Sources and Devices*. Nuclear Security Series No.5, Technical Guidance Reference Manual.
 19. John Bukombe, Stuart W. Smith, Hamza Kija, Asheeli Loishooki, Glory Sumay, Machoke Mwita, Grayson Mwakalebe and Emilian Kihwele, (2018). *Fire regulates the abundance of alien plant species around roads and settlements in the Serengeti National Park: Tanzania*
 20. Lee et al (2018). *Projected lifetime cancer risks from occupational radiation exposure among diagnostic medical radiation workers in South Korea, BMC Cancer Research Article: South Korea*
 21. Magina, F.B., Kyessi, A.G., & Kombe, J.W. (2020). *The Urban Land Nexus-Challenges and Opportunities of Regularising Informal Settlements: The Case Studies of Dar es Salaam and Mwanza in Tanzania*. *Journal of African Real Estate Research*, 5(1), pp.32-54.
 22. Mgonja, C.I. (2017). *Paper on Evaluation on use of industrial radiography for weld joints inspection: Tanzania*.
 23. Ministry of Finance and Planning (2016). *National Five Years Development Plan, 2016/2017 - 2020/2021: Tanzania*
 24. Ministry of Finance and Planning (2017-2022). *Approval for Disposals; Tanzania*
 25. Ministry of Finance and Planning (2019). *Voluntary National Review (VNR): Dodoma, Tanzania*
 26. Ministry of Finance and Planning (2019). *Public Assets Management Guideline: Tanzania*

-
27. Ministry of Finance and Planning (2021). *National Five Years Development Plan 2021/2022 - 2025/2026*: Tanzania
 28. Ministry of Finance and Planning (2022). *Database of Government Asset Management Information System (GAMIS)*: Tanzania
 29. Ministry of Works and Transport (2017-2022). *Valuation Reports*; Tanzania
 30. Ministry of Works and Transport (2022). *Database of Motor Vehicles*: Tanzania
 31. Mosha H.J. (2002). *Health Sectors Reforms in Tanzania*: Tanzania
 32. National Bureau of Statistics (2018). *Sustainable Development Data Gaps Assessment with ADAPT*: Dodoma Tanzania
 33. National Social Security Fund (2020). *Investment Policy*: Tanzania
 34. Nuhu, S., Mpambije, C.J. & Ngussa (2020). *Challenges in healthcare service delivery under public-private partnership in Tanzania*: Tanzania
 35. Oberlin, S.A. and Kassim, M.S. (2018). *Assessment of Factors Affecting Maintenance of Rural Water Supply Schemes in Kilolo District, Tanzania. A Case of Kipaduka Water Scheme*: Tanzania
 36. Paula A. Tibandebage, Haji H. Semboja, Phare Mujinja, and Henock Ngonyani (2001). *Private Sector Development the Case of Private Healthcare facilities*: Tanzania
 37. President's Office - Public Service Management and Good Governance (2016). *Guidelines of the Proceedings on Valuation of used Government Motor vehicles*: Tanzania
 38. President's Office - Public Service Management and Good Governance (1994/95). *Circular No. 4 of 1994 and No.5 of 1995 for Advancing Government Motor vehicles*: Tanzania
 39. Public Service Social Security Fund (2021). *Investment Policy*: Tanzania
 40. Rural Water Supply and Sanitation Agency (2019). *Monitoring Reports for the period of 2019/2020 - 2021/2022*: MoW, Tanzania

-
41. Tanzania National Parks (TANAPA) (2022). *Report on Extent and Severity of Invasive Alien Species in National Parks: Tanzania*
 42. The African Union, (2014). *Malabo Declaration on Accelerated Agricultural Growth: Ethiopia*
 43. The East African Community, (2015). *Geneva Forum on Agro-processing Trade: Tanzania*
 44. The e-Government Authority (2011). *e-Government Strategic Plan 2011/2017 - 2020/2021: Tanzania*
 45. The e-Government Authority (2014). *ICT Project Implementation Guideline: Tanzania*
 46. The e-Government Authority (2017, 2022). *Annual Financial Performance Reports (2017/2018 - 2021/2022): Tanzania*
 47. The e-Government Authority (2020). *e-Government Security Assessment Report: Tanzania*
 48. The e-Government Authority (2020). *ICT Steering Committee Minutes: Tanzania*
 49. The Ministry of Health (2019). *Functions of Regional Health Management System: Tanzania*
 50. The United Nations (2015). *The 2030 Agenda for Sustainable Development: USA*
 51. The United Republic of Tanzania (2004). *National Environmental Management Act: Tanzania*
 52. The United Republic of Tanzania (2017). *Agricultural Sector Development Programme (ASDP II): Tanzania*
 53. The United Republic of Tanzania (2017). *Magamba Nature Forest Reserve Management Plan: Tanzania*
 54. The United Republic of Tanzania (2018). *National Data Roadmap for Sustainable Development Lesson and Recommendations from 2016 - 2018: Tanzania*

-
55. The United Republic of Tanzania (2018). *National-Financial-Inclusion-Framework-NFIF-2018-2022*: Tanzania.
 56. The United Republic of Tanzania (2019). *The National Invasive Species Strategy and Action Plan (2019-2029)*: Tanzania
 57. The United Republic of Tanzania (2019). *Postharvest Management Strategy Implementation Plan*: Tanzania
 58. The United Republic of Tanzania (2015). *The National Biodiversity Strategy and Action Plan (NBSAP) 2015 - 2020*: Tanzania
 59. The United Republic of Tanzania (2015). *A Report on, Tanzania Industrial Competitiveness Report*: Tanzania
 60. The United Republic of Tanzania, (2017). *A Report on Assessment of Status of National Fod Security, 2017/2018-2021/2022*: Tanzania
 61. The United Republic of Tanzania (2017). *A Report on, Provision of Consultancy Services to Evaluate the Implementation of the Small and Medium Enterprises Development, Policy of 2003*: Tanzania
 62. The United Republic of Tanzania (2018). *National Post-Harvest Management Plan*: Tanzania
 63. The United Republic of Tanzania (2019). *A Report on Assessment of Households Vulnerability, 2019/2020 and 2020/2021*: Tanzania
 64. The United Republic of Tanzania (2022). *National Environmental Master Plan for Strategic Interventions (2022 - 2032)*: Tanzania
 65. The United Republic of Tanzania, Ministry of Natural Resources and Tourism-Tanzania Forest Services (TFS) Agency (2016). *Management Plan for Mount Rungwe Nature Forest Reserve (2016/2017 - 2020/2021)*: Rungwe District, Mbeya Region, Tanzania
 66. The United Republic of Tanzania, Ministry of Natural Resources and Tourism (2019). *Ngorongoro Conservation Area Invasive Plants Strategic Management Plan*: Tanzania
 67. United Nations (2015). *Resolution adopted by the General Assembly on 25 September 2015*: New York

68. United Republic of Tanzania (2008). *Social Security (Regulatory Authority) Act*: Tanzania
69. United Republic of Tanzania (2015). *the Social Security Schemes Investment Guidelines*: Tanzania
70. United Republic of Tanzania (2018). *The National Social Security Fund Act*: Tanzania
71. United Republic of Tanzania (URT) (2019). *Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2019*: Tanzania
72. URT (1996). *The National Science and Technology Policy*: Tanzania
73. URT (1997). *Ministry of Information, Communication and Information Technology, National Telecommunication Policy 2015*: Tanzania
74. URT (1999). *The National Health Insurance Fund Act*: Tanzania
75. URT (2000). *The Poverty Reduction Strategy Paper*: Tanzania
76. URT (2003). *Atomic Energy Act*: Tanzania
77. URT (2003). *Ministry of Information, Communication and Information Technology, National Information and Communication Policy*: Tanzania
78. URT (2004). *Atomic Energy (protection from ionising radiation) Regulations*: Tanzania
79. URT (2004). *Environmental Management Act*: Tanzania
80. URT (2006). *Ministry of Information, Communication and Information*: Tanzania
81. URT (2010). *Electronic and Postal communication Act (EPOCA)*: Tanzania
82. URT (2011). *Atomic Energy (Fees and Charges) Regulations*: Tanzania
83. URT (2011). *Atomic Energy (Radiation Safety in the Mining and Processing of Radioactive Ores), Regulations*: Tanzania
84. URT (2011). *Packaging and Transportation of Radioactive Material Regulations*: Tanzania

85. URT (2013). *National Cancer Control Strategy 2013/2014 - 2019/2020*: Tanzania
86. URT (2013). *National Nuclear Technology Policy*: Tanzania
87. URT (2015). *Health Sector Strategic Plan (HSSP IV & V) For the Period from July 2015 to June 2026*: Tanzania
88. URT (2015). *Ministry of Information, Communication and Information Technology, National ICT Policy Implementation Strategy 2016/2017 - 2020/2021*: Tanzania
89. URT (2015). *NHIF Strategic Plan (2015-2020)*: Tanzania
90. URT (2015). *Waraka Namba 1 wa Urasimishaji, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, 2019*: Tanzania
91. URT (2016). *National Information and Communications Technology Policy*: Tanzania
92. URT (2016). *Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi: "Mwongozo wa Kuandaa Mipango ya Urasimishaji Makazi Yaliyojengwa Kiholela, Agosti 2016*: Tanzania
93. URT (2017). *National-Health-Policy*: Tanzania
94. URT (2018). *NHIF First Quarter Performance Report*: Tanzania
95. URT (2019). *Mining Act*: Tanzania
96. URT (2019). *Budget Implementation Reports, The National Health Insurance Fund from 2019/2020 to 2021/2022*: Tanzania
97. URT (2019). *Fraud Investigation Reports, The National Health Insurance Fund from 2019/2020 to 2021/2022*: Tanzania
98. URT (2019). *President's Office - Public Service Management and Good Governance (2019) e-Government Strategy 2021/2022 - 2025/2026*: Dodoma, Tanzania
99. URT (2019). *Settlement Reports from the visited Healthcare Facilities from 2019/2020 to 2021/2022*: Tanzania

100. URT (2019). *Voluntary National Review (VNR), Empowering and Ensuring Inclusiveness and Equality*: Tanzania
101. URT (2020). *Ministry of Water (June, 2020): Five Year Medium Term Strategic plan 2019/2020 - 2023/24*: Tanzania
102. URT (2020). *Water Sector Status Report 2015 to 2020*: Ministry of Water, Tanzania
103. URT (2020). *CAG Annual General Report for Public Authorities*: Tanzania
104. URT (2020). *Ministry of Water Design, Construction, Supervision, Operation and Maintenance Manual; Volume IV, Operation and maintenance of water supply and maintenance of water supply and sanitation project - Fourth Edition*: Tanzania
105. URT (2020). *National Research and Innovation Monitoring Framework*: Tanzania
106. URT (2020). *NHIF AFYA NJEMA, Edition No. 14*: Tanzania
107. URT (2021). *Ministry of Education, Science and Technology - Annual Performance Report*: Tanzania
108. URT (2021). *NHIF Claims Management Manual*: Tanzania
109. URT (2021). *NHIF Quality Assurance Manual, 4th Edition*: Tanzania
110. URT (2022). *CAG Annual General Report for Public Authorities*: Tanzania
111. URT (2022). *NHIF AFYA NJEMA, Edition No. 18*: Tanzania
112. URT (2022). *Tathmini ya Urasimishaji Makazi Holela Ndani ya Mamlaka za Serikali Za Mitaa Nchini, 2022*: Tanzania
113. URT (2016). *The Implementation Strategy for the National Five - Year Development Plan 2016/2017 - 2020/2021, Volume I, the Action Plan*, Tanzania
114. URT (2016). *The national five year development plan 2016/2017 - 2020/2021*: Tanzania
115. URT (2021). *The Second National Five-Year Development Plan (FYDP II), 2015/2016 - 2020/2021*: Tanzania

116. URT (2021). *The Second National Five-Year Development Plan (FYDP II), 2015/2016 - 2020/2021*: Tanzania
117. URT, Ministry of Health (2007). *Health Policy*, Tanzania
118. URT, Tanzania Atomic Energy Commission (2018). “*Five Year Corporate Strategic Plan (CSP) 2018/2019-2022/2023*” Tanzania
119. URT, Tanzania Atomic Energy Commission (2020), “*Inspection Reports conducted between 2019/2020-2020/2021*” Tanzania
120. URT, Tanzania Atomic Energy Commission (2020), “*Internal Audit Report of 2019/2020*” Tanzania
121. URT, the Ministry of Health (1977). *The Health Laboratory (Regulation) Act No. 10*, Tanzania
122. URT, the Ministry of Health (1977). *The Private Hospitals (Regulation) Act No. 6*, Tanzania
123. URT, the Ministry of Health (2007). *The Health Laboratory Practitioners Act No. 22*, Tanzania
124. URT, the Ministry of Health (2008). *The Human Resource for Health Strategic Plan for the period 2008-2013*, Tanzania
125. URT, the Ministry of Health (2009). *Health Sector Strategic Plan III for the period 2009/10-2015/2016*, Tanzania
126. URT, the Ministry of Health (2013). *Standard Treatment Guidelines and Essential Medicines List*, Tanzania
127. URT, the Ministry of Health (2013). *Summary and Analysis of the Comprehensive Council Health Plans*, Tanzania
128. URT, the Ministry of Health (2017). *National Supportive Supervision Guidelines for Quality Healthcare services*. Tanzania



KIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 1: Tathmini ya muda uliotumika kati ya uwasilishaji wa mapendekezo na tarehe za utoaji wa taarifa za ushauri kati ya mwaka 2017 na 2022

| Muda (Siku) | Idadi ya Madokezo ya Ushauri | Asilimia (ya Jumla kuu) | Maoni |
|--------------------------|------------------------------|-------------------------|----------------|
| Kati ya Siku 0 hadi 14 | 44 | 7 | Kwa wakati |
| Kati ya Siku 15 hadi 30 | 26 | 4 | Nje ya wakati |
| Kiati ya Siku 31 hadi 60 | 26 | 4 | Nije ya wakati |
| Zaidi ya Siku 60 | 549 | 85 | Nje ya wakati |
| Jumla | 645 | 100 | - |

Chanzo: Taarifa ya ushauri wa miradi 2017-2022 kutoka Wakala wa Ununuzi Serikalini

